# JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**MKOA WA RUVUMA**

**KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KINACHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 28/12/2022**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Tunduru
S. L. P. 74,
57180 **Songea**

**Tel: +255 025-2602256 / 2602238**
**Fax: +255 025-2602144 / 2602128**
**Email**: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**Tovuti**: www.ruvuma.go.tz

**DISEMBA, 2022**

**YALIYOMO**

2.0 AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC)........................ 3

3.0 MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA.............................. 4

4.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 29 DISEMBA 2021. ..................................................................... 128

5.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MKOA KWA MWAKA 2021/2022, 2022/2023 KUISHIA TAREHE 30, NOVEMBA 2022 NA TAARIFA YA MAANDALIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024. ............................. 153

6.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KISEKTA................................. 179

6.1 UCHUMI NA UZALISHAJI (KILIMO, MIFUGO, UVUVI, MALIASILI NA USHIRIKA) ..................................................................................................................... 179

6.2 VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NA TAARIFA YA TIMU YA KUCHAMBUA, KUANDAA NA KUAINISHA MFUMO MZURI WA UWAJIBIKAJI KWA JAMII (CSR) WA WACHIMBAJI WA MADINI MKOA WA RUVUMA ................... 233

6.3 AFYA, LISHE NA USTAWI WA JAMII ........................................................... 251

6.4 ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI................................................................ 261

6.5 UTUMISHI NA UTAWALA ............................................................................. 277

7.0 TAARIFA ZA TAASISI NA MASHIRIKA ................................................................ 280

7.1 WAKALA WA HIFADHI YA CHAKULA KANDA YA SONGEA (NFRA).......... 280

7.2 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) MKOA WA RUVUMA ............... 282

7.3 OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU (NBS) MKOA WA RUVUMA - MATOKEO YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA 2022. .......................................................... 285

7.4 SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ............................................ 294

7.5 WAKALA MAJI MIJINI NA VIJIJINI (RUWASA)............................................ 309

7.6 MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA SONGEA (SOUWASA) .............316

7.7 WAKALA WA MISITU (TFS) - TAARIFA YA SHAMBA LA MITI WINO NA MPEPO ..........................................................................................................................323

7.8 CHUO CHA MAFUNZO YA UHIFADHI WA MALIASILI KWA JAMII – LIKUYU SEKAMAGANGA.......................................................................................................336

7.9 OFISI YA KAMISHNA MSAIDIZI WA ARDHI MKOA WA RUVUMA. .............342

7.10 IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI MKOA WA RUVUMA - WIZARA YA MAMBO YA NDANI .........................................................................................348

7.11 TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMABA NA RUSHWA (TAKUKURU) ..........352

7.12 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA MKOA WA RUVUMA .355

7.13 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA) – OFISI YA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI ...............................................366

7.14 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA BANDARI KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI JUNI 2022 .........................................................................377

8.0 TAARIFA ZA KAMATI ZA USHAURI ZA WILAYA (DCC) ....................................383

8.1 WILAYA YA SONGEA .........................................................................383

8.2 WILAYA YA TUNDURU.......................................................................392

8.3 WILAYA YA MBINGA .........................................................................395

8.4 WILAYA YA NAMTUMBO ....................................................................407

8.5 WILAYA YA NYASA ...........................................................................419

## 2.0 AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC)

## KINACHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA

## TAREHE 28 DESEMBA 2022

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 29/12/2021
4. Utekelezaji wa yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 29/12/2021.
5. Taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2021/2022, 2022/2023 kuishia tarehe 30, Novemba 2022 na Taarifa ya Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.
6. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kisekta
    - Uchumi na Uzalishaji (Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Maliasili na Ushirika)
    - Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Taarifa ya Timu ya Kuchambua, Kuandaa na Kuainisha Mfumo Mzuri wa Uwajibikaji Kwa Jamii (**CSR**) wa Wachimbaji wa Madini Mkoa wa Ruvuma
    - Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii
    - Elimu na Mafunzo ya Ufundi
    - Utumishi na Utawala
7. Taarifa za Utekelezajai wa shughuli za Taasisi na Mashirika ya umma.
    - Wakala wa Hifadhi ya Chakula Kanda ya Songea (**NFRA)**
    - Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA)** Mkoa wa Ruvuma.
    - Ofisi ya Taifa ya Takwimu **(NBS**) Mkoa wa Ruvuma - Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2022.
    - Shirika la Umeme Tanzania **(TANESCO)**
    - Wakala maji Mijini na Vijijini (**RUWASA**)

- Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea (**SOUWASA)**
- Wakala wa Misitu **(TFS)** - Taarifa ya Shamba la Miti Wino na Mpepo
- Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – LIKUYU SEKAMAGANGA
- Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma.
- Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma - Wizara ya Mambo ya Ndani
- Taasisi ya Kuzuia na Kupamaba na Rushwa **(TAKUKURU)**
- Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania **(TAA)** Mkoa wa Ruvuma
- Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji **(EWURA)** – Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
- Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari **(TPA)** Ziwa Nyasa
- Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (**TCRA)**

**8.** Taarifa za Kamati za Ushauri za Wilaya **(DCC)**

- Wilaya ya Songea;
- Wilaya ya Tunduru;
- Wilaya ya Mbinga;
- Wilaya ya Namtumbo;
- Wilaya ya Nyasa.

9. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti.
10. Kufunga Kikao.

## 3.0 MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA

## TAREHE 29/12/2021 MKOA WA RUVUMA

## 1.0 WALIOHUDHURIA

| | JINA | WADHIFA | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 1. | Brig.Gen. (Balozi) Wilbert A. Ibuge | Mkuu wa Mkoa | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg Stephen M. Ndaki | Katibu Tawala Mkoa | Katibu |
| 3. | Mhe. Eng. Stella Manyanya (Mb) | Mbunge wa Jimbo la Nyasa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Jonas W. Mbunda | Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Benaya Z. Kapinga | Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dkt. Damas D. Ndumaro (Mb) | Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Daimu Iddi Mpakate | Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama | Mbunge wa Jimbo la Madaba | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Jackline Msongozi | Mbunge Viti Maalumu | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Pololet K. Mgema | Mkuu wa Wilaya ya Songea | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Col. Laban E. Thomas | Mkuu wa Wilaya ya Nyasa | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Dkt. Julius K. Ningu | Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Julius Sunday Mtatiro | Mkuu wa Wilaya ya Tunduru | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Aziza Mangasongo | Mkuu wa Wilaya ya Mbinga | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Hairu H. Musa | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Michael L. Mbano | Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Stewart Nombo | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Teothanes T. Mlelwa | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Kelvin K. Mapunda | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Mbinga | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Desderius O. Haule | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Simon Kapinga | Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Juma Alfan Pandu | Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | Mjumbe |
| 23. | Dkt. Frederick Sagamiko | Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa Songea | Mjumbe |
| 24. | Ndg. Jimson Mhagama | Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Nyasa | Mjumbe |
| 25. | Ndg. Ambokile Paul | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | Mjumbe |
| 26. | Ndg. Chiza C. Marando | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Wilaya ya Tunduru | |
| 27. | Ndg. Juma Haji Juma | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga | Mjumbe |
| 28. | Ndg. Khashim S. Lugome | Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Songea. | Mjumbe |
| 29. | Ndg. Grace S. Quintine | Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mbinga | Mjumbe |
| 30. | Adv. Sajidu I. Muhsmed | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Madaba | Mjumbe |
| 31. | Dr. Jairy N. Khanga | Katibu Tawala Msaidizi Afya | Mjumbe |
| 32. | Ndg. Jumanne Mwankhoo | Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu | Mjumbe |
| 33. | Ndg. Bakari A. Mketo | Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Rasilimali watu | Mjumbe |
| 34. | Ndg. Eng. Gilbert D. Simya | Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu | Mjumbe |
| 35. | Ndg. Juma N. Fuluge | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Elimu | Mjumbe |

### 1.1 WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA

| NA | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jenista Mhagama (Mb) | Mbunge – Jimbo la Peramiho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Judith Kapinga (Mb) | Mbunge Mwakilishi Kundi la Vijana Taifa | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Dkt. Thea Ntara (Mb) | Mbunge Mwakilishi Kundi la Vyuo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hassan Zidadu Kungu (Mb) | Mbunge – Jimbo la Tunduru Kaskazini | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mariam M. Nyoka (Mb) | Mbunge Viti Maalum | Mjumbe |
| 6. | Ndugu Joel Mbewa | Katibu Tawala Msaidizi – Serikali za Mitaa | Mjumbe |
| 7. | Ndugu Jeremiah Sendoro | Katibu Tawala Msaidizi – Uchumi na Uzalishaji | Mjumbe |

### 1.2 KAMATI YA ULINZI NA USALAMA MKOA:

| | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| i. | Alpha Kisava | Ag. Mshauri Jeshi la Akiba Mkoa | Mwalikwa |
| ii. | A/Insp Chesco P. Mbata | Kaimu Kamanda Zimamoto Mkoa | Mwalikwa |
| iii. | Ndg. Joseph Elisafi | Afisa Usalama Mkoa | Mwalikwa |
| iv. | SACI – Tununasya Adam | Afisa Uhamiaji Mkoa | Mwalikwa |
| v. | ACP Willngton Kahumiza | Kamanda wa Magereza Mkoa | Mwalikwa |
| vi. | Ndg. Hamza Y. Mwenda | Kamanda Takukuru Mkoa | Mwalikwa |
| vii. | ACP Gwisail pagi | Ag. Kamanda wa Polisi Mkoa | Mwalikwa |
| viii. | IJ COL JM Ndunguru | Mkuu wa Kikosi 42 KJ | Mwalikwa |
| ix. | Philipo Ndaro | Mkuu wa Kambi 401 KV | Mwalikwa |

**1.3 MAKATIBU TAWALA WA WILAYA:**

| | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Pendo Daniel | Katibu Tawala Wilaya Songea | Mwalikwa |
| 2. | Ndg. Paulo N. Lugongo | Kaimu Katibu Tawala wilaya Nyasa | Mwalikwa |
| 3. | Ndg. Augustino S. Maneno | Kaimu Katibu Tawala Wilaya Tunduru | Mwalikwa |
| 4. | Ndg. Aden H. Nchimbi | Katibu Tawala Wilaya Namtumbo | Mwalikwa |
| 5. | Ndg.Mwanaid M. Mang`uru | Kaimu Katibu Tawala Wilaya Mbinga | Mwalikwa |

**1.4 WAALIKWA KUTOKA SEKRETARIETI YA MKOA:**

| | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Theresia R. Mselenga | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi | Mwalikwa |
| 2. | Ndg. Matha Mwakatika | Mhasibu | Mwalikwa |
| 3. | Ndg. Nelson L. William | Afisa Mifugo | Mwalikwa |
| 4. | Ndg. Hakimu Mafuru | Afisa Elimu Taaluma Mkoa | Mwalikwa |
| 5. | Ndg. Romanusi Komba | Mtaalamu wa TEHAMA | Mwalikwa |
| 6. | Ndg. Basil S. Amuli | Afisa Uvuvi | Mwalikwa |
| 7. | Dr. Magafu Majura | Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Songea | Mwalikwa |
| 8. | Ndg. Yahya A. Madenge | Afisa Tehama | Mwalikwa |
| 9. | Ndg. Walumbe Komba | Mkuu wa Kitengo TEHAMA | Mwalikwa |
| 10. | Ndg. Musa Nkolabigawa | Katibu wa Mkuu wa Mkoa | Mwalikwa |
| 11. | Ndg. Xsaveria Mlimira | Afisa Maendeleo ya jamii Mkoa | Mwalikwa |
| 12. | Ndg. Africanus Chale | Afisa Misitu Mkoa | Mwalikwa |
| 13. | Ndg. Mariam Juma | Afisa Maendeleo ya Jamii | Mwalikwa |
| 14. | Ndg. Ahmad H. Nammoe | Afisa Tawala Mkoa | Mwalikwa |
| 15. | Ndg. Mathew Mlele | Mkaguzi wa Ndani | Mwalikwa |
| 16. | Ndg. Onesmo F. Gama | Afisa Maendeleo ya Jamii | Mwalikwa |
| 17. | Ndg. Sunday S. Hebuka | Mtakwimu | Mwalikwa |
| 18. | Ndg. Deogratius D. Sibula | Afisa Mifugo Mkoa | Mwalikwa |
| 19. | Ndg. Paulo C. Msemwa | Afisa Kilimo Agr. | Mwalikwa |
| 20. | Ndg. Adelini Komba | Mkaguzi wa Ndani Serikali za Mitaa | Mwalikwa |
| 21. | Ndg. Grace Mafuru | Afisa Tawala Mkoa | Mwalikwa |
| 22. | Ndg. Frank Hosea | Mkadiriaji Majenzi | Mwalikwa |

| | | |
|---|---|---|
| 23. Ndg. Anzawe Chaula | Afisa Taaluma Mkoa | Mwalikwa |
| 24. Ndg. Regius Sanane | Mchumi | Mwalikwa |
| 25. Ndg. Onesmo Ngao | Afisa Kilimo Mkoa | Mwalikwa |
| 26. Ndg. Winfrida Barua | Mwangalizi wa Ofisi | Mwalikwa |
| 27. Ndg. Onesmo Mpuya | Afisa Kilimo Agri. | Mwalikwa |
| 28. Ndg. Joseph Martin | Afisa Biashara | Mwalikwa |
| 29. Ndg. Zachary Nhatunga | Mchumi | Mwalikwa |
| 30. Ndg. Albano Midelo | Afisa Habari | Mwalikwa |
| 31. Ndg. Aneth Ndonde | Afisa Habari | Mwalikwa |
| 32. Ndg. Amandus Chilumba | Afisa Serikali za Mitaa | Mwalikwa |
| 33. Ndg. January Haule | Mhasibu | Mwalikwa |
| 34. Ndg. Leonida Ngira | Mhasibu | Mwalikwa |
| 35. Ndg. Leodigard Riziki | Afisa Manunuzi | Mwalikwa |
| 36. Ndg. Humphrey Millanzi | Afisa Manunuzi | Mwalikwa |
| 37. Issa O. Nyika | EDMO | Mwalikwa |
| 38. Ndg. Upendo Kinemela | Afisa Hesabu | Mwalikwa |
| 39. Ndg. Mussa Hamsini | Mhasibu Msaidizi | Mwalikwa |
| 40. Ndg. Denis W. Chiwangu | Mtakwimu | Mwalikwa |
| 41. Ndg. Amina Tindwa | Afisa Serikali za Mitaa | Mwalikwa |

**1.5 VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA:**

| **JINA** | **WADHIFA** | **NAFASI** |
|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Richard Tawe | Katibu ACT | Mwalikwa |
| 2. | Ndg. Hamisi H. Kaisi | Katibu CUF | Mwalikwa |
| **3.** | Ndg. Oswald A. Nyoni | Katibu TLP | Mwalikwa |
| **4.** | Ndg. Paulo M. Geho | KATIBU TADEA | Mwalikwa |
| **5.** | Ndg. Ally S. Mapunda | Mwenyekti TADEA | Mwalikwa |
| **6.** | Ndg. Ibrahimu M. Komba | Katibu UPDP | Mwalikwa |
| 7. | Ndg. Ibrahim M. Komba | Katibu UDP | Mwalikwa |
| **8.** | Ndg. Juma Mtokani Haule | Mwenyekiti NCCR Mageuzi | Mwalikwa |

**1.6 WAALIKWA KUTOKA HALMASHAURI, WAKUU WA TAASISI ZA SERIKALI NA ZISIZO ZA SERIKALI**

| | **JINA** | **WADHIFA** | **NAFASI** |
|---|---|---|---|
| 1 | Emmanuel Godfrey Maneno | Afisa Mfawidhi RADC | Mwalikwa |
| 2 | Eng. Eugonics Thomas | Engineer TBA | Mwalikwa |
| 3 | Eng. Elia Kayeph | Kny. RM TEMESA | Mwalikwa |
| 4 | Christopher Ntandu | Ag. DLPO Mbinga DC | Mwalikwa |
| 5 | Habil Mwaimu | Kaimu Meneja TTC | Mwalikwa |
| 6 | Osward Mfaume | SIDO - Ruvuma | Mwalikwa |
| 7 | Lucas Mwimo | Branch director BOT Mtwara | Mwalikwa |
| 8 | Karim Ally | Meneja Kanda EWURA | Mwalikwa |
| 9 | Francis Mhina | CSO – SHZ EWURA | Mwalikwa |
| 10 | Stephen J. Bakari | Kaimu DPLO Nyasa | Mwalikwa |
| 11 | Nada T. Nyabas | Mkuu wa Chuo Songea TTC | Mwalikwa |
| 12 | Janeth Shitindi | Kaimu MEC Songea MC | Mwalikwa |
| 13 | Sebastian Loham | Afisa Mfawidhi LATRA | Mwalikwa |
| 14 | Eng. Rebman Ganshonga | RUWASA | Mwalikwa |
| 15 | Dr. Themistocles Nyeme | M/M/Chuo Songea | Mwalikwa |
| 16 | Wilson s. Ngonze | Meneja Mkoa GPSA | Mwalikwa |
| 17 | Jeremia S. Kilembe | Accountant NFRA | Mwalikwa |
| 18 | Issa A. Issa | Meneja (M) Bodi ya Tumbaku | Mwalikwa |
| 19 | Paresia Waziri | Meneja SOAGRO | Mwalikwa |
| 20 | Eng. Patrick Kibasa | MD SOUWASA | Mwalikwa |
| 21 | Donald Y. Makuwa | TPLO Mbinga TC | Mwalikwa |
| 22 | Mwadishi L. Nchimbi | DPLO – Madaba | Mwalikwa |
| 23 | Godbless S. Matowo | Kaimu OFC TFS – Songea | Mwalikwa |
| 24 | Erick Soko | Kaimu Mhifadhi Makumbusho ya Taifa | Mwalikwa |
| 25 | Abdul A. Milandu | RMO – Madini MADINI | Mwalikwa |
| 26 | Florence Mwakasege | Meneja TANESCO | Mwalikwa |
| 27 | Dr. Julius E. Frank | DRC OUT | Mwalikwa |
| 28 | Kasfory M. Timbula | GM TTGAVI | Mwalikwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 29 | Amina S. Hommdogani | RM TTGAM | Mwalikwa |
| 30 | Amos Kanige | DPLO – Namtumbo | Mwalikwa |
| 31 | Daudi Kashimba | Kaimu Meneja NHC | Mwalikwa |
| 32 | Rev, Suleman Nzyemba | Mchungaji Moravian | Mwalikwa |
| 33 | Domi Kapinga | Meneja RUCODIA | Mwalikwa |
| 34 | Mwantumu Athumani | RSM NBS | Mwalikwa |
| 35 | Salum Masamaki | M/Kiti Machinga Ruvuma | Mwalikwa |
| 36 | Yeremias Ngerangera | A/Habari – Namtumbo | Mwalikwa |
| 37 | Lilian C. Stephen | Mlinzi wa Jadi Mahakama | Mwalikwa |
| 38 | Elizabeth Ngowi | REO TCCIA | Mwalikwa |
| 39 | Jane Myau | PRINCIPAL Likuyu | Mwalikwa |
| 40 | Irene Mville | Afisa Masoko Likuyu | Mwalikwa |
| 41 | Bumu Masuba | Mrajisi Ruvuma | Mwalikwa |
| 43 | Amos Malemula | Kaimu Kamishna wa Ardhi Ardhi Mkoa | Mwalikwa |
| 44 | N.E. Mkanjabi | Meneja Vipimo | Mwalikwa |
| 45 | Daudi Mkoma | ACT – RIE Irrigation | Mwalikwa |
| 46 | Henry Chagenda | Eng NIDIC | Mwalikwa |
| 47 | Ibrahimu F. Kibasa | R/Manager TARURA | Mwalikwa |
| 48 | Emmanuel Sangalali | FDT – PPP Manager FDT IRINGA | Mwalikwa |
| 49 | Juma Mwanga | Manager SONAMCU | Mwalikwa |
| 50 | Hellen Chuma | RPO DPP | Mwalikwa |
| 51 | Antony Masebe | C II TAWA KON | Mwalikwa |
| 52 | Juma T. Nyumayo | The Editor Tujifunze | Mwalikwa |
| 54 | Yahya Mudhihir | Meneja NSSF | Mwalikwa |
| 55 | Japhet Jonh | C.A Mahakama | Mwalikwa |
| 56 | Bosco Mwingira | Kaimu DPLO Tunduru | Mwalikwa |
| 57 | Adrian Ngailo | Katibu CWT | Mwalikwa |
| 58 | Jordan Mchami | Meneja Songea Airport | Mwalikwa |
| 59 | Jacqueline Moyo | A/Habari Songea DC | Mwalikwa |

## 1.7 SEKRETATIETI YA KIKAO

| | JINA LA MJUMBE | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Deogratius Sibula | Afisa Mifugo | Sekretarieti |
| 2. | Onesmo Mpuya | Afisa Kilimo | Sekretarieti |
| 3. | Romanius F. Komba | Afisa TEHAMA | Sekretarieti |
| 4. | Sunday S. Hebuka | Mtakwimu | Sekretarieti |
| 5. | Anzawe Chaula | Afisa Elimu Taaluma | Sekretarieti |
| 6. | Sophia Gama | Katibu Muhtasi | Sekretarieti |
| 7. | Regius Sanane | Mchumi | Sekretarieti |
| 8. | Zachary Ngatunga | Mchumi | Sekretarieti |

## 2.0 AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KINACHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 29 DESEMBA 2021

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 12/01/2021.
4. Utekelezaji wa yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 12/01/2021.
5. Taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2020/2021 kuishia tarehe 30 Juni, 2021
6. Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2021/2022 kuishia tarehe 30, Novemba 2021 na Taarifa ya Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023
7. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Uchumi na Uzalishaji (Kilimo, Mifugo, Viwanda, Biashara, Uwekezaji, Uvuvi, Maliasili na Ushirika.
8. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Afya.
9. Taarifa ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma.
10. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Elimu.
11. Taarifa za Taasisi na Mashirika
    - Taarifa ya Maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi toka Ofisi ya Taifa ya Takwimu Mkoa wa Ruvuma
    - Taarifa ya utendaji kazi wa Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Ruvuma (TRA).
    - Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za huduma ya Maji (RUWASA).
    - Taarifa ya hali ya upatikanaji wa huduma ya Umeme Mijini na Vijijini na Mipango iliyopo (TANESCO)
    - Taarifa ya Maendeleo Kanda ya Kusini Mashariki – Ruvuma (BOT).

- Wakala wa Misitu (TFS). Maombi ya Kutangazwa Kwenye Gazeti la Serikali Hifadhi za Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Madaba
- Taarifa ya Shamba la Miti Wino
- Taarifa ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere
- Taarifa ya Shamba la Miti Mpepo
- Taarifa ya Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – LIKUYU SEKAMAGANGA
- Taarifa ya Program ya FORVAC
- Taarifa ya utekelezaji wa Shughuli za Ardhi Mkoa wa Ruvuma.
- Taarifa ya Utendaji Kazi wa Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma - Wizara ya Mambo ya Ndani
- Taarifa ya Ununuzi wa Mahindi kutoka Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)
- Taarifa ya utekelezaji kutoka (TAKUKURU)
- Taarifa ya Ewura – Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Kwenye Kikao cha RCC Ruvuma Desemba 2021.
- Taarifa ya Wakala wa Vipimo (WIMA) - Mkoa wa Ruvuma

12. Taarifa za Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC)
13. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti.
14. Kufunga Kikao.

**3.0 MUHTASARI NA. RCC: 01/12/2021 KUFUNGUA KIKAO**

## UTANGULIZI

Katibu Tawala wa Mkoa ambaye ni Katibu wa kikao alianza kwa kuwakaribisha wajumbe kushiriki katika kikao cha kamati ya ushauri ya Mkoa.Baada ya kufanya ukaribisho aliwatambulisha wajumbe wote mmojammoja na wengine katika makundi. Kabla ya Katibu Tawala Mkoa kumkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao aliwaeleza wajumbe kuwa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa ni kikao kinachoendeshwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1977 iliyoanzisha Sekretarieti za Mikoa. Aidha, Katibu Tawala Mkoa alieleza kuwa kikao hiki ni muhimu kwani hutoa ushauri juu ya maendeleo ya Mkoa. Baada ya kusema hayo, alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

## Kufungua kikao

Mhe. Mwenyekiti ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajalia afya wajumbe na kuwawezesha kushiriki katika kikao
hicho muhimu. Mwenyekiti pia alitambua uwepo wa viongozi mbalimbali, wakiwemo viongozi wa dini, Wataalam na wajumbe wote waliohudhuria katika kikao cha Ushauri cha Mkoa (RCC).
Mwenyekiti alieleza kuwa anayoheshima kubwa kwa kuwaona wajumbe wote na waalikwa wakishiriki katika kikao hiki, kikao hiki ni cha kwanza kwangu kukiendesha nikiwa kama mwenyekiti nawashukuru sana!!!!!. Lakini napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua nitumikie nafasi hii ya Mkuu wa Mkoa.

Mwenyekiti pia alieleza kuwa kikao hiki ni fursa ya kujadili masuala anuai na muhimu kwa maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma, hivyo ni wajibu wetu kujadili kwa kina taarifa/agenda mbalimbali zitakazowasilishwa mbele ya kikao hiki.

Mwenyekiti pia alieleza juu ya mpango mkakati wa kilimo cha pamoja (Block farming) na kilimo cha mkataba, katika mpango huu mazao yatakayohusika ni alizeti, soya na ufuta, Mkoa umeshabainisha jumla ya ekari **48,343.35** kwa ajili ya mpango huo, Mazao hayo yote yatauzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani. Kwa msimu wa mwaka **2021/2022** Mkoa umepanga kulima ekari **3,435** kwa ajili ya alizeti, **3,590** kwa ajili ya soya na **5,279** kwa ajili ya ufuta**.** Aidha Mkoa umepokea Mbegu za alizeti tani **52.271** kutoka katika Taasisi ya **ASA**, mbegu za alizeti zimesambazwa kwa wakulima kupitia Halmashauri kwa kuwauzia wakulima bei ya **3,500** kwa kilo, sambamba na hilo Mkoa pia utapokea mbegu za soya baada ya wiki moja toka sasa na kilo moja itauzwa kwa bei ya sh. **4,000.**

Aliendelea kueleza kuwa Mkoa wa Ruvuma kwa kipindi cha miaka minne sasa unaongoza kwa uzalishaji wa chakula, hivyo Mkoa kuendelea kuwa na upatikanaji wa chakula cha kutosha, kutokana na hali ya mvua kuwa sio nzuri kwa mwaka huu, nawasihi wananchi wote kutumia chakula kilichopo kwa uangalifu.

Mwenyekiti pia alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa **Tsh**. **Bilioni 15** kwa ajili ya ununuzi wa mahindi, lengo ni kuwawezesha wakulima kuuza mazao yao kwa bei nzuri na kuwawezesha kumudu gharama za kununua mbolea.

Mwenyekiti pia alieleza kuwa bei za mbolea zimepanda sana hivyo tuendelee kuwa na uvumilivu kwenye kilimo tuweze kuongeza pato la Mkoa na la mtu mmojammoja, pamoja na kupanda kwa bei ya mbolea aliwataka wakulima wazingatie maelekezo ya Wataalam yanayotolewa ya kutumia mbolea mbadala **mfano. Minjingu.** hususani mbolea zinazouzwa kwa bei ndogo. Kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea Serikali imefanya jitihada za kuagiza mbolea kwa kiasi kikubwa ili kuongeza upatikanaji wa mbolea katika nchi.

Aidha mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na kuuza mazao kwa mfumo wa stakbadhi ghalani Mkoa utaendelea na mfumo huo. Hivyo wadau wote tunatakiwa kusimamia mipango ya kilimo tuliyoiweka kwa kufanya kazi kwa kujituma ili kuongeza uzalishaji wa mazao.

Mwenyekiti aliwakumbusha wajumbe juu ya kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato kupitia kodi na ushuru ambazo zinatumika katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, Afya, elimu, ununuzi wa ndege na shughuli zingine za maendeleo.

Mwenyekiti pia alieleza kuwa Mhe. Rais katika kuendelea kuleta maendeleo ndani ya nchi, ameendeleza ujenzi wa Reli ya kisasa **(SGR)** na **tarehe 28 Disema 2021** alishuhudia kusainiwa mkataba wa ujenzi wa

**(SGR)** loti ya tatu ya Mwanza na Isaka, Pia Mhe. Rais anafungua nchi pamoja na kuiunganisha kwa kujenga barabara na Reli, ili kurahisisha usafiri na usafirishaji wa mizigo. Katika Mkoa wa Ruvuma, Reli ya Mtwara korido pia itajengwa na kwasasa upembuzi yakinifu unaendelea.

Mwenyekiti alieleza kuwa Mkoa wa Ruvuma umepakana na nchi jirani za Malawi na Msumbiji. Hii ni fursa kubwa sana kwa Mkoa katika kufanya biashara mbalimbali za kimaendeleo. Hivyo Mkoa ni muhimu kuendelea kudhibiti njia za magendo za kuingiza na kuuza bidhaa ili biashara zifanyike kwa uhalali.

Mwenyekiti pia alieleza kuwa ufaulu wa matokeo ya kidato cha sita kwa mwaka 2021 umekuwa mzuri kwani Mkoa umepata wastani wa asilimia **99.9.** Kwa upande ufaulu wa darasa la saba sio mzuri, hivyo ni lazima zifanyike jitihada za makusudi ili kuongeza ufaulu.

Mwenyekiti pia alieleza kuwa Mkoa wetu umeletewa fedha jumla ya Tshs. **10.24** bilioni za mradi **Na. 5441 TCRP** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **500** kwa shule za Sekondari, Shule Shikizi za Elimu Msingi na Mabweni **3** ya watoto wenye mahitaji maalium. Alitoa pongezi kwa Halmashauri kwa kusimamia ujenzi wa madarasa na mabweni hayo kikamilifu, kwani hadi sasa ujenzi umekamilika kwa asilimia **90** na asilimia **10** jitihada za kumalizia zinaendelea. Mwenyekiti alitoa maelekezo ya kukamilisha ujenzi wa mabweni **3** kufikia tarehe **20 Machi 2022.**

Mwenyekiti pia alieleza kuwa Mkoa unatakiwa kuendelea kujenga Hospitali, Vituo vya afya, Zahanati na nyumaba za watumishi, aidha Mkoa una mpango wa kujenga Hospitali ya Mkoa katika eneo la Mwengemshindo, hivyo wataalam wa ardhi wanatakiwa kupima na kupanga eneo litakalojengwa hospitali.Vilevile aliwataka wataalam wa ardhi kuendelea kupima maeneo mengine kwa kuweka maeneo ya vivutio ili mji uweze kukua kwa haraka.

Mwenyekiti pia alieleza kuwa Mkoa wa Ruvuma umeongoza kitaifa katika zoezi la chanjo ya **UVICO – 19.** ***'Hongera sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma''*** Mwenyekiti alitoa wito kwa wananchi ambao hawajachanja waendelee kuchanja.

Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa **10 : 23 Asubuhi**

Aidha Mwenyekiti baada ya kufungua kikao aliwasihi wananchi wote kila mmoja kwa imani yake amuombe Mungu kwa ajili ya kupatikana kwa mvua, na baadae aliwakaribisha Viongozi wa dini wawili (kikristo na Islamic) kwa ajili ya kuliombea Taifa

na Mkoa ili mvua iweze kunyesha. Maombi hayo yalifanyika, na siku hiyohiyo kufikia muda wa saa **9:00** Mvua ilianza kunyesha. Hakika mungu anajibu maombi!

#### 4.0 MUHTASARI NA. RCC: 02/12/2021: KURIDHIA AGENDA

Agenda za kikao zilisomwa mbele ya kikao na Wajumbe wote kwa pamoja waliziridhia kuwa ndo agenda za kikao.

#### 5.0 MUHTASARI NA. RCC: 03/12/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) CHA TAREHE 29/12/2021

Wajumbe wa kikao walipokea na kupitisha muhtasari ulioandaliwa ukurasa kwa ukurasa.

#### 6.0 MUHTASARI NA. RCC: 04/12/2021: UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) CHA TAREHE 29/12/2021

Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 29/12/2021 iliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe. Aidha, wajumbe walipitia yatokanayo na kujadili yafuatayo:-

**i. Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa NFRA)**

Wajumbe walihoji kuhusu kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Vihenge vya kuhifadhia mazao vya yanayosimamiwa na Wakala wa hifadhi ya chakula ya Taifa **(NFRA).** Kwani ujenzi huo umechukua muda mrefu toka ujenzi ulivyoanza.Kikao kilielekeza kuwa yafanyike mawasiliano na Nchi ya Poland kupitia Wizara ya Kilimo ili kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi wa Vihenge. majibu ya ufuatiliaji yawasilishwe katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kinachofuata.

**ii. TANESCO Mkoa wa Ruvuma kukamilisha miradi ya usambazaji wa Umeme**

Wajumbe walihoji kuhusu kuchelewa kwa utelekezaji wa usambazaji wa umeme mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na awamu ya tatu mzunguko wa pili,

mradi unaotekelezwa na Tanesco na Wakala wa Umeme Vijijini (REA).Kikao kilielekeza kuwa ufuatiliaji wa karibu ufanyike ili kuhakisha kuwa Wakandarasi wanaongeza kasi ya ya utekelezaji wa mradi ili iweze kukamilika kwa wakati.

iii. **Mkakati wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana katika Halmashauri ya Madaba.**

Wajumbe walipongeza mpango huu ulioanzishwa na Mhe. Christina Mndeme aliyekuwa Mkuu wa Ruvuma kuwa ni mpango mzuri kwa maendeleo ya elimu katika Mkoa wa Ruvuma hususani katika kuweka mazingira mazuri ya kusoma kwa watoto wetu.

Wajumbe walihoji juu ya hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana katika Halmashuri ya Wilaya ya Madaba, kwani ilielekezwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kilichofanyika tarehe 12/01/2021 katika ukumbi wa Manispaa ya Songea.

Fedha zilizokusanywa kutokana na makato ya shilingi **7** kwa kilo moja ya ufuta zielekezwe katika ujenzi wa wigo wa shule ya Msingi Ruhila.

Kikao kilielekeza kuwa Mkoa uongezwe wigo wa ukusanyaji wa fedha kwa kukusanya shilingi 7 kwa kilo katika mazao ya mahindi, korosho,kahawa, Tumbaku, Soya, Ufuta na Mbaazi, badala ya kukusanya katika zao moja tu ambalo ni ufuta. Lengo ni kukusanya fedha nyingi na kufanikisha ujenzi wa Shule ya Wasichana na baadae kujenga Shule ya Sekondari ya Wavulana. Wajumbe waliekeza utaratibu wa kukusanya fedha kutoka katika zao la mahindi ufanyike kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Wajumbe walielekeza kuwa baada ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Madaba, kupitia mkakati huohuo ijengwe pia Shule ya Sekondari ya Wavulana.

iv. **Salaam Maalum za pongezi kutoka kwa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.**

Mwakilishi wa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma ambae ni Mhe. Stella manyanya Mbunge wa Jimbo la Nyasa alitoa pongezi kwa Mhe. Mkuu wa  Mkoa wa Ruvuma kwa niaba ya Wabunge wote. Alieleza kuwa Wabunge wote kwa pamoja wanatoa pongezi nyingi kwa kumpata kiongozi wa Mkoa ambaye ni shujaa katika kusimamia maendeleo ya Mkoa, Aidha alimpongeza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa kusimamia vyema ujenzi wa Madarasa **500** na mabweni matatu ya watoto wenye mahitaji maalum, ambapo utekelezaji wake hadi sasa umekamilika kwa asilimia **90.**

Pia alitoa pongezi kwa Mkoa wa Ruvuma kwa kusimamia utoaji wa chanjo ya **COVID 19** kwa wananchi na kuufanya Mkoa wa Ruvuma kuongoza Kitaifa katika zoezi la utoaji wa chanjo.

## 7.0 MUHTASARI NA. RCC: 05/12/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MKOA KWA MWAKA 2020/2021 KUISHIA TAREHE 30 JUNI, 2021.

### 7.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021.

Katika mwaka 2020/21 Mkoa wa Ruvuma uliidhinishiwa kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs. 244,091,777,293.55** Kati ya fedha hizo **Tshs. 225,066,777,293.55** ni Ruzuku ya Serikali Kuu na **Tshs. 19,025,000,000.00** ni fedha za mapato ya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mkoa na Halmashauri zake zilipokea na kukusanya **Tshs. 192,959,450,685.01** sawa na **asilimia 79** ya fedha idhinishwa. Kati ya fedha hizo Ruzuku ya Serikali Kuu ni **Tshs. 177,201,837,789.05** na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ni **Tshs 15,737,612,895.96**

Matumizi hadi kufikia Juni, 2021 yalikuwa ni **Tshs. 188,055,415,934.91** sawa na **asilimia 97.46** ya fedha pokelewa na makusanyo ya ndani.

**7.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2020/21 kuishia Juni, 2021.**

Mkoa wa Ruvuma kwa mwaka 2020/21 uliidhinishiwa kutumia **Tshs. 169,182,702,005.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Tshs. 134,943,539,210.00** ni kwa ajili ya mishahara na **Tshs. 25,239,162,795.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida kufikia Juni, 2021 yalikuwa ni **Tshs 138,476,173,663.00** sawa na asilimia 81.85 ya fedha idhinishwa.

Aidha, matumizi ya fedha kufikia Juni, 2021 yalikuwa **Tshs 136,384,159,633.00** sawa na asilimia **98.49** ya fedha zilizopokelewa.

**7.3 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020/21**

Katika mwaka 2020/21 Mkoa ulitengewa **Tshs 55,884,075,288.55** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo **Tshs 28,925,291,135.6** ni fedha za ndani na fedha za nje ni **Tshs 26,958,784,152.95**. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kiasi cha **Tshs 38,725,664,126.05** zilipokelewa sawa na **asilimia 69.30** ya fedha tengwa.

Matumizi ya fedha za maendeleo kufikia Juni, 2021 yalikuwa **Tshs 35,913,643,405.95** sawa na **asilimia** 92.74 ya fedha pokelewa.

**7.4 Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2020/21**

Mkoa wa Ruvuma katika mwaka 2020/21 uliidhinishiwa kukusanya **Tshs. 19,025,000,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani. Kufikia Juni**,** 2021 kiasi cha **Tshs 15,760,612,895.96** zilikusanywa kutoka kwenye vyanzo hivyo ikiwa ni sawa na **asilimia 82.84** ya lengo la makusanyo. Aidha, kiasi cha **Tshs. 2,758,472,871,871.07** zilipelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. **Tshs**

**1,359,494,004.00** zilipelekwa katika vikundi vya wanawake, vijana na walemavu kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi katika vikundi hivyo.

## 7.5 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2020/2021 KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2020 – JUNI, 2021.

Katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2020/21 Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri umefanikiwa kupata mafanikio yafuatayo: -

**Sekta ya Elimu**

i. Kuongezeka kwa uandikishaji kwa wanafunzi wa darasa la awali na la kwanza ambapo wanafunzi waliandikishwa kwa zaidi ya silimia 100 ya lengo la uandikishaji. Hii inatokana na utekelezaji wa program ya Elimu Bila Malipo kwa elimu msingi.

ii. Kuratibu na kusimamia Mitihani ya kitaifa ya Darasa la saba, Kidato cha nne, sita pamoja na upimaji wa kitaifa wa darasa la nne na kidato cha pili kwa ngazi ya Mkoa na Halmashauri

iii. Kujengwa kwa Madarasa 191, Maabara 20, Matundu ya vyoo 447, mabweni/Daharia 7, majengo ya ofisi za walimu 6 na Nyumba za walimu 3.

iv. Ujenzi wa Ofisi 1 ya Udhibiti ubora katika Halmashauri ya Madaba

**Sekta ya Afya**

i. Upatikanaji wa madawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya ni wa kuridhisha;

ii. Kupungua kwa vifo vya akina mama wajawazito kutoka vifo 63/100,000 hadi 55/100,000 kutokana na uboreshaji na uanzishwaji wa huduma za dharura (CEmONC services) katika vituo vya afya vilivyoboreshwa na Serikali;

iii. Ujenzi wa zahanati sita (06) katika Halmashauri ya Mji Mbinga, Namtumbo na Nyasa umekamilika;

iv. Ujenzi wa wodi 9 katika hospital za wilaya ya Nyasa, Namtumbo na Songea;

v. Ujenzi wa matundu ya vyoo 60 na mfumo wa maji safi na taka katika Zahanati 8 na vituo vya Afya 2;
vi. Ujenzi wa Zahanati tatu (3) katika Halmashauri ya Mbinga mji, Tunduru na Nyasa.

**Sekta ya Maendeleo ya Jamii**

i. Utoaji wa mikopo kiasi cha **Tshs. 1,359,494,004.00** kwa vikundi vya wanawake 200, vijana 190 na watu wenye ulemavu 70.

**Sekta ya Kilimo na Mifugo**

i. Usambazaji wa vifaranga 1,000,000 vya samaki umefanyika kwa wafugaji binafsi na Taasisi

ii. Jumla ya mashamba ya mfano 86 yaliandaliwa na kutumika kuwaelimisha wakulima juu ya kanuni bora za kilimo.

iii. Lita 312 za dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo zimegawiwa kwa wafugaji.

iv. Kuendelea na umaliziaji wa maghala ya kuhifadhia mazao

v. Kuendelea kutoa mafunzo kwa vyama vya ushirika

vi. Ufuatiliaji na usimamizi wa Miradi ya maendeleo ya Kilimo cha Mazao ya chakula na mazao ya biashara

vii. Mkoa umeendela kufanya vizuri ambapo kwa kipindi cha miaka miwili (3) ya 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021 Mkoa umekuwa ndio mzalishaji wa kwanza wa mazao ya Chakula Kitaifa.

## 7.6 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI WA MWAKA 2020/21.

- Wananchi katika baadhi ya Kata/Vijiji kuchangia kwa kusuasua au kutochangia kabisa nguvu zao katika shughuli za maendeleo.
- Upungufu wa watumishi katika baadhi ya Idara za Halmashauri hususani Ujenzi, Afya, Kilimo, Elimu.
- Upungufu wa vyombo ya usafiri hasa magari.
- Mabadiliko ya mara kwa mara ya bei ya vifaa vya viwandani hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo
- Kuchelewa na kutotolewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kupelekea miradi kutotekelezwa kwa wakati.
- Urejeshaji mdogo wa mikopo inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

## 7.7 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA.

Katika kuhakikisha changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2020/21 zinapatiwa ufumbuzi mikakati ya kiutekelezaji iliwekwa kama ifuatavyo: -

- Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani, kuvipitia vilivyopo na kusimamia makusanyo ili kuongeza wigo wa mapato ya ndani ya Halmashauri na kuweza kutekeleza shughuli za maendeleo.

- Kuendelea na uhamasishaji wa wananchi katika kushiriki na kuchangia nguvu kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

- Kuimarisha na kufanya ufuatiliaji wa mikopo inayotolewa kwa vikundi.

- Kuendelea kuzingatia kutenga bajeti kwa miradi ambayo haijatekelezwa kutokana na kutopokelewa kwa fedha za maendeleo.

**Majadiliano;**

Wajumbe wa kikao walipokea na kuipitisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2020/2021 kuishia tarehe 30 Juni, 2021**.**

## 8.0 MUHTASARI NA. RCC: 06/12/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MKOA KWA MWAKA 2021/2022 KUISHIA TAREHE 30, NOVEMBA 2021 NA TAARIFA YA MAANDALIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 8.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/2022

Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Mipango na Uratibu aliwasilisha taarifa kuwa kwa mwaka 2021/22 Mkoa wa Ruvuma uliidhinishiwa kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs. 264,361,765,745.96** Kati ya fedha hizo **Tshs. 244,029,530,745.96** ni Ruzuku ya Serikali Kuu na **TshS 20,332,235,000.00** ni fedha za mapato ya ndani.

Hadi kufikia Novemba, 2021 Mkoa na Halmashauri zake zilipokea na kukusanya **Tshs. 86,051,916,089.75** sawa na **asilimia 32.55** ya fedha idhinishwa. Kati ya fedha hizo Ruzuku ya Serikali Kuu ni **Tshs. 78,773,114,096.39** na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ni **Tshs 7,278,801,993.36.** Matumizi kufikia Novemba, 2021 yalikuwa ni **Tshs 70,683,753,250.35** sawa na **asilimia 82.14** ya fedha pokelewa. Mchanganuo wa mapato na matumizi ni kama ifuatavyo: -

### 8.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2020/21 kuishia Novemba, 2021.

Mkoa wa Ruvuma kwa mwaka 2021/2022 uliidhinishiwa kutumia **Tshs**. **163,692,012,852.96** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Tshs. 140,707,686,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **Tshs 22,984,326,852.96** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida kufikia Novemba, 2021 yalikuwa ni **Tshs 57,928,652,855.90** sawa na asilimia **35.39** ya fedha idhinishwa.

Aidha, matumizi ya fedha kufikia Novemba, 2021 yalikuwa **Tshs 56,300,207,949.48 sawa** na asilimia **97.19** ya fedha zilizopokelewa.

### 8.3 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2021/22

Katika mwaka 2021/22 Mkoa ulitengewa Tshs **80,337,517,893.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo Tshs. 36,065,640,893.00 ni fedha za ndani na fedha za nje ni Tshs**. 42,148,211,000.00.** Hadi kufikia Novemba, 2021 kiasi cha Tshs. **20,844,461,240.49** zilipokelewa sawa na **asilimia 25.95** ya fedha tengwa. Matumizi ya fedha za maendeleo kufikia Novemba, 2021 yalikuwa Tshs. **7,104,743,307.51** sawa na asilimia 34.08 ya fedha pokelewa.

### 8.4 Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2021/22

Mkoa wa Ruvuma katika mwaka 2021/22 uliidhinishiwa kukusanya **Tshs 20,332,235,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani. Kufikia Novemba, 2021 kiasi cha **Tshs 7,278,801,993.36** zilikusanywa kutoka kwenye vyanzo hivyo ikiwa ni sawa na asilimia **35.80** ya lengo la makusanyo. Aidha, kiasi cha **Tshs 1,326,918,541.42** zilipelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. **Tshs. 432,163,459.00** zilipelekwa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi katika vikundi hivyo.

**8.5 Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 Katika Mkoa wa Ruvuma.**

Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Mipango na Uratibu aliwasilisha taarifa kuwa kwa mwaka 2021/22 Mkoa wa Ruvuma ulipokea fedha nje ya bajeti **TZS. 12,020,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO -19. Fedha hizi zimepangwa kutumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa **448** katika shule za sekondari, vyumba vya madarasa **52** katika shule Shikizi, Ujenzi wa mabweni matatu **(3)** katika shule maalumu za Msingi zenye watoto wenye ulemavu. Miradi mingine ni ujenzi wa nyumba **7** za watumishi wa afya, ujenzi wa jengo moja la huduma za wagonjwa Mahututi na Majengo matatu ya huduma za dharura (EMD)

Hadi kufikia tarehe 20 Disemba, 2021 jumla ya madarasa 350 yalikuwa yamekamilika sawa na 70%, vyumba 150 vipo hatu za ukamilishaji. Kwa upande wa Ujenzi wa majengo ya EMD, ICU na nyumba za watumishi yapo katika hatua za maandalizi ya ujenzi.

**8.6 MAPOKEZI YA FEDHA ZA UJENZI WA VITUO VYA AFYA KWA HALMASHAURI**

Mkoa umepokea jumla ya **TZS.2,750,000,000.00** nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya **11** katika Tarafa. Fedha hizi zimetokana na tozo ya miamala

ya simu ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora za afya karibu na maeneo yao. Taarifa ilipokelewa.

## 8.7 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2021/2022 KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2021 – NOVEMBA, 2021

**Sekta ya Elimu**

- Uwezeshaji wa posho za Wakuu wa Shule wa Sekondari 158, Walimu wa Kuu wa Shule za Msingi 785 na Maafisa Elimu Kata 175.

- Kufanyika kwa mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi na Sekondari pamoja na upimaji kw adarasa la nne (4) na kidato cha pili (2).

- Kuwajengea uwezo walimu 810 kwa kupata mafunzo kazini katika mambo anuai (TEHAMA, Lishe, Elimu ya mapambano na kujikinga na UVIKO-19, mafunzo ya uthibiti ubora wa elimu).

- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 710 na ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa 29 kwa shule za Msingi na Sekondari

- Kuanza ujenzi wa mabweni 3 kwa shule zenye mahitaji maalum na Ujenzi wa matundu ya vyoo 925 kwa shule za msingi na Sekondari.

**Sekta ya Afya**

- Hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ni ya kuridhisha

- Ujenzi wa vituo vya afya 11 katika tarafa zisizokuwa na vituo vya afya

- Kuanza kwa ujenzi wa vituo vya afya vitatu (3) kwa kutumia fedha za mapato ya ndani kwa Halmashauri ya Mbinga DC, Tunduru DC na Manispaa ya Songea

**Sekta ya Maendeleo ya Jami**

- Kutoa mikopo kwa vikundi 67 vya vijana, akina mama na watu wenye ulemavu kiasi cha Tshs **472,769,459.00**

**Sekta ya Kilimo na Mifugo**

- Kuendelea na umaliziaji wa maghala ya kuhifadhia mazao
- Kuendelea kutoa mafunzo kwa vyama vya ushirika
- Kuendelea na ujenzi wa soko la samaki katika mji wa Mbamba bay
- Kuanzisha kilimo cha pamoja (block farming) katika mazao ya Alizeti, Ufuta na Soya.
- Jumla ya tani **52.721** za mbegu bora za Alizeti aina ya Standard OPV zilizalishwa na Wakala Wa Mbegu (ASA), Mbegu za Korosho tani **7** Kutoka bodi ya Korosho na kusambazwa kwa wakulima
- Mkoa umeendelea kufanya vizuri katika uzalishaji wa mazao ya nafaka ambapo kwa kipindi cha miaka miwili (3) ya 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021 Mkoa umekuwa ndio mzalishaji wa kwanza wa mazao ya Chakula Kitaifa.
- Maafisa Ugani **152** kutoka mkoa wa Ruvuma wamepatiwa mbinu bora za kilimo kwenye mazao ya Korosho, Ufuta, Alizeti na Soya
- Majosho mapya **15** yanajengwa katika Halmashauri za Tunduru, Songea DC na Nyasa.

**Sekta ya Utawala**

- Kufanyika kwa vikao mbalimbali vya kisheria
- Kuendelea kulipa stahiki mbalimbali za watumishi
- Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Nyasa, Mbinga Dc na Madaba DC
- Kuanza ujenzi wa nyumba sita (7) za watumishi wa Sekta ya Afya.

**Sekta ya fedha**

- Kutolewa elimu kwa wafanyabiashara juu ya uboreshaji wa matumizi ya POS
- Kutoa elimu ya ulipaji wa Mapato ya Serikali
- Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya MSM na maduhuli ya serikali.

## 8.8 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI WA MWAKA 2021/22.

- Uwepo wa miradi mingi ya miaka ya nyuma (Viporo) isiyokamilika
- Mwamko mdogo wa wananchi katika kuchangia nguvu zao kwenye miradi inayotekeleza kwenye maeneo yao
- Uhaba wa watumishi kwa baadhi ya sekta kama Ujenzi, Afya na Elimu

- Upungufu wa Vyombo vya Usafiri kama magari katika badhi ya Halmashauri na RS

- Mabadiliko ya mara kwa mara kwa bei ya vifaa vya viwandani hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo

## 8.9 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA.

- Kuendelea Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki katika kutekeleza miradi inayojengwa katika maeneo yao

- Kuendelea kuomba vibali na kutenga fedha kwa ajili ya kuajiri watumishi

- Kuhakiki na kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani na kufunga mfumo wa makusanyo wa kieletroniki ili kuziba mianya ya uvujaji wa mapato na kuongeza mapato ya ndani.

- Kuendelea kuzingatia kutenga bajeti kwa miradi ambayo haijatekelezwa kutokana na kutopokelewa kwa fedha za maendeleo

## 8.10 TAARIFA YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Mipango na Uratibu aliwasilisha taarifa ya maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo hadi sasa yamefanyika mafunzo ya maboresho yaliyofanyika kwenye mfumo wa PlanRep kwa Wakuu wa Idara na Vitengo wa Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.Mafunzo yamefanyika kuanzia tarehe 06/12/2021 – 15/12/2021. Aidha, Mkoa umependekeza vipaumbele kwa idara na vitengo Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ambavyo

vitasaidia kuwa mwongozo wa uandaaji na upangaji wa mpango na bajeti kwa matumizi ya kawaida, Maendeleo na kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa kuingiza katika mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Majadiliano;**

Wajumbe wa kikao walipokea na kuipitisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mkoa kwa mwaka 2020/2021 kuishia tarehe 30 Novemba, 2021 pamoja na maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

## 9.0 MUHTASARI NA. RCC: 07/12/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHUMI NA UZALISHAJI (KILIMO, MIFUGO VIWANDA, *BIASHARA, UWEKEZAJI, UVUVI, MALIASILI NA USHIRIKA)*

### 9.1 SEKTA YA KILIMO

Mkoa una jumla ya hekta **4,007,746** ya eneo linalofaa kwa kilimo cha kawaida pamoja na kilimo cha umwagiliaji, eneo hili linastawisha mazao ya aina mbalimbali yakiwemo ya chakula na ya biashara, kwa sasa eneo linalolimwa ni wastani wa hekta **613,946** sawa na asilimia **15.32** ya eneo lote linalofaa kwa Kilimo**.** Hivyo Mkoa una ziada ya eneo la hekta **3, 393,800** sawa na asilimia **84.68.**

**(a) Mazao ya Chakula**

Mazao ya chakula yanayolimwa Mkoani hujumuisha Mahindi, Mpunga, Muhogo na Maharage. Mazao mengine ni Mtama, Ulezi, Mbaazi, Viazi Vitamu na Jamii ya Mikunde.

**(b) Mazao ya Biashara**

Mazao makuu ya biashara yanayolimwa ni Tumbaku, Kahawa na Korosho. Aidha, mazao mengine ya biashara ni Ufuta, Soya Alizeti, Tangawizi, Mbaazi na Karanga. Pamoja na kuwa Mahindi ni zao la chakula pia linatumika kama zao la biashara. Mkakati uliopo ni kupanua wigo wa mazao ya biashara kwa kuhimiza kilimo chenye tija na kuhakikisha kuwa, kila Wilaya inakuwa na zaidi ya zao moja la biashara. Aidha, uendelevu wa usalama wa chakula ndani ya mkoa na nchi kwa ujumla hutegemea kilimo cha mahindi ambapo Mkoa wa Ruvuma ni mzalishaji mkubwa.

### 9.1.1 Utekelezaji wa shughuli za kilimo kwa msimu wa mwaka 2020/2021

### 9.1.2 Mipango na Malengo ya Kilimo Msimu 2020/2021

Katika msimu huu wa kilimo wa mwaka 2020/2021 Mkoa ulilenga kulima hekta **709,782.3** za mazao ya chakula na biashara zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1, 866,638.00.** Kati ya hekta hizo, kilimo cha mazao ya chakula ni hekta **585,623.00** zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1, 590,629.00**na kilimo cha mazao ya biashara ni hekta **116,149.8** zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **84,509.1.**

### 9.1.3 Utekelezaji wa malengo ya kilimo msimu wa 2020/2021

Kufikia mwezi Juni, 2021 Mkoa ulilima hekta **613,946** (sawa na **asilimia 86.5)** ya lengo la kulima hekta **709,782.3** zilizotoa mavuno ya tani **1, 611,510** (sawa na **asilimia 86.3)** ya lengo la mavuno yaliyotarajiwa ya tani **1, 866,638.0** Kati ya hekta hizo za kilimo cha mazao ya chakula yalilimwa hekta **489,848** ambazo zimetoa mavuno ya tani **1, 384,705** na kilimo cha mazao ya biashara hekta zilizolimwa ni **114,376** ambazo zimetoa tani **68,009** za mavuno. Zao la Mahindi zimevunwa tani **816,242** kutoka hekta **276,488.**

### 9.1.4 Hali ya upatikanaji wa mbolea katika Mkoa wa Ruvuma Msimu wa 2020/2021

Katika msimu 2020/2021 jumla ya tani **43,000** za mbolea zimeingia Mkoani kupitia makampuni na mawakala wa mbolea sawa na asilimia **84.5** ya mahitaji ya Mkoa ambayo ni tani **50,910** za mbolea aina zote**.** Kiasi hiki cha mbolea kilitumika katika mashamba ya wakulima kwa ajili ya kuongeza uzalishaji. Aidha kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022 mbolea mbalimbali zimeendelea kuingia kupitia kwa wafanyafanyabiashara, na wakulima wameendelea kununua mbolea moja kwa moja kutoka kwa wafanyabiashara **(Makampuni na Agrodealors)** kwa bei Tofautitofauti

Kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea, zipo changamoto za uzalishaji zinaweza kujitokeza hususani baadhi ya Wakulima kushindwa kumudu gharama za mbolea, hali hii inaweza kupelekea wakulima kulima pasipo kutumia mbolea, jambo ambalo linaweza kupunguza uzalishaji wa mazao hususani mahindi. Hivyo Mkoa unashauri wataalam wa ugani waliopo katika Halmashauri, kata, pamoja na Vijiji kutoa elimu na kuhamasisha wakulima watumie mbolea za asili zilizofanyiwa majaribio na zikaonekana kufanya vizuri katika mazao mbalimbali.

### 9.1.5 Hali ya chakula

Hali ya upatikanaji wa chakula Mkoa wa Ruvuma ni nzuri kwa kiwango cha utoshelevu na ziada kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi na moja (11) mfululizo. Kwa kipindi cha miaka mitatu (**3**) mfululizo, yaani 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021 Mkoa umekuwa ndio wazalishaji wa kwanza wa mazao ya Chakula Kitaifa. Jambo hili linatokana na wakulima wenyewe kujituma, maelekezo ya wataalamu pamoja na usimamizi makini unaofanywa na viongozi wa Ngazi zote. Hivyo basi, katika msimu wa 2020/2021 hali ya upatikanaji wa Chakula ni nzuri ambapo mahitaji ya chakula aina ya wanga (Mahindi, Mpunga, Mihogo, Viazi nk) katika Mkoa wa Ruvuma ni tani **470,000** ikilinganishwa na tani **1, 384,705 za** mazao ya chakula cha wangakilichopatikana katika msimu wa kilimo 2020/2021. Matumizi ya chakula hicho ni katika msimu 2021/2022 na kupelekea kuwa na ziada ya tani **914,705** za mazao mengine ya chakula ambayo yanauzwa na kutumiwa na wahitaji wengine ndani na nje ya Mkoa**.**

### 9.1.6 Kilimo cha umwagiliaji

Mkoa wa Ruvuma unalo eneo linalofaa kwa umwagiliaji lenye hekta **197,108.3** kati ya hizo hekta **7,000** zimejengewa miundombinu na hekta **17,000** hazijajengewa miundombinu. Aidha, Mkoa una skimu **102** kati ya hizo skimu **42** zimeboreshwa skimu **19** zinafanya kazi na **23** hazifanyi kazi.

### 9.1.7 Kilimo cha Pamoja (Block Farming) na Kilimo cha Mkataba (Contract Farming)

Mkoa wa Ruvuma umeweza kuyatambua maeneo yanayofaa kwa kilimo cha pamoja na mkataba kiasi cha ekari **48,343.35** kutoka katika Halmashauri zake nane (**8**). Kwa msimu wa kilimo 2021/2022.

Kwa kuanzia katika kilimo cha pamoja msimu 2021/2022, Mkoa unaendelea kuwaunganisha wakulima na wawekezaji ili kulima mashamba yenye jumla ya ekari **12,204** ambapo kati ya hizo ekari **5,279** zitalimwa ufuta, ekari **3,590** soya na ekari **3,435** alizeti. Makadirio ya mahitaji ya Mbegu bora kwa ajili ya kilimo hicho ni tani **21** za ufuta, tani **72** za soya na tani **14** za alizeti. Wakulima wengine wa mazao hayo wataendelea kununua pembejeo kwenye maduka ya mawakala.

Kilimo hiki kitaongezeka zaidi hadi kufikia lengo kutengemeana na uwepo wa wawekezaji watakaochangamkia fursa kwa kuwapatia wakulima pembejeo na masoko. Kwa sasa zipo taasisi nyingi zinashirikiana na Mkoa katika sekta ya Kilimo kwa kutoa huduma mbalimbali kwa wakulima wa mazao ya soya, alizeti, ufuta na korosho katika Mkoa wetu ambao ni;

**TARI** Naliendele wameahidi kuleta mbegu bora za ufuta na korosho kwa wakulima kupitia vikundi vya ushirika na kutoa elimu ya kilimo bora kwa maafisa ugani wa kata na namna ya kuendesha kilimo cha pamoja.

**Taasisi ya ASA** wamesambaza mbegu bora za alizeti aina ya **STANDARD OPV** kiasi cha tani **52.721** na tayari mbegu hizo zimesambazwa kwa wakulima kuptia Halmashauri za Wilaya.

Mbegu hizi za alizeti zimeuzwa kwa Wakulima kwa gharama ya Tsh. **3,500** kwa kilo moja, mpango huu umepunguza gharama kwa wananchi kwa kiasi kikubwa sana kwani Mkulima kwa ekari moja anagharamia mbegu kwa **Tsh.10,500** tu, ikilinganishwa na gharama ya soko **Tsh. 70,000** kwa ekari moja**.**

Kaisi cha tani **52.721** za mbegu za alizeti zinatarajiawa kupandwa katika jumla ya ekari **17,573.7** sawa na hekta **7,029.5** ambazo zitazalisha jumla ya wastani wa kilo **10,544,220** za alizeti ghafisawa na tani **10,544.22** za alizeti ghafi**, ambazo zitazalisha Mafuta** kiasi cha lita **3,514,740** sawa na tani **3,514.74.**

Aidha, katika juhudi zilezile zilizofanywa na Mkoa na kupata Mbegu bora za alizeti, zimefanyika pia kwa upande wa zao la Soya, hivyo kupitia juhudi hizo Mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo umekubaliana na Kampuni ya Dar – Lyon kuletewa mbegu za Soya, tayari Mkoa umekusanya Mahitaji ya mbegu za Soya kiasi cha tani **100** na kuzituma katika Kampuni ya Dar – Lyon, mbegu hizo zitawasili kufikia tarehe **21 Disemba 2021** na Mbegu zitauzwa kwa wakulima kwa **Tsh. 4,000** kwa kilo.

Lengo la mpango huu ni kuongeza uzalishaji wa soya ili kufikia Mahitaji ya soko la Nchi China ya tani **100,000** kwa mwaka walioingia mkataba na Wizara na Kilimo na nchi ya china.

***NB. Sambamba Na Mkoa kufanya juhudi za kuagiza mbegu za alizeti na soya, pia wapo wadau mbalimbali wameendelea kuingiza na kusambaza mbegu za alizeti na mazao mengine katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wetu wa Ruvuma.***

**Shughuli nyingine zinazohusiana na maendeleo ya kilimo zilizotekelezwa katika Mkoa wa Ruvuma ni; pamoja na;**

- Kuendesha mafunzo ya mbinu bora za kilimo kwa maafisa ugani **152** kati **182** waliopo katika Mkoa wa Ruvuma, mafunzo hayo yaliendeshwa katika vituo vitatu ambavyo ni Tunduru, Songea na Mbinga, Lengo ni kuwajengea uwezo maafisa ugani katika kutekeleza majukumu yao ya kutoa elimu sahihi ya ugani kwa Wakulima juu ya mazao manne ambayo ni **korosho,ufuta,alizeti na soya**. Mafunzo hayo yaliendeshwa na Taasisi ya Utafiti TARI Naliendele kuanzia tarehe **8 – 13 Novemba 2021**.
- Kufanyika kwa kikao kikubwa cha wadau wa kilimo Mkoa wa Ruvuma, kikao hicho kiliendeshwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma **Mhe. Brig. Jen. (Balozi) Wilbert A. Ibuge**, lengo la kikao lilikuwa ni; kujadili mpango wa utekelezaji wa Kilimo cha pamoja (Block Farming), Mpango ambao umeanzishwa na Mkoa na unatekelezwa katika mazao matatu **ufuta, soya na alizeti**.
- Kutokana na kuanzisha mpango wa kilimo cha pamoja Mkoa uliamua kuandaa mwongozo ambao utatoa mwelekeo wa utekelezaji wa mpango huo, mwongozo utakapokamilika Wadau wote watapewa ili kuwa na urahisi wa utekelezaji.

### 9.2 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)

Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa msimu wa mwaka 2021Kanda ilipangiwa kununua tani **41,000** za mahindi na ununuzi ulianza tarehe **15 /08/2021** hadi kufikia **15 Disemba, 2021** kanda imenunua jumla ya tani **38,471** za mahindi zenye thamani ya shilingi **19, 235, 500,000.00**. Zoezi la ununuzi linaendelea

Mpaka sasa kanda katika maghala yake ina jumla ya tani **50,290** za mahindi zenye thamani ya shilingi **25, 145, 000,000.00.** Aidha njia kuu mbili (2) za ununuzi zinazotumika kununua ni vituo vya ununuzi na vikundi vya wakulima (Saccos na Amcos) kwa bei elekezi ya Tshs **500/=** kwenye vituo kikubwa/vikundi vya wakulima na **Tsh**. **500** kwa vituo vidogo. Kupitia ununuzi wa mahindi unaofanywa na kanda imewezesha kupatikana kwa ajira za muda na za kati kwa vijana **300** hadi **600**.

### 9.2.1 Mradi wa Kuhifadhi Chakula Kanda ya Songea

Kanda ya Songea ina Maghala sita (**6)** yenye uwezo wa kuhifadhi tani **29,000** za nafaka. Mradi katika kanda ya Songea unajenga vihenge vya kisasa (silos) **12** vyenye uwezo wa kuhifadhi nafaka tani **45,000** na maghala mawili (**2**) yenye jumla ya tani **10,000** kwa thamani ya Dola za Kimarekani milioni **10.16** ambazo ni sawa na shilingi bilioni **23.37** na ulitarajiwa kukamilika ifikapo Decemba, 2020. Kukamilika kwa mradi huu kutafanya Kanda ya Songea kuwa na uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani **84,000** ndani ya maghala na vihenge kwa wakati mmoja. Pamoja na vihenge hivi vya kisasa, mradi pia unajenga miundombinu wezeshi kama stoo ya vifaa, stoo ya viuatitifu, ujenzi wa ofisi, ujenzi wa maabara, ujenzi wa vyoo, kantini, uzio na barabara za ndani.

### 9.2.2 Maendeleo ya Utekelezaji wa Mradi Kanda ya Songea

Mradi katika kanda ya Songea unajengwa na mkandarasi M/S Feerum S.A kutoka nchini Poland kwa kushirikiana na kampuni ya kitanzania Civil Loth. Aidha msimamizi wa mradi (Meneja Mradi) ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Aidha, utekelezaji wa mradi umefika asilimia **71.75** ambapo ujenzi na usimikaji wa vihenge umefikia wastani wa asilimia **86**, ujenzi wa maghala na miundombinu mingine umefikia asilimia **38**. Aidha hadi kufikia Disemba 2021, Mkandarasi amelipwa Dola za Kimarekani milioni **7.0**, ambazo ni sawa na asilimia **68.8** ya malipo yote kwa kanda ya Songea.

## 9.3 SEKTA YA USHIRIKA

### 9.3.1 Hali ya Ushirika katika Mkoa wa Ruvuma

Mkoa una jumla ya Vyama vya Ushirika **305**, kati ya hivyo AMCOS **213**, Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) **83**, Vyama vingine **6** na Vyama Vikuu (UNION) **3** ambavyo ni TAMCU Ltd, SONAMCU Ltd, na MBIFACU Ltd.

Aidha mchanganuo wa Vyama vya Msingi (AMCOS) kwa ajili ya Kahawa ni vyama **105**, Korosho **44**, Tumbaku **41**, na mazao mchanganyiko **23**. Katika mwaka 2015 Mkoa ulikuwa na Vyama vya Ushirika **237** hadi kufikia mwaka 2021 Mkoa una vyama vya ushirika **305** na hivyo Mkoa umekuwa na ongezeko la Vyama vya Ushirika **68**. Vyama vya msingi vya zao la Kahawa na Korosho vinahudumia wakulima wa mazao ya Kahawa, Korosho na mazao ya nafaka katika maeneo yao kwa kufuata Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Vyama vya Msingi vya Zao la Tumbaku vinahudumia wakulima wanaolima mazao ya nafaka yanayouzwa kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

### 9.3.2 Mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi za Mazao pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Bodi *ya* Usimamizi wa Stakabadhi za ghala na wadau wa mazao ya ufuta, Soya, Mbaazi, korosho, kahawa unaratibu masoko ya mazao ya kipaumbele kwa njia ya minada inayosimamiwa na Vyama Vikuu Vya Ushirika (SONAMCU LTD, TAMCU LTD na MBIFACU LTD).

### 9.3.3 Uendeshaji wa Masoko (Mazao ya Ufuta, Soya na Mbaazi)

Uendeshaji wa masoko ya mazao ya Ufuta Mbaazi na Soya hufanyika kupitia wakulima kukusanya mazao kupitia Vyama vya Msingi **88** na Vyama Vikuu **2** kati ya hivyo Namtumbo vyama **44**, Songea **6**, Mbinga **2**, Nyasa **1** na Tunduru **35**.

**9.3.3.1 Zao la Ufuta**

Kwa msimu 2020/2021 jumla ya minada 29 ya ufuta ilifanyika ambapo jumla ya **kilo 8,326,686** za Ufuta ziliuzwa ambapo bei ya juu likuwa **sh.2,393** na bei ya chini **sh.1,998** na kuwapatia wakulima jumla ya **sh.17,221,852,087.**

Aidha; kwa vipindi vya misimu mitatu ya kilimo kutoka msimu wa kilimo **2018/2019** hadi kufikia Msimu **2020/2021** (tarehe **29 Julai 2021**) Mkoa wa Ruvuma ulikusanya Ufuta jumla ya kilo **28,989,711** na kuuza kwa wastani wa bei **sh.2,393** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha **sh.69,358,403.** Kabla ya mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuanza kutumika, zao la Ufuta liliuzwa kwa utaratibu wa soko huria kwa bei ya chini kati ya sh. **500 hadi sh.700** kwa kilo.

**9.3.3.2 Zao la Soya**

Kwa msimu **2020/2021** jumla ya **minada 10** ya zao la Soya ilifanyika ambayo ilianza tarehe **01/06/2021** hadi tarehe **26/07/202**1. Katika minada hiyo jumla ya **kilo 1,090,199** za Soya ziliuzwa ambapo bei ya juu ilikuwa **sh. 1,562 na bei ya chini sh.1,353** na kuwapatia wakulima jumla ya sh. **1,547,202,688.00**.

Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo mitatu mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2018/2019** hadi kufikia tarehe **29 Julai 2021** jumla ya kilo **4,963,088** za Soya zilikusanywa na kuuzwakwa wastani wa bei **sh.3,375** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha sh.**5,234,096,169.00**. Kabla ya mfumo wa Stakabadhi za ghala kuanza kutumika, zao la Soya liliuzwa kwa soko utaratibu wa soko huria kwa bei ya chini kati ya sh**. 500-600 kwa kilo**.

**9.3.3.3 Zao la Mbaazi**

Kwa msimu **2020/2021** jumla ya **minada 12** ya zao la Mbaazi ilifanyika ambayo ilianza tarehe **11/08/2021** hadi tarehe **23/09/202**1. Katika minada hiyo jumla ya **kilo**

**7,109,360.00** za Mbaazi ziliuzwa ambapo bei ya juu likuwa **sh. 1,428 na bei ya chini sh.990** na kuwapatia wakulima jumla ya **sh. 9,313,114,073**

Aidha, Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo mitatu mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2018/2019** hadi kufikia tarehe **16 Oktoba 2021** jumla ya kilo **12,165,680**za Mbaazi zilikusanywa na kuuzwakwa watani wa bei **sh. 993** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha sh.**12,080,537,241.** Kabla ya mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuanza kutumika, zao la Mbaazi liliuzwa kwa bei kati ya **sh.150 Hadi 200** kwa kilo.

### 9.3.4 Uendeshaji wa Masoko (Mazao ya Korosho na Kahawa)

#### 9.3.4.1 Zao la Kahawa

Hadi kufikia tarehe **10/12/2021** wakulima wa kahawa Mkoa wa Ruvuma wameuza kahawa kilo **12,122,126.25** (katika minada ya Mbinga, Mbozi na Moshi) na kupata shilingi **85,272,436,956.63** bei ya juu ikiwa ni Sh.**8, 301.42** na bei ya chini ikiwa **6,351.59**. Masoko ya kahawa bado yanaendelea.

Aidha, Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo minne mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2017/2018** hadi kufikia msimu **2020/2021** jumla ya kilo **63,908,344**za kahawa zilikusanywa na kuuzwakwa watani wa bei **sh. 4,000** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha **sh. 255,550,614,600**.

#### 9.3.4.2 Zao la Korosho

Kwa msimu wa**2020/2021** Mkoa ulikusanya jumla ya kilo **15,410,605** za Korosho zenye thamani ya shilingi bil.**35, 012,894,560**ambazoziliuzwa kwa wastani wa bei **sh. 2,273** kwa kilo.

Aidha, Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo minne mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2017/2018** hadi kufikia msimu **2020/2021** jumla ya kilo **79,535,246** za

Korosho zilikusanywa na kuuzwakwa wastani wa bei **sh.3,035** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha **sh.241, 384,627,192.**

Aidha, Msimu wa mauzo ya korosho kitaifa kwa mwaka 2021/2022 umefunguliwa rasmi tarehe 1 Oktoba, 2021 katika mkutano mkuu wa wadau wa korosho nchini uliofanyika katika ukumbi wa Mikutano Benki Kuu Mtwara. Mkoa wa Ruvuma nao umekwishafanya mkutano wa wadau ambao ulifanyika tarehe 4 Oktoba 2021 Wilayani Tunduru. Makadirio ya uzalishaji ni tani **25,000.** Hatahivyo tayari mnada wa kwanza kwa msimu wa mwaka 2021/2022 umefanyika tarehe 28 Oktoba, 2021 katika Wilaya ya Tunduru ambapo jumla ya kilo **Milioni 1.7** kwa bei ya Tshs.**2, 150** kwa kilo. Hadi kufikia tarehe 9/12/2021 jumla ya kilo zilizokusanywa ni**17, 675,278.00** zenye thamani ya Tsh. **36,674,758,934.00.**

#### 9.3.4.3 Usimamizi wa Uanzishaji wa kiwanda cha vifungashio

Chama kikuu cha Ushirika SONAMCU Ltd kimeanza ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mifuko au magunia yatakayotumika kufungashia mazao ya kilimo. Mpango huu umeanza utekelezaji wake katika robo ya Julai-Disemba 2019. Mpaka sasa majengo mawili yameezekwa na Maghala mawili (2) yapo hatua ya kuezekwa. Aidha, mchakato wa kupata Mashine za kiwanda unaendelea kwa hatua ya kutoa zabuni.

Mradi huu unatarajia kuongeza ajira na kupunguza/kuondoa gharama kubwa ya uagizaji na usafirishaji wa vifungashio katika kipindi cha masoko ya mazao ya wakulima ikiwa pamoja na kuongeza mradi wa kuongeza mapato ya chama kwa njia ya kuuza vifungashio.

#### 9.3.4.4 Uendelezaji wa Miradi ya Kiuchumi ya Vyama vya Ushirika

Serikali kupita vyama vya Ushirika imetekeleza na inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi ambapo jumla ya fedha kiasi cha Tsh **1,128,141,200** zinatekeleza miradi ifuatayo:

- Ujenzi wa kiwanda cha vifungashio cha chama kikuu SONAMCU Ltd wilayani Namtumbo;
- Ukarabati wa ghala la chama kikuu cha TAMCU Ltd;
- Ukarabati wa maghala 5 kati ya 7 ya chama kikuu cha MBIFACU Ltd;
- Ukarabati wa MBICU Hotel;
- Ununuzi wa magari 3 ya mizigo kwa ajili ya usafirishaji wa mazao ya kilimo ya wakulima kwa vyama vya Msingi Mruji, Mtiti na Sama vilivyopo Wilaya ya Tunduru;
- Usimamizi wa uendelezaji wa Mradi wa kiuchumi wa shamba la kahawa la chama kikuu cha MBIFACU Ltd;
- Ujenzi wa Mradi wa shule ya Sekondari ya Mahenge AMCOS Ltd; na
- Ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao ya wakulima la chama cha Msingi Kimuli (AMCOS).

## 9.4 SEKTA YA MIFUGO

Sekta ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kuleta mabadiliko makubwa na ya kisayansi

katika ufugaji kwa kufuata kanuni za ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na kutumia uhamilishaji (Artificial Insemination) na matumizi ya madume bora kufanya sensa ya wafugaji na mifugo iliyopo katika kila kijiji ili kujua takwimu halisi za mifugo na kuweza kupanga mikakati ya kuimarisha sekta hii.

### 9.4.1 Utekelezaji wa utoaji wa huduma za ugani

**Hali ya Mifugo katika Mkoa**

Takwimu za mifugo kwa kipindi cha mwaka 2020-2021 Mifugo imeongezeka kufikia **3, 318,854 ambapo** kati ya hiyo ng'ombe wa asili ni **199,154**; chotara ni **35,974;** Mbuzi wa asili ni **292,844;** chotara ni**517;** Kondoo**33,859**, Nguruwe **232,710;** Kuku wa asili ni

**2,358,045**; kisasa **72,929;** Bata **37,991;** Punda **1,013; paka ni 10,855 na mbwa ni 42,963** na mifugo mingine midogo midogo kama sungura wapatao **43,109**. Ongezeko la mifugo limepelekea mazao yatokanayo na mifugo kuongezeka kufikia tani**3, 425.76** za nyama ya ng'ombe mbuzi na kondoo, tani **1,615.8** za nyama ya nguruwe tani **2010.79**na tani **1,440** za nyama ya kuku. Uzalishaji wa maziwa umefikia lita **4,316,880** wakati uzalishaji wa mayai umefikia mayai **26, 522,221,** vipande vya ngozi za ng'ombe zilizozalishwa ni **16,560,** vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo ni **30,276.**

**9.4.2 Uendelezaji wa Nyanda za malisho kwa mfumo wa ranchi ndogo na udhibiti wa migogoro baina ya wakulima na wafugaji**

Wafugaji **125** wenye ng'ombe **38,000** kati ya wafugaji **145** walioingia kiholela Wilayani Tunduru wakiwa na ng'ombe **62,000**, wamepangwa kwenye vitalu **191** sawa na **asilimia 83** ya lengo la kuwapanga wafugaji.

Katika kutekeleza zoezi hili kwa Wilaya ya Tunduru ilitenga maeneo katika Vijiji kumi na tano (15) vya Mkowela, Liwangula, Tinginya, Tanga, Ngapa, Muhuwesi, Msagula, Majala, Twendembele, Kajima, Ngapa, Kindamba, Nangunguru, Chingulungulu na Misechela vyenye hekta **57,900** sawa na vitalu **286** vyenye ukubwa wa hekta **200** kila kimoja vilipimwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru;

Wafugaji **121** walipangwa kwenye vitalu **191** vyenye ukubwa wa hekta **39,000** kwa mfumo wa Ranchi ndogo.

Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Jumla ya hekta **38,542** zimetengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo katika vijiji vya Mhepai, Magwamila, Nambendo, Lilahi, Liweta, Kikunja na Litowa. Kwa mwaka wa fedha wa **2019/2020** Vijiji 4 vya Liweta, Kikunja, na Litowa vimefanyiwa matumizi bora ya ardhi kupitia mradi wa **FORVAC**.

Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa Jumla ya eneo lilotengwa kwa ajili ya malisho ni hekari **2,420.42** kwa vijiji **14** vilivyofanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi tukishirikiana na miradi ya wahisani. Maeneo hayo bado ya na malisho ya asili. Halmashauri ya Wilaya ya Madaba maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Mifugo ni hekta **28,500.**

### 9.4.3 Uendelezaji wa Mashamba ya Serikali:

Kumekuwepo na ongezeko la mifugo inayochungwa holela katika maeneo ya Mkoa yakiwemo mashamba ya wakulima na katika hifadhi za Taifa na misitu ya kijamii. Hali hiyo imejitokeza zaidi katika Wilaya ya Namtumbo na Tunduru. Hii imesababisha wakulima kuamua kulinda mazao yao ili yasiharibiwe au kuliwa na mifugo na hivyo hatua hiyo inayochukuliwa na wakulima imekuwa ikileta kutoelewana baina ya wakulima na wafugaji na wakati mwingine kusababisha matukio ya kuchukua sheria mkononi na kupelekea kujeruhiana. Aidha, kwa mifugo iliyoko kwenye hifadhi imekuwa ikisababisha tembo kukimbia kwenye hifadhi na kwenda kwenye makazi ya watu na hivyo kusababisha uharibifu wa mali za wananchi na wakati mwingine maafa yamekuwa yakitokea.

Mkoa umechukua hatua za kukutana na viongozi wa wafugaji kwa ajili ya kutatua changamoto hii, ambapo moja ya maelekezo kwa wafugaji kupitia viongozi ni kuwataka wafugaji kukaa katika maeneo waliyopangiwa na kuwa na mifugo kuendana na eneo walilo nalo. Pia kuzielekeza Halmashauri zenye wafugaji kutatua changamoto ya ukosefu wa miundombinu kwenye maeneo yaliyotengwa kwa kushirikiana na wafugaji. Mkoa umewataka wafugaji wenye vitalu kurejea kwenye maeneo yao waliyopangiwa na wasio na hualali kuondoka kwenye maeneo yasiyostahili kwa ufugaji. Pia viongozi wa Wilaya na Halmashauri kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ili kuhakikisha shughuli zote za kiuchumi zinafanyika kwenye maeneo husika.

### 9.4.4 Miundombinu ya Masoko na Biashara ya Mifugo

### 9.4.4.1 Uongezaji Thamani Zao la Maziwa

Taarifa iliwasilishwa kuwa katika jitihada za kuimarisha mnyororo wa thamani wa maziwa, Mkoa umefanya uchunguzi wa magonjwa ya kifua Kikuu (TB) na ugonjwa wa kutupa mimba (brucelosis) kwa ng'ombe wa maziwa **1,546** kwenye Halmashauri za Wilaya ya Namtumbo, Songea na Manispaa ya Songea.

### 9.4.4.2 Minada ya Mifugo na Zao la Nyama

Katika kuboresha minada ya mifugo na uongezaji thamani zao la nyama na kurahisisha biashara ya mifugo Mkoani, Mnada wa upili unaendeshwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba katika Kijiji cha Mtyangimbole (Madaba) na minada ya awali katika kijiji cha Muhuwesi (Tunduru) na Mhepai (Songea), Ligera na Lismonji (Namtumbo). Mkoa una viwanda viwili vya nyama Peramiho Misheni na Chipole kinachozalisha wastani wa Tani **200** za nyama kwa mwaka.

### 9.4.4.3 Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo

Katika kudhibiti magonjwa ya mifugo yaenezwayo na kupe Mkoa umeboresha na kujenga miundombinu mbalimbali ya udhibiti wa magonjwa ikiwemo ukarabati wa Majosho**11** katika Halmashauri za Tunduru, Nyasa, Songea Namtumbo na Mbinga Mji. Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa unategemea kujenga majosho mapya **15** katika Halmashauri za Tunduru **9**, Songea DC **5** na Nyasa **1** yenye thamani ya Tshs **244,000,000.00** fedha kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Aidha, katika kukabiliana na magonjwa ya mifugo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetoa dawa ya kuogeshea ya ruzuku kiasi cha Lita **312** ambazo zimegawiwa kwa kila Halmashauri kulingana na idadi ya majosho yanayofanya kazi. Pia, Katika kudhibiti magonjwa ya milipuko yaenezwayo kutoka kwa binadamu na wanyama Wizara ya Afya

na Wizara ya Mifugo kwa kushirikiana na OR-TAMISMI wametoa mafunzo kwa Wataalam wa mifugo wa Halmashauri katika kukabiliana na Milipuko ya magonjwa pindi yanapotokea.

### 9.4.4.4 Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo.

Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo Tanzania unasimamiwa kwa Sheria ya **Usajili, Utambuzi na UfuatiliajiMifugo Na.12** ya **Mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2011** na Kwa Mkoa wetu wa Ruvuma Halmashauri ziko kwenye hatua tofauti ya maandalizi ya kutekeleza zoezi hili. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Mkoa wametoa elimu ya kwa Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Idara za Mifugo na Uvuvi, Maafisa Tehama na Maafisa Utambuzi wa Halmashauri. Faida ya zozi hili la utambuzi ni; Kusaidia Kudhibiti wizi wa mifugo, Kuthibitisha umiliki wa mifugo hiyo, Fursa ya kibiashara kimataifa kwa kukidhi viwango, ushindani, na matakwa ya soko la kimataifa, Uhakika wa usalama wa chakula kwa kuifahamu idadi ya mifugo na jinsi ya kuvuna mifugo hiyo na mazao yake, pia itasaidia Kuepusha migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

### 9.4.4.5 Changamoto za Sekta ya Mifugo

i. Ukosefu wa miundombinu ya udhibiti wa magonjwa, soko la mifugo mfano majosho na barabara kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo kwa mfumo wa Ranchi ndogo, ukosefu wa maji na malisho kipindi cha kiangazi katika maneo ya malisho kinachopelekea wafugaji kuhama kipindi cha kiangazi.

ii. Ukosefu wa rasilimali fedha za kusimamia, kuratibu na kuendesha zoezi la utengaji na upimaji wa maeneo ya ranchi ndogo.

iii. Maeneo yaliyotengwa kutotosheleza kutokana na idadi kubwa ya mifugo iliyopo

iv. Uchache wa watumishi wa sekta ya Mifugo

#### 9.4.4.6 Mikakati ya kuboresha Sekta ya Mifugo

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mkoa umepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuzielekeza Halmashauri za Wilaya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mifugo;

ii. Kuzielekeza Halmashauri za Wilaya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya mpango wa matumizi bora ya ardhi na upimaji maeneo ya kuchungia

iii. Kuhamasisha utengaji wa maeneo ya Malisho na kujenga miundombinu rafiki ili kuondoa migogoro vaina ya Wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhí.

### 9.5 SEKTA YA UVUVI

Katika sekta ya uvuvi, Mkoa unategemea ziwa Nyasa, mito na mabwawa ya kufugia samaki. Hata hivyo tija itokanayo na vyanzo hivyo vya samaki haitoshelezi mahitaji ya Mkoa ambayo ni zaidi ya tani **18,000** kwa mwaka, hivyo tunapata samaki kutoka nje ya Mkoa wastani wa Tani **55** kwa mwezi, na uzalishaji wa samaki wa kufuga ni wastani wa tani **121.2** kwa mwaka. Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka **2019** hadi **2021** jumla ya wavuvi **7,620** walisajiliwa. Uzalishaji wa samaki katika Ziwa Nyasa ni wastani wa tani **8,411.4** kwa mwaka zenye thamani ya **Tshs. 5, 368, 387,187.00**.

#### 9.5.1 Uzalishaji wa Samaki Kwenye Mabwawa

Mkoa una wafugaji wa samaki **4,159** wenye jumla ya mabwawa **6,582 y**enye wastani wa uzalishaji wa tani **847.9** kwa mwaka. wananchi wanaendelea kuhamasishwa kufuga

samaki kwa tija katika mabwawa ili kuweza kukidhi mahitaji hayo kwa ajili ya chakula na kwa biashara pia. Ndani ya Mkoa kuna kituo kimoja**(1)** cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki cha Ruhila (**RADC)** kilichopo Manispaa ya Songea.

### 9.5.2 Fursa Katika Ufugaji wa Samaki

- Mwamko wa wananchi  wa Mkoa kuhamasika na ufugaji wa samaki;
- Uwepo wa vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo,mito, chemchem na mabwawa ya Asili/Malambo zaidi ya kumi na nne (**14**) katika Mkoa  yenye fursa ya ufugaji kwa kupandikiza au kufuga kwa njia ya vizimba(Cage culture);
- Uwepo wa ziwa Nyasa linalotoa fursa ya ufugaji kwa njia ya vizimba (cage culture);
- Uwepo wa mahitaji makubwa ya samaki katika Mkoa;
- Uwepo wa wafugaji wa samaki zaidi ya **4,159** na mabwawa ya samaki zaidi ya **6,582; na**

### 9.5.3 Matumizi ya zana Bora za Uvuvi.

Katika matumizi ya zana bora za uvuvi, jitihada zimewekwa ili kujenga uwezo wa wananchi kutambua madhara yatokanayo na matumizi ya zana haramu za uvuvi , utoaji wa elimu juu ya matumizi bora ya zana za kisasa za uvuvi zinazokubalika kisheria, kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kuhamasisha ufugaji bora wa kisasa na wenye tija.

### 9.5.4 Mikakati ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi.

- Kuhimiza matumizi ya zana bora za uvuvi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ambapo hadi kufikia juni 2021 zaidi ya wavuvi **5,316,**  wafugaji **4,159** na wadau

**242** wamefundishwa kuhusu njia bora za ufugaji wa samaki na utunzaji wa mazingira;

- Kuendeleza/kuboresha ujenzi wa miundombinu ya uvuvi hasa mialo(Land stations);
- Kutoa elimu endelevu ya uanzishaji wa vikundi vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi(**BMUs**) katika maeneo yote ya uvuvi;
- Kuhimiza uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba (*cage*) katika ziwa na mabwawa ya asili ili kupata mavuno mengi ya samaki yatakayofaa kwa ajili ya viwanda;
- Kukijengea uwezo kituo cha maendeleo ya ufugaji samaki Ruhila ili kiweze kuzalisha vifaranga bora na vya kutosha.
- Kila Halmashauri kuwa na kituo cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki ambapo vituo hivyo vitatumika pia kama mashamba darasa; na
- Kuendeleza doria za mara kwa mara ili kuzuia utumiaji na uingizaji wa zana haramu za uvuvi katika ziwa na mito pamoja na kuvikagua vyombo vyote na kuvisajili kisheria.

### 9.5.5 Usajili wa Wadau wa Uvuvi

Katika kipindi cha kuanzia Juni 2020 hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 wavuvi **4,435** walisajiliwa na leseni **1,289** za uvuvi zilitolewa.

### 9.5.6 Changamoto

- Uvuvi wa kutumia miti yenye sumu (Mtupa)
- Ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya kufanya doria za mara kwa mara;
- Uhaba wa watumishi wa kada ya uvuvi katika Mkoa wa Ruvuma

- Kusuasua kwa uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki katika Halmashauri za wilaya.
- Uchache wa vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali zaUvuvi (BMUs), mpaka sasa kuna BMU **1** tu kati ya **24** zinazohitajika;
- Ushiriki mdogo wa ulinzi shirikishi wa rasilimali za Uvuvi kwa wadau mbalimbali;
- Katika kipindi cha mwaka 2020/21,zana haramu za Uvuvi aina ya timba (***monofilament****)* pamoja na makokolo zenye urefu wa zaidi ya mita **7,000** na thamani ya zaidi ya shilingi **30,000,000/=**zilikamatwa na kikosi cha kulinda rasilimali za Uvuvi (**FRP)** Nyasa; na
- Uhaba wawataalamu wa sekta ya Uvuvi unadhoofisha shughuli za doria.

### 9.5.7 Mapendekezo ya Kutatua Changamoto

i. Halmashauri za Wilaya ziendelee kuomba kuajiri watumishi wapya hususani Halmashauri ya Nyasa ambayo inamahitaji makubwa ya watumishi wa kada ya uvuvi;

ii. Kuwahusisha wadau wote katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi hasa jamii ya wavuvi wenyewe ili rasilimali za uvuvi ziwe endelevu kwa kizazi kijacho;

iii. Halmashauri za wilaya zifanye doria za mara kwa mara katika mito ili kukomesha uvuvi haramu wa kutumia miti ya sumu;

iv. Kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki katika kila Halmashauri ya wilaya ili kukidhi mahitaji ya wafugaji; na

**v.** Kuhamasisha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki(floating pellets) ili kiweze kusaidia wadau wenye lengo la ufugaji wa samaki kwenye vizimba.

## 9.6 SEKTA YA VIWANDA, UWEKEZAJI NA BIASHARA

### 9.6.1 Hali ya Uwekezaji na Biashara

Mkoa wa Ruvuma umeendelea kutekeleza mkakati wa Taifa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kuwaonyesha wananchi fursa ili waweze kushiriki kikamilifu, kuhamasisha na kuratibu maboresho ya Sera, Sheria na Kanuni za Kisekta; kujenga uwezo wa wadau; na kutengeneza miongozo ya utekelezaji kupitia vikao mbalimbali vya majadiliano kama Baraza la Biashara.

### 9.6.2 Fursa za Uwekezaji

Katika Mkoa wa Ruvuma zipo fursa za uwekezaji katika Sekta za Kilimo, Biashara, Ufugaji, Misitu, Madini, Utalii, Mawasiliano, Umeme wa Maporomoko ya Maji, Uvuvi, Viwanda, Uendelezaji wa Makazi, Usafiri na Usafirishaji.

### 9.6.3 Maeneo ya Uwekezaji katika Mkoa wa Ruvuma ni kama ifuatavyo;

i. Ujenzi wa viwanda - vikubwa, vya kati na vidogo

ii. Usambazaji na uuzaji wa bidhaa za viwandani.

iii. Usindikaji wa mazao ya chakula hasa mazao ya Tangawizi, mazao ya mafuta, mbogamboga na matunda.

iv. Kilimo cha Umwagiliaji hasa uzalishaji wa zao la mpunga.

v. Kilimo cha mazao ya chakula, Mazao ya biashara,

vi. Uzalishaji wa mazao ya misitu - mbao na asali

vii. Ufugaji wa mifugo - ng’ombe, mbuzi, na wanyama wadogo

viii. Usindikaji wa bidhaa za mifugo - maziwa, nyama, ..nk

ix. Uvuvi - ufugajina usindikaji wa bidhaa za samaki.

x. Madini - Uchakataji wa madini

xi. Utalii - hifadhi ya wanyama, maeneo ya asili na uendeshaji wa hoteli.

xii. Umeme na maji

xiii. Ujenzi wa nyumba na makazi.

xiv. Usafiri na usafirishaji

xv. Kujenga maduka makubwa (shopping malls)

### 9.6.4 Miradi ya maendeleo ya kimkakati katika mkoa wa Ruvuma inayosaidia kuchagiza sekta ya biashara

Ili kuendelea kuleta maendeleo na kuboresha maisha ya wananchi Mkoa umekuwa ukitekeleza shughuli zifuatazo: -

**Biashara**

Mkoa umeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwa pamoja na TBS, Wakala wa Vipimo, BRELA, TIC, TRA na TAASISI ZA FEDHA katika kuwapatia huduma wafanyabiashara.

**Bandari ya Mbamba Bay na Ndumbi**

Serikali imenunua meli 3 zinazofanya kazi katika Ziwa Nyasa, kati ya hizo meli 2 ni za mizigo na meli 1 ni ya abiria na mizigo. Meli hizi zitainua uchumi wa wananchi wanaoishi kandokando ya Ziwa Nyasa.

**Usafiri wa Anga (Ndege)**

Serikali kupitia shirika la Ndege la Taifa (ATCL) imeanzisha safari za Ndege mpya Mara tatu (**3**) kwa wiki kati ya Songea na Mikoa mingine ya jirani. Kuimarika kwa safari za ndege kunafungua fursa za biashara na utalii na hivyo kuinua uchumi wa Mkoa wetu.

### 9.6.5 Mkakati wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji

Katika kutekeleza Mkakati wa kuboresha Mazingira ya Biashara na uwekezaji, Serikali inafanya yafuatayo;

a) Kuendelea kutenga na kupima maeneo maalum ya viwanda;

b) Kutangaza fursa na vivutio vilivyopo kwenye Halmashauri;

c) Uanzishwaji na Uimarishaji wa Mabaraza ya Biashara ya Wilaya na Mkoa;

d) Uanzishwaji wa kongano;

e) Kusimamia ipasavyo na kuziendeleza shughuli za kijasiriamali;

f) Ili kuongeza mitaji kupitia Halmashauri kuchangiakikamilifu asilimia kumi (10%) kwa ajili ya vikundi vya kijasiriamali vya vijana na wanawake pia na kuendeleza makundi maalum;

g) Kuendelea kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji;

h) Kila Halmashauri kuingia mkataba na Kampuni ya GS1 Tanzania.

### 9.6.6 Wajasiriamali Wadogo

Mkoa umeainisha maeneo ambayo wafanyabiashara wadogo watafanyia shughuli zao na tayari umeunda uongozi wa Machinga kwenye ngazi za Halmashauri na uongozi wa machinga ngazi ya Mkoa kwa lengo la kurahisisha njia ya majadiliano kati ya Serikali na kundi la Wajasiriamali wadogo ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoyatoa tarehe 15 Oktoba, 2021.

## 9.7 SEKTA YA MALIASILI NA UTALII

### 9.7.1 Misitu

Mkoa wa Ruvuma una lengo la Kupanda miti ya biashara eka 100,000 kwa muda wa miaka kumi (10) toka 2015 – 2025. Mradi huu unatekeleza kwa kupanda miti maeneo ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Vyuo, Mashule na Vijiji.Aina ya miti inayopandwa ni ile ambayo inafaa kwa ajili ya malighafi za viwanda vya mazao ya misitu ambayo ni Misindano (**Pine**), Milingoti (**Eucalyptus**) na Misaji (**Teak**).

Mkoa una lengo la Kuanzisha mashamba mapya mawili Teak Wilaya ya Tunduru na Nyasa pembezoni mwa miteremko ya safu za Liuli kwa kushirikiana na TFS. Kwa msimu unaokuja Mkoa kwa kushirikiana na TFS pamoja na FORVAC wameandaa miche ya miti ya biashara aina ya Teak, Pine na Eucalyptus ipatayo 4,000,000

### 9.7.2 Wanyamapori

Mkoa umeridhia kupandisha hadi Hifadhi mbili za misitu na mapori ya akiba (**Game Reserve**), mapori hayo ni Gesimasowa (764 $km^2$) na Litumbandyosi (494 $km^2$) ambayo ni Sehemu ekologia ya Selous Niassa. Lakini mpaka sasa bado hayajapta Tangazo la Serikali la kuwa na mapori ya akiba rasmi.

Mkoa una mpango wa kuanzisha mashamba ya Wanyamapori (**Wildlife Farms**) kwenye Jumuiya zote tano Kisiwa cha Lundo pamoja na Chuo cha Maliasili, Likuyusekamaganga ili wananchi wajifiunze toka hapo na Kuanzisha mashamba binafsi.

Mkoa unakabiliwa na changamoto kubwa ya Wanyamapori waharibifu hasa Tembo. Aidha kwa kipindi cha Miaka mitano iliyopita matukio ya Wanyamapori Waharibifu na wakali imekuwa ikiongezeka hivyo kupelekea ongezeko la fedha za kifuta jasho na kifuta machozi zinazolipwa kwa jamii athirika. Kwa mwaka 2019/2020 jumla ya wananchi 1**625** walioathirika na wanyamapori wakali na waharibifu dhidi ya mali na maisha ya binadamu. Aidha jumla ya ekari **2879.33** ziliharibiwa, wananchi wawili (**2**)

wamejeruhiwa na wananchi wane (4) wameuwawa. Kwa mwaka 2020/2021 jumla ya watu **435** wameathirika na wanyamapori na jumla ya ekari **2562.83** zimeharibiwa, watu waliowawa ni **7** na majeruhi ni **6**.

Malipo ya fedha ya kifuta jasho na kifuta machozi yamefanyika kwa Wilaya ya Tunduru ambapo takribani **Tsh. 270,650,000** zimelipwa kwa waathirika wa mwaka 2020/2021 na mwaka 2019/2020.Aidha, Pamoja na jitihada tunazokabiliana nazo katika kupambana na wanyamapori waharibifu kwa mali na maisha ya binadamu kwa kushirikiana na TANAPA na kikosi dhidi ya ujangili (KDU) tunapendekeza yafuatayo yafanyike ili wanyamapori tembo waweze kurejeshwa kwenye makazi yao

I. Wizara/TAWA/TANAPA kwa kushirikiana na halmashauri kuanzisha vituo vya askari vya kudumu vya kudhibiti wanyamapori waharibifu kwenye maeneo korofi, Wizara/TAWA/TANAPA kuziwezesha Halmashauri vitendea kazi (mahema, gari na mafuta, Silaha, Risasi na vilipuzi) kwa ajili ya kupambana na wanyamapori waharibifu hususani tembo

II. Wizara kutenga bajeti/fedha kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori kwenye Wilaya zenye changamoto.

III. Wizara kutumia ndege (drone, helcopter) kuwaondoa Tembo katika maeneo jirani na makazi ikiwemo hifadhi ya msitu wa Mlima Kipiki

IV. Kifuta jasho na kifuta machozi kilipwe kwa wakati ili kuondoa kelele kwa wananchi waliodhuriwa na wanyamapori.

### 9.7.3 Utalii

Mkoa wa Ruvuma una fursa za utalii wa kitamaduni na ikolojia. Baadhi ya fursa hizo ni kama mapori ya akiba ya wanyamapori ya `Selous` na Mwambezi, samaki wa

mapambo, fukwe za Ziwa Nyasa na maporomoko ya mto Ruvuma. Kwa upande wa utalii wa kitamaduni kuna majengo ya kihistoria, majumba ya kihistoria (Makanisa ya Peramiho, Lituhi na Lundu), Makumbusho ya vita vya Majimaji, Historia ya machifu wa Kiyao,Historia ya biashara ya utumwa, Historia ya wapigania uhuru Afrika, Jiwe kubwa la Mbuji, mapango ya wamatengo na pango la mlima Chandamali lililokuwa maficho ya Nduna Songea Mbano wakati wa Vita ya Majimaji.

Mkoa kwa kushirikiana na WWF tumeandaa mpango wa kukuza utalii wa Mkoa, kutengeneza filamu fupi ya matangazo, vipeperushi na jarida la kuonesha vivutio vya Mkoa.

**9.7.4 Utunzaji wa mazingira na Vyanzo vya maji.**

Mkoa baada ya kubaini kuwa kuna vyanzo vya maji vinaharibiwa na shughuli mbalimbali za wananchi kwa sasa mpango ulioko kwa sasa ni kuhakikisha kuwa vyanzo vyote vya maji vunkabidhiwa kwa Wakala wa Misitu TFS ili viweze kupimwa ,kuwekewa mipaka, kupanda miti rafiki kwa vyanzo vya maji na kuwa "***gazzeted"*** kwenye gazeti la Serikali. Hatua hii itasaidia kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji na kuvifanya kuwa endelevu.

**9.7.5 Taarifa ya Shamba la Miti Wino**

Hifadhi ya msitu wa Wino ni miongoni mwa mashamba 25 ya miti ya kupandwa yanayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Hifadhi hii kwa sasa ina ukubwa wa hekta **39,000** zinazoundwa na safu tatu (Wino 2000ha, Ifinga 29,000ha na Mkongotema **8,000** ha).

Hifadhi ya msitu wa Wino ulianza kuendelezwa na TFS mwaka 2010 ikihusisha eneo dogo la msitu wa asili wenye ukubwa wa hekta 2,000 (ambayo ndio safu ya Wino) na baadae mwaka 2014 na 2016 tulipata maeneo kutoka vijiji vya Mkongotema na Ifinga kama ilivyobainishwa hapo juu. Tangu tumeanza upandaji wa miti mpaka sasa

jumla ya hekta 5,046.8 zimepandwa miti ya jamii mbalimbali lakini sehemu kubwa ikiwa ni misindano.

### 9.7.6 Malengo ya Uanzishwaji wa Shamba

- Kuhifadhi maliasili zinazotaka kutoweka na vyanzo vya maji
- Ajira, Watumishi wa kudumu 15, mkataba 7, vibarua wa msimu 4,000.
- Mazao ya biashara kama mbao na nguzo za umeme kwa siku za usoni ili kuongeza mapato ya serikali
- Kuboresha mazingira na mandhari. Hali nzuri ya hewa (Carbon sink / Sequenstration) na mazingira ya kuvutia

### 9.7.7 Upandaji Miti

Shughuli za upandaji miti katika Shamba la miti Wino zimeendelea kufanyika kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji vinatunzwa vizuri kwa upatikanaji maji na mazao ya Misitu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Ambapo miche 5,788,000 ilizalishwa miche 5,592,559 ilipandwana miche 132,100 iligawiwa.

### 9.7.8 Shughuli za Kijamii

Katika kushirikiana na wananchi shamba limetoa mifuko **920** ya saruji, Simtank Moja (**1**), Madirisha ya aluminium **23**, Rangi lita **40**, Tiles boksi **40**, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na makanisa, Viriba kilogramu **30** na kuchangia kwenye miradi ya maji.

### 9.7.9 Mipango ya Shamba

Wakala wa huduma za misitu Tanzania kupitia shamba la miti ya kupandwa la Wino tunatekeleza mipango ya baadae kwa kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzwa

ipasavyo na upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya misitu na watumiaji wengine unakua endelevu kwa kizazi kilichopo na kijacho.

### 9.7.10 Taarifa ya Ufugaji Nyuki Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya eneo la km$^2$ **67,550** ambalo kati ya hizo km$^2$ **63,968** ni ardhi na km$^2$ 3,582 ni maji yanayojumlisha Ziwa Nyasa na mito mikubwa na midogo.

### 9.7.11 Lengo la Mkoa

Mkoa wa Ruvuma una lengo la kuwa na angalau mizinga **80,000**. Hii ina maana kuwa, kila Halmashauri iwe na angalau mizinga **10,000** na kuwa na viwanda 20 vya kuchakata mazao ya Nyuki, yaani kila Wilaya viwanda 4 ifikapo 2025. Utekelezaji wa lengo hili utashirikisha Wakala wa Huduma za Misitu, Halmashauri, Taasisi za Umma na zisizo za umma, Mashule, Vyuo, Makampuni na Watu binafsi.

### 9.7.12 Hali ya Ufugaji Nyuki ya Mkoa

Mpaka sasa Mkoa wa Ruvuma una juma ya mizinga 14,426 kati ya hiyo, mizinga ya kisasa ni 10,004 sawa na 69.34% na mizinga ya kienyeji ni 4,422 sawa na 30.65%. Mizinga hiyo yote inazalisha jumla ya kilo 16,186 za asali na kilo 36 za nta. Uzalishaji huu bado hauridhishi (Wastani wa mzinga 1 unazalisha kilo 1.12 badala ya kilo 10) kabisa ukilinganisha na fursa iliyopo ya kuwa na misitu mingi ya Miombo na mazao ya Alizeti na Kunde ambayo huchangia sana kwenye kuzalisha **necta**,

### 9.7.13 Kazi za Ufugaji Nyuki Zilizofanyika

Mradi wa Kuongeza Thamani Mazao ya Misitu (FORVAC) mpaka sasa umetengeneza mizinga 923 yenye thamani ya shilingi 107,239,650.00 ambayo wamegawa kwa vikundi 13 vya ufugaji Nyuki kwenye vijiji 6 vya Wilaya ya Mbinga. Jumla ya wafugaji Nyuki 473 wamepata mafunzo ya ufugaji Nyuki na uchakataji mazao yake. Mradi utaendelea kutoa

mafunzo na kugawa mizinga 900 kwenye kila Wilaya 4 zilizobaki ambazo ni Nyasa, Songea, Namtumbo na Tunduru.

### 9.7.14 Changamoto

i) Mwaka 2020 Chuo Kikuu cha Sokoine walishirikiana na Mradi wa FORVAC kufanya utafiti kwenye Mnyororo wa Thamani wa Ufugaji Nyuki Mkoani Ruvuma na walibaini matatizo yafuatayo:

- Ubovu wa barabara kuelekea kwenye Manzuki;
- Wafugaji hawana utaalam wa ufugaji Nyuki Kibiashara;
- Ukosefu wa mitaji ya kutengeneza mizinga na kununua vifaa vya kuvunia na kujikinga;
- Moto wa msituni ambao hutokea mara kwa mara kwenye misitu ya Miombo na maeneo ya mashambani;
- Ukosefu wa masoko ya uhakika ya kuuza asali na nta;
- Umbali mrefu kutoka kwenye makazi na maeneo ya hifadhi ambako manzuki zipo;

### 9.7.15 Hitimisho

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ufugaji nyuki  TFS, TaFF, FORVAC, WWF, TAWA, TANAPA, SUA, wamepanga yafuatayo: -

- Mkoa utashirikiana na wananchi Kuanzisha ufugaji nyuki kwenye maeneo ya jamii (Community Based Beekeeping).

- Kwenye maeneo yenye kilimo cha mazao ya mafuta kama alizeti, soya na ufuta (Block farming) ili kupata mazao ya nyuki na kuchevusha mazao ya kilimo.

- Mkoa unaendelea kushirikiana na TFS Kuanzisha ukanda wa ufugaji nyuki kwenye Hifadhi ya Mkongotema iliyopo Madaba.
- Mkoa unatarajia Kuanzisha kituo cha taarifa za ufugaji nyuki pamoja na cha kukusanyia mazao ya nyuki kwenye Ofisi za maliasili zilizopo Songea Mjini.
- Ili kuleta ufanisi kwenye elimu ya ufugaji nyuki na uchakataji wa mazao yake, mkoa utaazisha jumuiya (Association) za wafuga nyuki na wafanya biashara wa mazao ya nyuki angalau mmoja kila Wilaya. Jumuiya hizo zitafanya mtiririko wa taarifa za masoko na tekinolojia mpya to ngazi ya kimataifa, kitaifa, kimkoa, kiwilaya hadi kijijini.
- Mkoa utashirikiana na chuo cha Maliasili jamii Likuyusekamaganga kuanzisha mafunzo ya ufugaji nyuki ngazi ya VETA ambayo yatatoa elimu ya ufugaji nyuki na tekinolojia ya viwanda vya mazao ya nyuki kwa wananchi.

**Majadiliano**

Baada ya majadiliano wajumbe wa kikao walipokea na kuipitisha taarifa ya utekelezaji wa wa shughuli za Uchumi na Uzalishaji (Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Viwanda, Uwekezaji, Uvuvi, Maliasili na Ushirika).

## 9.0 MUHTASARI NA. RCC: 08/12/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA AFYA.

### 10.1 Huduma za Afya

Mkoa una jumla ya vituo **356** vinavyotoa huduma za afya. Kati ya vituo hivyo Hospitali ni **13** zikiwemo **6** za serikali, vituo vya afya **36** kati ya hivyo **10** ni vya mashirika ya dini, zahanati zipo **307** ambapo za serikali ni **246**, Mashirika ya dini ni **26, na 9** ni za mashirika ya umma na **26** ni za watu binafsi.

### 10.2 Mapokezi ya Fedha za Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo

Kwa mwaka 2020/2021 Mkoa umepokea jumla ya **Shilingi 1, 700,000,000.00** kwa ajili ya kujenga/kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya ambapo **Sh. 1,200,000,000.00** zilikuwa kwa ajili ya umaliziaji wa maboma **50** ya zahanati na Sh. **500,000,000.00** kwa ya kituo cha Afya Magazini.Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa umepokea kiasi cha **Tshs. 2,750,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika Tarafa **11** zisizokuwa na vituo vya afya. Aidha Mkoa umepokea fedha jumla ya **Tshs. 568,035,670.00** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi endelevu wa usafi na maji vijijini (Sustainable Rural Water Hygiene and Water Sanitation-SRWSS) kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji safi na tanki kwenye Zahanati 22 katika Halmashauri sita (6) za Mkoa wa Ruvuma.

Mkoa umepokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 kama ifuatavyo:

a) **Shilingi Milioni 630** kwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi wa sekta ya Afya.
**b)** **Shilingi Milioni 900** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya dharura (emergency **Medical Department-EMD)**
c) **Shilingi 250,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vya huduma za Wagonjwa mahututi (ICU)

### 10.3 Hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba

Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Hospitali ya Mkoa, Wilaya, vituo vya afya na zahanati imeendelea kuimarika. Ili kuimarisha upatikanaji wa dawa Mkoa unaendelea kusimamia na kuhakikisha matumizi sahihi ya mfumo wa ugavi wa uagizaji wa dawa

### 10.4 Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto

Vituo, vinavyotoa huduma za afya ya Uzazi na mtoto ni **324** sawa na asilimia **92.0** ya vituo vyote vinavyotoa huduma katika mkoa. Vituo **274** sawa na asilimia **85.0** vinatoa huduma ya uzazi wa mpango, vituo **309** Sawa na asilimia **95.3** vinatoa huduma ya uzazi

na kujifungua, vituo **287** sawa na asilimia **89.0** Vinatoa huduma ya chanjo na vituo **13** sawa na asilimia **38.2** ya vituo vya Afya (H/C) vinatoa huduma za CEMONC.

Kwa upande wa huduma ya wazazi, takwimu zinaonyesha kuwa kiwango cha akinamama waliojifungulia kituoni kimeongezeka kutoka asilimia **84.0** mwaka **2020** hadi asilimia **85.3** Disemba **2020**. Kiwango hiki ni juu ya lengo la taifa la asilimia **80.**

Idadi ya vifo vya wazazi imepungua kutoka vifo **31** sawa na vifo **55/100,000** mwaka **2020** hadi vifo **21** sawa na vifo **35/100,000** vya watoto waliozaliwa hai Disemba mwaka **2021**. Vifo viwili vilitolewa taarifa katika ngazi ya jamii. Sababu zilizochangia vifo hivyo ni Kutokwa na damu nyingi PPH. vifo **9** Sawa na asilimia **42** vimetokana na Kifafa cha Mimba vifo **4** sawa na asilimia **19** na Embolism vifo **3** sawa na asilimia **14**

Vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja kwa mwaka **2021** vimepungua kutoka **159** sawa na vifo **3/1000** ya watoto waliozaliwa hai mwaka **2020** hadi vifo **131** sawa na vifo **3/1000 Septemba** mwaka **2021**. Sababu zilizochangia vifo hivyo ni magonjwa ya watoto wachanga (perinatal condition). Vifo **41** sawa na asilimia **31.2** Prematurity, vifo **35** sawa na asilimia **26.7**, Pneumonia vifo **25** sawa na asilimia19**.0**, Malaria vifo **15** sawa na asilimia **11.4** Septicaemia vifo **6** sawa na asilimia **4.6** na Anaemia vifo **6** sawa na asilimia **4.6**.

Takwimu za vifo vya watoto chini ya **miaka mitano** vilivyotolewa taarifa ngazi ya vituo na jamii kwa mwaka **2021** vilikuwa **204** sawa na vifo **4/1000** ya watoto waliozaliwa hai. Idadi ya vifo hivi imepungua ukilinganisha na vifo **261** sawa na vifo **5/1000** ya watoto waliozaliwa hai mwaka **2020**. Sababu zinazoongoza kwa vifo hivyo ni Neonatal condition vifo **76** sawa na asilimia **37.2**, Pneumonia vifo **49 saw**a na **24.0** malaria vifo **44** sawa na asilimia **21.0**, Anaemia vifo **21** sawa na asilimia **10.0 na** Septicaemia vifo **14** sawa na asilimia **6.8** ya vifo vyote.

### 10.5 Hali ya chanjo

Katika kipindi cha Januari hadi Oktoba mwaka 2021 Mkoa umekuwa na mafanikio makubwa katika utoaji wa chanjo mbalimbali kama ifuatavyo;

Chanjo ya kifua kikuu (BCG) ni **147%,** chanjo ya kuzuia kupooza (Polio) **92%,** chanjo ya Donda koo, kukakamaa na kifaduro (DTP3) **120%** chanjo ya kuzuia homa ya mapafu (Pneumonia) **119%,** chanjo ya kuzuia kuharisha (Rota virus) **122%,** chanjo ya surua (Measles Rubella) **105%,** chanjo ya Pepopunda (Td) kwa wajawazito **107%** na chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 ni **84%.**

Mkoa umeendelea kutoa chanjo ya ugonjwa wa Korona ikiwa ni jitihada za kupambana na ugonjwa huu ambapo kwa kipindi cha kuanzia tarehe 04 Agosti, 2021 hadi tarehe 12 Oktoba, 2021 jumla ya watu **140,462** wamepatiwa chanjo ya korona. Kati ya hao **44,549** walichanjwa chanjo aina ya **JJ** na chanjo aina ya **Sinopharm** dozi ya pili wamechanjwa watu **30,608** sawa na asilimia **97.8** ya dozi **31,291** zilizopokelewa awali, na **65,305** wamechanjwa dozi ya kwanza. Hadi sasa kiwango cha Uchanjaji wa chanjo ya korona tumefikia asilimia **13.8** ya lengo la kuchanja asilimia **60** ya wakazi wa Mkoa wa Ruvuma.

### 10.6 Shughuli za Udhibiti UKIMWI

Kati ya jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 356; vituo 318 (89%) vinatoa huduma za upimaji wa VVU (HTS); vituo 306 (86%) vinatoa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT); vituo 127 (36%) vinatoa huduma za tiba na matunzo ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (CTC); vituo 40 (11%) vinatoa huduma za dawa kinga kabla ya kudhurika na VVU (PrEP); vituo 31 (9%) vinatoa huduma za tohara ya kitabibu kwa vijana balehe na wanaume (VMMC) na vituo 6 (2%) vinatoa huduma za tohara ya kitabibu kwa watoto wachanga wa kiume (EIMC).

Kiwango cha maambukizi ya VVU katika Mkoa wa Ruvuma ni asilimia 5.6 (THIS 2016/2017); ambapo maambukizi kwa wanawake ni asilimia 6.6 na wanaume asilimia

4.5. Kiwango hiki kipo juu kwa asilimia 0.9 ya kiwango cha kitaifa ambacho ni asilimia 4.7. Aidha, kiwango hiki cha maambuzi katika Mkoa kimepungua kwa asilimia 1.4 kutoka asilimia 7 mwaka 2011 (THMIS 2011/2012).

Katika utekelezaji wa malengo ya Kitaifa ya afua za VVU/UKIMWI ya 95-95-95 ifikapo mwaka 2025, kufikia Robo ya Julai – Septemba, 2021 katika Mkoa wa Ruvuma; asilimia 91 ya Watu Wanaoishi na VVU (WAVIU) katika Mkoa wanatambua hali zao za maambukizi; aslimia 99 ya WAVIU wanaotambua hali zao za maambukizi wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs) na asilimia 94 ya WAVIU wanaotumia dawa za ARVs wamefubaza makali ya VVU (DHIS-2

### 10.7 Huduma za Ustawi wa Jamii

#### 10.7.1 Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF)

Mkoa wa Ruvuma unatekeleza Mfuko wa Afya ya Jamii, Hadi kufikia 15 Disemba, 2021 jumla ya kaya 21,722(6%) zimeandikishwa kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF). Lengo la taifa ni kuhakikisha 30% ya wananchi wote wanajiunga na Mfuko.

Katika kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2021 mkoa umelipa jumla ya **Tshs. 228,291,436.72** mara mbili ya kiasi kilicholipwa kwa kipindi cha Januari hadi Disemba, 2020 (**Tshs. 121,392,142.77)** kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vilivyowahudumia wanachama wa iCHF.

#### 10.7.2 Usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya Miaka Mitano (U5BR)

Mkoa unaendelea kutekelezwa mpango wa usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano bure ulioanza Machi, 2020 katika Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma. Lengo la Mkoa wa Ruvuma ni kusajili na kuwapatia vyeti watoto 242,140, ambapo hadi tarehe 15 Disemba, 2021 mkoa umesajili na kutoa vyeti kwa watoto **236,618 (97.7%).**

### 10.7.3 Huduma za Lishe

Mkoa unatekeleza viashiria mbalimbali vilivyomo katika mkataba wa Lishe.Katika kipindi cha Julai–Septemba, 2021, viashiria nane (**8)** kati ya (**9)** vimetekelezwa kwa ufanisi wa zaidi ya asilimia **95** na kufanya Mkoa kuendelea kufanya vizuri katika viashiria hivyo. Viashiria hivyo ni pamoja na vikao vya kamati ya lishe, simamizi shirikishi wa afua za lishe, ukaguzi wa chakula, utoaji wa nyongeza ya matone ya vitamini A kwa watoto wenye umri wa miezi **6 – 59,** utoaji wa vidonge vya kuongeza wekundu wa damu kwa wajawazito, unasihi wa ulishaji wa watoto wachanga na wadogo

### 10.7.4 Mambo yanayosababisha lishe duni ni: -

i. Ulaji duni wa chakula unaotokana na kula milo michache na kiasi kisichotosheleza mahitaji ya virutubishi mwilini, hii pia hujumuisha kutowanyonyesha watoto ipasavyo.
ii. Magonjwa ya mara kwa mara yanayoondoa hamu ya kula na, kusababisha ufyonzaji duni wa virutubishi na huongeza mahitaji ya virutubishi mwilini.
iii. Matumizi mabaya ya chakula mfano kuuza chakula chote, kutumia nafaka kutengenezea pombe nk.
iv. Utayarishaji mbaya wa chakula unaopoteza virutubishi kama kuosha mboga za majani baada ya kukatakata.
v. Upungufu katika matunzo ya makundi maalumu (watoto wadogo, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha, wazee na wagonjwa) Makundi haya yanahitaji matunzo na huduma muhimu za kiafya kama vile chanjo, kupata vidonge vya nyongeza, kutibu maradhi na huduma za kilishe.

Katika kuhakikisha jamii inaondokana na tatizo hili la lishe ni muhimu kuendelea kuelekeza nguvu katika kusimamia utekelezaji wa mikataba ya lishe ngazi ya halmashauri, kata na vijiji / Mitaa ili jamii iweze: -

a) kubadili tabia na kuzingatia ulaji unaofaa.

b) Kupata elimu sahihi ya lishe kwa kupitia njia mbalimbali kama vyombo vya habari vilivyopo, ngoma za asili, viongozi wa dini na kimila.
c) Kupata elimu sahihi ya lishe katika kipindi cha siku 1000 za uhai wa mtoto (yaani toka mimba ilipotungwa hadi mtoto anapofikisha umri wa miaka 2) -
d) Mkoa na halmashauri kuhakikisha fedha inayotengwa kwa shughuli za lishe inatolewa na kufanya shughuli za lishe kama zilivyotengwa.

**Majadiliano;**

Baada ya kuwasilisha taarifa wajumbe waliohoji kuhusu upungufu wa dawa katika Vituo vya kutolea huduma za afya hususani katika vituo vya afya na Zahanati.Wajumbe pia walihoji kuhusu suala la udumavu kuendelea kukua katika Mkoa wa Ruvuma, wakati Mkoa ndio unaongoza katika uzalishaji wa mazao ya chakula.

Wajumbe pia walihoji kuhusu suala la uchache wa wananchi kujiunga na mfuko wa iCHF Kuwa hadi sasa wananchi waliojiunga mfuko huo kwa matibabu ni wachache sana ukilinganisha na idadi ya watu waliopo katika Mkoa wa Ruvuma.

Wajumbe walihoji juu ya uchakavu wa kituo vya afya vya Mkongo na Mputa, kuwa vipo katika hali mbaya sana na vinahitaji kutengewa bajeti ili vikarabatiwe.

Wajumbe walihoji kuhusu utofauti kati ya mfuko wa Ushirika Afya ambayo wananchi wanachnagia **57,000** na bima ya afya wanayochangia sh. **30,000**. Maelezo yalikuwa ushirika afya anachangia mmoja mmoja sh. **57,000** na Bima ya afya **30,000** inayochangiwa ni kwa familia nzima.

**Kuhusu suala la uhaba wa dawa;** Kikao kilielekeza kuwa zitolewe taarifa yakiwemo matangazo katika maeneo ya kutolea huduma za afya juu mchanganuo wa dawa muhimu zinazopaswa kutolewa kupitia mfuko wa iCHF ili watu wananchi wazifahamu na kuuelewa utaratibu wa dawa zinazotolewa na mfuko huo, lengo ni kuepuka mkanganyikoa uliopo wa wananchi kutokufahamu dawa zinazotolewa na mfuko.

**Kuhusu suala la udumavu;** kikao kilielekeza kuwa uhamashaji, na utoaji elimu uendelee ili wananchi wawe na uelewa juu ya madhara yatokanayo na na udumavu na hatimaye waweze kuzingatia milo kamili na bora, vilevile kikao kilielekeza kuwa Halmashauri ziendelee kutenga fedha kwa ajili ya kuhamasisha na kutoa elimu juu kupambana na udumavu.

**Kuhusu suala la wananchi kujiunga katika mfuko wa iCHF:** Kikao kilielekeza kuwa; kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko ili kufikia lengo la Kitaifa la asilimia **30**

## 11.0 MUHTASARI NA. RCC: 09/12/2021: TAARIFA YA UJENZI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA RUVUMA.

**Majadiliano;**

Taarifa ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa katika eneo la Mwenge Mshindo katika Manispaa ya Songea lilipokelewa na wajumbe wote na kupongeza kwa mpango huo mzuri, sambamba na pongezi zilizotolewa na wajumbe, walielekeza kuwa; eneo la Mwengemshindo ambako Hospitali itajengwa lazima wataalam wa ardhi wapime eneo hilo.

Wajumbe pia walielekeza kuwa ili mji ukuwe ni lazima maeneo yote yapimwe hivyo Wataalam wa ardhi katika Halmashauri wahakikishe suala la upangaji miji lizingatie utengaji wa maeneo ya vivutio/ maeneo yanayopendezesha mji kwa mfano bustani na maeneo ya kupumuzikia.

## 12.0 MUHTASARI NA. RCC: 10/12/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ELIMU

### 12.1 Elimu ya Awali na Msingi

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya shule za msingi **818**, kati ya hizo za Serikali ni **785** na zisizo za Serikali ni **33**. Mkoa umeendelea na zoezi la uandikishaji wa wanafunzi wa awali kwa mwaka wa masomo utakao anza mwezi januari 2022. Hadi kufikia Disemba 20, 2021 maoteo ya wanafunzi wa madarasa ya awali kwa mwaka 2022 ni **39,546** kati yao wavulana **19871** sawa na asilimia **50.2 na** wasichana **19,675** sawa na asilimia **49.7.** Hali ya uandikishaji kimkoa bado iko chini kwani idadi ya wanafunzi walioandikishwa

hadi Disemba 20 ni 16223 sawa na asilimia **39.9** wasichana wakiwa ni **7953** sawa na asilimia 39.4 na wavulana ni **8269** sawa na asilimia **40.3**

Aidha, maoteo ya wanafunzi wa darasa la kwanza kwa mwaka 2022 ni jumla ya wanafunzi **42623** kati ya hao wavulana **21401** sawa na asilimia **50.2%** na wasichana **21222** sawa asilimia **49.7%,** Kimkoa hadi kufikia tarehe 20 Disemba jumla ya wanafunzi **17068** wameshaandikishwa kujiunga na darasa la kwanza januari 2022 sawa na asilimia **42.4%** ikiwa wavulana ni **8680** sawa na asilimia **20.4%** na wasichana **8388** sawa na asilimia **19.7%**.Hivyo hali ya uandikishaji kwa Mkoa bado ipo chini na jitihada za ziada zinahitajika.

### 12.2 Idadi ya wanafunzi darasa la Awali-VII mwaka 2021

Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Disemba, 2021 ulikuwa na idadi ya wanafunzi wa darasa la Awali hadi la VII **390,855** Kati yao wavulana **195,651** na wasichana **195,204.**

### Walimu wa Shule za Msingi hadi Disemba, 2021.

Hadi kufikia Disemba, 2021 mahitaji ya walimu wa shule za msingi ni **10,071**, Waliopo **5,922** hivyo upungufu ni walimu **4,149.**

### 12.3 Hali ya ufaulu wa mtihani wa darasa la saba 2021

Mwaka **2021** wanafunzi wa darasa la saba wapatao **39,614** walisajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba. Wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi walikuwa ni **39,604** sawa na asilimia **99.9.** Wanafunzi waliofaulu mtihani walikuwa **28356** sawa na asilimia **73.1** ambapo wanafunzi wote waliofaulu wamechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari.

## 12.4 Hali ya samani katika shule za Msingi

Hadi kufikia Disemba, 2021 Mkoa una mahitaji ya madawati **126,248** yaliyopo ni **105,401** na upungufu ni **21206**. Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Wilaya zake umeendelea na jitihada mbalimbali ili kuweza kuondoa upungufu uliopo.

#### 12.5 Hali ya majengo katika shule za Msingi

Hadi kufikia Disemba, 2020 Mkoa ulikuwa na mahitaji ya vyumba vya madarasa **9,308**; yaliyopo ni **5,726** na upungufu ni **3,582**. Kwa upande wa matundu ya vyoo Mkoa ulikuwa na mahitaji **15,774** yaliyopo ni **7,897** na upungufu ni **7,877**.

#### 12.6 Elimu ya Sekondari

Mkoa una jumla ya shule za sekondari **214** zikiwemo **158** za Serikali na **56** ni shule za binafsi. Kati ya shule **158** za Serikali, shule tano **(5)** ni za bweni na shule **153** ni za kutwa. Kati ya shule **214** zenye kidato cha tano na sita ni **34** (Serikali **22** na zisizo za Serikali **12**).

#### 12.6.1 Walimu wa Shule za Sekondari hadi Disemba, 2021.

Hadi kufikia Disemba, 2021 mahitaji ya walimu wa shule za sekondari ni **4041**, Waliopo **3168** hivyo upungufu ni walimu **873.**

#### 12.6.2 Hali ya ufaulu wa kidato cha nne

Mkoa wa Ruvuma kitaaluma unaendelea kufanya jitihada za makusudi ili kuweza kupata matokeo mazuri zaidi. Mwaka 2020 Mkoa ulikuwa na ufaulu wa asilimia **89.4**% Juhudi za kupandisha ufaulu na kudhibiti udanganyifu ziliendelea kufanyika.

### 12.6.3 Ufaulu wa kidato cha Sita 2021

Mkoa umeendelea kufanya jitihada kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika matokeo ya kidato cha Sita. Mwaka 2021 Mkoa umepandisha ufaulu na kupata wastani wa ufaulu wa 99.9.

### 12.6.4 Miundombinu ya shule za sekondari

Miundombinu ya shule za sekondari imekuwa ikijengwa ili kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia yakiwemo madarasa, majengo ya utawala, nyumba za walimu, Mabweni, Maktaba, maabara na vyoo.

#### 12.6.5 Samani

Hadi kufikia Disemba, 2021 hali ya samani katika shule za sekondari kwa ajili ya wanafunzi ni, mahitaji ya meza ni **78558,** zilizopo zikiwa ni **68537** na Upungufu ni **10731**. Mahitaji ya viti ni **78538**, vilivyopo ni **69252** upungufu ni viti **10016**

#### 12.6.6 Maabara

Maabara za sayansi hadi kufikia Disemba, 2020 ni kama ifuatavyo; mahitaji ni **471,** zilizopo ni **352** pungufu ni **119**.

#### 12.6.7 Utekelezaji wa miradi ya EP4R, Awamu ya 9 na ujenzi wa vyoo vya kisasa kwa bajeti ya mwaka 2020/2021

Hadi kufikia Oktoba, 2020 Mkoa wa Ruvuma ulikuwa umekwishapokea Jumla ya Tshs **6,149,428,112** kupitia Mradi wa EP4R awamu ya 8 fedha za mwaka 2019/2020 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi

**792,048,111.72** ni kwa ajili ya ukarabati wa wa shule Kongwe ya Tunduru Sekondari. Miundombinu mingine iliyojengwa ni ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, mabweni, mabwalo, na majengo ya utawala.

Pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo Mkoa ulipokea **Tsh.1, 054,591,028.59** kutoka Serikalini kwa ajili ya ujenzi wa vyoo bora vya kisasa vya wanafunzi na walimu kupitia mradi wa SWASH (School Water, Sanitation and Hygiene) ambapo jumla ya vyoo 60 vyenye matundu **800** vimejengwa, kati ya vyoo hivyo **42** vikiwa na matundu **732** ni vya wanafunzi na vyoo **18** vyenye matundu **68** ni vya walimu.

#### 12.6.8 Mapokezi ya Fedha za Ukamilishaji wa Maboma ya Vyumba vya Madarasa

Kwa mwaka wa fedha 2019/2021 Mkoa kupitia halmashauri zake umepokea kiasi cha **Tshs. 6,088,978,791.00** kutoka Hazina kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa, Ujenzi wa matundu ya vyoo pamoja na ukarabati wa vyumba vya madarasa shule za msingi na sekondari.

### 12.6.9 Utekelezaji wa Programu ya Elimu Bila Malipo

Sera ya utoaji wa Elimu Bila Malipo inaendelea kutekelezwa ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Novemba 2021 Mkoa umepokea kiasi cha **2,325,234,963.64** ambazo zimesaidia katika uendeshaji wa shule na kuboresha na kuimarisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi na sekondari ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada.

### 12.6.10 Michango na Ushiriki wa Asasi na mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo ya elimu.

Mkoa umekuwa ukishirikiana vizuri na wadau mbalimbali katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya Elimu, katika kusaidia uboreshaji wa mazingira ya ujifunzaji na kufundishia. Mkoa tunatambua jitihada za wadau hawa ambao kwa mwaka **2020/2021** wametoa misaada ya shilingi **1,030,194,451.17** michango hiyo imekuwa ikielekezwa kwemye ujenzi na uboreshaji wa miundombinu, vifaa kwa kujifunzia, huduma ya chakula shuleni vifaa vya TEHAMA pamoja na utolewaji wa elimu rika kwa wanafunzi,Mkoa unatambua asasi na mashirika kama vile *Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO),Benki ya NMB,Tanzania Project, Kalamu Education Foundation, Social Action Trust Fund (SATF),* ***Tanzania mission to the Poor and Disabled*** *(PADI), Research Triangle Institute (RTI)*

### 12.6.11 Mapokezi ya Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na UVIKO -19

Mkoa umepokea mgao wa jumla ya shilingi 10,240,000,000 kwa mchanganuo ufuatao; vyumba vya madarasa 448 yenye thamani ya shilingi **8,960,000,000.00** kwa shule za sekondari, vyumba 52 katika vituo shikizi vya shule za msingi vyenye thamani ya shilingi **1,040,000,000.00** na mabweni matatu yenye thamani ya shilingi **240,000,000.00** kwa shule za msingi zenye mahitaji maalumu. Kupitia mpango huu wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO19.

#### 12.6.12 Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

Utoaji wa elimu unahusisha Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ambayo ni Elimu Endelevu inayotekelezwa katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma. Elimu Nje ya Mfumo Rasmi inayojumuisha Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA), Mpango wa Elimu ya Sekondari kupitia Ujifunzaji huria (Open Learning) unaojumuisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa mtihani wa Maarifa (QT). Hadi kufikia Disemba, 2020 kuna vituo **109** katika shule za msingi vinavyotekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA). Utekelezaji wa

Mpango wa Elimu ya sekondari katika vituo **125** vinavyoaandaa wanafunzi wa mtihani wa Maarifa **(QT)** na utekelezaji wa elimu ya ufundi stadi katika vituo vya ufundi stadi **24**.

Utekelezaji wa **elimu maalum** unafanyika katika shule zote za msimgi na sekondari. Kwa sasa kuna vituo **302** katika shule zilizobainisha watoto wenye mahitaji maalum.

#### 12.6.13 Elimu ya Ufundi Stadi

**Eneo hili linajumuisha utoaji wa elimu katika vyuo vya ufundi (VETA)** na vyuo vya ufundi stadi vya kati. Kwa sasa Mkoa una vyuo 3 vya Serikali vya ufundi stadi kati ya hivyo 2 vinatoa huduma ya ufundi ambavyo ni VETA Songea na VETA Namtumbo. Chuo cha VETA Nyasa ujenzi umekamilika. Aidha kuna chuo cha VTC Kiuma kilichopo Tunduru ambacho kinamilikiwa na taasisi ya dini. Hata hivyo elimu ya ufundi inatolewa katika vituo vya ufundi vidogo ambapo kwa sasa kuna vituo vya ufundi stadi **24**.

#### 12.6.14 Michezo

Mkoa wa Ruvuma Kwa Kipindi Cha Januarii 2021 Hadi Disemba Imeendelea Kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Kwa Kuhakikisha Michezo Inaendelea Kufanyika na Kushiriki Katika Mashindano Mbalimbali. Ushiriki katika mashindano ya shule za Msingi (UMITASHUMITA), na Mashindano ya UMISSETA kitaifa na kufanikiwa kutoa wachezaji wawili walio chaguliwa kujiunga na timu ya Taifa itakayo shiriki katika mashindano wanafunzi ya Afrika Mashariki na kati ambao ni **Longinus Venent Mapunda** kutoka wilaya ya **Songea** na **William Ngindo** kutoka wilaya ya Nyasa kwa upande wa **(UMITASHUMITA**) wanafunzi walio chaguliwa ni **Fadhili Abdallah** na **Abdalah Mahamoud** wote kutoka **Wilaya ya Tunduru.**

a) Michezo kwa shule za msingi na Sekondari
   Mkoa umeshiriki katika mashindano hayo yaliyofanyika mkoani Mtwara mkoa wetu haukufanya vizuri kwa timu zilitolewa katika hatua ya robo na hivyo kushindwa kupata ushindi katika UMITASHUMTA Mkoa ulikuwa wa 26 na katika UMISSETA Mkoa ulikuwa nafasi ya 24.

b) Mashindano ya SHIMIWI

   Mashindano haya huhusisha watumishi wa serikali wa wizara na idara za serikali Mkoa wa Ruvuma ulipata **ushindi wa kwanza katika mchezo wa bao**

c) Mashindano ya **SAMIA TAIFA CUP**

Mashindano haya hujumuisha wananchi kwa ujumla wake na lengo la mashindano haya ni kupata vipaji ambavyo vitatumika katika timu za Taifa na vilabu mbalimbali vinavyoshiriki ligi za kitaifa. Katika mashindano haya Mkoa wa Ruvuma imekuwa **mshindi wa tatu katika mchezo wa mpira wa miguu Kitaifa.**

Aidha, vijana wawili wa sanaa ya Muziki wa kizazi kipya wamepata ufadhili wa masomo katika chuo cha Sanaa Bagamoyo kwa muda wa mwaka mmoja na wanamichezo sita kuchaguliwa katika timu za Taifa na vilabu kama Jedwali Linavyoonesha.

Hatua za kuboresha michezo

1. Kila Halmashauri imeagizwa kuwana vitalu ambavyo vitawaandaa wanamichezo kuepuka maandalizi ya zimamoto.
2. Shule ya sekondari ya Mahanje ya Halmashauri ya Madaba kuwa shule inayopokea wanafunzi wenye vipaji vya michezo mbalimbali kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma ili kukuza vipaji vyao. Wanafunzi hawa ni wale waliofika ngazi ya taifa na kufaulu mitihani yao ya elimu ya msingi.
3. Kuendelea kuwashirikisha wananchi katika shughuli za kuchangia na kuendeleza Michezo katika Mkoa wetu wa Ruvuma
4. Kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika jogging na michezo mbalimbali ya asili ya Mtanzania
5. Timu ya majimaji kuwa katika mchakato wa kuwa kampuni ili kuboresha mwenendo wake

### 12.6.15 Changamoto Katika Sekta ya Elimu

i. Wazazi kuhamia mashambani mbali na shule na kuwaacha wanafunzi peke yao hivyo kusababisha baadhi yao kuwa watoro na kuacha masomo.
ii. Baadhi ya wazazi kutokuchangia chakula cha mchana shuleni kwa ajili ya wanafunzi
iii. Upungufu wa Walimu hasa katika shule za Msingi
iv. Kutokuwa na shule za bweni zinazokidhi mahitaji
v. Upungufu wa miundombinu, samani na hosteli

### 12.6.16 Mikakati ya Kuinua Ubora wa Elimu Kuongeza Taaluma

a. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala wa elimu katika ngazi za elimu za Halamshauri na shule.
b. Kuhimiza na kufuatilia ufanyikaji wa mtihani ya upimaji wa mara kwa mara kwenye madarasa yote.
c. Kutoa ushauri kwa halmashauri kufanya urekebishaji wa ikama ya walimu.
d. Kuhimiza utoaji wa motisha kwa wanafunzi, walimu, shule na halmashauri zinazofanya vizuri kwenye taaluma.
e. Kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa utoaji wa chakula kwa wanafunzi wawapo shuleni wakati wa mchana.
f. Kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwemo ujenzi utakaoanza wa shule maalum ya Kitaifa ya wasichana itakayojengwa Kijiji cha Migelegele katika wilaya ya Namtumbo

**Majadiliano;**

Waajumbe walihoji juu mkakakti wa uliopo wa ujenzi wa Tawi la Chuo kikuu cha Sokoine katika sehemu tatu ambazo ni; Tunduru kama tawi litakalohusika utoaji wa mafunzo ya Kilimo, Madaba – mafunzo ya Misitu na Nyasa – Mafunzo ya Utalii.Wajumbe pia walihoji juu ya mkakati wa ujenzi wa vyuo vya VETA katika Wilaya ya Tunduru, Madaba, Mbinga,

Wajumbe pia walihoji juu ya kuanza kutoa mafunzo chuo cha VETA cha Wilaya ya Nyasa, kwani hadi sasa ukamilishaji wa chuo bado haujafanyika na mafunzo hayajaanza kutolewa.

**Kuhusu ujenzi wa Chuo cha Kilimo (SUA)**

Kikao kilielekeza kuwa Ifanyike jitihada ya kuongeza msukumo wa kuomba Chuo Cha Kilimo Sokoine (SUA) kuanzisha Tawi la Chuo katika Halmashauir ya Wilaya ya Madaba, Tunduru na Nyasa ambapo maeneo yameshatengwa.

**Kuhusu chuo cha VETA - Nyasa kuanza kutoa mafunzo**

Kikao kilielekeza kuwa Chuo cha VETA Nyasa kianze kutumika.

**Kuhusu mkakati wa ujenzi wa Chuo Cha VETA Wilaya ya Tunduru**

Zifanyike jitihada za kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya VETA Mbinga na Tunduru.

## 13.0 MUHTASARI NA. RCC: 11/12/2021: TAARIFA ZA TAASISI NA MASHIRIKA.

### 13.1 Taarifa ya maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi toka Ofisi ya Taifa ya Takwimu Mkoa wa Ruvuma.

Taarifa iliwasilishwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatarajia kufanya Sensa ya sita (6) ya watu na makazi mwaka 2022 tangu kupata uhuru, Sensa hiyo itajumuisha taarifa za Majengo yote nchini na matumizi yake pamoja na Anwani za Makazi. Nchi yetu inaingia kwenye historia ya kutumia mfumo wa kielektroniki katika kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu za sensa ya watu na makazi kwa kutumia kishikwambi (tablet). Aidha tofauti na sensa zilizopita sensa ya mwaka 2022 itahusisha udodosaji wenye maswali 97 katika dodoso kuu tofauti na ilivyokuwa kwenye sensa ya mwaka 2012.

### 13.1.1 Utengaji wa Maeneo

Kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu inaendelea ndani ya mkoa, hadi sasa zoezi la kutenga maeneo limekamilika katika kata 61, vijiji 221, na vitongoji 1,488, ambayo ni sawa na asilimia 42.8 ya kazi nzima.

### 13.1.2 Hitimisho

Mafanikio ya zoezi la Sensa yanategemea ushiriki wa wadau wote wa Sensa wakiwemo: viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa; viongozi wa taasisi za dini na wananchi kwa ujumla. Ili kufanikisha hili, Sensa imekuwa ni moja ya agenda inayojadiliwa katika vikao mbalimbali vya viongozi mkoani kwa lengo la kutoa hamasa na kujenga uelewa juu ya umuhimu wa Sensa na wajibu/majukumu ya wadau katika kuleta ufanisi na tija katika zoezi la ufanyikaji wa Sensa. Elimu na hamasa kuhusu Sensa itaendelea kutolewa kwa wadau/wananchi kupata matokeo bora ya Sensa ya Watu na Makazi itakayosaidia kufanya maamuzi sahihi katika mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Kwa kushirikiana pamoja tutaweza kuwa na Sensa yenye mafanikio na sifa ya kuigwa barani Afrika.

**Majadiliano.**

Wajumbe walihoji juu ya uhamasishaji na utoaji elimu kwa wananchi juu ya kushiriki katika sensa ya Watu na Makaazi.Pia wajumbe pia walihoji juu utoaji elimu ya teknolojia itakayotumika katika zoezi la sensa kwa watu watakaoshiriki katika zoezi la ukusanyaji wa takwimu.

**Wajumbe walielekeza** kuwa ufanyike uhamasishaji na utoaji elimu kwa wananchi katika kushiriki kwenye sensa ya watu na makaazi, sambamba na utoaji elimu ya teknolojia itakayotumika kwa watu watakaoshiriki katika zoezi la kukusanya takwimu. Ili

kuepuka upotofu uliojitokeza katika sensa ya mwaka 2012 ya watu kutoshiriki katika baadhi ya maeneo hususani Wilaya ya Tunduru.

Wajumbe pia walielekeza kuwa wataalam watakaohusika katika zoezi la sensa ni wale waliofunzwa vizuri, na sio kufanya upendeleo wa kuweka ndugu au watu ambao hawakidhi vigezo.

### 13.2 Taarifa ya utendaji kazi wa mamlaka ya Mapato Mkoa wa Ruvuma (TRA). Mwaka 2021/2022

#### 13.2.2 Sura ya Mkoa

Mkoa wa Kodi wa Ruvuma una Wilaya tano ambazo ni Songea, Mbinga, Tunduru, Namtumbo na Nyasa. Kwa sasa Mkoa wa kodi wa Ruvuma una ofisi nne za wilaya ambazo ni Songea, Mbinga, Namtumbo na Tunduru na vituo viwili vya forodha ambavyo ni Mkenda-Nakawale na Mbamba Bay. Wilaya ya Nyasa bado hatujaanzisha ofisi ya Idara ya Kodi za ndani.

#### 13.2.3 Idadi ya Walipakodi

Katika ukusanyaji wa kodi Mkoa umesajili walipakodi **20,642** ambapo walipakodi walio hai (active) ni **14,191** na walipa kodi wasio hai (dormant) ni **6,451**. Idadi ya walipa kodi waliosajiliwa kwenye kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ni **316** na idadi ya walipakodi walionunua na wanaotumia mashine za EFD ni **2,716**.

#### 13.2.4 Taarifa ya Utendaji wa Kazi kwa kipindi cha Mwaka 2020/2021 na kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2021 – Oktoba 2021.

Mkoa wa Kodi wa Ruvuma ulipangiwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 16,365,090,734.95** kwa mwaka 2020/2021 ambapo Idara ya Kodi za Ndani ilitakiwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 15,639,362,250.62** na Idara ya Forodha ilitakiwa kukusanya **Tshs. 725,728,484.33.**

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 tulifanikiwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 16,984,706,090.00** ikiwa ni ufanisi wa **asilimia 104**.

Aidha, kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Mkoa umepangiwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 21,160,639,530.16** ambapo **Tshs. 20,906,022,329.49** ni mapato ya ndani na **Tshs. 254,617,200.67** ni ushuru wa forodha. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Oktoba 2021** lengo la makusanyo lilikuwa **Tshs. 6,437,844,432** na tumefanikiwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 5,834,683,301** sawa na asilimia **91** ikiwa ni ukuaji wa mapato ya **Tshs. 287,184,318.13** sawa na asilimia 5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha uliopita. Katika makusanyo hayo Idara ya Kodi za Ndani imechangia **Tshs. 5,517,455,624.23** na Idara ya Forodha imechangia Tshs. **317,227,677.00.**

#### 13.2.5 Changamoto

Taarifa ilionesha kuwa Mamlaka ya Mapato inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i. Mwitikio usioridhisha wa wananchi kutoa na kudai risiti za EFD kwenye mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali.
ii. Kushuka kwa bei ya mazao (mahindi) ikilinganishwa na miaka iliyopita na hivyo kupelekea walipa kodi kushindwa kulipa kodi zao kwa wakati.
iii. Ukosefu wa mifumo ya uhakika ya TEHAMA kwenye baadhi ya ofisi za Mamlaka ya Mapato Wilaya (Mbinga na Namtumbo).
iv. Upungufu wa wafanyakazi hususani kwenye vitengo vya ukusanyaji wa mapato.
v. Upungufu wa vitendea kazi yaani magari, pikipiki na vifaa vya ofisini.
vi. Ukosefu wa nyumba za kuishi kwa wafanyakazi walioko vituo vya forodha vya mpaka wa Mkenda – Nakawale na Mbamba bay.
vii. Mwitikio mdogo wa walipakodi kuhudhuria semina za kodi na hivyo kuwa na uelewa mdogo wa masuala ya kodi.

#### 13.2.6 Mikakati ya uboreshaji wa mazingira ya biashara ili kufanikisha malengo kwa kipindi kijacho

Katika kuhakikisha malengo ya ukusanyaji kodi yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha **2021/2022** kiasi cha Tshs. **21,160,639,530.16** yanafikiwa, Mamlaka ya Mapato imeweka mikakati ifuatayo: -

i. Kuendelea kutoa elimu na kuongeza idadi ya semina kwa wafanyabiashara na wananchi juu ya faida za kulipa kodi.
ii. Kuendelea na uhamasishaji wa ulipaji kodi wa hiyari.
iii. Kuongeza wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya na kubaini vyanzo vipya vya kodi.
iv. Kuendelea kujadili changamoto za wafanyabiashara kwa kuhusisha wadau mbalimbali wa kodi ikiwemo Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT) na TCCIA.
v. Kuanzisha vilabu vya kodi kwa wanafunzi wa shule za sekondari (Tax Clubs) ili kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari kutoka ngazi za chini.
vi. Kuimarisha usimamizi wa maadili ya watumishi wakati wa utendaji kazi.

**Majadiliano.**

Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuwasilishwa na kuipitisha.

## 13.3 Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za huduma ya Maji (RUWASA) Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Disemba, 2021

### 13.3.1 Hali ya Huduma kwa Sasa

Manispaa ya Songea ina wakazi wapatao 203,309 kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Taifa iliyofanyika mwaka 2012. Ongezeko (*Growth rate*) kwa mwaka ni 4.4%, hivyo kwa mwaka 2021 Manispaa inakadiriwa kuwa na Wakazi 299,543. Wakazi waliopo katika kata za mjini ni 251,501 kati yao 215,630 wanapata huduma ya maji sawa na asilimia 85.7.

Mahitaji ya maji ni wastani wa meta za ujazo **17,897** kwa siku mwaka 2021 katika maeneo ya katikati ya mji na **25,862** katika maeneo yote ya Manispaa. Uzalishaji wa maji ghafi ni wastani wa mita za ujazo **9,362** kwa siku (Oktoba 2021).

### 13.3.2 Mpango wa Kuboresha Huduma Katika Manispaa ya Songea

Manispaa ya Songea ni miongoni mwa miji 28 nchini Tanzania ambayo itanufaika na mradi wa maji kwa ufadhili wa Serikali ya India kupitia Exim bank. Mhandisi mshauri amekamilisha usanifu na sasa Wizara ya Maji inaendesha zoezi la kupata wazabuni wa utekelezaji wa mradi huo. Mradi huo utawezesha ujenzi wa:

- Bwawa la Mahilo lenye uwezo wa kuhifadhi maji 5,000,000 $m^3$
- Matanki manne yenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 18,200
- Upanuzi wa mtandao wa bomba za usambazaji km 190.4 katika manispaa ya Songea.

Mamlaka inatarajia kutekeleza miradi miwili ya maji kupitia programu ya UVIKO-19:

i) Kuboresha huduma ya maji katika kata ya Tanga (Pambazuko na Mlete) kupitia mpango wa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO 19

   - Kujenga nyumba 2 za kusukuma maji
   - Kujenga mtandao wa bomba za usambazaji km 18
   - Kujenga tanki la maji lenye uwezo wa lita 150,000.
   - Kujenga vituo 10 vya kuchotea maji

ii) Kuboresha huduma ya maji katika kata ya Ruvuma na Mshangano kupitia msaada wa Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ):

   - Kuongeza mtandao wa bomba za usambazaji km 12.4
   - Kujenga vituo vya kuchotea maji 30 ikihusisha Ruvuma 15 na Mshangano 15.
   - Kuunga wateja wa majumbani katika eneo litakalopitiwa na mradi.

iii) RUWASA imepewa maelekezo kutekeleza miradi mbalimbali ya maji katika maeneo ya pembezoni mwa halmashauri ya manispaa ya Songea kupitia programu ya PBR. Miradi hiyo inatekelezwa kwa kutumia wataalamu wa ndani kwa kushirikiana na SOUWASA.

### 13.3.3 Taarifa ya huduma ya maji mjini Mbinga

i. Mji wa Mbinga una wakazi wapatao 51,865 ambao wanapata huduma ya maji safi ni 36,737 sawa na asilimia 70.8

ii. Idadi ya wateja ni 3,468 ambao wote wamefungiwa dira

iii. Mahitaji ya maji ni mita za ujazo 5,490 kwa siku wakati uzalishaji ni mita za ujazo 2,800 kwa siku.

iv. Mamlaka ina matanki 4 yenye ujazo wa mita 700 na bomba za usambazaji km 50.2

v. Kiwango cha huduma ni saa 18 kwa siku

vi. Mpango uliopo ni kukamilisha mradi wa kupanua mtandao katika kata za Bethlehemu, Matarawe na Ruhuwiko pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji cha Mkele na bomba za kusafirisha maji hadi katika kipunga maji (BPT) ambacho kibali chake utekelezaji mradi huo unaogharimu Tsh 300,000,000 kimetolewa na Wizara ya Maji.

### 13.3.4 Taarifa ya hali ya maji katika mji wa Tunduru

i. Mji wa Tunduru una wakazi 68,340 kwa mwaka 2021 na wakazi wanaopata huduma ya maji safi ni 45,200 Sawa na asilimia 66

ii. Idadi ya wateja ni 2,353 ambao wamefungiwa dira ni 2,115 sawa na 90%

iii. Mahitaji ya maji ni mita za ujazo 4,100 kwa siku na uzalishaji ni mita za ujazo 2,390

iv. Mamlaka ina matanki 6 yenye ujazo wa mita 560 na bomba za usambazaji km 79

v. Kiwango cha huduma ni saa 12 kwa siku

vi. Mpango uliopo ni kupanua mtandao katika maeneo yasiyofikiwa na huduma ya maji utakaogharimu Tsh 456,000,000 kupitia bajeti ya mwaka 2021/2022 ambapo Wizara ya Maji imetoa kibali. Pia kupitia programu ya quickwin itakaogharimu Tsh 300,000,000.00, Mamlaka imepanga kuongeza uzalishaji kwa kuchimba kisima na kulaza bomba za kusafirisha maji kutoka chanzo hadi katika matenki ya Frank Weston na Jeshini.

### 13.3.5 Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji kwa Fedha za NWF

Mamlaka kwa kushirikiana na RUWASA inatekeleza miradi ya maji katika Halmashauri ya wilaya ya Songea na Mbinga ambayo utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali.

**Majadiliano.**

Wajumbe walihoji kuhusu uvamizi unaofanywa na wananchi kwa kufanya shughuli za kilimo katika vyanzo na hifadhi ya Mto Ruvuma. Kikao kilielekeza kuwa ziendelee kufanyika jitihada za kuwaondoa watu wote waliovamia vyanzo vya maji, na kuendesha shughuli za kibidamu katika maeneo ya vyanzo na hifadhi ya mito. Mamlaka ya bonde la Mto Ruvuma na bonde la Nyasa kufanya upimaji na utambuzi wa mipaka na kuweka alama katika maeneo ya vyanzo na hifadhi za mito.

## 13.4 Taarifa ya hali ya upatikanaji wa huduma ya Umeme Mijini na Vijijini na Mipango iliyopo (TANESCO)

Mkoa wa Ruvuma una wilaya tano (5) ambazo makao makuu ya Wilaya zote tayari zimefikiwa na umeme wa Gridi ya Taifa ambazo ni Songea, Namtumbo, Tunduru, Mbinga na Nyasa. Hadi kufikia mwezi October 31, 2021 Mkoa ulikuwa na jumla ya wateja **75,760**

### 13.4.1 Hali ya Upatikanaji wa Umeme

Kiujumla hali ya upatikanaji wa umeme ni ya kuridhisha kwa wilaya zote, tunaendelea na kuimarisha miundombinu ili kuhakikisha umeme unapatikana muda wote na ni wa uhakika kwa wilaya zote.

### 13.4.2 Kufua na Kupokea Umeme

Tarehe 15/09/2018 mkoa uliunganishwa kwenye umeme wa Grid katika wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga na Nyasa, Mkoa pia unapata umeme kutoka kwa wawekezaji binafsi wa kampuni ya **TULILA** na **ANDOYA** ambao wana uwezo wa kufua Megawatt 6 kwa kipindi cha mvua na kuingiza kwenye GRID ya Taifa. Na wilaya ya Tunduru iliunganishwa na Umeme wa Gridi ya Taifa mnamo tarehe 20/12/2019 baada ya kukamilika ujenzi wa line ya msongo wa kati (33KV) km 65 kuunganisha wilaya ya Tunduru kwenye Gridi ya Taifa kutokea Namtumbo. Mahitaji ya juu ya umeme katika mkoa ni wastani wa **MW 17.50**

Mkoa una vituo viwili vya kupokea na kupoza umeme kutoka kwenye Gridi ya Taifa (Grid Substations)

### .13.4.3 Uunganishaji wa Wateja

Wateja waliounganishiwa umeme kwa kipindi cha Julai 2020 mpaka June 2021 ni 9,582 ukilinganisha na lengo la mkoa la kuunganisha wateja 6500 kwa mwaka sawa na asilimia **147.4%,** Pia kwa mwaka huu wa fedha wateja waliounganishwa kuanzia tarehe 1/07/2021 hadi 31/10/2021 ni 5,480 sawa na asilimia **84.3%** ya lengo la mwaka mzima.

### 13.4.4 Mtandao wa Usambazaji Umeme Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma una mtandao mkubwa wa usambazaji wa umeme wenye mashine umba (Transformer) **636** na urefu wa kilomita **1,590.9** kwa msongo wa kilovoti 33, kilomita **150.2** kwa msongo wa kilovoti 11 na kilomita **1,937.41** kwa msongo wa kilovoti 0.4/ 0.23 (LT).

### 13.4.5 Miradi inayotekelezwa na TANESCO Kutumia Bajeti Za Ndani ya Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

TANESCO Mkoa wa Ruvuma una jumla ya miradi 47 katika mwaka uliopita wa bajeti ya 2021/22 kwa mchanganuo ufuatao: -

**i.** Miradi ya kuboresha miundombinu (Voltage Improvement projects) - jumla ya bajeti **832,296,282**

ii. Miradi ya kuongeza miundo mbinu (New extension projects) 18- jumla ya bajeti **1,758,096,239.93**

**iii.** Miradi ya matengenezo ya miundombinu (Repair and maintenance projects) - jumla ya bajeti **1,221,830,998.87.**

iv. Miradi yote ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji

### 13.4.6 Miradi wa Umeme Unaofadhiliwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA)

**REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza (R3R1)**

- Namba ya mkataba: **AE/008/2016-2017/HQ/G/9 LOT 6**
- Eneo la utekelezaji: Wilaya za Songea, Mbinga, Nyasa, Namtumbo na Tunduru
- Mkandarasi: Namis Corporate Ltd
- Gharama za mradi: **(TZS) 43,869,003,071.89 na** Fedha za Kimarekani **(USD) 7,483,076.98 zikiwa pamoja na ongezeko la thamani.**
- Muda wa kuanza: 28/08/2017
- Muda wa kumaliza: 31/12/2021
- Lengo la mradi: kupeleka umeme kwenye vijiji **177**

**13.4.7 Wigo Pamoja na Nyongeza**

Baada ya Mkandarasi kufanya upembuzi yakinifu kulibainika kuwa na ongezeko la umbali wa kilomita 691.03 kwa msongo wa kati kilovolti 33 ili kuvifikia vijiji vilivyopo kwenye mkataba.

**13.4.8 Hatua za Utekelezaji wa Mradi hadi Kufikia Tarehe 18/11/2021**

Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia 99.49% za Upeo wa mradi kadiri ya Mkataba uliosainiwa awali na 94.13% za upeo wa mradi pamoja na Nyongeza ya mkataba. Aidha, ufungaji wa **transfoma 191** umekamilika na **vijiji 144** vimepatiwa umeme kati ya vijiji **177** ambapo hatua mbalimbali za ujenzi zinaendelea. Pia **wateja 7005** wa awali wameunganishwa kati ya lengo la kuunganisha wateja **9778** mradi utakapokamilika.

## 13.4.9 Changamoto

i. Kuchelewa kuidhinishwa kwa nyongeza ya mradi (addendum) hivyo kupelekea kuchelewa kumaliza mradi

ii. Kasi ndogo ya mkandarasi kwenye kutekelezaji wa mradi

iii. Wigo mdogo ulioidhinishwa

### 13.4.10 Taarifa ya Utekelezaji ya Mradi R3R2-LOT25 Mpaka Tarehe 17/11/2021

- Namba ya mkataba: **AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 25**
- Eneo la utekelezaji: Wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa
- Mkandarasi: Namis Corporate Ltd
- Gharama za mradi: TZS 35,281,367,752.46 (pamoja na VAT)
- Muda wa kuanza: 28/08/2021
- Muda wa kumaliza: 07/03/2023
- Lengo la mradi: kupeleka umeme kwenye vijiji 163

### 13.4.11 Upeo wa Mradi

Upeo wa Mradi kwa mkataba uliosainiwa ni kuviwashia umeme vijiji 163 baada ya REA kukamilisha kuwapatia wakandarasi nyongeza ya mkataba kwa ajili ya vijiji vilivyorukwa. Vijiji vyote vilivyokuwa vimerukwa kwa sasa vimeingizwa kwenye mkataba na

kupelekea kuongezeka idadi ya vijiji mpaka kufikia 163 kutoka 143 vilivyokuwa kwenye mkataba wa awali na vijiji 5 wakati wa survey vimeonekana vina umeme

### 13.4.12 Hatua za Utekelezaji wa Mradi Wilaya ya Songea, Mbinga na Nyasa hadi Tarehe 18/11/2021

Mpaka sasa kazi ya survey imeshafanyika katika vijiji vyote na mkandarasi yupo kwenye hatua ya kuagiza vifaa vinavyotoka nje ya nchi na vifaa vya ndani ya nchi waya peke yake ndio umeshafanyiwa ukaguzi kiwandani. Mpaka sasa kijiji cha **Kiyaha** kilichopo kata ya Matili kimewashiwa umeme na tayari wateja wa awali wameunganishwa na huduma.

#### 13.4.13 Taarifa ya Utekelezaji ya Mradi R3R2-LOT26 Mpaka TAR. 17/11/2021

- Namba ya mkataba: **AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 26**
- Eneo la utekelezaji: Wilaya za Namtumbo na Tunduru
- Mkandarasi: Whitecity Guangdong JV,
- Muda wa mkataba: Miezi 18
- Gharama za mradi: TZS 36,678,446,302.59 (VAT Inclusive)
- Muda wa kuanza: 15/07/2021
- Muda wa kumaliza: 14/01/2023
- Lengo la mradi: kupeleka umeme kwenye vijiji 99

### 13.4.14 Hatua za Utekelezaji wa Mradi Wilaya za Tunduru na Namtumbo

Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia 3.72% za Upeo wa mradi kadiri ya Mkataba
na kazi za ujenzi zinaendelea. Vifaa vinavyotoka nje ya nchi vinategemewa kufika mwezi Januari 2022.

#### 13.4.15 MAFANIKIO

i. Tumefanikiwa kufungua ofisi ndogo sita (6) katika wilaya za Mbinga (Litembo, Likwela na Maguu), Tunduru (Mbesa na Nakapanya), na wilaya ya Songea (Madaba) ili kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi.

ii. Kuunganishwa na Grid ya Taifa na kuongeza idadi ya watumiaji wa umeme waliounganishwa kupitia mradi huu mkubwa

iii. Tunaishukuru serikali kwa kutupatia gari kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya REA na kitengo cha dharula, haya ni mafanikio makubwa katika serikali yetu

#### 13.4.16 CHANGAMOTO

i. Madeni sugu ya Taasisi za serikali na watu binafsi.

ii. Uchomaji wa mashamba ambao unaathiri miundombinu ya shirika.

iii. Wigo mdogo (scope) wa miundombinu inayofadhiliwa na Selikari kupitia wakala wa umeme vijijin REA hivyo kupelekea kuwa na changamoto kubwa na maswali mengi wakati wa utekelezaji. (Mfano mradi wa Makambako – Songea. Na REA)

**Majadiliano**

Wajumbe walihoji juu ya kasi ndogo ya usambazaji wa umeme katika maeneo mengi nchini hususani katika Mkoa wa Ruvuma.

Wajumbe walielekeza kuwa TANESCO iendelee kuomba na kutenga fedha za kutosha ili kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme ili umeme ufike katika maeneo mengi.

### 13.5 Taarifa ya Maendeleo ya Uchumi wa Kanda ya Kusini Mashariki – Ruvuma (BOT).

#### 13.5.1 Mwenendo wa Uchumi

##### 13.5.1.1 Pato la Taifa

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu, uchumi wa Mkoa wa Ruvuma umeendelea kuimarika, ambapo Pato la Taifa (GDP) kwa bei za mwaka husika liliongezeka kutoka shilingi bilioni 3,147 mwaka 2014 hadi kufikia shilingi bilioni 5,624 mwaka 2020 (**Kielelezo Na. 1**). Ongezeko hili limechangiwa zaidi na uzalishaji katika

shughuli za kilimo na madini. Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 3.8 ya Pato la Taifa ukichukua nafasi ya kumi kati ya Mikoa 26 ya Tanzania Bara katika kuchangia kwenye Pato la Taifa. Pia, Mkoa wa Ruvuma uliongoza katika kuchangia kwenye Pato la Taifa ikilinganishwa na Mikoa mingine ya Kanda ya Kusini Mashariki ya Lindi, Mtwara na Pwani.

Wastani wa pato kwa mtu (*GDP per capita*) katika mkoa wa Ruvuma umeendelea kuongezeka na kuwa juu ya wastani wa pato kwa mtu kitaifa (**Kielelezo Na. 2**). Wastani wa pato kwa mtu kwa mwaka kwa mkoa wa Ruvuma liliongezeka kutoka shilingi 2,195,638 mwaka 2014 hadi kufikia shilingi 3,396,983 mwaka 2020, ikilinganishwa na wastani wa pato kwa mtu kitaifa la shilingi 2,653,790 kwa mwaka.

#### 13.5.1.2 Mfumuko wa Bei

Katika mwaka 2020/21, mfumuko wa bei wa mkoa wa Ruvuma ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.2, ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka ulitangulia. Mfumuko huo uliendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 2.1 katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2021. Pia, mfumuko huo wa bei ulikuwa chini ikilinganishwa na kipindi cha Julai hadi Septemba 2020 (**Kielelezo Na 3**). Aidha, mfumuko wa bei za vyakula uliopungua kutoka wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2020/21na hadi asilimia 2.7 katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2021. Hali hii ilisababishwa na kuimarika kwa ugavi wa chakula na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2020/21.Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula uliongezeka hadi kufikia wastani asilimia 3.1 katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2021, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.8 mwaka 2020/21.

#### 13.5.1.3 Bei za Mazao ya Chakula

Kwa ujumla, bei za jumla za mazao makuu ya chakula (*staple foods*) katika mkoa wa Ruvuma zilishuka katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2021, ikilinganishwa na bei za mwaka 2020/21 na katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2020

isipokuwa bei za viazi mviringo na ulezi Kushuka kwa bei kulitokana na kuimarika kwa ugavi wa vyakula, pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao husika ikilinganishwa na msimu wa kilimo uliotangulia. Bei ya mahindi kwa mfano ilishuka hadi wastani wa shilingi 30,386 kwa gunia la kilo 100 katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2021 kutoka shilingi 45,983 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. Halikadhalika, bei ya mchele kwa gunia la kilo 100 ilipungua kutoka shilingi 176,275 hadi shilingi 166,408, na bei ya maharage kutoka shilingi 184,943 hadi shilingi 154,697.

#### 13.5.1.4 Shughuli za Kiuchumi

##### 13.5.1.5.1 Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2020/21, tani 1,341,740 za mazao ya chakula zilizalishwa katika mkoa wa Ruvuma, kati ya hizo mazao ya nafaka yalikuwa tani 998,550 na mazao yasiyo nafaki, tani 343,190. Kiasi kilichozalishwa kilizidi uzalishaji wa mwaka uliotangulia kwa tani 90,229, na mahitaji ya mwaka 2021/22 kwa tani 783,312, ikiwa ni sawa na kiwango cha utoshelevu wa chakula (*Self-Sufficiency Ratio, SSR*) cha asilimia 240.3 Ziada ya chakula ilijitokeza zaidi kwenye uzalishaji wa mazao ya nafaka yaliyokuwa na ziada ya tani 603,483, ikilinganishwa na mazao yasiyo nafaka yaliyokuwa na ziada ya tani 179,829.

Mkoa wa Ruvuma ndio unaozalisha mazao ya nafaka kwa wingi zaidi ikilinganishwa na mikoa mingine ya Kanda ya Kusini Mashariki ya Lindi, Mtwara na Pwani. Kwa upande wa mazao yasiyo nafaka, mkoa wa Ruvuma ni wa tatu katika Kanda kwa kuzalisha mhogo kwa wingi baada ya mkoa wa Pwani na Mtwara. Aidha, Mkoa wa Ruvuma unaongoza katika kuzalisha wa maharage, ndizi na viazi vitamu.

### 13.5.1.5.2 Hifadhi ya Taifa ya Chakula

Katika mwaka 2020/21, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Songea ilinunua tani 14,299.8 za mahindi kutoka kwa wakulima na kuhamisha tani

2,941.1 kwenda katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Makambako. Hali hii ilisababisha hifadhi ya mahindi katika Kanda ya Songea kuongezeka hadi kufikia tani 21,063.9 mwishoni mwa mwaka 2020/21 kutoka tani 9,705.1 mwaka uliotangulia (**Jedwali Na. 5**). Hata hivyo, uwezo wa kuhifadhi mazao katika Kanda ya Songea unatarajia kuongezeka kutoka tani 29,000 hadi tani 84,000 mara tu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa vihenge (silos) 12 na maghala mawili ya kisasa ya kuhifadhia mazao. Mradi wa ujenzi wa vihenge na maghala unaendelea na hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2021, ujenzi wa vihenge 10 ulikuwa umekamilika.

#### 13.5.1.5.3 Ununuzi wa Mazao ya Biashara

Mazao ya biashara yanayozalishwa katika mkoa wa Ruvuma ni pamoja na korosho, ufuta, kahawa na tumbaku. Mkoa huu huzalisha takriban asilimia 10 ya korosho yote inayozalishwa nchini. Katika mwaka 2020/21 kiasi cha tani 208,686.1 za korosho kiliuzwa kwenye minada na soko la awali, ambapo mkoa wa Ruvumaulichangia asilimia 7.4 (au tani 15,342). Aidha, kiasi cha tani 214,915 cha korosho ghafi kiliuzwa nje ya nchi mwaka 2020/21, na kuipatia nchi dola za Kimarekani milioni 233.5, Zao la korosho ndilo linaloongoza katika kuipatia nchi fedha za kigeni.

Kwa upande wa uzalishaji wa zao la ufuta, Mkoa wa Ruvuma huchangia kati ya asilimia 7 na 12 ya ufuta unaozalishwa katika Kanda ya Kusini Mashariki. Katika mwaka 2020/21, ununuzi wa ufuta ulikuwa tani 78,444.3, huku mkoa wa Ruvuma ukichangia tani 6,107.4. Katika mwaka 2020/21, tani 12,476.7 za kahawa na tani 531.8 ya tumbaku ziliuzwa katika minada, ikiwa ni sawa na wastani wa asilimia 20 ya kahawa na asilimia 1.6 ya tumbaku yote iliyouzwa nchini katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

#### 13.5.1.6 Mifugo

Katika mwaka 2020/21, thamani ya mifugo (hususan ngombe, mbuzi na kondoo) iliyouzwa katika masoko yaliyosajiliwa iliongezeka kwa asilimia 63.9 hadi shilingi billioni 88.6, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 27.7 ya thamani ya mifugo yote iliyouzwa, baada ya mkoa wa Pwani uliochangia asilimia 49.8.

#### 13.5.1.7 Uvuvi

Thamani ya samaki waliouzwa katika masoko yaliyosajiliwa katika Kanda ya Kusini Mashariki iliongezeka kwa asilimia 42.6 hadi kufikia shilingi bilioni 66.4 mwaka 2020/21, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, huku Mkoa wa Ruvuma ukichangia asilimia 3.3, baada ya mkoa wa Pwani uliochangia asilimia 82.1, na mkoa wa Lindi, asilimia 12.4 (**Jedwali Na 10**). Hata hivyo, sekta ya uvuvi imeendelea kukumbwa na changamoto kadhaa zikiwemo uvuvi haramu, ukosefu wa vitendeakazi bora vya kuvua samaki kwenye kina kirefu cha bahari, pamoja na kutokuwepo kwa viwanda vya kuchakata samaki ili kuongeza thamani.

#### 13.5.1.8 Misitu

Katika mwaka 2020/21, sekta ndogo ya misitu ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 19.7 katika Kanda ya Kusini Mashariki ikilinganishwa na shilingi bilioni 16.2 mwaka uliotangulia, sawa na ongezeko la asilimia 21.6. Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 5.9 ya mapato yote, baada ya mkoa wa Mtwara uliochangia asilimia 9.1, mkoa wa Lindi, asilimia 15.6, na mkoa wa Pwani, asilimia 69.5. Mapato haya yalitokana zaidi na kuongezeka kwa mahitaji ya mkaa, magogo na nguzo. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji ya magogo katika viwanda vinavyotumia malighafi ya misitu, na mahitaji ya matumizi ya mkaa katika kaya.

#### 13.5.1.9 Madini

Katika miaka ya hivi karibuni, sekta ya madini imeendelea kuimarika katika Kanda ya Kusini Mashariki, ikichangiwa zaidi na uanzishwaji wa masoko ya madini ya mikoa. Masoko haya yanaongeza uwazi, mazingira wezeshi ya biashara, na upatikanaji wa soko la uhakika la madini hasa kwa wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu na vito. Thamani ya madini yaliyochimbwa katika Kanda ya Kusini Mashariki iliongezeka kwa asilimia 16.1 mwaka 2020/21 na kufikia shilingi bilioni 555.2, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 42.8ya thamani na asilimia 38.3ya mapato yote. Uchimbaji wa makaa ya mawe unaongoza kwa kuchangia asilimia 95.8 thamani ya madini.

#### 13.5.1.10 Biashara ya Mipakani

Biashara baina ya nchi jirani na mikoa ya Kanda ya Kusini Mashariki (*cross border trade*) imeendelea kuimarika. Katika mwaka 2020/21, Kanda ilikuwa na ziada ya biashara (*trade surplus*) ya shilingi milioni 5,095.5, sawa na ongezeko la asilimia 70.5 (**Jedwali Na. 13**). Kuongezeka kwa ziada katika biashara kulitokana na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa nje ya mipaka hususan saruji, juice na unga wa mahindi, pamoja na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa nje hasa mbao na mafuta ya kupikia. Kwa ujumla, bidhaa ziliuzwa zaidi kwenye nchi ya Msumbiji (asilimia 77.9), ikifuatiwa na Comoro na Malawi. Aidha, asilimia 6.6 ya thamani ya bidhaa zote zilipita katika mipaka ya Mbambabay na Mkenda katika mkoa wa Ruvuma, wakati Bandari ya Mtwara, na mipaka ya Mtambaswala na Kilambo katika mkoa wa Mtwara zilichangia asilimia 93.4 ya thamani ya bidhaa zote.

#### 13.5.1.11 Matarajio na Mapendekezo

##### 13.5.1.11.1 Matarajio

Uchumi wa Mkoa na Ruvuma na wa Kanda ya Kusini Mashariki kwa ujumla unatarajiwa kuendelea kuimarika katika siku zijazo kutokana na kuendelea kutekelezwa kwa miradi mbali mbali ya maendeleo, kuongezeka kwa uzalishaji katika shughuli za kiuchumi

hususan kilimo, viwanda, ujenzi, madini, umeme na gesi asilia. Aidha, mfumuko wa bei unatarajia kuwa tulivu ukichangiwa na uwepo wa ziada ya chakula iliyopatikana katika msimu wa kilimo wa mwaka 2020/21, pamoja na usambazaji wa chakula kutoka katika mikoa mingine nchini. Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa maghala ya kisasa (*silos*) katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Songea kutaongeza uwezo wa Wakala wa kuhifanya mahindi zaidi na hivyo kuhakikisha kuwepo kwa usalama wa hali ya chakula katika ukanda wa kusini mwa Tanzania na nchikwa ujumla.

**13.5.1.11.2 Mapendekezo**

Ili uchumi wa mkoa wa Ruvuma uendelee kuimarika, tunatoa mapendekezo yafuatayo:

i. Mkoa unashauriwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili kukusanya takwimu za shughuli za kiuchumi katika kila halmashauri. Hii itasaidia mkoa kujua picha halisi ya uchumi wa mkoa na pato la mwananchi mmoja mmoja. Pia itawezesha mkoa kuainisha shughuli za kiuchumi zinazotakiwa kuwekewa mkazo zaidi. Chapisho la pato la kila halmashauri na mkoa linaloanisha mchango wa shughuli mbalimbali za kiuchumi lilichapishwa mara ya mwisho mwaka 2010 likionyesha takwimu za mwaka 2001, 2005 na 2006.

ii. Kwa kuwa mkoa wa Ruvuma unazalisha kiasi kikubwa cha mazao ya nafaka ikilinganishwa na mahitaji, ipo fursa ya kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya nafaka ili kuongeza thamani ya mazao hayo, na kuongeza kipato cha mkulima.

iii. Kwa kuwa mahitaji ya mafuta ya kupikia ni makubwa ikilinganishwa na uzalishaji hapa nchini, mkoa unashauriwa kuhamasisha wakulima kuzalisha alizeti ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kupikia na hivyo kukabiliana na tatizo la upungufu wa mafuta ya kupikia katika mkoa na nchi kwa ujumla.

iv. Kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo kama vile ngozi na maziwa ili kuongeza thamani ya mazao ya mifugo ili kuongeza tija kwa wafugaji.

v. Asilimia kubwa ya korosho inayozalishwa nchini inauzwa nje ya nchi bila ya kuongezewa thamani, ipo haja ya kuendelea kuhamasisha ubanguaji wa korosho inayozalishwa katika mkoa wa Ruvuma ili kuongeza thamani, ajira na mapato ya serikali. Aidha, kwa kuwa zao la korosho linaongoza kwa kuipatia nchi fedha za kigeni, upo umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

vi. Mkoa unashauriwa kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa madini hasa dhahabu na vito ili kutumia fursa zitokanazo na uwepo wa masoko ya madini katika mkoa. Hali hii pia itasaidia kuongeza mapato ya serikali yatokanayo na uuzaji wa madini hayo.

vii. Mkoa pia unashauriwa kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika mkoa ili kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo na kuongeza idadi ya watalii, mapato na ajira.

**Majadiliano.**

Wajumbe walihoji kuhusu uhalisia wa takwimu mbalimbali zinazokusanywa na BOT.kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo katika Taifa.

Kikao kilielekeza kuwa Mkoa kupitia Halmashauri zake ushirikiane na Ofisi ya Takwimu ya Taifa ili kuwa na Takwimu sahihi kwani zinazotumika sasa ni za zamani sana na hazina uhalisia.

## 13.6 Wakala wa Misitu (TFS) Maombi ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali hifadhi za vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Madaba

### 13.6.1 Maombi ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali hifadhi za vijiji vya Halmashauri ya Songea na Madaba

Wilaya ya Songea ina Hifadhi za vijiji saba na mmoja ya Halmashauri ya Madaba ambazo zilitengwa, kupimwa na kupitishwa kuwa Hifadhi na mikutano ya vijiji na baadae na baraza la Madiwani na kupitishwa kuwa Hifadhi kwa mujibu wa sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002 kifungu cha 32.

**Hifadhi za Halmashuri ya Madaba ni kama ifuatavyo: -**

i) Hifadhi ya Misitu ya kijiji cha Mkongotema (340 ha)
ii) Hifadhi ya Misitu ya kijiji cha Wino (2006 ha)
iii) Hifadhi ya Misitu ya kijiji cha Ifinga (31,684.5 ha)
iv) Hifadhi ya Misitu ya Halmashauri ya Madaba (518 ha)

v) Hifadhi ya Wanyamapori ya kijiji cha Ifinga (37,207 ha)

**Hifadhi za Halmashauri ya Songea ni kama Ifuatavyo: -**

i)Hifadhi ya Misitu ya kijiji ya Mitumbati (7,697.75 ha)

ii)Hifadhi ya Misitu ya kijiji ya Lihiga (4,940.56 ha)

iii)Hifadhi ya Misitu ya kijiji cha Lupagaro (5,262.0 ha)

Kutangazwa kwa Hifadhi hizi kwenye gazeti la serikali kutaimarisha ulinzi wa kisheria na kuzuia uvamizi wa maeneo hayo na badala yake kutaimarisha uhifadhi wa miti ya asili, wanyamapori, vyanzo vya maji na udongo. Hifadhi hizi zitatumika kufuga nyuki na Kupanda miti maeneo ambayo hayana miti ya asili.

Baada ya taarifa kuwasilishwa, Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa **(RCC) cha tarehe 29/12/2021** kilipokea taarifa na maombi ya Wakala wa Misitu ya kutangaza kwenye gazeti la serikali kama ilivyo ombwa. Wajumbe walipokea maombi hayo na kuazimia yafuatayo: -

**Kuhusu kijiji cha Ifinga kumilika sehemu ya eneo la hifadhi ya wanyapori.**

Wajumbe wameazimia Mkoa kutoa ombi maalum kwa Wizara ya Maliasili na Utalii la kuomba sehemu ya eneo la hifadhi ya Wanyamapori katika kijiji cha Ifinga limilikiwe na Kijiji.

**Kuhusu kutangazwa kwa hifadhi katika gaeti la Serikali.**

Wajumbe wameazimia Mkoa kufanya maombi Wizara ya Maliasili na Utalii maombi ya Wakala kutangaza kwenye gazeti la Serikali hifadhi za vijiji vya Halmashauri ya Songea na Madaba kuwa hifadhi za misitu za vijiji.

## 13.8 Taarifa ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere

### 13.8.1 Taarifa Fupi ya Hifadhi Iliyowasilishwa katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Ruvuma

Hifadhi ya Taifa Nyerere ilitangazwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Namba 923 la tarehe 29.11.2019 ikiwa na ukubwa wa Kilomita za Mraba 30,893. Hifadhi hii ilitokana na kumegwa kutoka kwenye Pori la Akiba la Selous ambalo lilianzishwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Namba 275 la mwaka 1974 likiwa na ukubwa wa takribani Kilomita za mraba 50,000.

**13.8.2 Utendaji Kazi**

Mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali, uongozi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA ulihamishia watumishi na vitendea kazi tayari kukabidhiwa rasmi hifadhi ya Taifa Nyerere na mnamo mwezi March, 2020 makabidhiano yalikamilika na kuanza rasmi shughuli za usimamizi wa Hifadhi.

**Shughuli za awali zilizoanza ilikuwa ni pamoja na:-**

**13.8.3 Shughuli za Ulinzi**

Tangu kuanzishwa kwa Hifadhi hii, shughuli za ulinzi zimeendelea kuimarishwa kwa kuongeza askari na vifaa. Katika kipindi hicho tumefanikiwa kuzuia uhalifu kwa kuwakamata majangili na vifaa au silaha walizokuwa wakizitumia kufanyia ujangili na kuwafikisha watuhumiwa kwenye vyombo vya sheria.

Kazi ya utatuzi wa migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali/waharibifu imekuwa ikifanyika katika maeneo mbalimbali yanayopakana na hifadhi kwa ushirikiano na KDU na Halmashauri za Wilaya.Jumla ya matukio 388 yameripotiwa na kushughulikiwa.

**13.8.4 Utalii**

Shughuli za utalii zimekuwa zikiendelea upande wa Kaskazini mwa hifadhi hususani eneo la Matambwe ambalo tangu awali lilikuwa likitumika kupokea watalii. Hata hivyo mpango unaoandaliwa umeshaainisha maeneo mbalimbali ya uwekezaji ndani ya hifadhi na uboreshaji wa miundombinu ya kuwezesha shughuli za utalii kufanyika. Mpango wa kuendeleza maeneo ya utalii hasa kwa kanda za Msolwa, Ilonga, Likuyu Sekamaganga, Kalulu na Liwale iko mbioni kuanza ikiwa ni pamoja na ukarabati wa barababara, vivuko, viwanja vya ndege, ujenzi wa malango ya kupokea wageni na maeneo ya malazi kwa wageni.

### 13.8.5 Mahusiano ya Jamii

Idara ya mahusiano ya jamii kwa kushirikiana na TAWA na mashirika yasiyo ya kiserikali imekuwa ikiendelea na kazi za kuelimisha jamii kuhusu sheria na mambo mbalimbali ya hifadhi pamoja na uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi. Idara ya mahusiano ya jamii upande wa Nyerere kusini imetoa elimu ya uhifadhi katika ofisi za wakuu wa wilaya ya Namtumbo na Tunduru na kuutambulisha ujirani mwema pia ofisi za wakurugenzi wa wilaya zote mbili pamoja na idara zinazohusika na uhifadhi na idara za elimu.

### 13.8.7 Shughuli mbalimbali zilizofanywa na idara ya mahusiano ya jamii kanda ya kusini katika Wilaya za Namtumbo na Tunduru.

- Wilaya ya Namtumbo tumefanya mikutano katika kata tatu ambazo ni Likuyu, Kitanda na Mgombasi. Jumla ya vijiji nane vimefikiwa.

- wilaya ya Tunduru jumla ya kata nne zimefikiwa na mikutano ya hadhara imefanyika katika vijiji saba ambavyo ni Kalulu, Mbungulaji, Kajima, Kindamba, Jaribuni, Twendembele na Misyaje.

### 13.8.8 Ikolojia

Shughuli za ikolojia zimekuwa zikifanyika kwa kukusanya takwimu mbalimbali za hali ya hewa, maji, mimea, wanyama, kuratibu uchomaji wa mioto ya awali (early burning).

### 13.8.9 Changamoto

- Kuporomoka kwa shughuli za utalii kulikosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa uviko 19 ambapo idadi ya wageni na mapato yaliporomoka hivyo kusababisha shughuli nyingi za uhifadhi kutotekelezwa kwa kiwango kulichokusudiwa.

- Utofauti wa mpaka ulioainishwa kwenye tangazo la Serikali namba 923 la mwaka 2019 na uhalisia uwandani. Hali hii imelazimu hifadhi kuwasiliana na mamlaka husika na wadau wengine ili kwenda uwandani kuhakiki/kutafsiri (ground truthing) mpaka kwa kutumia nyaraka hizo kazi ambayo imeshaanza kwa mkoa wa Morogoro itaendelea kwenye maeneo mengine.

### 13.8.10 Hitimisho

Hifadhi inatoa rai kwa wadau wote kuchangamkia fursa zilizopo katika kuwekeza kwenye sekta ya utalii ndani na nje ya hifadhi hasa kwenye nyanja za ujenzi wa mahoteli, kambi za wageni, usafirishaji, biashara mbalimbali na huduma nyingine kwa wageni.

**Majadiliano.**

Baada ya kuwasilishwa wajumbe walijadili na kuipitisha.

### 13.9 Taarifa ya Shamba la Miti Mpepo

Shamba la Miti Mpepo ni miongoni mwa Mashamba 23 ya Miti yanayosimamiwa na kuhudumiwa na **Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS),** chini ya **Wizara ya Maliasili na Utalii**. Shamba hili lilianzishwa likiwa na ukubwa wa Hekta 2,017 Ha, kisha zikafika hekta 3,905ha ambazo zote zipo Wilayani Nyasa.Eneo la Shamba kwa sasa ni takribani hekta 20,905ha ambazo zipo Wilaya za Nyasa, Songea na Namtumbo.Pia Shamba limefanikiwa kupata eneo lenye jumla ya hekta 50,000 wilayani Tunduru kwa

ajili ya uanzishwaji wa Shamba jipya la Miti mara baada ya kukamilisha taratibu kadhaa za umilikishaji wa eneo hilo kisheria.

### 13.9.1 Fidia ya Ardhi na Mali za Wanachi

Shamba limelipa fidia jumla ya Tshs. 271,223,778.00 kwa wananchi 63 waliopisha mradi wa upandaji miti katika kata ya Mpepo kwa eneo la hekta 657.04 baada ya kufanyiwa uthamini na Mthamini Mkuu wa Serikali.

### 13.9.2 Utekelezaji Mipango Kazi ya Shamba

Shamba la Miti Mpepo hadi sasa limeshapanda jumla ya hekta 1840ha ambapo hekta 1240ha zimepandwa miti jamii ya Misindano(*Pines*) katika tarafa ya Mpepo wilayani nyasa na Liwilikitesa Wilayani Mbinga na hekta 400ha imepandwa miti jamii ya Misaji(Mitiki) katika pori la hifadhi ya Kipiki, Wilayani Namtumbo na 200ha zimepandwa misaji (teak) Liuli Wilaya ya Nyasa pia miundombinu ya bustani tayari imesimikwa kwa ajili ya uzalishaji wa miche aina ya misaji (teak).

Shamba lina bustani tatu mpepo,ndongosi na liuli yenye jumla ya miche 1,500,000 ikijumuisha miche aina ya misindano (pine) pamoja na misaji (teak).

### 13.9.3 Huduma za Jamii

Shamba la Miti Mpepo pia limekuwa likishiriki kikamilifu katika kuchangia huduma za kijamii kulingana na bajeti ya kila mwaka. Miongoni mwa michango ya Shamba kwa huduma za kijamii ni kama ifuatavyo:

i. Shamba linatoa ajira za kudumu na za muda takribani 3000 kwa mwaka

ii. Shamba toka mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 limefanikiwa kutoa bure jumla ya Miche ya Miti 294,847 (190,198 miche ya Misaji(Teak) na miche ya Misindano (Pines) 104,649) katika vijiji vya Kipiki, Mtetema, Kihurunga, Mpepo, Lunyele na Wilaya ya Mbinga

iii. Shamba pia linatoa elimu ya misitu kupitia kitengo chake cha Uenezi

iv. Shamba limechangia kuboresha miundombinu ya barabara katika kijiji cha Lusewa kwa kukwangua barabara yenye urefu wa kilomita 10 pamoja na kujenga Culverts kwenye maeneo muhimu yaliyokuwa hayapitiki kipindi cha masika.

v. Shamba limetoa mabomba ya maji jumla 33 katika Kijiji cha Mtetema (17) na shule ya sekondari Mpepo (16).

vi. Shamba limetoa mabati 60 kwaajili ya kijiji cha Mtetema.

vii. Shamba limetoa Saruji mifuko 60 kwaajili ya Shule ya Msingi Kihurunga.

viii. Shamba limetoa Viriba kilo 40 na mbegu za miti kilo 42 kwaajili ya vijiji vya Lunyele, Kihurunga, Mtetema, na Mpepo.

ix. Shamba limetoa bati 60 na rola za maji 11 kwa ajili ya shule ya sekondari ya Stella Manyanya na mifuko ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya mtendaji kijiji cha mpepo

### 13.9.4 Changamoto

1. Ubovu wa barabara kutoka Nyoni hadi Mpepo inayopitika kwa taabu hasa kipindi cha masika .

2. Ukosefu wa umeme Mpepo kwa ajili ya shughuli za kiofisi za kila siku.

**Majadiliano.**

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe kwa pamoja waliijadili na hatimaye kuipitisha.

### 13.10 Taarifa ya Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – LIKUYU Sekamaganga

Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) – Likuyu Sekamaganga kilianzishwa mwaka 1995 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii - Idara ya Wanyamapori na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani chini ya Shirika Lake la ufundi (GTZ).

#### 13.10.1 Malengo ya kuanzishwa kwa Chuo

Kutekeleza Sera ya wanyamapori inayosisitiza ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili.

#### 13.10.2 Mahali Chuo Kilipo

Chuo kipo umbali wa kilometa 110 kutoka Songea na Kilometa 40 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Namtumbo. Kipo jirani na maeneo muhimu kiuhifadhi ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kusini, Ushoroba Wa Selous Niassa na Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii - Mbarang'andu. Kilirithi mojawapo ya maeneo yaliyokuwa yakitumika kama kambi ya wakimbizi kutoka Msumbiji.

#### 13.10.3 Idadi ya Wanafunzi Waliopo Chuoni kwa Sasa

Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi takriban 200 wanaoendelea na mafunzo mbalimbali.

#### 13.10.4 Mafanikio

##### 13.10.4.1 Mafunzo

Tangu kuanzishwa kwake Chuo kimeshafanikiwa kutoa mafunzo kwa takriban wananchi 5000 katika kozi mbalimbali.

#### 13.10.4.2 Uboreshaji wa mafunzo na miundombinu

- Usajili wa Chuo katika Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)
- Uanzishaji wa kozi ya Astashahada ya awali ya wanaongoza watalii
- Uboreshaji wa majengo (Ujenzi wa maktaba na chumba cha kompyuta, ujenzi wa bwalo na jiko)
- Ununuzi wa basi kwa ajili ya mafunzo (Abiria 50)

#### 13.10.4.3 Kuimarisha ushirikiano

Ushirikiano kati wadau wa Chuo ikiwemo wadau wa Maendeleo (WWF, USAID/PROTECT, GIZ, Kfw, SECAD) umezidi kuimalika

### 13.10.5 Changamoto na Namna ya Kukabiliana Nazo

a. **Ukosefu wa umeme:** Kwa sasa Chuo kinatumia mfumo wa umeme jua ambao hautoshelezi kuendesha shughuli nyingine za kiofisi pamoja na jenereta ambapo ni gharama kubwa kujiendesha. Tunaomba Mkoa uangalie namna ya kusaidia Chuo na Taasisi nyingine kama TANAPA na Shule ya sekondari ya Selous ziingizwe kwenye mradi wa umeme wa REA unaoendelea kwa sasa katika kijiji cha Likuyu Sekamaganga.

b. **Ukosefu wa Maji**: Chuo kinatumia maji ya kisima yanayosukumwa kwa kutumia jenereta na mashine. Hali hii inafanya Chuo kitumie gharama kubwa sana na hasa kunapokuwa na wanafunzi wengi. Japokuwa mfumo wa maji tayari umeshafika Chuoni kupitia mradi wa maji unaoendelea katika kijiji cha Likuyu

Sekamaganga, lakini maji bado hayafiki Chuoni. Naomba Mkoa uangalie namna ya kusaidia ili Chuo kipate maji ya uhakika.

**13.10.6 Mipango ya Baadae**

Kuendelea kuboresha miundombinu na mafunzo kwa:

i) Kuanzisha kozi nyingine ikiwemo astashahada ya waongoza watalii na ufugaji nyuki

ii) Kukarabati majengo yaliyopo na kujenga mengine ikiwemo mabweni, madarasa na nyumba za watumishi

iii) Kuanzisha manzuki ya Chuo na mabwawa ya samaki kwa ajili ya mafunzo na kuongeza kipato cha Chuo

iv) Kujenga mabanda kwa ajili ya kulala wageni (Watalii)

**13.10.7 HITIMISHO**

Natoa shukrani za dhati kwa Uongozi wa Mkoa wa Ruvuma kwa ushirikiano wa hali ya juu ambao Chuo kinapata ili kukiwezesha kutekeleza majukumu yake. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa ushirikiano kwa Mkoa ili kuhakikisha dhana ya uhifadhi shirikishi inakuwa endelevu kwa manufaa ya jamii na Taifa kwa Ujumla.

**Majadiliano.**

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe kwa pamoja waliijadili na hatimaye kuipitisha.

**13.11 Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za programu ya kuboresha mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu (FORVAC) - Mkoa wa Ruvuma**

Program ya Kuboresha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu yaani FORVAC ni Programu inayotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Serikali ya Finland. programu inafanya kazi zake kwa ushirikiano na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na PO-RALG.

### 13.11.1 Maeneo ya Programu ya FORVAC Kitaifa

Programu ya FORVAC inafanya kazi katika Kanda 3, kwenye Mikoa ya Tanga, Dodoma, Manyara, Lindi na Ruvuma katika wilaya zifuatazo hapa chini: -

- TANGA (Handeni, Kilindi), DODOMA (Mpwapwa), MANYARA (H/W Kiteto), LINDI (Nachingwea, Ruangwa na Liwale), RUVUMA **(**H/W Songea, Mbinga, Nyasa, Namtumbo na Tunduru**)**

### 13.11.2 Lengo Kuu la Programu:

Kuongeza faida za Kiuchumi, Kijamii na Kimazingira kutokana na Usimamizi Endelevu wa Raslimali za Misitu

### 13.11.3 Shughuli Zilizotekelezwa na Programu kwa Kipindi cha Robo ya Kwanza ya 2021/22

i. Kuunda/kuuhisha kamati za maliasili za vijiji- (VNRCs) pamoja na kuzifundisha majukumu na Wajibu wa kamati za maliasili kwenye vijiji 38 kwenye Halmashauri tano (5) kwa mkoa wa Ruvuma
ii. Kuendelea kuaandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji kwenye vijiji 11 na kufanya jumla ya vijiji 21 ambavyo mipango yake imeandaliwa na kupitishwa na kuthibitishwa kwa hatua mbali mbali kuanzia ngazi ya Vijiji hadi Taifa.
iii. Kuendelea kutenga maeneo ya Hifadhi ya Misitu ya Vijiji - (VLFRs) yenye ukubwa wa eneo la hekta 114, 357 kwenye vijiji 38 vya programu.(Kiambatanisho Na. 1)

iv. Kuwezesha vikundi vya wapandaji wa miti kwenye vijiji vinne vya Liuli, Lipingo, Mkali A na Mkali B kwenye wilaya ya Nyasa kupanda jumla ya hekta 270 za miti ya miti na kufanya jumla ya hekta 408 za mitiki zilizokwishapandwa (Kiambatanisho Na. 2).

v. Kutoa mafunzo ya kudhibiti moto wa msitu na uhifadhi wa mazingira kwa kamati za maliasili za vijiji kwenye vijiji 38 vilivyoko kwenye Programu.

vi. Kusaidia vitendea kazi kama vile mashine moja ya kuchakatia magogo (Mobile Saw mill) inayomilikiwa na vijiji 9; kwa wilaya ya Songea vijiji vitano (5) na wilaya ya Namtumbo vijiji vinne (4). Pikipiki Saba (7) aina ya Yamaha na kufanya jumla ya Pikipiki 15 zilizotolewa na Programu kusaida shughuli za uhifadhi. Kugawa mavazi maalum na Viatu kwa kamati za Nane (8) za Maliasili za vijiji kwenye Halmashauri za Songea (4), Tunduru (3) na Namtumbo (1).

vii. Kuandaa na kuwezesha mafundi seremala 18 kutoka vijiji sita vya Programu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kuhudhuria mafunzo ya utengenezaji wa mizinga ya kisasa ya kufugia nyuki.

viii. Kuandaa mipango ya Uvunaji endelevu wa mbao kwenye misitu minane (8) ya vijiji kwenye Halmashauri za wilaya za Songea (4), Tunduru (3) na Namtumbo (1).

ix. Kuandaa Machapisho na Makala mbalimbali zinazoelea shughuli za Programu.

### 13.11.5 Shughuli/Kazi Kuu Zitakazowezeshwa na Programu kwa Mwaka wa 2021/2022

a) Kuboreka kwa mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye sekta ya misitu

- Kuhakiki mipaka ya vijiji na kuandaa Cheti cha Ardhi ya Kijiji kwenye vijiji vinne vya wilaya ya Namtumbo

- Kuandaa Mipango ya Usimamizi na Uvunaji Endelevu kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji sita kwenye wilaya za Tunduru (2), Namtumbo (2) na Songea (2).

- Kuboresha mnyororo wa thamani mazao misitu kwa kununua mashine moja ya msumeno inayohamishika ya kuchakata magogo na mtambo wa kukaushia mbao kwa kutumia nishati ya jua.

- Kuwezesha Kamati za maliasili kufanya Doria kwenye misitu 38 ya Hifadhi ya Vijiji na Watalaam wa Halmashauri kutoa huduma za ugani kwa kununua vitendea kazi kama pikipiki na mavazi rasmi kwa ajili ya kufanya doria,

- Kuwezesha Halmashauri za Wilaya kuanzisha ushirika wa Wafugaji wa nyuki katika wilaya tano za mkoa wa Ruvuma ambazo ni Tunduru, Namtumbo, Songea, Mbinga na Nyasa.

- Kuwezesha wananchi wa vijiji vitano vya Liuli, Lipingo, Mkali A, Mkali B na Nkalachi kuendelea na shughuli za upandaji miti ya misaji/mitiki kwenye eneo la ukubwa wa Hekta 100.

b) Kuongezeka kwa uwezo wa wadau katika kuhamasisha na kuendeleza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu

- Kujenga uwezo wa Serikali za vijiji na Kamati za Maliasili kwenye usimamizi shirikishi wa raslimali za misitu na kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu

- Kuwezesha ziara za mafunzo kwa jamii na watalaam wa wilaya kwenye maeneo yaliyofanikiwa kupitia sekta ya usimamizi shirikishi wa misitu nchini

- Kuwezesha jamii na Watalaam wa Wilaya kushiriki makongamano ya Kisayansi yanayohusu mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na nyuki

- Kuwezesha semina kwa wana habari za Uhifadhi wa mazingira ili kuwajengea uwezo wa kuandika habari juu ya Uhifadhi wa misitu na mazingira

c) Uwepo kwa mfumo mathubuti wa huduma za Ugani, Mawasiliano na Ufuatialiji wa shughuli za Programu

- Kuwezesha jamii wanufaika wa programu na Wataam wa Halmashauri za Wilaya kushiriki maonyesho ya wajasiriamali Kimkoa, kikanda na Kitaifa kwa nia ya kujifunza na fursa ya kutangaza bidhaa za mazao ya misitu wanazozizalisha
- Kuboresha huduma za Ugani na Mawasiliano katika sekta ya misitu

d) Uwepo wa sera na sheria wezeshi za kuendeleza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na usimamizi endelevu wa misitu

- Kuboresha Sera na Sheria za kuendeleza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu
- Utekezaji wa sheria za misitu, utawala na biashara ya mazao mbao zilizovunwa kwenye misitu iliyohalarishwa kuvunwa

**13.11.6 Shughuli Mtambuka**

Haki sawa katika kutekeleza mradi ukizingatia:

Uwazi & Uwajibikaji (utawala bora), kujituma na kupata matokeo, Kuwa na uwazi na shirikishi, Kuhusisha makundi yote katika jamii na hata wasiojiweza, Haki ya kushiriki katika utoaji wa maamuzi, utumiaji na kugawanaji faida kutokana na maliasili ya misitu sawa (Right to participate in decision making, utilisation and benefit sharing of forest resources), Wananchi ndiyo wenye haki na wajibu wa kubeba majukumu ya kusimamia maliasili (Rights holders & Duty bearers), Kuhamasisha wanawake kushiriki katika mafunzo ya kuongeza ujuzi wa biashara na shughuli za kuongeza kipato etc, Kuzingatia usawa kwa jinsi zote,Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia mbinu stahiki.

### 13.11.7 Changamoto Zilijitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Programu

- Uhaba wa vitendea kazi mfano magari hasa kwa ngazi za Halmashauri kwa ajili ya usafiri wa wafanyakazi wa Halmashauri(PLUM Team) wanapoenda kutekelezaji shughuli za pogramu
- Kutofautiana kwa Ramani za Upimaji (survey plans) na hali halisi ya mipaka ya vijiji, hali hii husababisha migogoro ya ardhi.
- Uchomaji wa moto ovyo ambapo husababisha uharibifu wa misitu na wakati mwingine kupelekea kuungua kwa viumbe hai ndani ya misitu
- Uharibifu wa misitu ya vijiji unaofanywa hasa na wafugaji kwa kuingiza mifugo kwenye la misitu ya Hifadhi.
- Mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 ulipelekea kuchelewa katika kutekeleza baadhi ya shughuli za program

**Majadiliano.**

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe kwa pamoja waliijadili na hatimaye kuipitisha.

## 13.12 Taarifa ya utekelezaji wa Shughuli za Ardhi Mkoa wa Ruvuma.

#### 13.12.1 Kazi Zinazofanyika Tangu Kuanzishwa kwa Ofisi

Tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Ardhi Mkoa, Ofisi imesimamia na kutekeleza kazi za upangaji, upimaji, umilikishaji, uthamini, usajili wa Hati na nyaraka mbalimbali, utatuzi wa migogoro ya Ardhi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

#### 13.12.2 Upimaji wa Viwanja na Mashamba

Katika kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi tarehe 15 Novemba 2021, jumla ya viwanja **16,463** na mashamba **07** yamepimwa katika maeneo ya mijini na vijijini kwa ajili ya makazi na matumizi mengine.

### 13.12.3 Umilikishwaji Ardhi na Usajili wa Hati

Katika mwaka wa Fedha 2020 / 2021, Mkoa wa Ruvuma ulipangiwa lengo la kuandaa na kusajili Hati miliki 1,000 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, jumla ya **Hati miliki 857 zimeandaliwa na kusajiliwa** sawa na asilimia **85.7** ya lengo. Aidha jumla ya miamala **701** ikiwemo ya rehani na uhamisho wa milki imesajiliwa.

Aidha katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mkoa umepangiwa kuandaa na kusajili Hati miliki 2,000 na miamala 2,000. Hadi kufikia tarehe 15 Novemba 2021, jumla ya Hati miliki 397 sawa na asilimia 20 zimeandaliwa na kusajiliwa. Aidha katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi tarehe 15 Novemba 2021 (kwa mwaka wa fedha 2021/2022) jumla ya miamala 369 sawa na asilimia 19 ikiwemo ya rehani na uhamisho wa milki imesajiliwa.

### 13.12.4 Mipango Miji na Vijiji

Jumla ya michoro **43** yenye jumla ya viwanja **19,445** vya matumizi mbalimbali kutoka Mamlaka za upangaji imepokelewa, kukaguliwa na kuidhinishwa.

### 13.12.5 Urasimishaji wa Makazi holela Mjini

Katika kipindi hiki, jumla ya viwanja **9,505** vimerasimishwa katika baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma kwa gharama ya Tshs **115,200,000**.

### 13.12.6 Mipango Kabambe ya Miji (Master Plan)

Mkoa wa Ruvuma una miji minne (04) iliyoandaliwa Mipango Kabambe ya kuongoza uendelezaji Miji (Master Plan/Interim Land use Plan). Miji hiyo ni Manispaa ya Songea, Tunduru, Namtumbo na Mbinga Mji. Mipango hii hata hivyo ilishapitwa na wakati isipokuwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea pekee ambayo imefanikiwa

kuandaa Mpango Kabambe (Songea Master Plan 2017-2037) ambao uliidhinishwa tarehe 15/10/2019 na kuzinduliwa na Mhe. William V. Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tarehe 10/08/2020. Hata hivyo, Katika kipindi hiki, Halmashauri ya Mji wa Mbinga na Wilaya ya Tunduru zimeanza maandalizi ya awali kuandaa Mpango Kabambe (Master Plan) kwa ajili ya kuongoza matumizi ya Ardhi katika makao makuu ya Halmashauri hizo kwa kipindi cha miaka 20 ijayo. Tayari uandaaji wa Andiko la Mradi kwa ajili ya kupata fedha za kuandaa Mpango Kabambe kwa ajili ya Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru limekamilika.

### 13.12.7 Uthamini

Katika Kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi tarehe 15 Novemba 2021, taarifa za Uthamini 242 za madhumuni mbalimbali zenye thamani ya Tshs. 37,929,860,000/=

### 13.12.8 Migogoro ya Ardhi

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma imekuwa ikipokea malalamiko yanayohusu mipaka ya Vijiji, mipaka ya vijiji na maeneo kwa ajili ya shughuli za Uhifadhi, migogoro ya wawekezaji na Vijiji yalipo maeneo ya wawekezaji hao, migogoro inayotokana na ucheleweshwaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi na migogoro kati ya wamiliki wa ardhi na Halmashauri zetu.

Mojawapo ya mgogoro mkubwa ambao Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imefanikiwa kushiriki kuumaliza kwa kushirikiana na Ofisi za Kanda ya Kusini za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Namtumbo na Wilaya ya Songea ambao usuluhishi wake ulifanyika mwezi Agosti, 2019. Migogoro mingine kama vile mgogoro kati ya pori la akiba la Liparamba na Vijiji vya Mseto, Liparamba, Mitomoni na Konganywita, kazi ya kutafsiri mipaka ya hifadhi imeanza.

Pia, mgogoro kati ya wananchi wa vijiji vya Liuli, Mkali A, Mango, Songambele na Mkarachi tathimini ya maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa kwa ajili ya Mradi wa Panda miti kibiashara imefanyika ili kujua kila mwananchi anadai ardhi ya ukubwa gani.

### 13.12.9 Makusanyo ya Maduhuli Ya Serikali

Katika mwaka wa Fedha 2020 / 2021, Mkoa wa Ruvuma ulipangiwa lengo la kukusanya jumla ya **Tshs. 4,600,000,000.00** ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, jumla ya **Tshs. 1,234,718,406.31** zilikusanywa sawa na asilimia **27%** ya lengo.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mkoa umepangiwa kukusanya jumla ya Tshs. 3,000,000,000.00 Hadi kufikia tarehe 10 Octoba 2021, jumla ya Tshs. 590,828,759.32 zimekusanywa kutokana na Kodi ya pango la Ardhi na tozo mbalimbali za Ardhi sawa 20%

**Majadiliano.**

Wajumbe walihoji kuhusu utatuzi wa Mgogoro wa maeneo unaoendelea kati ya wananchi waliopo mpakani mwa Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Mbinga.Wajumbe waliekeleza kufanyike vikao vya maridhiano kupitia kikao kati ya Mkuu ya Mkuu wa Wilaya ya Nyasa na Mkuu wa Wilaya ya Mbinga.

## Taarifa ya Utendaji Kazi wa Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma - Wizara ya Mambo ya Ndani

### 13.13.1 Utangulizi

Idara ya Huduma za Uangalizi ni Idara ambayo ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo inasimamia na kuratibu utekelezaji wa Adhabu Mbadala ya Gereza kupitia Sheria ya Huduma kwa Jamii Na.6/2002, (The Community Service Act, No.6 of 2002) na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia Sura 247, Marejeo ya Mwaka 2002 (The Probation Act, CAP. 247 RE: 2002) ambapo mfungwa anatumikia

adhabu yake kwenye jamii kwa kufanya kazi za Kijamii katika ofisi ya serikali atakayopangiwa kwa **masaa manne (04) kwa siku kuanzia jumatatu hadi ijumaa**. Lengo ni kupunguza msomangano Magerezani, hivyo kuipunguzia serikali gharama za kuwahudumia wafungwa wakiwa gerezani.

Katika kipindi hicho tumefanikiwa kuingiza wafungwa **sitini na nne (64)** kwenye programu:

- Wanaume **arobaini na sita (46)**, mmoja kutoka gerezani na arobaini na tano kutoka mahakamani
- Wanawake **kumi na wanane (18)** wote kutoka mahakamani

### 13.13.2 Utekelezaji wa Kazi za Idara

Mpaka sasa katika utekelezaji wa kazi za Idara katika Mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kuzifikia Wilaya 2 za Songea na Mbinga katika utekelezaji wa kazi zake.

### 13.13.3 Usimamizi na ufuatiliaji wa wafungwa kwenye maeneo ya kazi/maeneo wanayoishi.

Kwa kipindi cha Disemba, 2020 mpaka Novemba, 2021 hakuna wafungwa waliokiuka masharti na kupewa onyo, waliorudishwa gerezani kwa kukiuka masharti, waliotoroka na kukamatwa waliofariki au wafungwa waliohama kwenda Wilaya nyingine.

Katika utekelezaji wa kazi wa Programu ya Huduma kwa Jamii, matokeo chanya yamepatikana kwa wafungwa baada ya kumaliza adhabu ambayo ni pamoja na

- Wafungwa kubadilika kitabia na kimatendo na hasa kutambua haki zao za kifungo cha nje,

- Familia zimeimarika watoto wamepata fursa ya kutunzwa na wazazi wote wawili na kupata huduma zote muhimu toka kwa wazazi wawili.

- Taasisi za serikali zimefanikiwa kupata wahudumu hivyo kupunguza gharama za uendeshaji katika taasisi hizo.

Kupitia utekelezaji wa Programu hii Serikali imeokoa kiasi cha Tsh. 23,625,000.00 kwa wafungwa 64 kufanya kazi za usafi wa mazingira kwenye Taasisi. Pia serikali imeokoa kiasi cha Tsh 16, 87500.00 za kuwahudumia wafungwa hao wakiwa gerezani.

#### 13.13.4 Uhamasishaji wa kuitangaza idara ya huduma za uangalizi mkoa wa ruvuma.

Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Huduma za Uangalizi kupitia Maafisa Probesheni walishiriki shughuli mbalilmbali ikiwemo kushiriki wiki ya SHERIA nchini, kuhudhuria Vikao vya Kusukuma Mashauri (CASE FLOW MANAGEMENT COMMITTEE) katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Ruvuma na Mahakama ya Wilaya ya Songea kwa nyakati tofauti. Ambapo tulipata nafasi ya kuwaeleza wajumbe wa vikao hivyo kuhusu Idara ya Huduma za Uangalizi pamoja na kazi zinazosimamiwa na Idara yetu. Miongoni mwa kazi hizo ni: -

i. Kuratibu na kusimamia kifungo mbadala wa gereza

ii. Kutoa ushauri nasaha kwa wafungwa na kuwaunganisha wafungwa na taasisi zinazotoa huduma hasa kwa wale wenye mahitaji maalumu, kukagua sehemu wanazofanyia kazi, kuwaunganisha wafungwa na familia zao pindi wanapomaliza vifungo vyao.

### 13.13.5 Matarajio.

Tunategemea kuendelea kuitangaza Idara yetu katika vyombo vya habari hasa redio zilizopo Mkoani Ruvuma. Pia kuzifikia Wilaya za Mkoa huu ambazo bado hatujazitembelea kwa lengo la kuitambulisha Idara yetu na kuongeza uelewa kwa jamii inayotuzunguka, vilevile kuongeza ufanisi wa kazi katika mkoa wetu.

#### 13.13.6 Changamoto

1. Uchache wa watumishi na hali ya Kijiografia ya Mkoa inasababisha kutowafikia wananchi kwa wakati katika kutoa Huduma ya Kifungo mbadala ya Gereza

2. Ushiriki mdogo wa Gereza la Songea katika kutekeleza program za adhabu mbadala licha ya kutoa elimu mara kadhaa gerezani hapo.

### 13.13.7 Mapendekezo

(i) Tunaiomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kutusaidia kuunganishwa na wadau wengine hasa Magereza ili kuweza kutekeleza program hii ya vifungo vya nje na kuwafikia watu wengi zaidi katika mkoa wa Ruvuma.

(ii) Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa ikishirikiana na wadau wengine itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa vifungo mbadala ya Gereza kupitia Sheria za Huduma kwa Jamii na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia.

### Majadiliano

Taarifa iliwasilishwa na kupitishwa na Wajumbe

## 13.13 Taarifa mapamabano dhidi ya rushwa (TAKUKURU) kwa maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma.

Mapambano dhidi ya rushwa yanaendelea kuwa ni agenda ya kudumu katika shughuli za mbio za mwenge wa Uhuru. Adhima hii inatokana na Rushwa kuendelea kuwa

kikwazo kikubwa katika maendeleo ya nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania kwani rushwa inadhuru uwezo wa mtu

#### 13.14.1 Uchunguzi na mashtaka.

Katika kipindi cha kutoka julai 2020 hadi kufikia Septemba 30, 2021 taarifa /malalamoko yaliyopokelewa yalikuwa ni **663** ambapo taarifa zote zilifanyiwa kazi, na kati ya taarifa hizo majalada yaliyofunguliwa kwa ajili ya kuchunguzwa ni **88** na majalada **39** kati ya hayo uchunguzi wake ulikamilika, kesi mpya **9** zilifunguliwa na zinaendelea mahakamani, Aidha uchunguzi kwa kipindi hicho ulihusu zaidi ubadhilifu kwenye manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato ya serikali na ubadhilifu wa fedha katika vyama vya ushirika.

#### 13.14.2 Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

Serikali kupitia TAKUKURU hapa mkoani Ruvuma imefanya kazi ya uchambuzi wa mifumo pamoja kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma kwenye miradi **54** yenye thamani ya shilingi **9,447,944,485.19** kazi hizo zilifanyika katika sekta za afya, elimu, barabara, maji ujenzi na miundombinu. Katika miradi hiyo iliyofuatiliwa/kaguliwa mradi miwili imefunguliwa majalada ya uchunguzi, na miradi iliyokuwa na kasoro ndogondogo kupitia vikao kazi pamoja na kuelimishwa, wahusika walishauriwa namna ya kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo ili ikamilike bila kuwa na mapungufu yoyote.

#### 13.14.3 Elimu kwa umma

TAKUKURU mkoa wa Ruvuma imeendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ambapo kwa kipindi hicho imeweza kuimarisha klabu **350** za wapinga Rushwa mashuleni, imetoa semina **198** kwa makundi mbalimbali, imefanya mikutano **177** ya hadhara kwa wananchi sehemu mbalimbali, imefanikiwa kufanya maoneshao **13,** kurusha vipindi **26** redioni na kuandaa Makala **24** za mapambano dhidi ya Rushwa.

**Majadiliano**

Taarifa iliwasilishwa na kupitishwa na Wajumbe

## 13.14 Taarifa ya Ewura – Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Kwenye Kikao cha RCC Ruvuma Desemba 2021.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inahudumuia Mikoa sita (6) ya Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Njombe na Ruvuma.

Majukumu ya Mamlaka yameainishwa katika Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania kuwa ni:

a) Kutoa leseni kwa watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa

b) Kupanga au kuidhinisha bei na tozo katika sekta zinazodhibitiwa

c) Kuweka viwango vya bidhaa na huduma kwa kushirikiana na TBS

d) Kusimamia utoaji huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo husika

e) Kuzingatia usalama na uhifadhi wa mazingira wakati wa kutoa huduma

f) Kuelimisha wananchi kuhusu masuala yanayodhibitiwa na Mamlaka.

g) Kutatua migogoro kati ya mtoa huduma na mpokea huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka.

### 13.15.1 Sekta ya Umeme

Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inasimamia shughuli ya Kiufundi na Kiuchumi katika Sekta ya Umeme katika Mikoa yote sita ya kanda hii. Katika Mkoa wa Ruvuma mtoa huduma mkubwa

wa nishati hiyo ni TANESCO na hufanyiwa ukaguzi wa kila mwaka kwa kuangalia kuwa anazingatia viwango vya kiufundi kwenye miundo mbinu yake na pia viwango vya utoaji huduma kwa wateja wake. Katika kutekeleza wajibu wake, EWURA inatoa leseni kwa mafundi umeme wa kazi mbalimbali. Kwa Mkoa wa Ruvuma kuna jumla ya mafundi umeme **35 wenye leseni.** Ila kuna jumla ya maombi **31** ya mafundi umeme ambao wanaomba kuhuisha leseni zao na mengine ni maombi mapya.

Pai, Ofisi ya EWURA kanda ya nyanda za juu kusini ilitoa semina kwa mafundi umeme 120 kutoka wilaya mbalimbali za Mkoa wa Ruvuma ambao waliohudhuria kwenye semina hiyo iliyofanyika mwezi Novemba 2021.

#### 13.15.1.1 CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA UMEME

Uwepo wa kundi kubwa la mafundu umeme (vishoka) ambao hawana vyeti vya kitaaluma vitakavyowawezesha kuomba leseni zinazotolewa na Mamlaka.

### 13.15.2 SEKTA YA MAFUTA YA PETROLI

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ina jumla ya Vituo vya Wauzaji mafuta wa rejareja (***Retail outlets***) 254 hadi kufikia Oktoba 2021. Idadi hiyo inajumuisha Watumiaji binafsi wa mafuta (***Consumer Installation***), Viwanda vidogo vya kujazia gesi ya kupikia majumbani (***LPG refilling***) na Wasambazaji wa gesi ya kupikia majumbani (***LPG distributors)*** na

Katika Mkoa wote wa Ruvuma, kuna vituo (facilities) **55** kama ifuatavyo:

a) Vituo vya Wauzaji mafuta wa rejareja (***Retail outlets***): **48**
b) Watumiaji binafsi (***Consumer installation***): **3**
c) Viwanda vigogo vya kujazia gesi ya majumbani (***LPG refilling***): **1**
d) Wasambazaji wa gesi ya kupikia majumbani (***LPG distributors***): **3**

Katika kipindi cha kuanzia Julai mpaka Oktoba 2021, EWURA ilifanya **ukaguzi wa kawaida** (**Compliance monitoring**) kwenye Mikoa ya Ruvuma na Mbeya na kukagua vituo17. Kati ya hivyo vituo 5 vya mkoa wa Ruvuma havikuweza kukutwa na makosa yoyote. Mbali na matokeo ya ukaguzi huo, pia kuna kampuni moja ilipewa adhabu ya

kulipa faini ya **TZS 1,000,000/=** kwa kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwa ajili ya matumizi yake bila kupata kibali kutoka EWURA.

Katika kanda pia kulifanyika ukaguzi kwa mwezi Julai 2021 kwenye vituo 114 kwa kuangalia vituo vinavyouza bidhaa ya mafuta kulingana na **bei elekezi** (cap price monitoring) na vituo vyote vilivyokaguliwa viliuza bidhaa zao kufikia / chini ya bei elekezi ikiwemo vituo vya Mkoa wa Ruvuma.Katika kipindi cha mwezi Julai mpaka Oktoba 2021 Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliweza kutoa leseni 24 zaa biashara ya mafuta na mazao yake ikiwemo LPG. Kati ya Leseni hizo 24 zilizotolewa, leseni tano (5) zilitolewa katika vituo vilivyopo Mkoa wa Ruvuma ambavyo. Vilevile EWURA ilitoa vibali 11 vya ujenzi wa vituo vya mafuta kati ha hivyo viwili vilitolewa katika mkoa wa Ruvuma.

#### 13.15.2.1 Changamoto katika Sekta ya Mafuta

Baadhi ya Vituo vya mafuta kujengwa bila kufuata utaratibu wa ujenzi na baadhi kutokidhi mahitaji ya leseni. Ushauri wetu ni kwamba Halmashauri / Manispaa husika ziangalie namna bora ya kushirikiana na EWURA na wadau wengine katika kuhakikisha ujenzi unakuwa na vibali husika (EWURA, NEMC na Manispaa/Halmashauri wanaotoa hati ya umiliki wa ardhi) kabla ya ujenzi kutekelezwa.

### 13.15.3 Sekta ya Maji

Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inasimamia Mamlaka za Maji 20. Katika sekta ya Maji kuna aina nne za ukaguzi.

- Ukaguzi maalum (**special inspection**) - kufuatilia utendaji mbovu wa Mamlaka,
- Ukaguzi wa kawaida wa utendaji wa Mamlaka (**compliance monitoring**) - ukaguzi unahusisha kuangalia miuodombinu, ikiwemo uunganishaji wa wateja wapya na ubora wa huduma kwa mteja),
- Ukaguzi wa kuhakiki taarifa za mamlaka (**data verification**) – unafanyika kama sehemu ya maandalizi ya kuandika Taarifa ya Utendaji wa Mamlama za Maji

- Ukaguzi wa ubora wa maji (**water quality monitoring**).

#### 13.15.3.1 Changamoto Sekta ya Maji

Uzalishaji wa Maji wa Mamlaka zote hizo Nne (4) ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya Maji kwa maeneo hayo, hususani wakati wa kiangazi. Pia, kuna tatizo la baadhi ya Mamlaka kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha ili kutoa huduma ipasavyo.

### 13.15.4 Usuluhishi wa Migogoro

EWURA pia inashughulikia malalamiko yanayohusiana na Sekta zote tunazozidhibiti. Miongoni mwa malalamiko ni bili za maji, kuuziwa mafuta yasio na ubora, malalamiko mbalimbali ya umeme, malalamiko ya bei za bidhaa na malalamiko ya huduma nk.

Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 mpaka Oktoba 2021, Ofisi ya EWURA ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilipokea jumla ya malalamiko **13**, kati ya hayo, sita (**6)** ni ya umeme, Lalamiko moja (**1)** ni la kuhusu maji na malalamiko sita (**6)** ni kuhusu Mafuta. Ofisi ya Kanda iliweza kuyapatia ufumbuzi malalamiko tisa (**9**), kati ya hayo manne (**4)** ni ya umeme na matano (**5)** ni ya Mafuta. Katika malalamiko manne (**4)** yaliyobakia, Lalamiko moja (1) liko kwenye ngazi ya kesi (**Hearing**) na malalamiko matatu (**3)** yanasubiri vikao vya muafaka au usuluhishi (**Mediation**).

Hivyo, tunaomba ushirikiano kwa wadu wote mliopo hapa kuwa na taarifa kwamba EWURA ndio inashughulikia malalamiko kati ya Mteja na Mtoa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA. Pale panapotokea malalamiko basi Wananchi waeleweshwe kwamba wayawasilishe EWURA kupitia fomu ya malalamiko inayopatikana katika ukurasa wa Mamlaka kupitia tovuti (www.ewura.go.tz) au kwa kufika Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliyopo Jijini Mbeya, Mtaa wa Karume kwenye jengo la NHIF, Ghorofa ya sita.

## Majadiliano.

Wajumbe walihoji kuhusu kutozwa gharama kubwa wananchi wanaowekeza miundombinu ya vituo vya mafuta vijijini, jambo ambalo linawakatisha tamaa wawekezaji, na kupelekea huduma ya upatikanaji wa mafuta vijijini kuendelea kuwa mbaya.

Wajumbe walielekeza kuwa sekta ya EWURA iangalie uwezekano wa kufanya marekebisho katika sheria na inayosimamia uwekezaji wa vituo vya mafuta vijijini na kuiwasilisha bungeni kama mswaada utakaojadiliwa na wabunge na hatimaye kuweza kuweka sheria na kanuni zitakazokuwa rafiki katika uwekezaji wa vituo vya mafuta Vijijini

### 13.16 Wakala wa vipimo Mkoa wa Ruvuma

#### 13.16.1 Maendeleo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wakala wa Vipimo

Jukumu kuu la taasisi ya Wakala wa Vipimo ni kumlinda mlaji katika sekta ya Biashara, Afya, Usalama na Mazingira. Kwa kutekeleza jukumu hilo, Taasisi ya Wakala wa Vipimo mkoa wa Ruvuma imeweza kufanya yafuatayo: -

#### 13.16.2 Uhakiki wa vipimo mbalimbali

**a) Ukaguzi wa mizani ya wafanya Biashara**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Tumeweza kukagua na kuhakiki Vipimo **11,377** Katika wilaya na Halmashauri zote za mkoa wa Ruvuma. Vipimo hivyo ni pamoja na **Mizani ya mezani, Mizani ya Mazao na Mizani ya kuninginiza**

**b) Ukaguzi wa Mizani ya Madini**

Katika sekta ya madini, jumla ya mizani **33** za wafanyabiashara wa madini imekaguliwa katika Masoko ya madini mkoa wa Ruvuma hususani Tunduru na Songea.

### c) Ukaguzi wa Mizani katika Sekta ya Afya

Katika Sekta ya Afya (Binafsi na Serikali), tumefanya ukaguzi wa mizani inayopima uzito wa wagonjwa mbalimbali katika zahanati, Vituo vya Afya pamoja hospitali.

### d) Ukaguzi wa mizani katika AMCOS na Watunza Maghala ya Kuhifadhia Mazao

Katika musimu wa mwaka 2021/2022 Taasisi imefanya ukaguzi wa mizani inayokusanya Ufuta, korosho ghafi na Kahawa kwa lengo la kuwalinda wakulima.

Aidha, mizani ya Watunza maghala na Vyama vikuu vya MCC CO.LTD na CMS TANZANIA LTD zilihakikiwa kabla ya kuanza msimu

### e) Ukaguzi wa Mizani ya Barabarani inayomilikiwa na TANROADS

Katika kuendelea kusimamia Sheria ya Wakala wa Vipimo sura ya 340 pamoja na kanuni zake Taasisi imeendelea kufanya ukaguzi na uhakiki wa Mizani mitatu (3) ya Barabarani (Weighbridge) inayomilikiwa na Tanroads kwa lengo la kuleta usawa kwa watumiaji wa barabara (TANROADS na Wasafirishaji)

Mizani hiyo ni Luhimba barabara ya Songea-Njombe, Lipokea barabara ya Songea Mbinga na Sisi kwa Sisi barabara ya Tunduru-Masasi. Kwa kushirikiana na TANROADS ukaguzi na upimaji unafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) kwa ajili ya kulinda ufanisi wake.

### f) Uhakiki wa pampu za kujazia mafuta kwenye Vituo Vya mafuta.

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2021, Jumla ya pampu za kujazia mafuta zipatazo **225** kwenye vituo **37** vinavyouza mafuta zilipimwa ili kubaini usahihi wake. Kati ya hizo Jumla ya pampu **206** zilikutwa zikiwa sahihi na pampu **19** zilifungwa kwa ajili ya marekebisho.

### g) Uhakiki wa Mita za maji

Taasisi ya Wakala wa Vipimo imeendelea kuhakikisha kwamba mita za maji wanazofungiwa wateja wa Mamlaka za maji ni sahihi na salama. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi desemba, 2021 jumla ya mita **1,600** zimehakikiwa na kufungwa lakiri ya Serikali tayari kwa matumizi.

#### 13.16.2.1 Uhakiki na Ukaguzi na Bidhaa Zilizofungashwa

Katika kuhakikisha kwamba mwananchi ananunua bidhaa sawa na thamani ya fedha yake, Taasisi imeweza kufanya ukaguzi wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu vilivyopo mkoa wa Ruvuma pamoja na bidhaa zilizoko sokoni ambazo zimefungashwa nje ya mkoa wetu ili kubaini ujazo na uzito wake.

#### 13.16.2.2 Ukaguzi wa Kushtukiza katika Maeneo Mablimbali

Katika dhana ya kalinda jamii kuepukana na madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya Vipimo katika Sekta ya Biashara, Usalama, Mazingira na Afya, taasisi inaendesha kaguzi za kushtukiza katika sekta mbalimbali pamoja na maeneo mbalimbali. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Decemba, 2021 Taasisi imefanya jumla ya Kaguzi za kushtukiza (Operations) **138** katika Halmashauri nane (8) za mkoa wa Ruvuma. Jumla ya wafanyabishara **57** walikutwa na makosa katika kada mbalimbali kama inavyoonyesha hapa chini: maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi.

### 13.16.3 Matumizi ya Vipimo Batili

i. **Mapambano juu ya Matumizi ya Vipimo batili**

Taasisi imeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ili kujenga uelewa juu ya madhara yanayoweza kutokea.

ii. **Madhara ya kutumia Vipimo Batili**

a) Kukiuka sheria ya vipimo

b) Kumpunja mlaji kwa kuuza chini ya kipimo

c) Kuua biashara kwa kuuza bidhaa zaidi ya kipimo

d) Kinyume na maandiko ya dini zetu

**iii. Ufungashaji Batili**

Taasisi ya Wakala wa Vipimo katika kupambana na Matumizi ya Vipimo Batili imekuwa ikifanya operation mbalimbali kwa lengo la kuzuia Lumbesa hususani mazao ya Shamba na majini. Lumbesa ni mzigo unaofungashwa zaidi ya uzito uliokubalika kisheria (uzito usiozidi kilogram 100 kwa kifungashio kimoja).

**Majadiliano**

Taarifa iliwasilishwa na kupitishwa na Wajumbe

## 14 MUHTASARI NA. RCC: 12/12/2021 TAARIFA MIHUTASARI YA KAMATI ZA USHAURI WILAYA (DCC)

Taarifa za Mihutasari ya Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) ziliwasilishwa Wilaya kwa Wilaya na Wajumbe wote kwa pamoja walipitisha taarifa hizo kwa pamoja kama zilivyowasilishwa.

## 15.0 MUHTASARI NA. RCC: 13/12/2021 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.

- Pamoja na kujadili mambo makubwa ya maendeleo ni muhimu pia kulipa kipumbele eneo la michezo ili kuinua vipaji vya vijana na kuwawezesha kujiajiri kwani michezo ni ajira. Kikao kilielekeza kuwa Halmashauri zinapotenga fedha katika bajeti zao wanapaswa kutenga fedha ili kuinua vipaji vya Vijana.
- Wajumbe walihoji kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa timu ya Majimaji, kuwa ni mbovu ndio maana timu inafanya vibaya katika michezo mbalimbali. Kikao kilielekeza kuwa timu ya Majimaji

iendeshwe kibiashara kama kampuni; ili ipatikane tija katika maendeleo ya timu, kwa kufanya hivyo itawezesha wachezaji kujituma na kutohamia katika timu nyingine kwa sababu ya mishahara midogo.

- Wajumbe walihoji kuhusu Mgogoro wa ardhi uliopo kati ya vijiji vilivyopo katika mpaka wa Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Mbinga. Mgogoro huu umedumu kwa muda mrefu sasa. Kikao kilielekeza kuwa Wakuu wa Wilaya mbili ya Nyasa na Mbinga wafanye kikao cha kutatua mgogoro wa ardhi. Na majibu ya yawasilishwe katika kikao kinachofuata cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).
- Wajumbe walihoji kuhusu kodi/tozo za matumizi ya maji anazotozwa Mwekezaji wa Kampuni ya Siliverland ni kubwa sana na inapelekea wawekezaji wasiende kuwekeza katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba. Kikao kilielekeza kuwa taasisi za EWURA, NEMC, Bonde la Ziwa Nyasa na Halmashauri ya Wilaya ya Madaba washughulikie changamoto hii ili Mwekezaji Kampuni ya Silverland aweze kuendelea na uwekezaji.

- Wajumbe walihoji kuhusu Kampuni ya Siliverland kubadilisha matumizi ya eneo, ambapo matumizi yaliyokususdiwa ni; uzalishaji wa mazao na badala yake wanazalisha mbegu. Jambo ambalo limepelekea Halmashauri kukosa mapato.
- Viongozi wa Bandari wapewe mwaliko ili wahudhurie katika vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC)

## 16.0 MUHTASARI NA. RCC: 14/12/2021: KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti kabla ya kufunga kikao alieleza mambo yafuatayo; kufikia tarehe **05 Januari 2022** Halmashauri zote zinatakiwa kukamilisha ujenzi na kukabidhi madarasa **500** yanayojengwa kupitia fedha za maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya **UVICO – 19. (Mradi Na. 5441 TCRP).** Vilele mabweni matatu yanayojengwa kupitia mpango huo ujenzi wake ukamilike kufikia tarehe **20 Machi 2022.** Mwenyekiti alieleza pia juu ya changamoto zilizopo katika maendeleo na uendelezaji wa timu ya majimaji, alieleza kuwa timu ya majimaji haiwezi kusonga mbele bila kuwa na mkakati wa kuindeleza hususani kifedha, hivyo Mkoa pamoja na wadau wote tunatakiwa kutafuta namna ya kuifanya timu ijiendeshe kama Kampuni. Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa **9:46 Alasiri**

**UMETHIBITISHWA**

**…………………………..** **……………………………**

**MWENYEKITI** **KATIBU**

**TAREHE …………………….**

**4.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA YA SONGEA TAREHE 29 DISEMBA 2021.**

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Muhtasari na. RCC: 04/12/2021: Utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha tarehe 29/12/2021 | kuchelewa kwa utelekezaji wa usambazaji wa umeme mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na awamu ya tatu mzunguko wa pili, mradi unaotekelezwa na Tanesco na Wakala wa Umeme Vijijini (REA). | Kikao kilielekeza kuwa ufuatiliaji wa karibu ufanyike ili kuhakikisha kuwa Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya usambazaji wa umeme Vijijini ili iweze kukamilika kwa wakati. | Meneja TANESCO - Mkoa | Kufuatana na maelekezo ya kikao ufuatiliaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza (REA III round one) unaotekelezwa na Mkandarasi **M/s Namis Corporate Ltd** uliongezeka na kusababisha **mradi kukamilika tangu Juni 2022.** Mkandarasi kwa sasa yupo katika kipindi cha matazamio (defect liability period) na akiendelea na kazi ya kuunganisha wateja na kufanya marekebisho yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mradi.<br><br>Utekelezaji wa mradi wa kupelekea umeme awamu ya tatu mzunguko wa pili nao umeendelea kuimarika kama ifuatavyo<br><br>a) Kwa lot 25 kupitia mkataba-**AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 25** unaotekelezwa na mkandarasi **M/s Namis** |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Corporate Ltd,** katika Wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa mpaka sasa vijiji 25 kati ya 168 vimeshawashwa na mradi **umeshafika asilimia 15%** Mkanadarasi bado yupo eneo la mradi na ufuatiliaji wa karibu unaendelea na mkandarasi ameongeza kasi ya kuleta vifaa vya ujenzi.<br><br>b) Kwa Lot 26 kupitia mkataba namba **AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 26** unaotekelezwa na Mkandarasi **M/s Whitecity Guangdong JV** katika Wilaya za Tunduru na Namtumbo mpaka sasa vijiji 4 vimeshawashwa kati ya vijiji 99. **Utekelezaji wa mradi umeshafikia 32.34%** na mkandarasi bado yupo eneo la mradi na amefanikiwa kusimamisha nguzo katika vijiji 48 kati ya 98. Mkandarasi pia ameongeza kasi ya kuleta vifaa vya utekelezaji wa mradi. |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Na.** | **Halmashauri** | **Hali ya Utekelezaji** |
| | | Kuchelewa kwa ujenzi wa mabweni yanayojengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupitia mradi **Na 5142 TCRP** | Kikao kilielekeza kuwa ujenzi wa Mabweni matatu ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ukamilike kabla ya tarehe 05 Januari 2022. | Wakurugenzi Songea MC, Mbinga TC na Tunduru DC | 1 | Songea MC | Mradi umekamilika lakini hautumiki kutokana na changamoto ya maji vyooni. Kwasasa Halmashauri imepokea Tsh. 60,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa uzio. Sehemu ya fedha hiyo itatumika kuchimba kisima kujenga *raiser tank* na kuweka pampu ya maji. Utekelezaji umeanza. |
| | | | | | 2 | Mbinga TC | Mradi umekamilika ikiwa ni pamoja na Vitanda 50. Bweni hilo linatarajia kuanza kutumika mwezi Januari, 2023. |
| | | | | | 3 | Tunduru DC | Ujenzi umekamilika kwa 90%, Bado ununuzi wa Tanki la maji pamoja na kukamilisha mfumo wa maji safi na Majitaka, ununuzi wa magodoro 80 hayajanunuliwa kutokana ukosefu wa fedha. Ili kukamilisha mradi huu, Halmashauri inatarajia kutumia mapato mengineyo yakiwemo ya |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ndani ili kukamilisha mradi huu kwa kazi chache zisizokamilika zikiwemo zilizotajwa. |
| | | Utekelezaji wa ujenzi wa Shule Sekondari ya Wasichana ya Mkoa katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba | 1. Kikao kilielekeza kuwa Mkoa upanue wigo wa uchangiaji wa fedha za ujenzi za Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa, kwa kukata tozo ya sh. 7 kwa kila kilo moja kwa mazao ya Soya, mbaazi, ufuta, Kahawa, Korosho pamoja na zao la Mahindi ambapo | Katibu Tawala wa Mkoa, Wakurugenzi, Vyama vya Ushirika, Meneja - NFRA | Mpaka sasa kiasi cha mahindi yaliyonunuliwa na NFRA katika msimu wa kilimo 2021/202 ni **Tani 6,441,857,** hivyo kiasi kilichopaswa kulipwa kutokana na makato ya Tsh. 7 kwa kilakilo ya mahindi ni **Tsh. 45,092,999.00**. Hadi sasa kiasi cha **Tsh. 24,809,092.00** tu kimeshalipwa kwa ajili ya ujenzi wa shule ya wasichana ya Mkoa katika Halmashuri ya Wilaya ya Madaba ambacho kinatokana na malipo yaliyofanyika kwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Namtumbo. Kiasi kilichobaki (**Tsh. 20,283,907.00)** kitalipwa baada ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Halmashauri za Wilaya za Nyasa, Mbinga na Madaba kuwasilisha maombi ya madai ya kulipwa NFRA.<br><br>Kwa upande wa zao la ufuta jumla ya **kilo 7,970,176.6** ziliuzwa |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | utaratibu wa makato katika zao la Mahindi utapitia kwa Wakala wa Hifadhi ya chakula (NFRA). | | kupitia stakabadhi ya mazao ghalani kwa msimu wa kilimo wa 2021/2022. Kiasi kilichopaswa kuchangiwa kutokana na makato ya Tsh. 7 kwa kila kilo ni **Tsh. 55,791,236.20**. Mpaka sasa hakuna Halmashauri iliyochangia ujenzi kupitia ununuzi huu wa ufuta. Kwa mazao mengine yaliyobaki (Soya, Mbaazi, Kahawa na Korosho) yataanza kukwata msimu wa kilimo wa 2022/2023. |
| | | | 2. Kikao kilielekeza pia kuwa baada ya kukamilisha ujenzi wa shule ya wasichana ya Mkoa, mchakato wa ujenzi wa shule ya maalumu ya wavulana katika eneo litakalokubaliwa uanze mara moja. | | Mchakato wa ujenzi utaanza baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa. |
| | | Kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Mradi wa Vihenge vya Wakala | Kikao kilielekeza kuwa Majadiliano ya kupata ufumbuzi wa kusimama kwa mradi wa ujenzi | Meneja NFRA Kanda ya Ruvuma | Kikao cha tarehe 30.08.2022 cha majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania, Serikali ya Poland na Mkandarasi Feerum S.A walikubaliana Mkandarasi Feerum S.A kukabidhi site ili serikali ya Tanzania kupitia NFRA iweze kuendelea/kuanza mchakato |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) | wa Vihenge ufanyike kwa haraka ili huduma ya kuhifadhi nafaka zianze kutolewa kwa haraka. | | wa kupata mkandarasi mwingine wa kuendelea na ujenzi wa mradi, kwa kushirikiana na serikali ya Poland. Hadi sasa Mkandarasi hajakabidhi mradi lakini TBA kwa upande wa Serikali ameshafanya hesabu ya mwisho ya mradi (final account) kinachosubiriwa kwa sasa ni maamuzi ya serikali ya Tanzania na Poland kuhusu kukamilishwa kwa mradi. |
| 02 | Muhtasari na. RCC: **08/12/2021**: taarifa ya utekelezaji wa shughuli za afya**.** | Idadi ndogo ya wananchi wanaojiunga na mfuko wa iCHF<br><br>Kwa ajili ya kupata matibabu | Kikao kilielekeza kuwa Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko wa iCHF, ili Mkoa uweze kufikia lengo la kitaifa ambalo ni asilimia **30**. | RMO, Wakurugenzi wa Halmashauri. | Uhamsishaji wa wananchi kujiunga na iCHF umeendelea kufanyika kupitia mikutano ya hadhara na vikao mbalimbali. Aidha, Halmashauri zimekumbushwa kuhamasisha wananchi kujiunga na iCHF kwa barua yenye **Kumb. Na.FA.91/138/01B/59** ya tarehe 19 Julai, 2022. Pia uandikishaji umeongezeka toka kaya **21,722** mwaka 2021 sawa na asilimia **6** ya lengo hadi kaya **26,017** mwaka 2022 sawa na asilimia **7.4** ya lengo ikiwa ni ongezeko la asilimia **1.4** kwa mchanganuo ufuatao:-<br><br>**Na.** \| **Halmashauri** \| **Kaya** \| **Asilimia**<br>1 \| Songea MC \| 2,549 \| 4.4<br>2 \| Mbinga TC \| 2,579 \| 8.5<br>3 \| Songea DC \| 2,510 \| 7.4 |

<table>
<tr><th>Na</th><th>MUHTASARI Na.</th><th>HOJA</th><th>AGIZO</th><th>MHUSIKA</th><th>UTEKELEZAJI</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td><td></td><td><table>
<tr><td>4</td><td>Mbinga DC</td><td>4,965</td><td>8.5</td></tr>
<tr><td>5</td><td>Tunduru DC</td><td>6,659</td><td>8.1</td></tr>
<tr><td>6</td><td>Namtumbo DC</td><td>3,488</td><td>7.6</td></tr>
<tr><td>7</td><td>Nyasa DC</td><td>1,631</td><td>4.4</td></tr>
<tr><td>8</td><td>Madaba DC</td><td>1,636</td><td>13.4</td></tr>
</table></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td>Wananchi kulalamikia upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya.</td><td>Kikao kilielekeza kuwa Waganga wafawidhi wa vituo vya afya wabandike orodha ya dawa zinazopatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya.</td><td>RMO, DMO</td><td>Orodha ya dawa na vifaa tiba vyote vinavyopatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya zimebandikwa katika mbao za matangazo kwenye vituo vya kutolea huduma na imesaidia kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu upatikanaji wa dawa muhimu.</td></tr>
<tr><td></td><td></td><td>Mkoa kuendelea kuwa na tatizo la</td><td>Kikao kilielekeza kuwa Halmashauri zote</td><td>RMO, DMO, Wakurugenzi</td><td>Elimu ya Lishe imeendelea kutolewa katika ngazi za jamii kupitia vikao na mikutano mbalimbali inayofanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na ngazi ya Mkoa. Aidha elimu pia</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th>Na</th><th>MUHTASARI Na.</th><th>HOJA</th><th>AGIZO</th><th>MHUSIKA</th><th>UTEKELEZAJI</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td>watoto wenye Udumavu</td><td>ziendelee kuhamasisha, kutoa elimu kutenga na kutumia fedha kiasi cha shilingi 1000/= kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano (5) kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe ili kupambana na tatizo la udumavu.</td><td>wa Halmashauri</td><td>inatolewa katika ngazi za shule na vituo vya kutolea huduma za afya pindi mzazi/mlezi anapomleta mtoto kliniki. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mkoa kupitia Halmashauri zake ulitenga jumla ya TZS. 384,669,907.8 na kutumia TZS. 241,573,560 ambapo kila mtoto alipata kiasi cha TZS. 1,026.2 na kufanya Mkoa kufikia kima cha chini cha TZS. 1000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka 5 kadiri ya maelekezo ya Serikali. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitenga na kutoa fedha kwa ajili ya Watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa Mchanganuo ufuatao: -
<table>
<tr><th>Na.</th><th>Halmashauri</th><th>Fedha tengwa</th><th>Fedha Tumika hadi Novemba, 2022</th><th>%</th></tr>
<tr><td>1</td><td>Songea MC</td><td>39,860,000</td><td>24,404,000</td><td>61.2</td></tr>
<tr><td>2</td><td>Mbinga TC</td><td>23,971,068</td><td>7,526,000</td><td>31.4</td></tr>
<tr><td>3</td><td>Songea DC</td><td>38,729,712</td><td>6,570,000</td><td>17.0</td></tr>
</table>
</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th>Na</th><th>MUHTASARI Na.</th><th>HOJA</th><th>AGIZO</th><th>MHUSIKA</th><th>UTEKELEZAJI</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td><td></td><td>
<table>
<tr><td>4</td><td>Mbinga DC</td><td>92,711,750</td><td>37,140,000</td><td>40.1</td></tr>
<tr><td>5</td><td>Tunduru DC</td><td>71,204,134</td><td>21,254,600</td><td>29.9</td></tr>
<tr><td>6</td><td>Namtumbo DC</td><td>39,432,000</td><td>5,070,000</td><td>12.9</td></tr>
<tr><td>7</td><td>Nyasa DC</td><td>23,823,206</td><td>11,744,000</td><td>49.3</td></tr>
<tr><td>8</td><td>Madaba DC</td><td>25,543,048.3</td><td>9,143,999</td><td>35.8</td></tr>
<tr><td colspan="2">JUMLA</td><td>355,274,918.3</td><td>122,852,599</td><td>34.6</td></tr>
</table>
</td></tr>
<tr><td>03</td><td>Muhtasari na. RCC: 09/12/2021: taarifa ya ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa wa ruvuma.</td><td>Upimaji na upangaji wa maeneo, katika eneo itakapojengwa Hospitali ya Mkoa pamoja na maeneo mengine.</td><td>1. Kikao kilielekeza kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea ahakikishe eneo litakalojengwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa linapatikana na upimaji</td><td>Mkurugenzi wa Manispaa</td><td>Eneo kwa ajili ya ujenzi limepatikana na tayari Kazi ya upimaji wa eneo imeanza na mchoro wa mipango miji umeandaliwa na kupitishwa ngazi ya wizara ili kuruhusu upimaji ufanyike.<br><br>Hata hivyo ujenzi wa jengo la OPD, jengo la mionzi na nyumba ya Mtumishi upo katika hatua za ukamilishaji. Sanjari na ujenzi wa majengo Serikali tayari imeshatoa baadhi ya vifaa tiba kama CT scan na mashine ya X-ray kwa ajili ya hospitali hiyo.</td></tr>
</table>

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | unafanyika haraka sana. | | |
| | | | 2. Kikao kilielekeza kuwa Halmashauri zisimamie upimaji wa ardhi kuhakikisha suala la upangaji miji linazingatia utengaji wa maeneo ya vivutio/kupendezesha miji kwa mfano, bustani na maeneo ya kupumzikia. | Kamishina wa Ardhi, Wakurugenzi wa Halmashauri. | **Na.** / **Halmashauri** / **Utekelezaji**<br>1 / Songea MC / Kutenga na kupima maeneo tajwa kwa kila mchoro mpya wa eneo unapoandaliwa. Jumla ya maeneo 11 yametengwa kwa ajili ya vivutio ndani ya Manispaa.<br>2 / Mbinga TC / Halmashauri imetekeleza agizo hilo kwa kupima viwanja kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha viwanja katika eneo la Makongowela Kata ya Kilimani na eneo la Tugutu – Meru lililopo kata ya Ruhuwiko.<br>3 / Songea DC / Jambo hili tayari limetekelezwa kwani upangaji na upimaji katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea- Lundusi limezingztiwa na linaendelea kuzingatiwa katika |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | uandaaji wa Mipango kwenye maeneo ambayo tayari yametangazwa kuwa ya Mipango Miji kwa mfano Peramiho. |
| | | | | | 4 | Mbinga DC | Eneo inapojengwa hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imepimwa kwa kuzingatia Ramani ya Mipangomiji. Hata hivyo Ramani ya mpangilio wa majengo ndani ya kiwanja husika umeaandaliwa na kufuatwa. Katika mpango huo maeneo ya kupumzikia yamepewa kipaumbele ikiwa ni pamoja na kuacha miti ya asili kwa ajili ya vivuli na kivutio |
| | | | | | 5 | Tunduru DC | Halmashauri kupitia Idara ya Ardhi inaendelea kuzingatia utengaji wa maeneo ya vivutio kupendezesha Mji kwa maeneo yote yatakayopimwa viwanja. Kwa mwaka 2022 Halmashauri imepima na kutenga maeneo mawili (2) yenye viwanja zaidi ya 1500 vya matumizi mbalimbali kati ya hivyo viwanja nane (8) ni kwa ajili |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

| | | |
|---|---|---|
| | | ya maeneo ya vivutio kwa ajili ya kupendezesha Mji. |
| 6 | Namtumbo DC | Tayari maeneo 6 ya miji midogo ya Lusewa, Nahoro, Mageuzi, Namtumbo, Hanga na Mkongo gulioni yameandaliwa michoro ya Mipango Miji. Ambapo jumla ya viwanja 1,301 vimepimwa. |
| 7 | Nyasa DC | Agizo limezingatiwa, Halmashauri itahakikisha suala la upangaji miji linazingatia utengaji wa maeneo ya vivutio/kupendezesha miji kwa mfano, bustani na maeneo ya kupumzikia kwa maeneo ambayo yanaendelea kupimwa. |
| 8 | Madaba DC | Zoezi Limetekelezwa katika kata ya Lituta kwa vijiji vya Lituta na Mtepa na Kata ya Mahanje kwa vijiji vya Mahanje na Madaba. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **04** | Muhtasari na. RCC: | 1. Kuchelewa | Kikao kilielekeza kuwa | Katibu Tawala | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilifanya mawasiliano na uongozi wa |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | 10/12/2021: taarifa ya utekelezaji wa shughuli za elimu | kwa ujenzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA). | zifanyike jitihada za kuongeza msukumo wa kuomba Chuo Cha Kilimo Sokoine (SUA) kuanzisha Tawi la Chuo katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, Tunduru na Nyasa ambapo maeneo yameshatengwa. | Mkoa. | Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) kuhusu maombi ya kuanzishwa kwa tawi la chuo hicho katika Mkoa wa Ruvuma. Aidha uongozi wa Chuo ulitoa majibu kuwa kwa sasa Chuo hakina bajeti ya kuanzisha tawi jipya la Chuo hicho Mkoani Ruvuma kwa kuwa nguvu kubwa imeelekezwa katika kuimarisha tawi la chuo hicho katika Mkoa wa Katavi.<br><br>Kwa sasa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) wameanza mchakato wa kuanzisha tawi la chuo hicho katika Mkoa wa Ruvuma ambapo eneo lenye ukubwa wa ekari 70 limetengwa katika mtaa wa Mlete eneo la PAmbazuko Manispaa ya Songea. |
| | | 2. Wilaya ya Tunduru kutokuwa na Chuo Cha Mafunzo Stadi (VETA) | Kikao kilielekeza kuwa zifanyike jitihada za kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya VETA Mbinga na Tunduru. | Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya Tunduru na Mbinga | 1. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kupitia barua yenye Kumb. Na. TDC/E.204/12 ya tarehe 04 Agosti, 2022 imeomba fedha kwa Mtendaji Mkuu wa VETA kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA.<br><br>2. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imetenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa chuo na sasa ipo katika mchakato wa |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kupata Hati ya umiliki wa eneo. Baada ya kukamilisha mchakato huo, Halmashauri itaomba fedha za ujenzi wa chuo |
| | | 3. Kuchelewa kuanza kwa mafunzo ya Chuo Cha VETA Nyasa | Kikao kilielekeza kuwa Chuo cha VETA Nyasa kianze kutumika. | Katibu Tawala Mkoa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa | Udahili wa Wanafunzi umeanza mwezi Oktoba, 2022 na Mafunzo yanatarajiwa kuanza rasmi mwezi Januari, 2023 |
| **05** | Muhtasari na. RCC: 11/12/2021: taarifa za Taasisi na mashirika. | Uhamasishaji na utoaji elimu kwa wananchi juu ya kushiriki katika sensa ya Watu na Makaazi. | Kikao kilielekeza kuwa viongozi wa kila ngazi katika Mkoa na Wilaya kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki | Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Meneja Ofisi ya | Uhamasishaji wa wananchi kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi ulifanyika kupitia njia mbalimbali kama ifuatavyo:-<br>1. Kutumia vyombo vya Habari kama Radio zilizopo Mkoani kufikisha elimu kwa wananchi.<br>2. Kupitia vikao, makongamano na matamasha mbalimbali yaliyofanyika ndani ya Mkoa wa Ruvuma na kugawa |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. | Takwimu Mkoa. | vipeperushi.<br><br>3. Kuwa na Banda la sensa takribani kwenye kila tamasha ili kutoa ujumbe wa Sensa pamoja na kujibu maswali mbalimbali ya wananchi yahusuyo Sensa. Mfano. Kwenye maadhimisho ya sikukukuu ya wakulima yaani nanenane na Royal tour iliyofanyika Mkoani Ruvuma.<br><br>4. Kugawa vipeperushi kwenye mikusanyiko ya watu.<br><br>5. Kwa kuwa Ajenda kubwa mwaka huu ilikuwa ni Sensa ya Watu na makazi, Hivyo viongozi wote wakiongozwa na Mh. Mkuu wa Mkoa walikuwa wakizungumzia umuhimu wa Zoezi zima la Sensa ya Watu na Makazi katika shughuli yeyote iliyohusisha mikusanyiko ya watu.<br><br>6. Halmashauri zimefanya matamasha, makongomano na ligi mbalimbali za mipira zilizokuwa na lengo la kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa siku ya Sensa ya watu na makazi. |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 7. Kuzitumia kamati zote za Sensa kuanzia ngazi ya Mkoa hadi kitongojini ili kuhamasisha Sensa. |
| | | Wananchi kuvamia katika maeneo ya chanzo cha maji na hifadhi ya Mto Ruvuma na kusababisha uharibifu wa mazingira. | 1. Kikao kilielekeza kuwa ziendelee kufanyika jitihada za kuwaondoa watu wote waliovamia vyanzo vya maji, na kuendesha shughuli za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo na hifadhi ya mito. Pamoja na kufanya upimaji na utambuzi wa mipaka na kuweka alama katika maeneo ya vyanzo na hifadhi za | Mamlaka ya bonde la Mto Ruvuma, na Bonde la Ziwa Nyasa | 1. Wananchi waliovamia vyanzo vya maji katika eneo la vyanzo vya maji vya Lupembe A, B, C na D ambavyo vipo katika Wilaya ya Mbinga na Namahove na Kubandisi ambavyo vipo Halmashauri ya Wilaya ya Madaba wameondolewa na maeneo hayo yamewekewa alama (beacons) na yamepandwa miti 6000.<br>2. Katika kuwaondoa watu waliovamia vyanzo vya maji, Mamlaka ya bonde la mto Ruvuma wameandaa mabango yenye ujumbe wa makatazo ya kuendeleza shughuli za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo na hifadhi ya mito ambavyo yapo mbioni kusimikwa na kufanyiwa uzinduzi |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | mito. | | |
| | | Maombi ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali hifadhi za vijiji vya Halmashauri ya Songea na Madaba | 1. Kikao kilielekeza kuwa Mkoa upeleke ombi maalum Wizara ya Maliasili na Utalii la kuomba sehemu ya eneo la hifadhi ya Wanyamapori katika kijiji cha Ifinga limilikiwe na Kijiji. | Katibu Tawala Mkoa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na Songea | Maombi yamewasilishwa ngazi ya Wizara kwa hatua za utekelezaji. |
| | | | 2. Kikao kilielekeza kuwa Mkoa kutuma maombi Wizara ya Maliasili na Utalii ya kutangaza kwenye | Katibu Tawala Mkoa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya | Maombi yamewasilishwa ngazi ya Wizara kwa hatua za utekelezaji. |

<table>
<tr><th>Na</th><th>MUHTASARI Na.</th><th>HOJA</th><th>AGIZO</th><th>MHUSIKA</th><th>UTEKELEZAJI</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>gazeti la Serikali hifadhi za vijiji vya Mitumbati, Lihiga, Lupagaro katika Halmashauri ya Songea na vijiji vya Mkongotema, Wino, Ifinga na Madaba katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kuwa hifadhi za misitu za vijiji.</td><td>Madaba na Songea</td><td></td></tr>
<tr><td>06</td><td>Muhtasari na. RCC:13/12/2021 mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti.</td><td>Mkoa kutokuweka mikakati ya kuendeleza michezo kwa vijana.</td><td>Kikao kilielekeza kuwa Halmashauri zote ziweke mikakati ya kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana katika</td><td>Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya zote</td><td><table>
<tr><th>Na.</th><th>Halmashauri</th><th>Utekelezaji</th></tr>
<tr><td>1</td><td>Songea MC</td><td>Kukusanya takwimu za vilabu vya michezo na watu wenye vipaji binafsi katika kata zote21 ambapo hadi sasa tumekusanya takwimu za kata 5 na mitaa 11 ambapo</td></tr>
</table></td></tr>
</table>

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | sekta ya michezo. | | | | vilabu 13 na wasanii 24 wamebainika. |
| | | | | | 2 | Mbinga TC | Michezo kwa lengo la kuibua vipaji imeanzishwa katika shule 6 za Sekondari |
| | | | | | 3 | Songea DC | Mikakati ya Halmashauri ya kukuza na kuendeleza Vipaji vya Vijana katika Sekta ya Michezo ni kama ifuatavyo<br><br>1. Kusimamia ufundishaji wa somo la michezo kwa nadharia na vitendo ili kila Mwanafunzi kupata fursa ya kujifunza na kushiriki katika michezo kuanzia ngazi ya darasa, shule na mashindano ya nje ya |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | shule kwa ajili ya kuibua vipaji.<br><br>2. Kusimamia ufanyikaji wa mashindano ngazi ya Kata, Klasta ili kupata wanafunzi wenye vipaji kwa ajili ya kuunda timu bora ya Wilaya ili kuendeleza vipaji vya wanafunzi.<br><br>3. Kugharamia mashindano ya Mkoa na Taifa ili kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana pamoja na kuongeza chachu kwa wanafunzi kupenda michezo. |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 4 | Mbinga DC | Halmashauri imetenga eneo la uwanja kwa ajili ya michezo mbalimbali lilipo eneo la kiamili, Pia tumeandaa ligi mbalimbali kwa ajili ya kuhamasisha kukuza na kuendeleza michezo na kuandaa mabonanza mbalimbali ya michezo Sanaa na utamaduni |
| | | | | | 5 | Tunduru DC | Utekelezaji unaendelea kufanyika. Tunduru tumeanzisha kikundi cha uhamasishaji wa michezo yote kwa ujumla ndani ya Wilaya ya Tunduru chenye washiriki zaidi 15. |
| | | | | | 6 | Namtumbo DC | Kufufua michezo mashuleni, ambapo kila shule ya msingi na sekondari imeandaa viwanja vya michezo na pia walimu wakuu waliagizwa kununua vifaa vya michezo kupitia mgao wa |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Capitation Grant.<br><br>Mafanikio yameshaanza kuonekana ambapo halmashauri yetu ya Namtumbo ilifanya vyema katika mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA. Kimkoa tulikuwa mabingwa wa Volleyball kwa shule za msingi na sekondari, mpira wa miguu tulipata nafasi ya pili.<br><br>Hata hivyo tunaendelea na uhamasishaji wa walimu ili wajiunge kwa wingi katika vyuo vya michezo. |
| | | | | | 7 | Nyasa DC | Agizo limezingatiwa, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kwa kushirikiana na chama cha Mpira wa miguu na wadau wa michezo |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | imeendelea kuendesha mashindano (Ndondo Cups) katika ngazi za kata na Wilaya iliibua vipaji vya vijana. Aidha, Halmashauri imeweza kuwaruhusu walimu watatu (3) kwenda kusomea kozi ya michezo. Pia, Halmashauri ipo kwenye mkakati wa kuanza ujenzi wa uwanja wa kisasa wa mpira katika kata ya Kilosa. |
| | | | | | 8 | Madaba DC | Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa michezo imeendelea kutekeleza programu ya uibuaji wa vipaji vya michezo kwa vijana katika ngazi ya vijiji, kata na Halmashauri ya wilaya ya Madaba. Kwa sasa ligi za Vijiji kwa Vijiji linaendelea. |
| | | Mgogoro wa ardhi uliopo kati ya vijiji vilivyopo katika | Kikao kilielekeza kuwa kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya | Wakuu wa Wilaya za Nyasa na Mb | Mgogoro umemalizika baada ya kufanyika kwa vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama vya Wilaya ya Mbinga na Nyasa pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kufanya ziara ambapo | | |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mpaka wa Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Mbinga. | (Nyasa na Mbinga) kwa kushirikiana na viongozi wa Halmashauri kuendelea na jitihada za kutatua mgogoro wa ardhi katika pande hizo mbili zenye mvutano na kuwasilisha taarifa ya utatuzi wa mgogoro katika kikao cha kamati ya ushauri ya Mkoa (RCC) kinachofuata. | inga | alitoa maelekezo kuwa kuendeleza mikutano ya ujirani kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi kutokuvamia hifadhi na TFS kulinda mipaka na kutunza hifadhi. |
| | | Mwekezaji wa shamba la Siliverland kutozwa Tozo kubwa. | Kikao kilielekeza kuwa mamlaka zinazohusika wahakikishe wanashughulikia maombi ya mwekezaji Ndolela Silverland L.td wa shamba la Ndolela-Madaba kupunguziwa viwango vya Tozo ili | EWURA, NEMC, Bonde la Ziwa Nyasa na Halmashauri ya Wilaya ya Madaba | Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Madaba imefanya mawasiliano na ofisi ya Bonde la ziwa Nyasa. Aidha, suala hilo limewasilishwa katika Wizara husika kwa Utatuzi. |

| Na | MUHTASARI Na. | HOJA | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | mwekezaji aendelee kufurahia uwekezaji. | | |
| | | Kukosekana kwa watu wa kujibu hoja zinazohusiana na mambo ya bandari. | Kikao kilielekeza kuwa Katika kila vikao vya Bodi ya Barabara na kamati ya ushauri ya Mkoa (RCC) wahusika kutoka mamlaka ya Bandari wawe wanaalikwa na kuwasilisha taarifa zao | Katibu Tawala Mkoa, Meneja TANROAD | Meneja wa Bandari ya Ziwa Nyasa amepewa maelekezo ya kuhudhuria vikao hivyo kwa barua yenye Kumb. Na. BC.265/283/01/H/134 ya tarehe 14 Septemba, 2022. Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imewasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli zao Mkoani Ruvuma. |

## 5.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MKOA KWA MWAKA 2021/2022, 2022/2023 KUISHIA TAREHE 30, NOVEMBA 2022 NA TAARIFA YA MAANDALIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

### 5.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/2022.

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Mkoa wa Ruvuma uliidhinishiwa na Bunge kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi **244,824,103,177.53** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yalikuwa ni Shilingi **164,375,177,177.53** na miradi ya maendeleo ni Shilingi **80,448,926,000.00.** Kati ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa Shilingi **31,535,092,000.00** ni fedha za ndani, Shilingi **42,811,225,000.00** ni fedha za maendeleo za nje na Shilingi **6,102,609,000.00** ni fedha za miradi ya maendeleo kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri.

Kwa upande wa matumizi ya kawaida ya shilingi **164,375,177,177.53** zilizotengwa shilingi **139,969,062,534.00** ni mishahara ya watumishi na matumizi mengineyo ni shilingi. **24,406,114,643.53.** Kati ya fedha za matumizi mengineyo shilingi **12,767,900,281.11** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu na shilingi **11,638,214,362.42** ni matumizi mengineyo ya Mapato ya ndani ya Halmashauri.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mkoa na Halmashauri zake zilipokea na kukusanya **Tshs. 246,797,526,092.16** sawa na asilimia **101.1** ya fedha idhinishwa. Kati ya fedha hizo Ruzuku ya Serikali Kuu ni **Tshs. 225,374,553,384.48** na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ni **Tshs 21,422,972,707.68.**

Matumizi kufikia Juni, 2022 yalikuwa ni **Tshs. 213,206,146,579.79** sawa na **asilimia 86.4** ya fedha pokelewa na makusanyo ya ndani. Mchanganuo wa mapato na matumizi ni kama inavyoonesha katika jedwali namba 1 na namba 2.

### 5.1.1 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2021/22 kuishia Juni, 2022.

Mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida kufikia Juni, 2022 yalikuwa ni **Tshs 158,106,423,557.42** sawa na **asilimia 96.2** ya fedha idhinishwa.

Aidha, matumizi ya fedha kufikia Juni, 2022 yalikuwa **Tshs 156,889,442,642.31** sawa na asilimia **99.2** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na. 1 linaonesha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa, kilichotolewa na kilichotumika kufikia Juni, 2022 kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa, pokelewa na matumizi kwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kufikia Juni, 2022**.

| Na. | Taasisi | Fedha idhinishwa 2021/2022 | Fedha Pokelewa kufikia Juni, 2022 | Asilimia | Matumizi kufikia Juni, 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Sekretarieti ya Mkoa | | | | | |
| | Mishahara | 2,861,308,000.00 | 2,529,879,145.00 | 88.4 | 2.529,879,145.00 | 100 |
| | Matumizi mengineyo | 2,985,802,400.00 | 2,978,001,536.00 | 99.7 | 2,958,629,863.00 | 99.4 |
| **Jumla RS** | | **5,847,110,400** | **5,507,880,681.00** | **94.2** | **5,488,506,008.00** | **99.6** |
| 2 | Halmashauri | | | | | |
| | Mishahara | 137,107,754,534.00 | 139,947,861,462.48 | 102.1 | 139,089,912,880.48 | 99.4 |
| | Matumizi Mengineyo | 21,420,312,243.53 | 12,650,681,413.94 | 59.1 | 12,311,023,753.63 | 97.3 |
| **Jumla Halmashauri** | | **158,528,066,777.53** | **152,598,542,876.42** | **96.3** | **151,400,936,634.11** | **99.2** |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | | **164,375,177,177.53** | **158,106,423,557.02** | **96.2** | **156,889,442,642.31** | **99.2** |

### 5.1.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2021/22

Katika mwaka 2021/22 Mkoa ulitengewa **Tshs 80,448,926,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo **Tshs 31,535,092,000.00** ni fedha za ndani na fedha za nje ni **Tshs 42,811,225,000.00**. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 kiasi cha **Tshs 67,268,129,827.06** zilipokelewa sawa na **asilimia 83.6** ya fedha tengwa.

Matumizi ya fedha za maendeleo kufikia Juni, 2022 yalikuwa **Tshs 56,316,703,937.48** sawa na **asilimia** 83.7 ya fedha pokelewa. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa, pokelewa na matumizi kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri kuishia Juni, 2022 ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa, pokelewa na Matumizi katika Mkoa kuishia Juni, 2022**.

| Na. | Taasisi | Fedha idhinishwa 2021/2022 | Fedha Pokelewa kufikia Juni, 2022 | Asili mia | Matumizi kufikia Juni, 2022 | Asili mia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **Sekretarieti ya Mkoa** | | | | | |
| | Fedha za Ndani | 1,460,652,000.00 | **1,877,560,540.00** | 128.5 | **1,877,547,540.00** | 100 |
| | Fedha za Nje | 663,014,000.00 | **394,980,232.25** | 59.6 | **382,430,751.82** | 96.8 |
| | **Jumla RS** | **2,123,666,000.00** | **2,272,540,772.25** | **107.0** | **2,259,978,291.82** | **99.4** |
| 2. | **Halmashauri** | | | | | |
| | Fedha za Ndani | 36,177,049,000.00 | 35,846,158,318.97 | 99.1 | 24,715,266,148.76 | 68.9 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Fedha za Nje | 42,148,211,000.00 | 35,800,605,177.15 | 84.9 | 29,341,429,496.90 | 82.0 |
| **Jumla Halmashauri** | | **78,325,260,000.00** | **71,646,763,496.12** | **91.5** | **54,056,725,645.66** | **75.4** |
| **Jumla Maendeleo Mkoa** | | **80,448,926,000.00** | **73,919,304,268.37** | **91.9** | **56,316,703,937.48** | **76.2** |

### 5.1.3 Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2021/22

Mkoa wa Ruvuma katika mwaka 2021/22 uliidhinishiwa kukusanya **Tshs. 19,333,322,006** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani. Kufikia Juni**,** 2022 kiasi cha **Tshs 21,422,972,707.68 zilikusanywa** kutoka kwenye vyanzo hivyo ikiwa ni sawa na **asilimia 110.8** ya lengo la makusanyo. Aidha, kiasi cha **Tshs. 6,651,174,441.31** zilipelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. **Tshs 1,524,518,713.61** zilipelekwa katika vikundi vya wanawake, vijana na walemavu kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi katika vikundi hivyo. Jedwali Na. 3 linaonesha malengo na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri, fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maendeleo na vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**Jedwali Na. 3: Malengo na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri, Fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maendeleo na vikundi vya wanawake na vijana kufikia Juni, 2022**.

| Na. | Taasisi | Lengo la Makusanyo 2021/22 | Makusanyo kufikia Juni, 2022 | Asilimia (%) | Fedha zilizopelekwa kwenye Miradi ya Maendeleo | Fedha zilizopelekwa kwenye vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **Sekretarieti ya Mkoa** | 3,000,000.00 | 4,420,000.00 | 147.3 | N/A | **N/A** |
| 2. | **Serikali za Mitaa** | | | | | |
| | Tunduru DC | 4,227,913,000.00 | 4,418,651,204.67 | 103.3 | 2,139,851,710.00 | 264,570,167.99 |
| | Mbinga DC | 4,009,448,000.00 | 4,549,317,329.13 | 113.5 | 1,488,378,999.83 | 435,900,000.00 |
| | Namtumbo DC | 1,501,000,000.00 | 1,659,926,188.31 | 110.6 | 344,447,552.00 | 61,828,000.00 |
| | Songea DC | 1,537,306,806.00 | 1,780,749,173.36 | 115.8 | 712,299,669.34 | 126,230,680.00 |
| | Mbinga TC | 1,930,708,200.00 | 2,301,641,894.14 | 119.2 | 614,463,056.00 | 129,630,002.00 |
| | Songea MC | 4,329,012,000.00 | 4,912,810,519.00 | 113.5 | 1,011,267,624.14 | 356,700,000.00 |
| | Madaba DC | 1,022,764,000.00 | 997,792,064.85 | 97.6 | 151,628,000.00 | 79,000,000.00 |
| | Nyasa DC | 722,170,000.00 | 797,664,337.53 | 110.45 | 188,437,830.00 | 70,659,863.22 |
| **Jumla ya Halmashauri** | | **19,330,322,006.00** | **21,418,552,707.68** | **110.8** | **6,651,174,441.31** | **1,524,518,713.61** |
| **Jumla Kuu** | | **19,333,322,006.00** | **21,422,972,707.68** | **110.8** | **6,651,174,441.31** | **1,524,518,713.61** |

### 5.1.4 Baadhi ya mafanikio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 katika kipindi cha Julai, 2021 – Juni, 2022.

#### Utawala na Rasilimali Watu

i. Mkoa wa Ruvuma (RS) iliongoza na kushika nafasi ya kwanza kitaifa kwa utendaji Bora na kupata tuzo iliyotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.
ii. Hali ya ulinzi na usalama imeendelea kuimarika ndani ya Mkoa na maeneo yote ya mipaka na nchi jirani;
iii. Vikao mbalimbali vya kisheria katika ngazi zote za utawala vimeendelea kufanyika;
iv. Kupungua kwa matukio ya kutoa na kupokea Rushwa kwa kuimarisha utoaji wa elimu kwa wananchi;
v. Mkoa umefanikiwa kujenga ofisi za makao makuu ya Halmashauri 3 za Nyasa, Madaba na Mbinga Dc kwa gharama ya shilingi **5,050,000,000.00** kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.
vi. Mkoa umefanikiwa kujenga nyumba 11 za viongozi na watumishi wa Mkoa na Halmashauri kwa gharama ya shilingi **2,089,999,800**

**Elimu**

i. Mkoa umefanikiwa kujenga shule mpya 11 za Sekondari katika Halmashauri zote 8 za Mkoa wa Ruvuma kwa gharama ya shilingi Bilioni **7,700,000,000.00**.Ujenzi huu unajumuisha shule ya Mkoa ya Wasichana inayojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa gharama ya shilingi bilioni **3,000,000,000.00.**
ii. Mkoa umefanikiwa kujenga vyumba vya madarasa 792 ya elimu msingi na sekondari yakijumuisha madawati, viti na meza kwa gharama ya Shilingi Bilioni **14.93**
iii. Mkoa umefanikiwa kujenga mabweni 5 ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kwa gharama ya shilingi Milioni 640.
iv. Mkoa ulipokea fedha kiasi cha Tshs. **400,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa Maabara 23 za Shule za Sekondari kupitia fedha za Tozo na Serikali Kuu.

**Afya na Ustawi wa Jamii**

**i.** Mkoa umefanikiwa kujenga Vituo vya Afya **12** kupitia fedha za Tozo na Serikali Kuu na Wafadhili kwa gharama ya shilingi **Bilioni. 7,845**.

**ii.** Mkoa umefanikiwa kujenga nyumba 9 za watumishi wa Afya (3 in 1) kwa gharama ya shilingi Milioni **856.585.**

iii. Mkoa umefanikiwa kujenga vituo vya Afya vitatu **(3)** kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa gharama ya Tshs**. 1,500,000,000.00.**

iv. Mkoa umefanikiwa kujenga majengo matatu (3) ya huduma za dharura (EMD) Kwa gharama ya Shilingi Milioni **900.**

v. Mkoa umefanikiwa kujenga jengo moja (1) la wagonjwa mahututi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa gharama ya shilingi milioni **250**

vi. Mkoa umefanikiwa kujenga zahanati **21** kwa gharama ya Tshs. **1,050,000,000.00**

vii. Mkoa unaendelea na ujenzi wa Hospitali 5 za Wilaya ya Nyasa, Mbinga DC, Madaba DC na Songea DC kwa gharama ya Shilingi Bilioni **3.4**

viii. ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa awamu ya kwanza unaendelea kwa gharama ya shilingi **2,700,000,000.00.** Ujenzi huu unahusisha jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la mionzi na nyumba ya mtumishi.

ix. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya imeendelea kuimarika, kwani upatikanaji umeongezeka na kufikia asilimia 96;

x. Mkoa wa Ruvuma ulipata tuzo ya kuongoza kitaifa mfululizo kuanzia Julai 2021 hadi Mei 2022 katika utoaji wa chanjo ya UVIKO-19.

xi. Pia Mkoa ulipata vyeti viwili katika ngazi ya kitaifa (cheti cha kwanza ni cha kuongoza katika utoaji wa chanjo ya UVIKO 19 katika kipindi cha Julai 2021 hadi 5 Novemba, 2021, na cheti cha udhibiti wa upotevu wa chanjo (overall wastage) ambayo mkoa ulikuwa ni **1.4%.** tu.

xii. Mkoa wa Ruvuma ulishika nafasi ya kwanza kitaifa katika utoaji wa huduma za chanjo za kawaida (Halmashauri 6 zilikuwa na kiwango cha uchanjaji kwa zaidi ya **90%** ya chanjo ya ugonjwa wa Surua) ambayo ni sawa na wastani wa **75%.**

xiii. Mkoa unaendelea kutekeleza kwa mafanikio afua za lishe ambapo tathmini iliyofanyika Mkoa wa Ruvuma umekuwa mshindi wa nne **(4)** kitaifa katika utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa mwaka 2022;

xiv. Mkoa umefanikiwa kuvuka lengo katika zoezi la utaoaji wa huduma za chanjo ya Polio kwa awamu zote 4 za kampeni ya kitaifa (awamu ya kwanza **(122%)** na ya pili (**131%)** Mkoa ulishika nafasi ya kwanza kitaifa.

**Uchumi na Uzalishaji**

i. Mkoa umeendelea kufanya vizuri katika sekta ya Kilimo ambapo kwa kipindi cha miaka minne (**4**) mfululizo (2018/2019, 2019/2020, 2020/2021 na 2021/2022 Mkoa umekuwa ndio mzalishaji wa kwanza wa mazao ya Chakula Kitaifa (Mahindi, Mpunga, Mihogo, Viazi nk). Katika msimu wa 2021/2022 hali ya upatikanaji wa Chakula ni nzuri kwani Mkoa uliweza kuzalisha tani **1,256,362** na hivyo kuwa na ziada ya tani **787,190** za mazao ya Chakula;

ii. Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya huduma za ugani na taasisi ya utafiti wa mazao TARI Naliendele na Uyole walitoa Mafunzo kwa Maafisa Ugani **281** wa Halmashauri **8** za Mkoa wa Ruvuma. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo Maafisa Ugani wanaosimamia mazao ya Soya, Alizeti, Ufuta, Korosho na Mahindi.

iii. Mkoa ulipokea pikipiki **281** kwa ajili ya Maafisa ugani wa Kata na Vijiji waliopo Mkoa wa Ruvuma ili kuwezesha kuwafikia wakulima kwa urahisi.

iv. Mkoa kwa kushirikiana na Kampuni ya OCP ulifanikiwa kuendesha zoezi la upimaji wa Afya ya Udongo katika vijiji 100 vya mkoa wa Ruvuma.

v. Mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejenga Majosho **11** katika Halmashauri za Tunduru majosho tisa **(9),** Songea DC Josho moja **(1)** na Nyasa Josho moja **(1)**

vi. Miundombinu ya masoko imeendelea kuboreshwa kwa kujenga soko la kisasa katika kijiji cha Peramiho kupitia TASAF.

**Ukusanyaji wa mapato na Maduhuli ya Serikali.**

vii. Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Ruvuma kwa Mwaka 2021/2022 ilifanikiwa kukusanya **TZS.19,851,876,946** ambayo ni sawa na asilimia **102%** ya lengo la kukusanya **TZS. 19,542,077,000**;

viii. Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, ilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 21,595,567,298** sawa na **asilimia 180** ya lengo la mwaka la shilingi bilioni **12,000,000,000.00**

ix. Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) kwa mwaka 2021/2022 zilifanikiwa kukusanya Shilingi **22,209,630,978.46** sawa na asilimia **108.25 ya lengo la kukusanya shilingi 20,516,758,060 .**

**Usambazaji wa nishati ya Umeme**

i. Jumla ya Wateja wapya **12,129** waliunganishiwa umeme kwa kipindi cha Julai 2021 mpaka June 2022 ni **12,129** ukilinganisha na lengo la kuunganisha wateja **7,500** kwa mwaka sawa na asilimia **161.7%,**

**Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana**

i. Mkoa umefanikiwa kutoa kiasi cha Tsh **2,515,084,713.61** kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo kati fedha hizo Tshs **1,524,518,713.61** zilitokana na asilimia 10 kutoka kwenye makusanyo ya mwaka 2021/2022 na Tshs **990,566,000.00** kilitokana na Marejesho ya mikopo ya miaka ya nyuma.

### 5.1.5 Changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/2022.

i. Fedha za miradi kutolewa kwa viwango sawa nchi nzima (flat rates) bila kuzingatia umbali na tofauti za kijiografia za Mikoa, Wilaya na Halmashauri. (Darasa mil.20 & 12.5, bweni mil.80 &100, nyumba mil.90 nk)

ii. Ukubwa wa eneo la Mkoa wa Ruvuma (Kilomita za mraba **67,372**) na umbali uliopo kati ya Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya**,** hivyo kuongeza gharama za uendeshaji ukilinganisha na bajeti ya uendeshaji inayotengwa;

iii. Upungufu na uchakavu wa magari yaliyopo katika Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri;

### 5.1.6 Mikakati ya Kutatua Changamoto

i. Mkoa umewasilisha Ofisi ya Rais TAMISEMI mapendekezo ya gharama za ujenzi wa miundombinu mbalimbali kulingana na mazingira ya Mkoa wa Ruvuma.

ii. Kuendelea kuiomba Serikali kuridhia maombi ya kugawa maeneo ya kiutawala hususani Wilaya ya Tunduru pamoja na kuongeza fedha za uendeshaji wa shughuli za Mkoa na Halmashauri;

iii. Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari mapya

iv. Kuendelea kuwasilisha maomba vibali vya ajira ili kuongeza idadi ya watumishi;

v. Maombi ya kujengwa barabara hiyo yamewasilishwa katika Mamlaka/Wizara husika na tathmini ya gharama za ujenzi imefanywa na kuwasilishwa.

### 5.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 kwa kipindi cha kuishia Novemba, 2022 (Julai 2022 - Novemba 2022)

#### 5.2.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/2023

Katika mwaka 2022/23 Mkoa wa Ruvuma uliidhinishiwa kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs. 271,162,170,165.83** Kati ya fedha hizo **Tshs. 250,451,604,789.83** ni Ruzuku ya Serikali Kuu na **TshS 20,710,565,376.00** ni fedha za mapato ya ndani.

Hadi kufikia Novemba, 2022 Mkoa na Halmashauri zake zilipokea na kukusanya **Tshs. 107,881,169,074.90** sawa na **asilimia 39.8** ya fedha idhinishwa. Kati ya fedha hizo Ruzuku ya Serikali Kuu ni **Tshs. 98,348,159,711.00** na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ni **Tshs9,533,009,363.90.** Matumizi kufikia Novemba, 2022 yalikuwa ni **Tshs 86,096,138,613.56** sawa na **asilimia 79.8** ya fedha pokelewa. Mchanganuo wa mapato na matumizi ni kama ifuatavyo: -

#### 5.2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2022/23 kuishia Novemba, 2022.

Mkoa wa Ruvuma kwa mwaka 2022/2023 uliidhinishiwa kutumia **Tshs**. **167,717,088,022.09** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Tshs. 150,332,615,999.00** ni kwa ajili ya mishahara na **Tshs 16,678,280,023.09** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida kufikia Novemba, 2022 yalikuwa ni **Tshs 72,269,577,833.64** sawa na asilimia **43.1** ya fedha idhinishwa.

Aidha, matumizi ya fedha kufikia Novemba, 2022 yalikuwa **Tshs 70,690,835,722.76 sawa** na asilimia **97.8** ya fedha zilizopokelewa.

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa, pokelewa na matumizi kwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kufikia Novemba, 2022 kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri.**

| Na. | Taasisi | Fedha idhinishwa 2022/2023 | Fedha Pokelewa kufikia Novemba, 2022 | Asilimia | Matumizi kufikia Novemba, 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | **Sekretarieti ya Mkoa** | | | | | |
| | Mishahara | 2,840,678,000.00 | 1,292,709,558.50 | 45.5 | 1,292,709,558.50 | 100 |
| | Matumizi Mengineyo | 3,546,870,000.00 | 1,455,537,500.00 | 41.0 | 1,206,444,030.05 | 82.9 |
| **Jumla RS** | | 6,387,548,000.00 | 2,748,247,058.50 | 43.03 | 2,499,153,589.55 | 90 |
| 2. | **Halmashauri** | | | | | |
| | Mishahara | 147,491,937,999.00 | 64,290,465,878.00 | 43.6 | 64,149,731,978.00 | 99.8 |
| | Matumizi Mengineyo | 13,837,602,023.09 | 5,230,864,897.14 | 37.8 | 4,041,950,156.21 | 77.3 |
| **Jumla Halmashauri** | | **161,329,540,022.09** | **69,521,330,775.14** | **43.1** | **68,191,682,134.21** | **98.1** |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | | **167,717,088,022.09** | **72,269,577,833.64** | **43.1** | **70,690,835,722.76** | **97.8** |

### 5.2.3 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/23

Katika mwaka 2022/23 Mkoa ulitengewa Tshs **82,734,516,767.74** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo **Tshs. 38,649,108,309.80** ni fedha za ndani na fedha za nje ni **Tshs. 44,085,408,457.94.** Hadi kufikia Novemba, 2022 kiasi cha Tshs. **26,078,581,877.36** zilipokelewa sawa na **asilimia 31.5** ya fedha tengwa. Matumizi ya fedha za maendeleo kufikia Novemba, 2022 yalikuwa Tshs. **15,405,302,890.80** sawa na asilimia **59.1** ya fedha pokelewa. Mchanganuo wa fedha za

maendeleo zilizoidhinishwa, pokelewa na matumizi kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri kuishia Novemba, 2022 ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa, pokelewa na Matumizi katika Mkoa kuishia Novemba, 2022**.

| Na | Taasisi | Fedha idhinishwa 2022/2023 | Fedha Pokelewa kufikia Novemba, 2022 | Asilimia | Matumizi kufikia Novemba, 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | **Sekretarieti ya Mkoa** | | | | | |
| | Fedha za Ndani | 1,699,695,000.00 | 1,654,709,000.00 | 97.4 | 221,054,000.00 | 13.4 |
| | Fedha za Nje | 586,026,000.00 | 13,180,000.00 | 2.3 | 5,540,000.00 | 42.0 |
| **Jumla RS** | | **2,285,721,000.00** | **1,667,889,000.00** | **73.0** | **226,594,000.00** | **13.5** |
| 2. | **Halmashauri** | | | | | |
| | Fedha za Ndani | 36,949,413,309.80 | 17,929,697,625.82 | 48.5 | 10,311,850,900.80 | 57.5 |
| | Fedha za Nje | 43,499,382,457.94 | 6,480,995,251.54 | 14.9 | 4,866,857,990.00 | 75.1 |
| **Jumla Halmashauri** | | **80,448,795,767.74** | **24,410,692,877.36** | **30.3** | **15,178,708,890.80** | **62.2** |
| **Jumla Mkoa** | | **82,734,516,767.74** | **26,078,581,877.36** | **31.5** | **15,405,302,890.80** | **59.1** |

### 5.2.4 Utekelezaji wa Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2022/23

Mkoa wa Ruvuma katika mwaka 2022/23 uliidhinishiwa kukusanya **Tshs 20,710,565,376.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani. Kufikia Novemba, 2022 kiasi cha **Tshs 9,533,009,363.90** zilikusanywa kutoka kwenye vyanzo hivyo ikiwa ni sawa na asilimia **46.0** ya lengo la makusanyo. Aidha, kiasi cha **Tshs 2,919,958,601.25** zilipelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. **Tshs. 734,295,903.05** zilipelekwa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi katika vikundi hivyo. Jedwali **Na. 6** linaonesha malengo na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri, fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maendeleo na vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**Jedwali Na. 6 Malengo na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri, Fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maendeleo na vikundi vya wanawake na vijana kufikia Novemba, 2022**.

| Na | Taasisi | Lengo la Makusanyo 2022/23 | Makusanyo kufikia Novemba, 2022 | Asilimia (%) | Fedha zilizopelekwa kwenye Miradi ya Maendeleo | Fedha zilizopelekwa kwenye vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **Sekretarieti ya Mkoa** | 5,000,000.00 | 780,000.00 | 15.6 | N/A | **N/A** |
| 2. | **Serikali za Mitaa** | | | | | |
| | Namtumbo | 1,274,000,000.00 | 681,783,258 | 53.5 | 125,100,000 | 40,000,000 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Songea DC | 1,095,600,000.00 | 497,627,002 | 45.4 | 306,991,486 | 58,873,325.46 |
| | Nyasa | 1,361,264,000.00 | 516,545,314 | 37.9 | 64,098,250 | 0.00 |
| | Madaba | 1,125,526,376.00 | 444,963,951.37 | 39.5 | 31,000,000.00 | 16,000,000.00 |
| | Mbinga DC | 3,509,273,000.00 | 2,551,831,108.85 | 72.7 | 740,626,613.11 | 177,562,224.49 |
| | Songea MC | 5,517,867,000.00 | 2,228,805,585.76 | 40.4 | 653,393,751.64 | 252,000,000.00 |
| | Tunduru DC | 4,705,800,000.00 | 1,629,567,217.41 | 34.6 | 644,748,580.50 | 114,706,255.10 |
| | Mbinga TC | 2,116,235,000.00 | 981,105,926.00 | 46.4 | 353,999,920.00 | 75,154,098.00 |
| **Jumla** | | **20,710,565,376.00** | **9,533,009,363.90** | **46.0** | **2,919,958,601.25** | **734,295,903.05** |

### 5.2.5 Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo katika utekelezaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa ya kidato cha kwanza 2023.

Mkoa wa Ruvuma ulipokea fedha nje ya bajeti **TShs.3,120,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **156 v**ya kidato cha kwanza 2023 katika shule za sekondari. Mchanganuo wa Fedha hizo ni kama inavyoonesha kwenye jedwali namba 7.

**Jedwali Na. 7: Mchanganuo wa Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya kidato cha kwanza 2023.**

| HALMASHAURI | IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA | MGAO WA FEDHA | VILIVYOKAMILIKA | HATUA YA UKAMILISHAJI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| TUNDURU DC | 10 | 200,000,000.00 | 10 | 0 | 100 |
| MBINGA DC | 10 | 200,000,000.00 | 0 | 10 | 0 |
| MBINGA TC | 11 | 220,000,000.00 | 6 | 5 | 52 |
| NAMTUMBO DC | 17 | 340,000,000.00 | 3 | 14 | 17.6 |
| SONGEA DC | 10 | 200,000,000.00 | 7 | 3 | 95 |
| MADABA DC | 10 | 200,000,000.00 | 1 | 9 | 10 |
| NYASA DC | 12 | 240,000,000.00 | 8 | 4 | 67 |
| SONGEA MC | 76 | 1,520,000,000.00 | 0 | 76 | 0 |
| **JUMLA** | **156** | **3,120,000,000.00** | **35** | **121** | **22.4** |

Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2022 jumla ya vyumba **35** vya madarasa vimekamilika sawa na asilimia 22.4 na vyumba **121** vipo hatua za ukamilishaji.

### 5.2.6 Mapokezi ya fedha za ujenzi wa vituo vya afya na nyumba za watumishi kwa halmashauri

Mkoa umepokea jumla ya **TShs. 980,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vitatu na nyumba nne za watumishi wa halmashauri. Fedha hizi zimetokana na ruzuku ya serikali kuu na mapato ya ndani ya Halmashauri ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora karibu na maeneo yao. Mchanganuo wa fedha ni kama inavyonesha kwenye jedwali namba 8.

**Jedwali Na 8. Mapokezi ya Fedha za Ujenzi wa Vituo vya Afya na nyumba za watumishi wa halmashauri**

| HALMASHAURI | IDADI VITUO VYA AFYA | KIASI CHA FEDHA KWA VITUO VYA AFYA | IDADI YA NYUMBA ZA WATUMISHI | KIASI CHA FEDHA NYUMBA ZA WATUMISHI |
|---|---|---|---|---|
| SONGEA MC | 0 | 0 | 0 | 0 |
| TUNDURU DC | 0 | 0 | 0 | 0 |
| MBINGA DC | 1 | 250,000,000.00 | 4 | 390,000,000.00 |
| SONGEA DC | 0 | 0 | 4 | 240,000,000.00 |
| NYASA DC | 1 | 50,000,000.00 | 0 | 0 |
| MADABA DC | 1 | 50,000,000.00 | 0 | 0 |
| MBINGA TC | 0 | 0 | 0 | 0 |
| NAMTUMBO DC | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **3** | **350,000,000.00** | **8** | **630,000,000.00** |

**Miradi mingine inayotekelezwa**

**Jedwali Na 9: Miradi Mingine Inayotekelezwa na Halmashauri.**

| NA | HALMASHAURI | AINA YA MRADI | KIASI CHA FEDHA CHA MRADI |
|---|---|---|---|
| 1 | SONGEA MC | Ujenzi wa Madarasa | 227,250,000 |
| | | Ukamilishaji wa mabweni 2 | 60,000,000 |
| | | Ununuzi wa vifaa tiba katika zahanati | 50,000,000 |
| | | Ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vya afya | 150,000,000 |
| | | Ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati 1 | 50,000,000 |
| | | Ujenzi wa hospitali ya wilaya awamu ya pili | 500,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | **JUMLA** | **1,037,250,000** |
| 2 | TUNDURU DC | Mfuko wa Jimbo | 135,950,000.00 |
| | | Ukarabati wa hospitali kongwe za halmashauri | 900,000,000.00 |
| | | Fedha za mitihani darasa la nne (SFNA 2022) | 261,518,000.00 |
| | | Fedha za Mitihani ya darasa la saba (PSLEE 2022) | 120,042,000.00 |
| | | fedha za mitihani kidato cha pili (FTNA 2022) | 179,645,000.00 |
| | | Fedha za Mitihani Kidato cha nne (CSEE 2022) | 261,518,000.00 |
| | | Elimu bure Shule za Msingi (EMBM) | 335,913,531.39 |
| | | Elimu bure shule za Sekondari (EMBM) | 475,995,800.00 |
| | | Tozo ya upandaji miti | 44,012,084.50 |
| | | Ununuzi wa vifaa tiba kwa zahanati | 100,000,000.00 |
| | | Ukamilishaji wa zahanati | 200,000,000.00 |
| | | Ununuzi wa vifaa tiba kwa vituo vya afya | 300,000,000.00 |
| | | Ujenzi wa madarasa shule kongwe za Msingi | 100,000,000.00 |
| | | Ukamilishaji wa madarasa msingi | 100,000,000.00 |
| | | Mfuko wa Jimbo | 135,950,000.00 |
| | | TASAF | 1,778,703,691.00 |
| | | UNICEF CHANJO | 39,565,250.00 |
| | | **JUMLA** | **5,468,813,356.89** |
| 3 | MBINGA DC | EP4R | 160,000,000 |
| | | **JUMLA** | **160,000,000.00** |
| 4 | SONGEA DC | Umaliziaji wa ujenzi wa zahanati za Magima na Mtimira B | 100,000,000 |
| | | Fedha za kuchochea miradi ya maendeleo (CDCF) | 75,205,000 |
| | | Ujenzi wa shule mpya ya Msingi lizaboni | 250,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Ukarabati shule ya msingi Liweta | 100,000,000 |
| | | Ujenzi Stand ya Mabasi kijiji cha parangu | 225,145,486.29 |
| | | Ujenzi nyumba ya Mtumishi na Kisima cha maji Zahanati ya mdunduwalo | 170,995,797.32 |
| | | **JUMLA** | **921,346,283.61** |
| 5 | NYASA DC | MAJENGO YA UTAWALA YANAYOENDELEA | 448,402,504.81 |
| 6 | MADABA DC | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Bwalo Shule Ya Sekondari Wino | 50,000,000.00 |
| | | Ukamilishaji wa Ujenzi Wa Bweni Shule Ya Sekondari Matetereka | 80,000,000.00 |
| | | Ujenzi wa Nyumba 4 za Walimu Shule Za Msingi (Mtazamo, Igawisenga, Madaba, Kifaguro) | 200,000,000.00 |
| | | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati ya Mahanje | 50,000,000.00 |
| | | Ukamilishaji Wa Maabara 3 Katika Shule Za Sekondari (Madaba, Lilondo, Matetereka) | 90,000,000.00 |
| | | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 750,000,000.00 |
| | | Ukamilishaji wa darasa 1 shule ya msingi Mbangamawe | 18,750,000.00 |
| | | **JUMLA** | **1,238,750,000.00** |
| 7 | MBINGA TC | 0 | 0 |
| 8 | NAMTUMBO DC | 0 | 0 |
| **JUMLA** | | | **18,100,721,785.81** |

### 5.2.7 Baadhi ya Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa Fedha 2022/20223 kuishia Novemba, 2022

i. Kukamilisha kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa 35 ya kidato cha kwanza mwaka 2023 kati ya vyumba 156 vinavyotakiwa kujengwa.

ii. Kufanyika kwa vikao mbalimbali vya kisheria

iii. Kuendelea kulipa stahiki mbalimbali za watumishi

iv. Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Nyasa na Mbinga

v. Kuanza maandalizi ya ujenzi wa Nyumba ya Katibu Tawala Mkoa, Nyumba ya Mkuu wa Wilaya Mbinga na Ofisi mbili (2) za Maafisa Tarafa.

vi. Maandalizi ya Mashamba Darasa nane (8) ya Malisho na Mashamba darasa matatu (3) ya kuku.

vii. Kuendelea kutoa mafunzo kwa vyama vya ushirika

viii. Ufuatiliaji na usimamizi wa Miradi ya maendeleo ya Kilimo cha Mazao ya chakula na mazao ya biashara

ix. Kuendelea na ujenzi wa soko la samaki katika mji wa Mbamba bay

### 5.2.8 Changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2022/2023.

i. Kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi, bidhaa nyinginezo na huduma huduma mbalimbali, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

ii. Fedha za miradi ya elimu na afya kutolewa kwa viwango sawa nchi nzima (flat rates) bila kuzingatia umbali na tofauti za kijiografia za Mikoa, wilaya na Halmashauri. (Darasa mil.20 & 12.5, bweni mil.80 &100, nyumba mil.90 nk)

iii. Ukubwa wa eneo la Mkoa wa Ruvuma (Kilomita za mraba **67,372**) na umbali uliopo kati ya Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya**,** hivyo kuongeza gharama za uendeshaji ukilinganisha na fedha zinazotolewa;

iv. Upungufu na uchakavu wa magari katika Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri;

v. Upungufu wa watumishi katika Idara mbalimbali hususani katika Idara ya ujenzi, afya, elimu, kilimo, mifugo, fedha na Wathamini.

### 5.2.9 Mikakati ya Kutatua Changamoto

i. Kununua vifaa vya ujenzi moja kwa moja viwandani ili kupata unafuu wa bei
ii. Kupunguza matumizi yasiyo ya lazima
iii. Kuendelea kuiomba Serikali kuridhia maombi ya kugawa maeneo ya kiutawala hususani Wilaya ya Tunduru pamoja na kuongeza fedha za uendeshaji wa shughuli za Mkoa na Halmashauri;
iv. Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari mapya na kufanya matengenezo ya magari yaliyopo.
v. Kuendelea kuwasilisha maombi ya vibali vya ajira ili kuongeza idadi ya watumishi na kuborehsa utoaji wa huduma mbalimbali.

## 5.3. Taarifa ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

Mkoa umeanza maandalizi ya mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kuainisha vipaumbele mbalimbali vya kisekta kwa kuzingatia nyaraka na miongozo mbalimbali iliyopo ya kimkoa na kitaifa ili kuhakikisha Mpango na Bajeti ya Mkoa unaendana na vipaumbele vya kitaifa vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, Mpango wa II wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021- 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 nk.

Sambamba na miongozo hiyo, Mpango na bajeti ya 2023/2024 utazingatia mwongozo wa Mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024 uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango ambao unaainisha na kutoa maelekezo mahususi yanayopaswa kuzingatiwa na Wizara, Mashirika, Taasisi za Umma, Wakala za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa uandaaji wa Mipango na bajeti. Pamoja na kuzingatia vipaumbele vya Mwongozo wa mpango na bajeti, pia Mkoa utazingatia Vipaumbele vya Mkoa kama

vilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Mkoa wa miaka mitano (5) kuanzia **2021/2022** hadi **2025/2026,** Mipango Mikakati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma.

Baadhi ya Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya 2023/2024 ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali namba 10..

**Jedwali Na 10: Vipaumbele vya Mkoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2023/24**

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE |
|---|---|---|
| **1.** | **Utawala na Rasilimali Watu** | (i) Kuendelea kusimamia na kudumisha masuala ya ulinzi na usalama ndani ya Mkoa pamoja na usimamizi wa mipaka kwa kuratibu vikao vya ujirani mwema.<br>(ii) Kuimarisha utawala bora kupitia uratibu na uendeshaji wa vikao vya kisheria, kiutawala, uboreshaji wa Serikali mtandao na ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa Umma (D by D);<br>(iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWA)<br>(iv) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kutenga fedha kwa ajili kujenga,kukamilisha na kukarabati nyumba na Ofisi za wakuu wa Wilaya,Wakurugenzi wa Halmashauri,Tarafa, Kata na Vijiji na nyumba za watumishi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo ambayo hayana ofisi na nyumba za viongozi na watumishi; |
| **2** | **Afya na Ustawi wa Jamii** | (i) Kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya na kuviwekea vifaa tiba |

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE |
|---|---|---|
| | | na dawa.<br><br>(ii) Kuboresha huduma za afya na lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya huduma za afya kwa kutenga bajeti ya uratibu, usimamizi na kujenga uwezo kuhusu masuala ya lishe sambamba na kutenga katika bajeti shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe.<br><br>(iii) Kusimamia na kufuatilia ubora (Quality) na utoaji wa huduma za Afya katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati<br><br>(iv) Kuendelea kutoa elimu ya kupambana na na kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa hatari ya kuambukiza ikiwemo ugonjwa wa Ebola, UVIKO 19, na Ukimwi.<br><br>(v) Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Jamii ulioboreshwa (iCHF).<br><br>(vi) Kuwajengea uwezo watumishi wa Idara ya Afya katika vituo vya kutolea huduma za Afya katika Halmashauri. |
| **3.** | **Elimu na Mafunzo ya Ufundi** | (i) Kundelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati miundombinu ya shule.<br><br>(ii) Kuendelea kutekeleza Mpango wa kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo;<br><br>(iii) Kuuwezesha mafunzo kazini kwa walimu katika ufundishaji wa mada mbalimbali. |

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE |
|---|---|---|
| | | (iv) Kuboresha ufundishaji wa masomo ya sayansi na ufundi kwa kusambaza vifaa vya kufundishia masomo ya sayansi na kujenga maabara na karakana za ufundi. |
| **4** | **Kilimo na Mifugo** | (i) Kuendelea kuongeza uzalishaji na tija (production and productivity) kwa mazao ya chakula  na biashara ili kuongeza kiwango cha utoshelevu na ziada ya chakula.<br><br>(ii) Kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo kupata utaalam na mbinu bora za kilimo na ufugaji kwa watalam wa kilimo na wakulima, wafugaji na wavuvi wakubwa ambao wapo kwenye maeneo yao ili kukuza uwezo na kuendeleza kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara;<br><br>(iii) Kuendelea kusimamia upatikanaji na matumizi saahihi ya pembejeo na zana  bora za kilimo ili kuongeza tija katika uzalishaji;<br><br>(iv) Kuwezesha uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja (**block farming**) kwa ajili ya kilmo cha mazao ya kimkakati kama ufuta, korosho,kahawa na soya).<br><br>(v) Kuanzisha Kongani za Kilimo na mazao ya Kilimo<br><br>(vi) Kuhamasisha ujenzi wa Maghala makubwa ya kuhifadhia mazao ya kilimo |
| **5** | **Usafiri na Usafirishaj i (barabara)** | (i) Kuimarishaji usafiri na usafirishaji kwa kuendelea na Ujenzi wa barabara na madaraja, kukarabati na matengenezo ya barabara za Vijijini na Mijini kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020,Mpango Mkakati wa Mkoa pamoja maeneo ya kimkakati ndani ya Mkoa (kilimo,madini, maeneo mapya ya makazi na huduma. |

| NA | SEKTA | VIPAUMBELE |
|---|---|---|
| 6 | **Nishati (Umeme)** | (i) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini na mijini inayotekelezwa na REA na TANESCO pamoja na kuendelea kuwaunganishia nishati ya umeme wananchi ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme kwa ujumla (overall electricity access level) |
| 7 | **Fedha na tehama** | (ii) Kuendelea kuimarisha na kusimamia Mifumo ya Kielektroniki ya Ukusanyaji wa Mapato (LGRIS),mifumo ya matumizi (MUSE,FFARS etc) ili kupunguza mianya ya upotevu wa mapato ya serikali sambamba na kuendelea kuhimiza matumizi ya mifumo ya malipo Serikalini (GePG).<br><br>(iii) Kuendelea kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vilivyopo. |
| 9 | **Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi** | (iv) Kuendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu inayotokana na **10%** ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu **(4:4:2).**<br><br>(v) Kuendelea kusimamia na kutekeleza Mpango wa Kunusuru kaya Masikini (Social Welfare Benefits) unaotekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF II).<br><br>(vi) Kuendelea kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali kama viwanda, kilimo cha kimkakati, biashara nk. |

Kwa kuzingatia ukomo wa bajeti na vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2023/24 Mkoa wa Ruvuma fungu **82** unatarajia kuwasilisha maombi ya

kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 267,530,798,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Fedha hizo zinajumuisha Shilingi.**180,932,942,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi. **86,497,856,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na Shughuli mbalimbali za maendeleo.

### 5.3.1 Matumizi ya Kawaida.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Ruvuma na Halmashauri zake unatarajia kuwasilisha maombi ya kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi.180,932,942,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo,Shilingi. **153,907,956,000.00** ni Mishahara ya watumishi na **Shilingi. 27,024,986,000.00** ni Matumizi Mengineyo. Aidha, bajeti ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni **Shilingi. 6,419,485,740.00** na Shilingi.**174,513,456,260.00 ni** kwa ajili ya Halmashauri.

### 5.3.2 Matumizi ya Maendeleo

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri zake unatarajia kuwasilisha maombi ya kuidhinishiwa makadirio ya jumla ya **Shilingi. 86,497,856,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi. 34,172,550,000.00** ni fedha za ndani, **Shilingi. 45,511,358,000.00** ni fedha za nje na Fedha za maendeleo mapato ya ndani ni **Shilingi 6,813,948,000.00.** Fedha maendeleo kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ni **Shilingi. 2,285,721,000.00** na Halmashauri ni **Shilingi. 84,212,135,000.00.**

## 6.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KISEKTA

## 6.1 UCHUMI NA UZALISHAJI (KILIMO, MIFUGO, UVUVI, MALIASILI NA USHIRIKA)

### 6.1.1 SEKTA YA KILIMO

Mkoa wa Ruvuma una fursa ya kupata mvua nyingi, ardhi nzuri inayofaa kwa kilimo na inayokubali kuzalisha takribani mazao aina zote. Mazao ya chakula yanayolimwa ni Mahindi, Mpunga, Muhogo, Maharage, Mtama, Ulezi, Mbaazi na Viazi Vitamu. Mazao ya biashara ni Tumbaku, Kahawa, Korosho, Ufuta, Soya, Alizeti, Tangawizi, Mbaazi na Karanga. Mazao ya bustani ni pamoja na Parachichi, Embe, Machungwa, Matikiti, Ndizi, Papai na Mbogamboga. Hekta **4,007,746** zinafaa kwa kilimo, hadi sasa eneo linalolimwa ni wastani wa hekta **583,279** sawa na asilimia **15** ya eneo lote**,** na kufanya Mkoa kuwa na ziada ya hekta **3,424,467** sawa na asilimia **85.** Aidha, Mkoa wa Ruvuma umeendelea kuwa mzalishaji mkubwa wa zao la mahindi ambalo linategemewa kwa ajili ya usalama wa chakula.

#### 6.1.1.1 Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo kwa Msimu wa Mwaka 2021/2022

**a) Mipango na Malengo ya Kilimo Msimu wa 2021/2022**

Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022 Mkoa ulilenga kulima jumla ya hekta **651,157** za mazao ya chakula, biashara na mazao ya bustani zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1,785,500.** Kati ya hekta hizo kilimo cha mazao ya chakula ni hekta **522,396** zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1,458,462** na kilimo cha mazao ya biashara ni hekta **116,150** zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **84,509.** Kwa mazao ya bustani hekta **12,611** zilizotarajiwa kutoa mavuno ya tani **242,529.**

**b) Utekelezaji wa Malengo ya Kilimo Msimu wa 2021/2022**

Kufikia mwezi Juni, 2022 Mkoa ulikwishalima hekta **583,279** za mazao ya chakula, biashara na mazao ya bustani sawa na **asilimia 89.56 ya** lengo ambazo zimetoa

mavuno ya tani **1, 541,659** sawa na **asilimia 86.34** ya lengo la mavuno. Kwa upande wa mazao ya chakula hekta **442,014** zililimwa ambazo zimetoa mavuno ya tani

**1,256,362** na katika kilimo cha mazao ya biashara hekta zilizolimwa ni **127,418** ambazo zimetoa jumla ya tani **101,059.** Aidha kwa upande wa mazao ya bustani hekta **13,848** zililimwa na kutoa mavuno ya Tani **184,238**

#### 6.1.1.2. Mipango na Malengo ya Kilimo Msimu wa 2022/2023

Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023 Mkoa umelenga kulima jumla ya hekta **930,082** za mazao ya chakula, biashara na Mazao ya bustani zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1,965,072.** Kati ya hekta hizo kilimo cha mazao ya chakula ni hekta **569,070** zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **1,638,808 na** kilimo cha mazao ya biashara ni hekta **337,572** zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **102,379 Kwa** mazao ya bustani hekta **23,399** zinazotarajiwa kutoa mavuno ya tani **223,886.**

**Jedwali Na.11: Malengo ya Kilimo kwa Kila Halmashauri**

| Halmashauri | Malengo ya Kilimo msimu wa 2022/2023 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mazao ya Chakula | | Mazao ya Biashara | | Mazao ya Bustani | | Jumla Kuu | |
| | hekta | tani | hekta | tani | hekta | tani | hekta | tani |
| Songea DC | 124,205 | 419,266 | 17,479 | 11,069 | 8,217 | 126,939 | **149,901.00** | **557,273.60** |
| Songea MC | 21,901 | 79,219 | 1,087 | 1,945 | 1,385 | 22,901 | **24,372.50** | **104,065.00** |
| Madaba | 64,901 | 229,530 | 2,879 | 8,889 | 1,468 | 33,747 | **69,247.90** | **272,165.79** |
| Mbinga DC | 91,643 | 223,192 | 30,307 | 14,679 | 1,877 | 25,567 | **123,826.58** | **263,438.57** |
| Mbinga TC | 57,434 | 106,017 | 13,627 | 4,676 | 8,611 | 876 | **79,672.00** | **111,568.60** |
| Nyasa DC | 96,097 | 280,659 | 13,259 | 6,210 | 1,197 | 8,406 | **110,553.00** | **295,274.44** |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Namtumbo DC | 43,201 | 144,402 | 15,816 | 12,490 | 241 | 1,997 | **59,258.00** | **158,889.40** |
| Tunduru DC | 69,690 | 156,523 | 243,118 | 42,421 | 403 | 3,453 | **313,210.56** | **202,397.07** |
| **Jumla ya Mkoa** | **569,070** | **1,638,808** | **337,572** | **102,379** | **23,399** | **223,886** | **930,041.54** | **1,965,072.46** |

### 6.1.1.3 Hali ya Upatikanaji wa Chakula

Hali ya usalama wa chakula kwa Mkoa wa Ruvuma ni nzuri kwa kiwango cha utoshelevu na ziada kwa zaidi ya miaka kumi na mbili (12) mfululizo. Chakula kilichozalishwa **katika msimu 2021/2022** kinatumika kwa msimu huu **2022/2023** ambapo mazao ya chakula zilizalishwa tani **1,256,362 na m**ahitaji ya chakula ndani ya Mkoa kwa **msimu 2022/2023** ni tani **469,172** na kuufanya Mkoa kuwa na ziada ya chakula tani **787,190** ambazo zimeendelea kuuzwa kwa lengo la kuwaongezea wananchi kipato

### 6.1.1.4 Upatikanaji wa Mbolea kwa Msimu wa 2021/2022 na Mfumo wa Ruzuku ya Mbolea Msimu wa 2022/2023

**i. Hali ya Upatikanaji wa Mbolea katika Mkoa wa Ruvuma Msimu wa 2021/2022**

Katika msimu 2021/2022 jumla ya tani **33,501.07** za mbolea ziliingia katika Mkoa kupitia makampuni na mawakala wa mbolea ambao ni Premium, Export Trading, Afrisian, DRTC, Minjingu, STACO, YARA na Mohamed Entreprises. Mahitaji ya mbolea za aina zote kwa Mkoa ni Jumla ya tani **50,524.50.** Aidha, Hali ya upatikanaji wa mbolea ilikuwa ya kuridhisha, kiasi cha mbolea kilichosambazwa katika Mkoa wa Ruvuma ni tani **30,374.21** sawa na asilimia **76.98** ya mbolea zilizoingia.

**Jedwali Na 12. Gharama ya mbolea kwa mfuko wa kilo 50 kwa msimu wa mwaka 2021/2022 sokoni.**

| Mbolea | UREA | SA | CAN | DAP |
|---|---|---|---|---|
| Bei | 126,000 | 84,000.00 | 110,000.00 | 132.000.00 |

Kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea, zipo changamoto za uzalishaji zilizo jitokeza hususani baadhi ya Wakulima kushindwa kumudu gharama za mbolea, hali hii ilipelekea wakulima kulima pasipo kutumia mbolea za viwandani.

### ii. Mfumo wa Mbolea za Ruzuku Msimu wa Kilimo 2022/2023

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) unatekeleza mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa Wakulima msimu wa 2022/2023. Mfumo huu unaenda sambamba na zoezi la kusajili wakulima wote, mawakala na makampuni yanayoingiza mbolea.

**a) Usajili wa Mawakala**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya mawakala **131** waliosajiliwa ambao wanahudumia kwenye Halmashauri zote nane kama jedwali 13 linavyoonesha.

**Jedwali Na 13. Idadi ya mawakala**

| Na | Halmashauri | Idadi ya Mawakala |
|---|---|---|
| 1. | Songea Mc | 30 |
| 2. | Songea DC | 44 |
| 3. | Madaba | 0 |
| 4. | Mbinga DC | 1 |
| 5. | Mbinga TC | 29 |
| 6. | Nyasa | 0 |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Namtumbo | 19 |
| 8. | Tunduru | 8 |
| **Jumla** | | **131** |

Mawakala wenye vigezo wamejisajili kwenye mfumo wa Ruzuku wa kidigitali unaoratibiwa na TFRA. Aidha, makampuni ya mbolea yamewasilisha majina ya mawakala watakaosambaza mbolea kwa wakulima.

b) **Usajili wa Wakulima**

Wakulima waliosajiliwa tangu zoezi la usajili lilipoanza tarehe **15 Agosti 2022** kupitia vitabu ni wakulima **225,623.00** kati ya hao **115,931.00** wameshaingizwa kwenye mfumo na wameanza kupata mbolea**.**

Katika usajili wa wakulima utaratibu unaotumika katika usajili ni kama ifuatavyo;

i) Wakulima wote wanasajiliwa katika maeneo wanayolima;
ii) Wakulima wanasajiliwa katika hatua mbili hatua ya kwanza ni kwenye kitabu ambapo taarifa za mkulima zinajazwa ikiwemo jinakamili, namba ya simu, ukubwa wa eneo analolima, ainaya mazao anayozalisha;

Baada ya mkulima kusajiliwa katika kitabu taarifa zake zinapandishwa/kuingizwa kwenye mfumo, mara baada ya taarifa za mkulima kuingizwa kwenye mfumo, mkulima anapata namba kupitia meseji. Namba hiyo ndio itakayotumika katika kununulia mbolea za ruzuku kwa Wakala. Jedwali namba 4 linaonesha Idadi ya Wakulima waliosajiliwa.

**Jedwali Na 14. Idadi ya Wakulima**

| NA | Halmashauri | Idadi ya Vitabu | Malengo ya kuandikisha | Idadi ya Wakulima walioandikishwa kwenye | Idadi ya Wakulima waliosajiliwa kwenye |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | Vitabu | Mfumo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea DC | 130 | 46,000 | 38,752.00 | 10,256.00 |
| 2 | Songea MC | 110 | 32,500 | 18,622.00 | 16,721.00 |
| 3 | Madaba | 160 | 26,196 | 20,100.00 | 14,500.00 |
| 4 | Namtumbo | 210 | 77,947 | 50,990.00 | 33,894.00 |
| 5 | Tunduru | 250 | 128,421 | 27,000.00 | 1,570.00 |
| 6 | Nyasa | 170 | 29,224 | 17,158.00 | 13,886.00 |
| 7 | Mbinga DC | 330 | 65,000 | 38,301.00 | 19,744.00 |
| 8 | Mbinga TC | 170 | 23,000 | 14,700.00 | 5,360.00 |
| | **Jumla ya Mkoa** | **1,530.00** | **428,288.00** | **225,623.00** | **115,931.00** |

**iii. Bei ya Mbolea ya Ruzuku.**

Mbolea zilizoingizwa kwenye ruzuku ni **DAP, UREA, CAN, SA, na NPKs.** Katika kila kituo cha mauzo, mbolea za aina zote zikiwemo mbolea za **YARA** na **MINJINGU** zinauzwa kwa bei ya ruzuku na zoezi hili limeanza mwezi **Agosti, 2022** kwa makampuni ya Premium, Export Trading, YARA na OCP Tanzania**.**

**Jedwali Na 15. Bei za Kila Aina ya Mbolea**

| Na | Aina ya Mbolea | Bei ya Soko (Tsh.) | Bei ya Mkulima yenye ruzuku (Tsh.) | Ruzuku ya Serikali (Tsh) |
|---|---|---|---|---|
| 01 | DAP | 132,000.00 | 70,000.00 | 62,000.00 |
| 02 | UREA | 126,000.00 | 70,000.00 | 56,000.00 |
| 03 | CAN | 110,000.00 | 60,000.00 | 50,000.00 |
| 04 | SA | 84,000.00 | 50,000.00 | 34,000.00 |
| 05 | NPKs | 124,000.00 | 70,000.00 | 54,000.00 |

#### 6.1.1.5 Mafunzo kwa Maafisa Ugani

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya huduma za ugani na taasisi ya utafiti wa mazao TARI Naliendele na Uyole walitoa Mafunzo kwa maafisa ugani **281** wa Halmashauri za Songea DC, Songea MC, Namtumbo, Madaba, Tunduru, Mbinga DC, Mbinga TC na Nyasa za Mkoa wa Ruvuma. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo Maafisa Ugani wanaosimamia mazao ya Soya, Alizeti, Ufuta, Korosho na Mahindi.

#### 6.1.1.6 Vitendea kazi kwa Maafisa Ugani

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan alitoa pikipiki **7000** kwa maafisa ugani wa Kata na Vijiji kwa nchi nzima ambapo katika Mkoa wetu wa Ruvuma tulipata mgao wa pikipiki **281**, hivyo maafisa ugani wote wa Kata na Vijiji waliopo katika Mkoa wa Ruvuma kila mmoja alipata pikipiki moja. Aidha tunatarajia kupata seti moja ya vifaa vya kutolea Huduma za Ugani.

#### 6.1.1.7 Afya ya Udongo

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia taasisi yake ya TARI Uyole na Kampuni ya OCP ilitoa taarifa ya hali ya Afya ya udongo ya Mkoa wa Ruvuma kuwa unaumwa na unahitaji matibabu. Sababu kubwa ya udongo kufikia hatua hii ni kutokana na kuwepo kwa matumizi makubwa ya Pembejeo hususani mbolea pasipo kupima afya ya udongo na kuutibia. Hivyo Kampuni ya OCP iliamua kuwezesha gharama za upimaji wa Afya ya Udongo katika vijiji 100 vya mkoa wa Ruvuma (Jedwali Na.16) ambapo zoezi la kuainishaji vijiji vitakavyowakilisha udongo wa Mkoa mzima ulifanyika kwa kushirikiana na maafisa kilimo, umwagiliaji na ushirika wa kila Halmashauri

Uchaguzi wa vijiji hivi ulizingatia maeneo yenye uzalishaji mkubwa, aina ya mazao yanayolimwa na uwakilishi mzuri wa maeneo haya kwa aina ya udongo na jiografia ya maeneo hayo. Mpaka sasa upimaji umeshafanyika na matokeo ya vijiji husika yameshawasilishwa kwenye hivyo vijiji, na kinachofuata ni kusubiri taarifa ya kimkoa ambayo inaandaliwa na wataalam wa afya ya udongo kutoka kituo cha utafiti Uyole (TARI-Uyole) ambapo taarifa hii itawasilishwa kwa wadau wote wa mkoa ikihusisha hali

ya afya ya udongo kwenye maeneo yetu na mapendekezo sahihi ya matumizi ya mbolea.

**Jedwali Na. 16: Vijiji vilivyochaguliwa katika kila Halmashauri**

| Na | SONGEA DC | SONGEA MC | MADABA | MBINGA DC | MBINGA TC | NYASA | NAMTUMBO | TUNDURU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilagano | Kihekwa | Igawiseng a | Lukarasi | Ruvuma Chini | Kwambe | Mawa | Nalasi |
| 2 | Mpandangind o | Nangwahi | Lilondo | Mkako | Masimeli | Litoromelo | Msindo | Masugulu |
| 3 | Litapwasi | Sinai | Mateterek a | Kigonsera | Kihungu | Mbaha | Nambalama | Makande |
| 4 | Lusonga | Mwanamong a | Mahanje | Mihango | Utiri | Nkaya | Msisima | Nandembo |
| 5 | Litisha | Liwumbu | Kipingo | Amani Makolo | Sepukila | Ngingama | Nahoro | Mchuluka |
| 6 | Parangu | Mdundiko | Mkongote ma | Lipumba | Makatani | Kingerikiti | Libango | Pacha Nne |
| 7 | Ndongosi | Masigira | Gumbiro | Muhongozi | Ukomo | Mawasilian o | Likuyu Mfuate | Chingulung ulu |
| 8 | Magagura | Mlete | Ngadinda | Mbuji | Myangayang a | Lumeme | Mtumbatimaji | Nakapanya |
| 9 | Kikunja | Mhombezi | Mtyangim bole | Kibanga | Luwaita | Kikole | Kitanda | Kitanda |
| 10 | Maposeni | Ndilimalitemb o | Luhimba | Kihereketi | Mateka | Malungu | Namanguli | Uwanja wa Ndege |
| 11 | Mpitimbi | | | Likwela | | | Mkongo Gulioni | Masonya |
| 12 | Lilahi | | | Kitesa | | | Njomlole | Matemanga |
| 13 | Peramiho B | | | Matekela | | | Namali | Hulia |

| Na | SONGEA DC | SONGEA MC | MADABA | MBINGA DC | MBINGA TC | NYASA | NAMTUMBO | TUNDURU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Muunganozomba | | | Mkuka | | | Ligunga | Kidodoma |
| 15 | Lugagara | | | Maguhu | | | Magazini | Mkonda |
| | **15** | **10** | **10** | **15** | **10** | **10** | **15** | **15** |

### 6.1.1.8 Kilimo cha Umwagiliaji

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya hekta **197,108.2** zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji na hekta **7,388.3** zimeendelezwa,hii ni sawa na asimilia **3.7**.

**I. Skimu Za Umwagiliaji Zinazofanya Kazi**

Mkoa una skimu **102** kati ya hizo skimu **42** zimeboreshwa skimu **23** zinafanya kazi na **19** hazifanyi kazi. Skimu 23 zinazofanya kazi zina ukubwa uliogawanyika katika makundi mawili, eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji **hekta 5,420** na eneo linalomwagiliwa lenye ukubwa wa **hekta 1,182** kama **(Jedwali Na.17)** kinavyoonesha ambapo uzalishaji wake ni kati ya magunia ya mpunga 25 hadi 40 kwa ekari, kiasi hiki cha uzalishaji kinaridhisha kwani husababisha mkoa kupata zaidi ya tani 15,930 za mpunga kwa msimu.

**II. Skimu Za Umwagiliaji Zisizofanya Kazi**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya skimu 19 ambazo hazifanyi kazi zenye ukubwa uliogawanyika katika makundi mawili eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 3,844 na eneo linalomwagilia lenye ukubwa wa hekta 1110 kutokana na miundombinu iliyokuwa imejengwa hapo awali kuathirika na mafuliko katika kipindi cha msimu wa mvua kwa mwaka 2019/20, lakini pia katika orodha hiyo baadhi ya skimu hazijajengwa kabisa kutokana na serikali kutoelekeza fedha hizo kama ilivyokuwa imepangwa katika bajeti. **(Jedwali Na.18)**.

## Jedwali Na.17: Skimu Za Umwagiliaji Zinazofanya Kazi

| S/NA. | Halmashauri | Jina la skimu | Eneo linalofaa kwa umwagiliaji (ha) | Eneo linalomwagiliwa (ha) | Uzalishaji (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tunduru | Kitanda | 600 | 100 | 3900 |
| | | Lekindo | 150 | 25 | 825 |
| | | Madaba na. 1 | 200 | 100 | 300 |
| 2 | Nyasa | Kimbande | 260 | 237 | 900 |
| | | Ngindo | 250 | 141 | 1,125 |
| | | Ngingama | 40 | 10 | 180 |
| 3 | Songea DC | Namatui | 220 | 100 | 636 |
| | | Mpitimbi B | 200 | 88 | 600 |
| | | Njoka | 120 | 33 | 660 |
| | | Ndongosi | 1,200 | 28 | 600 |
| | | Nakahuga | 270 | 96 | 686 |
| 4 | Mbinga DC | Litumbandiyosi | 250 | 82 | 750 |
| | | Msangamabuni | 300 | 70 | 700 |
| | Namtumbo | Msanjesi | 100 | 45 | 560 |
| | | Amani | 90 | 70 | 630 |
| 5 | | Njomlole | 120 | 62 | 350 |
| | | | | | |
| | | Namahoka | 150 | 30 | 780 |
| | | Kitanda | 100 | 60 | 540 |
| | | Mchomoro | 60 | 60 | 360 |
| | | Luhimbalilo | 50 | 20 | 225 |
| | | Nambecha | 40 | 20 | 40 |
| 6 | Madaba | Hanga Ngadinda | 400 | 55 | 248 |
| | | Mbangamawe | 250 | 50 | 600 |
| **JUMLA** | | **23** | **5,420** | **1,582** | **16,195** |

## Jedwali Na.18: Skimu Za Umwagiliaji Zisizofanya Kazi

| | | | |
|---|---|---|---|
| **HALMASHAURI** | **JINA LA SKIMU** | **ENEO LINALOFAA KWA UMWAGILIAJI (Ha)** | **ENEO LINALOMWAGILIWA (Ha)** |
| Tunduru DC | Legezamwendo | 220 | 200 |
| | Misyaje | 200 | 175 |
| | Naikula | 250 | 200 |
| | Madaba | 600 | 350 |
| Namtumbo DC | Mtakuja | 300 | 300 |
| | Mwangaza | 250 | 250 |
| | Nambecha | 40 | 40 |
| | Liyuni | 140 | 100 |
| | Likuyuseka | 44 | 25 |
| | Mtonya | 75 | 75 |
| Songea DC | Muhukuru | 350 | 50 |
| | Ndongosi | 200 | 135 |
| Madaba DC | Luhimba | 55 | 25 |
| Mbinga DC | Luhagara | 150 | 65 |
| Nyasa DC | Kwambe | 200 | 100 |
| | Mkalachi | 150 | 100 |
| | Koyogo | 200 | 150 |
| Songea MC | Subira | 250 | 200 |
| | Kiekwa | 170 | 45 |
| **Jumla** | **19** | **3,844.00** | **2,585.00** |

**Jedwali Na 19. Idadi ya Skimu za Umwagiliaji Zilizoboreshwa Kwa Kila Halmashauri**

| Halmashauri | Songea MC | Songea DC | Tunduru DC | Namtumbo DC | Nyasa DC | Mbinga DC | Mbinga TC | Madaba DC |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Skimu za Umwagiliaji** | 2 | 7 | 7 | 14 | 6 | 3 | 0 | 3 |

### III. Usajili wa Skimu

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa WA Ruvuma imefanikiwa kusajili skimu **42** katika kipindi cha mwaka **2020/2021** kati ya skimu **102** ili kuendana na mabadiliko ya Sheria

**Na. 4, 2013** ya Umwagiliaji iliyopitishwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni sehemu wa utekelezaji wa maagizo.

Pia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa katika mwaka **2022/2023** imejipanga kukamilisha zoezi la usajili wa **skimu 60** zilizobaki ili serikali iweze kuendelea na zoezi la kuelekeza fedha katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya usanifu, ujenzi na ukarabati wa skimu zilizoathiriwa na mafuriko katika vipindi vya miaka mitatu mfululizo **2019-2021.**

Katika **Jedwali Na. 20** linaonesha idadi ya skimu zilizosajiliwa na tume ya umwagiliaji.

**Jedwali Na.20: Idadi ya Skimu Zilizosajili**

| Na. | Scheme Name | Name of IO | Controll Number | REG. NO | Reg. Datea | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Namatuhi | Umoja wa Umwagiliaji Namatuhi | 995780000976 | NO. 081 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 2. | Njoka | Umoja wa Umwagiliaji Njoka | 995780000975 | | | Songea Vijijini |
| 3. | Madaba | Chama cha Umwagiliaji Madaba | 995780001105 | No. 226 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 4. | Misyaje | Chama cha Wakulima Misyaje | 995780001106 | NO. 227 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 5. | Machemba | Chama cha Wakulima Machemba | 995780001104 | NO. 228 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 6. | Mdabwa | Chama cha Wakulima Mdabwa | 995780001107 | NO. 229 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 7. | Chinunje | Skimu ya Chinunje | 995780001093 | NO. 230 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 8. | Kitanda-Tunduru | Skimu ya Kitanda | 995780001043 | | 19-November,2021 | Tunduru |
| 9. | Masonya | Umoja wa Wakulima Masonya | 995780001033 | NO. 232 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 10. | Nambalapi | Skimu ya Nambalapi | 995780001034 | NO. 244 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 11. | Mkalekawana | Skimu ya Mkalekawana | 995780001035 | NO. 242 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 12. | Legezamwendo | Skimu ya Legezamwendo | 995780001095 | NO. 234 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 13. | Lekindo | Skimu ya Lekindo | 995780001096 | NO. 233 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 14. | Mbati | Skimu ya Mbati | 995780001094 | NO. 243 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 15. | Kangomba | Skimu ya kangomba | 995780001188 | NO. 235 | 19-November,2021 | Tunduru |

| Na. | Scheme Name | Name of IO | Controll Number | REG. NO | Reg. Datea | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 16. | Mtonya | Skimu ya Mtonya | 995780001187 | NO. 236 | 19-November,2021 | Namtumbo |
| 17. | Naikula | Skimu ya Naikula | 995780001197 | NO. 237 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 18. | Mchengamoto | Skimu ya Mchengamoto | 995780001198 | NO. 238 | 19-November,2021 | Tunduru |
| 19. | Nyomboka | Chama cha Umwagiliaji Nyomboka | 995780001225 | NO. 239 | 19-November,2021 | Nyasa |
| 20. | Lundo | Chama cha Umwagiliaji Lundo | 995780001224 | No. 240 | 19-November,2021 | Nyasa |
| 21. | Mnkalachi | Chama cha Umwagiliaji Mnkalachi | 995780001226 | No. 241 | 19-November,2021 | Nyasa |
| 22. | Lipupuma | Chama cha Umwagiliaji Lipupuma | 99578000956 | | 19-November,2021 | Namtumbo |
| 23. | Njomlole | Chama cha Umwagiliaji Njomlole | | | 19-November,2021 | Namtumbo |
| 24. | Nasya | Chama cha Umwagiliaji Nasya | 99578000977 | | 19-November,2021 | Tunduru |
| 25. | Naluwale | Chama cha Umwagiliaji Naluwale | | | 19-November,2021 | Tunduru |
| 26. | Mkatamo | Chama cha Umwagiliaji Mkotamo | 99578000979 | | 19-November,2021 | Tunduru |
| 27. | Luhimbalilo | Chama cha umwagiliaji Luhimbalilo | 99578000955 | | 19-November,2021 | Namtumbo |
| 28. | Kitanda-Tunduru | Chama cha umwagiliaji Kitanda | 99578000954 | No. 231 | 19-November,2021 | Namtumbo |
| 29. | Ndongosi | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Ndongosi | | NO. 090 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 30. | Morogoro | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Morogoro | | NO. 089 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 31. | Muhukuru Lilai | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Muhukuru Lilai | | NO. 088 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 32. | Nambendo | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Nambendo | | NO. 088 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 33. | Parangu | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Parangu | | NO. 086 | 10-May-18 | Songea Vijijin i |
| 34. | Litapwasi | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Litapwasi | | NO. 087 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 35. | Litisha | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Litisha | | NO.084 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 36. | Mpitimbi A | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Mpitimbi A | | NO. 083 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 37. | Mpitimbi B | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Mpitimbi B | | NO. 082 | 10-May-18 | Songea Vijijini |

| Na. | Scheme Name | Name of IO | Controll Number | REG. NO | Reg. Datea | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 38. | Nakahuga | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Nakahuga | | NO.080 | 10-May-18 | Songea Vijijini |
| 39. | Hanga Ngadinda | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Hanga Ngadinda | | NO. 007 | 18-Dec-16 | Songea Vijijini |
| 40. | Amani | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Amani | | NO. 049 | 20-Oct-17 | Namtumbo |
| 41. | Msanjesi | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Msanjesi | | NO. 072 | 26-Mar-18 | Namtumbo |
| 42 | Namahoka | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Namahoka | | | 19-November,2021 | Namtumbo |

## IV. Ada ya Huduma ya Umwagiliaji na Tozo ya Urejeshaji wa Gharama za Uwekezaji katika Miundombinu ya Umwagiliaji.

Katika kila skimu ya Umwagiliaji kila mkulima wa umwagiliaji anayemiliki eneo ndani ya skimu anawajibika kutoa Ada ya Huduma za Umwagiliaji ambayo ni asilimia tano (5%) ya watani wa uzalishaji kwa ekali kwa kila msimu.

Aidha, Wamwagiliaji wanawajibu wa kurejesha gharama za uwekezaji wa gharama za ujenzi wa miundombinu ya miradi ya umwagiliaji ambayo serikali imewekeza ili kuiwezesha sreikali kuendelea kupanua eneo la umwagiliaji katika maeneo mengine yenye uhitaji.

## V. Ukadiriaji wa Viwango Vya Ada na Tozo

Baada ya mavuno, kamati ya usimamizi, Bodi za usimamizi za vyama vya wamwagiliaji kwa kusaidiana na Wataaalamu wa kilimo, watakokotoa wastani wa uzalisjai ulioafikiwa kwa ekali kwa kila zao linalolimwa katika skimu na kupata kiwango cha ada na tozo.

## VI. Ukusanyaji, Usimamizi na Matumizi ya Fedha za Ada na Tozo

Ofisi ya Umwagiliaji mkoa imefanikiwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa vyama na wakulima katika baadhi ya skimu kuhusu ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya fedha za ada na tozo, zoezi hili bado niendelevu tunaendelea nalo, kwa hiyo basi ili kupata matokeo tunahitaji ushirikiano kwa Maafisa kilimo wa Wilaya na walewaliopo katika maeneo ambayo yana skimu za Umwagiliaji.

Katika kulitekeleza hilo tumetoa maelekezo katika skimu **42** kwamba zifungue akaunti maalumu ya ada zimekwisha fanya hivyo.

Kwa mujibu wa aya ya 84 (3) ya kanununi za Umwagiliaji (2015), na kanuni ya marekebisho ya kanuni ya mwaka 2021, Ada ya 5% ya Huduma ya Umwagiliaji zitalipwa na wakulima pia zitahifadhiwa katika akaunti maalumu ya skimu.

Katika Mkoa wa Ruvuma ni skimu **42** zilizolipa Ada ya mwaka kati ya skimu 102 kiasi cha tshs 100,000 sawa na jumla ya tshs **4,200,000**, Wakati Ada ya Huduma za Umwagiliaji asimilia tano (5%) kwa ajili ya urejeshaji wa gharama za ujezi ni skimu **1** ya Muhukuru Lilahi iliyopunguza deni la **tshs 300,000** kati ya **tshs 1,000,000** kwahiyo skimu zote **101** hazijalipa.

**Jedwali Na.21: Ulipaji wa Ada kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji**

**(i) Skimu zilizojengewa miundombinu ya umwagiliaji**

| Mgawanyo wa Fedha za Ada ya Huduma za Umwagiliaji | Asilimia |
|---|---|
| Mfuko wa maendeleo ya UMwagiliaji | 50% |
| Huduma ya Uendeshaji na Matunzo ya Skimu | 50% |

**(ii) Skimu zisizojengewa miundombinu ya umwagiliaji**

| Mgawanyo wa Fedha za Ada ya Huduma za UMwagiliaji | Asilimia |
|---|---|
| Mfuko wa maendeleo ya Umwagiliaji | 25% |
| Huduma ya Uendeshaji na Matunzo ya Skimu | 75% |

**VII. Ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji Skimu ya Muhukuru Lilahi**

Katika mwaka wa 2022/2023 skimu ya umwagiliaji Muhukuru Lilahi imepatiwa fedha kiasi cha shilingi **915,744,605.00 na Mkandarasi**: M/S Muungano General Enterprises Co. Ltd atatekeleza kazi zote za ujenzi. Msimamizi wa kazi ni Mhnadisi wa Umwagiliaji Mkoa wa Ruvuma na Mwajiri Tume ya taifa ya Umwagiliaji **S.L.P 146, DODOMA.**

Mkandarasi alikabidhiwa kazi tarehe 25.09.2022, alianza kazi rasmi tarehe 01.09.2022 na anatarajia kuifanyakazi hii ya ujenzi kwa muda wa miezi 12 sawa ni siku 365.

**a) Kazi Atakazo Fanya Mkandaradi**

i. Ukarabati na ujenzi wa banio

ii. Urudishaji wa mto katika mkondo wake

iii. Ujenzi wa eneo mto ulipochepusha maji kwa kutumia **GABIONI.**

iv. Ujenzi Mfereji mkuu 1.7km
v. Ujenzi wa mifereji ya ndani ya shamba
vi. Ujenzi wa vigawa maji, viangusha maji na vivusha maji
vii. Ujenzi wa barabara ya shambani hadi kijijini 5km

**b) Kazi zilizofanywa na mkandarasi hadi hivi sasa**

i. Mandalizi ya awali
ii. Ujenzi wa kambi
iii. Usafishaji wa eneo la kazi katika banio, mfereji, na mto
iv. Kupima mfereji kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi
v. Ukusanyaji Mawe
vi. Ukusanyaji wa Mchanga

### 6.1.1.9 Kilimo cha Pamoja (Block Farming),

Mkoa wa Ruvuma umeainisha maeneo ya uwekezaji katika Kilimo cha pamoja **(Block Farming),** jumla ya hekta **25,171.91** zimetambuliwa kupitia Halmashauri. Maeneo haya ndio yatakayotumika kwa kilimo cha pamoja na uwekezaji. Eneo lililoainishwa kwa kuandaliwa ramani (GPS Coordinates) yameoneshwa katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na.22: Maeneo yaliyotambuliwa kwa kilimo cha pamoja katika Halmashauri**

| Halmashauri | Kijiji | Eneo (hekta) |
|---|---|---|
| Songea DC | Lilahi | 64.052 |
| | Liweta | 5.84 |
| | Magwamila A | 107.392 |
| | Magwamila B | 105.508 |
| | Matimila | 4,343.11 |
| | Nambendo | 107.392 |
| | Ndongosi | 19.208 |
| **Jumla Ndogo** | | **4,752.50** |
| Songea Manispaa | Tanga | 12.046 |
| | Mjimwema | 9.2468 |
| **Jumla Ndogo** | | **21.2928** |
| Madaba DC | Ndelenyuma | 222.48 |
| | Ndelenyuma-Livalamba | 73.64 |
| | Kipingo | 364.272 |
| | Mtyangimbole | 176.852 |
| | Ngadinda | 60.212 |
| | Mbangamawe | 196 |
| | Magingo | 400 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,493.46** |
| Namtumbo | Limamu | 266.13 |
| **Jumla Ndogo** | | **266.13** |
| Tunduru | Marumba | 909.424 |
| | Molandi | 1097.24 |
| | Misyage | 1948.152 |
| | Mbatamila | 7,308.74 |
| | Ngapa | 983.576 |
| | Songambele | 894.164 |
| | Mtonya | 588.72 |
| | Mindu | 760.876 |
| | Sauti Moja | 1125.048 |
| | Mkowela | 1601.944 |
| | Mwenge | 999.848 |
| **Jumla Ndogo** | | **18,217.74** |
| Nyasa DC | Hinga | 42.32 |
| **Jumla Ndogo** | | **42.32** |
| Mbinga DC | Kiyaka | 20 |
| **Jumla Ndogo** | | **20** |
| Mbinga TC | Kihungu | 100.8 |
| | Kilimani | 120 |

| Halmashauri | Kijiji | Eneo (hekta) |
|---|---|---|
| | Mpepai | 200 |
| **Jumla Ndogo** | | **420.8** |
| **Jumla Kuu ya Mkoa** | | **25,171.91** |

#### 6.1.1.10 Ujenzi wa Maghala Vijijini

Mkoa wa Ruvuma kupitia Wizara ya Kilimo una mpango wa kujenga maghala 31 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 kila moja katika Halmashauri za Madaba (11), Songea DC (12) na Namtumbo (8) kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 kupitia program ya ujenzi wa maghala kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya nafaka.

Mbali na kigezo cha uzalishaji, maeneo hayo yamezingatia uwepo wa miundombinu ya barabara na umeme, ujenzi huu wa maghala kupitia programu hii kitaifa Ruvuma tumepewa asilimia 50 ya maghala yote yatakayojengwa Tanzania bara (Maghala 62). Hatua za awali za maandalizi zimeshafanyika kwa kuyatambua maeneo, kusafisha na kuwafikisha Wakandalasi kwenye maeneo hayo. Aidha, Wizara ya Kilimo inaendelea kukamilisha taratibu za mwisho ili kazi ianze.

Pamoja na mradi huu, serikali kupitia mpango wa matokeo makubwa sasa(BRN) ilikuwa na ujenzi wa maghala 25 katika Halmashauri ya Songea na Madaba, maghala 5 yalikamilika na mengine yako katika hatua mbalimbali za ujenzi, Wizara ya kilimo inaandaa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maghala haya .

### 6.1.1.11 Mipango na Malengo ya Kuendeleza Zao la Parachichi

#### i. Kilimo cha Parachichi

Mkoa wa Ruvuma sambamba na kuzalisha mazao mengine pia unazalisha zao la parachichi, uzalishaji wa zao hili awali haukufanyika kibiashara na wakulima walikuwa wakizalisha mbegu za kienyeji. Soko la parachichi hizi lilikuwa ni la ndani ambapo wakulima walikuwa wakiuza katika masoko kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Katika msimu wa mwaka **2021/2022** Mkoa umezalisha tani **1,768** katika eneo la hekta **2,446.** Uzalishaji huu unafanyika hasa katika Halmashauri za Wilaya tano ambazo ni Madaba DC, Mbinga DC, Mbinga TC, Nyasa DC pamoja na Songea DC.

### ii. Mpango wa Kuendeleza Zao la Parachichi

Mkoa umelenga kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi kama zao lingine la biashara kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujipatia fedha hususani katika miezi ya Februari mpaka Mei. Mkoa umeanza mpango huu kwa kuongeza eneo la uzalishaji kutoka hekta **2,446** zinazozalisha tani **1,768** hadi kufikia hekta **10,000** zitakazozalisha tani **37,500** ifikapo mwaka **2025.** Uzalishaji huu utafikiwa kwa kuweka mikakati itakayoongeza tija ya uzalishaji. Mfano tija ya uzalishaji kwa eneo kwa sasa ipo chini, ambapo uzalishaji kwa eneo la hekta moja ni tani **0.7228.** Miongoni mwa mikakati inayotekelezwa na iliyopangwa kutekelezwa na Mkoa katika kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi ni;

Kuwezesha vikundi vya wakulima, mpango huo unafanywa na Mkoa kwa kushirikiana na wabia wa Maendeleo kutoka Taasisi ya **SAGCOT**, Kupitia Kongani ya Ihemi. Utekelezaji huu unafanyika kupitia vikundi vya Wakulima kama ifuatavyo;

- Kuwaunganisha Wakulima katika vikundi;
- Kuwapatia mbegu za parachichi na kuzipanda katika kitalu;
- Kuwafundisha wakulima namna ya Kuanzisha kitalu cha miche ya parachichi;
- Kuwafundisha wakulima namna ya kubadi (grafting);
- Kuwafundisha wakulima namna ya kuandaa shamba;
- Kuwafundisha wakulima namna ya Kupanda miche mashambani; na
- Kuwafundisha wakulima namna ya kuhudumia miche ya parachichi

Hadi sasa Mkoa umezifikia kata **5** na vikundi **10** kwa mchanganuo ufuatao;

**Jedwali Na.23: Idadi ya Kata na Vikundi Vilivyofikiwa na Mradi**

| Na | Halmashauri | Kata | Vikundi | wanachama | Ekari | Idadi ya miche |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Songea DC | Litapwasi – Lyangweni | 1 | 47 | 47 | 4000 |
| | | Uyahudini | 1 | 30 | 30 | 3000 |
| | | Ndongosi – Namatuhi | 1 | 50 | 50 | 5000 |
| | | Liganga | 1 | 37 | 37 | 1500 |
| | | Selekano | 1 | 57 | 57 | 4,000 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Peramiho- Nguvu moja | 1 | 64 | 64 | 6000 |
| | | Mbinga mhalule | 1 | 15 | 15 | 1500 |
| | | Nakahegwa | 1 | 10 | 10 | |
| | | Shule ya Sekondari Liganga | | | 1 | 100 |
| | | Shule ya Sekondari Peramiho | | | 1 | 100 |
| | | Kanisa Katoliki Peramiho | | | 3 | 300 |
| 02 | Mbinga DC | Magereza | | | 5 | 500 |
| 03 | Namtumbo DC | Hanga Monasteli ST. Nicholous | | | 5 | 500 |
| **Jumla Kuu** | | | | | **324** | **32,400** |

## 6.1.2 SEKTA YA USHIRIKA

### 6.1.2.1 Utangulizi

Mkoa una jumla ya Vyama vya Ushirika **293**, kati ya hivyo AMCOS **222**, Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) **62**, Vyama vingine **6** na Vyama Vikuu (UNION) **3** ambavyo ni TAMCU Ltd, SONAMCU Ltd, na MBIFACU Ltd.

Mchanganuo wa Vyama vya Msingi (AMCOS) kwa ajili ya Kahawa ni vyama **111**, Korosho **47**, Tumbaku **42**, na mazao mchanganyiko **22**. Vyama vya msingi vya zao la Kahawa, Korosho na Tumbaku pia vinahudumia wakulima wa mazao ya nafaka katika maeneo yao kwa kufuata Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.

### 6.1.2.2 Utekelezaji wa Shughuli za Ushirika

### i. Usajili wa Vyama vya Ushirika

Ofisi ya Mrajisi Msaidizi wa Mkoa inaendelea na jukumu la usajili wa Vyama vya Ushirika ambavyo vinawasilisha maombi kupitia Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 kuishia mwezi Novemba, 2022 jumla ya vyama vitatu (3) vya msingi vimeandikishwa. Vyama hivyo ni **Umami, Kimaki Na Mkilimasi**

**ii. Ufutaji wa Vyama**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imefuta Vyama vya Ushirika vya Kifedha kutoka katika rejista ya Vyama tarehe 26 Julai 2022. Vyama vilivyofutwa katika Mkoa wa Ruvuma ni 23 ambavyo ni Vyama vya Kifedha (SACCOS). Sababu za kufutwa kwa vyama hivyo ni kushindwa kutekeleza majukumu ya kuandikishwa kwayo ikiwemo kushindwa kutoa huduma za mikopo kwa wanachama.

**Jedwali Na 24: Vyama vya Kifedha (SACCOS) vilivyofutwa Tarehe 26 Julai 2022**

| **Na** | **Jina La Chama** | **Halmashauri** |
|---|---|---|
| 1 | Tujiunge | Tunduru |
| 2 | Ukombozi | Tunduru |
| 3 | Mataka | Tunduru |
| 4 | Jikwamue | Tunduru |
| 5 | Ruhekei | Nyasa |
| 6 | Dassota | Nyasa |
| 7 | Narwi | Namtumbo |

| Na | Jina La Chama | Halmashauri |
|---|---|---|
| 8 | Kitanda | Namtumbo |
| 9 | Ligera | Namtumbo |
| 10 | Luchili | Namtumbo |
| 11 | Lusewa | Namtumbo |
| 12 | Mkongo | Namtumbo |
| 13 | Mgombasi | Namtumbo |
| 14 | Ruhuwiko Sekondari | Songea Manispaa |
| 15 | Beroya Sekondari | Songea Manispaa |
| 16 | Songea Kwanza | Songea Manispaa |
| 17 | Veta | Songea Manispaa |
| 18 | Tancoal | Mbinga Dc |
| 19 | Kilimo | Mbinga Dc |
| 20 | Jiendeleze | Mbinga Tc |
| 21 | Tujikomboe Mpitimbi | Songea Dc |
| 22 | Kilagano | Songea Dc |
| 23 | Hoja | Songea Dc |

**iii. Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika**

Jukumu la ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Ushirika limeendelea kutekelezwa ambapo Vyama **204** vimekaguliwa na COASCO (Ukaguzi wa Nje) kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022. Aidha Ukaguzi wa Ndani umefanyika kwa vyama **163** kupitia Maafisa Ushirika wa Halmashauri. Katika kipindi cha Julai-Septemba 2022 Ukaguzi wa nje umefanyika kwa AMCOS **38** na ukaguzi wa ndani umefanyika kwa Vyama **34.** Mapungufu yaliyobainishwa katika ukaguzi ni pamoja na; Uandishi wa nyaraka usioridhisha, Mwitikio mdogo wa kukaguliwa, Utunzaji usioridhisha wa mali za Chama katika rejista ambapo mali nyingi haziingizwi vitabuni na kutokuwa na mikataba kwa watendaji. Mafunzo yameendelea kutolewa kwa watendaji ili kuboresha utendaji kazi na kuleta ufanisi.

**iv. Elimu na Mafunzo**

Kamati ya Elimu Mkoa (KAMEURU) inayoongozwa na Mrajis Msaidizi inaendelea na utoaji wa elimu kwa wadau mbali mbali wa Vyama vya Ushirika. Julai,2021 hadi Juni 2022 Idadi ya Vyama vilivyopata mafunzo ni **105**.

Katika miezi ya Julai – Novemba,2022 mafunzo yametolewa kwa Vyama vya Ushirika **17** ambapo jumla ya washiriki 292 walipata mafunzo. Kati ya hao, wanaume **125** na wanawake **167**. Lengo la mafunzo ni kuvijengea Vyama uwezo ili vifanye kazi kulingana na Sheria na Kanuni zake.

#### 6.1.2.3 Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani

Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi za Mazao pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia *Bodi ya* Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na wadau wa mazao ya Ufuta, Soya, Mbaazi, Korosho, Kahawa unaratibu masoko ya mazao ya kipaumbele kwa njia ya minada inayosimamiwa na Vyama Vikuu vya Ushirika (SONAMCU LTD, TAMCU LTD na MBIFACU LTD).

Mfumo wa Stakabadhi ulianza kupitia zao la Korosho msimu wa 2016/2017 na Mazao mchanganyiko (Soya, Ufuta na Mbaazi) ulianza msimu 2018/2019. Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unatekelezwa kwa kuzingatia Mwongozo ulioandaliwa kwa ushirikiano wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi ya Usimamizi wa Maghala.

#### 6.1.2.4 Uendeshaji wa Masoko (Mazao ya Ufuta, Soya na Mbaazi)

Uendeshaji wa masoko ya mazao ya Ufuta, Mbaazi na Soya hufanyika kupitia wakulima kukusanya mazao kupitia Vyama vya Msingi **95** na Vyama Vikuu **2,** kati ya hivyo Namtumbo vyama **44**, Songea **13**, Mbinga **5**, Nyasa **1** na Tunduru **35**.

**(i) Zao la Ufuta**

Kwa msimu wa kilimo 2021/2022 minada ya Ufuta ilianza katika Ghala la Lilambo OTC tarehe 31/05/2022 na kuishia tarehe 10/08/2022, jumla ya minada 20 imefanyika ambapo Songea na Namtumbo (chini ya SONAMCU) minada **15** na Tunduru (TAMCU) **5**. Jumla ya kilo zilizouzwa ni **7,970,176.60** zenye thamani ya shilingi **23,407,997,111.65.**

Aidha; kwa vipindi vya misimu minne ya kilimo kutoka msimu wa 2018**/2019** hadi kufikia Msimu **2021/2022** Mkoa wa Ruvuma ulikusanya Ufuta jumla ya kilo **36,959,888** na kuuza kwa wastani wa bei **sh. 2,508** na kuwapatia wakulima jumla ya Fedha **sh. 87,961,918,144.00.** Kabla ya mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuanza kutumika, zao la Ufuta liliuzwa kwa utaratibu wa soko huria kwa bei ya chini kati ya sh**. 500 hadi sh.700** kwa kilo. Jedwali namba 25 linachanganua.

**Jedwali Na.25 : Mwenendo wa Mauzo ya Ufuta Kwa Misimu Minne Kupitia Vyama Vya Ushirika**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha kwa kulima (TSh) |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | 8,428,268 | 2,952 | 24,882,415,441 |
| 2019/2020 | 12,234,757 | 2050 | 23,153,671,988.58 |
| 2020/2021 | 8,326,686 | 2,157 | 17,221,852,087.00 |
| 2021/2022 | 7,970,176.60 | 2,874 | 22,703,978,627.45 |
| **JUMLA** | **36,959,888** | **2,508** | **87,961,918,144.00** |

**(ii) Zao la Soya**

Kwa msimu wa kilimo **2021/2022** imefanyika minada saba **(7)** ambapo mnada wa kwanza ulianza tarehe 14/06/2022 na kuishia tarehe 24/08/2022, jumla ya kilo **5,152,290.40** zenye thamani ya kiasi cha shilingi **6,267,650,000.70.**

Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo minne mfululizo kutoka msimu wa **2018/2019** hadi kufikia **2021/2022** jumla ya kilo **10,184,254.00** za Soya zilikusanywa na kuuzwa kwa wastani wa bei **sh. 1139** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha sh. **11,501,746,169.70** Kabla ya mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuanza kutumika, zao la Soya liliuzwa kwa soko utaratibu wa soko huria kwa bei ya chini kati ya sh**. 500-600** kwa kilo. Jedwali namba 26 linaonesha mchanganuo.

**Jedwali Na.26: Mwenendo wa Mauzo ya Soya Kwa Misimu Minne Kupitia Vyama Vya Ushirika**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha za Mkulima (TSh) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | 2,643,944 | 765 | 2,021,697,476.00 |
| 2019/2020 | 1,297,821 | 1,283 | 1,665,196,005.00 |
| 2020/2021 | 1,090,199 | 1,327 | 1,547,202,688.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 5,152,290 | 1181 | 6,267,650,000.70 |
| **JUMLA** | **10,184,254.00** | **1139** | **11,501,746,169.70** |

**(iii) Zao la Mbaazi**

Kwa msimu wa kilimo **2021/2022** imefanyika minada kumi na moja **(11)** ambapo ilianza tarehe **30/08.2022** katika Wilaya ya Tunduru na kuishia tarehe 29/10/2022. Tunduru imefanya minada sita (6) na Namtumbo minada mitano (5). Katika minada hiyo kumi na moja jumla ya **kilo 6,646,826.00** za Mbaazi ziliuzwa ambapo bei ya wastani ni shilingi **880** na kufanya jumla ya malipo kuwa shilingi **5,583,675,414.03.**

Aidha, Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo minne mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2018/2019** hadi **2021/2022** jumla ya kilo **17,5 18,812,506**

za Mbaazi zilikusanywa na kuuzwa kwa wastani wa bei **sh. 857.25** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha sh. **17,664,212,655** Kabla ya mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuanza kutumika, zao la Mbaazi liliuzwa kwa bei kati ya **sh.150 Hadi 200** kwa kilo. Jedwali namba 27 linachanganua.

**Jedwali Na.27: Mwenendo wa Mauzo ya Mbaazi Kwa Misimu Minne Kupitia Vyama Vya Ushirika**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha Zilizopatikana (TSh) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2018/2019 | 775,543 | 724 | 561,805,805 |
| 2019/2020 | 4,280,777 | 515 | 2,205,617,364 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 7,109,360 | 1,310 | 9,313,114,072 |
| 2021/2022 | 6,646,826 | 880 | 5,583,675,414 |
| **JUMLA** | **18,812,506** | **857.25** | **17,664,212,655** |

#### 6.1.2.4 Uendeshaji wa Masoko (Mazao ya Korosho na Kahawa)

### (i) Zao la Kahawa

Msimu wa masoko wa 2022/2023 minada ya kahawa ilianza tarehe 8/09/2022 huko Moshi. Mpaka kufikia tarehe 24/11/2022 imekwishafanyika minada nane (katika minada ya Mbinga, Songwe na Moshi) yenye kilo **3,068,717.50** na kupata dola **9,032,528.68** sawa na shilingi **20,910,313,151.45** bei ya juu ikiwa ni Sh. **7882.67** na bei ya chini ikiwa **4,747.37. Minada bado inaendelea**

**A**idha, Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo mitano **(5)** mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2017/2018** hadi kufikia msimu **2020/2021** jumla ya kilo **77,664,927.75** za kahawa zilikusanywa na kuuzwa kwa watani wa bei **sh. 4,638** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha **sh. 353,263,592,542.45**.Mchanganuo wa mauzo umeoneshwa hapo chini.

**Jedwali Na.28 : Kahawa Zilizouzwa na Fedha Iliyopelekwa Kwa Wakulima**

| Msimu | Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha Zilizopatikana (TSh) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 15,393,500 | 4,300 | 66,192,050,000 |
| 2017/2018 | 20,162,900 | 3,700 | 74,602,730,000 |
| 2018/2019 | 15,675,100 | 4,086 | 64,048,458,600 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 12,676,844 | 4,000 | 50,707,376,000 |
| 2020/2021 | 13,756,583.75 | 7103 | 97,712,977,942.45 |
| **JUMLA** | **77,664,927.75** | **4638** | **353,263,592,542.45** |

**(ii) Zao la Korosho**

Kwa msimu wa masoko **2022/2023** minada ilianza tarehe 10/11/2022.Hadi kufikia tarehe 24/12/2022 Mkoa ulikusanya jumla ya kilo **6,123,688** za Korosho zenye thamani ya shilingi bil. **11,406,932,180** ambazo ziliuzwa kwa wastani wa bei **sh. 1852.33** kwa kilo. **Minada inaendelea.**

Aidha, Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo minne mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2017/2018** hadi kufikia msimu **2020/2021** jumla ya kilo **104,819,739.00** za Korosho zilikusanywa na kuuzwa kwa wastani wa bei **sh. 2,801** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha **sh. 291,995,086,617.54**

**Jedwali Na.29: Ununuzi wa Korosho Katika Misimu Mitano (5) na Wastani wa Bei.**

| Msimu | Korosho Zilizo Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei | Fedha Zilizopatikana (TSh) Bilioni |
|---|---|---|---|
| 2017/2018 | 20,912,569 | 3,815 | 79,777,589,485.68 |
| 2018/2019 | 18,586,248 | 3,300 | 61,334,618,400.00 |
| 2019/2020 | 24,625,824 | 2,650 | 65,246,638,727.00 |
| 2020/2021 | 15,410,605 | 2,273 | 35,025,780,579.00 |
| 2021/2022 | 25,284,493 | 1971 | 50,610,459,425.86 |
| **JUMLA** | **104,819,739.00** | **2,801** | **291,995,086,617.54** |

### (iii) Uendeshaji wa Zao la Tumbaku

Kwa msimu wa masoko **2022/2023** Mkoa ulikusanya jumla ya kilo **550,836** za tumbaku zenye thamani ya dola za kimarekani **831,766** ambazo ziliuzwa kwa wastani wa bei **USD. 1.37** kwa kilo.

Aidha, Mkoa wa Ruvuma kwa vipindi vya misimu ya kilimo mitano mfululizo kutoka msimu wa kilimo **2017/2018** hadi kufikia msimu **2021/2022** jumla ya kilo **4,070,403.33**

za tumbaku zilikusanywa na kuuzwa kwa wastani wa bei **USD. 1.39** na kuwapatia wakulima jumla ya fedha **USD. 5,757,545.22**

**Jedwali Na.30 : Ununuzi wa Tumbaku Katika Misimu Mitano (5) na Wastani wa Bei.**

| Msimu | Tumbaku Zilizo Nunuliwa (Kgs) | Wastani wa Bei USD | Fedha Zilizopatikana USD |
|---|---|---|---|
| 2017/2018 | 804,947.28 | 1.23 | 990,962.30 |
| 2018/2019 | 1,247,814.75 | 1.49 | 1,864,382.12 |
| 2019/2020 | 785,659.30 | 1.41 | 1,108,740.80 |
| 2020/2021 | 731,143 | 1.32 | 961,664.00 |
| 2021/2022 | 550,836 | 1.37 | 831,766.00 |
| **JUMLA** | **4,120,400.33** | **1.39** | **5,735,515.22** |

#### 6.1.2.5 Uendelezaji wa Miradi ya Kiuchumi ya Vyama Vya Ushirika

Serikali kupita vyama vya Ushirika imetekeleza na inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi kama ifuatayo:

- Usimamizi wa uendelezaji wa ujenzi wa kiwanda cha vifungashio cha chama kikuu SONAMCU Ltd wilayani Namtumbo.
- Ukarabati wa maghala 5 kati ya 7 ya chama kikuu cha MBIFACU Ltd
- Ukarabati wa MBICU Hotel
- Usimamizi wa uendelezaji wa Mradi wa kiuchumi wa shamba la kahawa la chama kikuu cha MBIFACU Ltd
- Ujenzi wa Mradi wa shule ya Sekondari ya Mahenge AMCOS Ltd
- Ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao ya wakulima la chama cha Msingi Kimuli na Namitili (AMCOS)

#### 6.1.2.6 Uendelezaji wa Kilimo Cha Zao la Ufuta, Soya na Mbaazi

Mkoa wa Ruvuma katika msimu wa 2022/2023unaendelea na utekelezaji wa mpango wa kilimo cha mazao haya kupitia kilimo cha pamoja (block Farming). Ikiwa na lengo la kuongeza uzalishaji na kuweza kumpatia tija mkulima.

#### 6.1.2.7 Maandalizi ya Msimu wa Korosho

Msimu wa mauzo ya Korosho Kitaifa umefunguliwa rasmi Septemba 8 2022 katika Mkutano Mkuu wa wadau wa korosho nchini uliofanyika katika ukumbi wa Familia Takatifu Bombambili Songea katika Mkoa wa Ruvuma. Mkoa unatarajia kufanya Mkutano wa wadau wa Korosho hivi karibuni. Makadirio ya uzalishaji ni tani 32,000 sawa na kilo 32,000,000.

#### 6.1.2.8 Mafanikio Katika Usimamizi wa Mazao

i. Wakulima kupata bei nzuri ya mazao hususani mazao yanayouzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
ii. Kuwepo kwa ushirikiano nzuri kwa wadau wa stakabadhi ghalani kwa ngazi zote;
iii. Kuwepo kwa matumizi sahihi ya vipimo/ mizani, ambayo inasaidia mkulima asinyonywe
iv. Uamshaji wa Vyama vya Msingi sinzia ambavyo kwa sasa vinafanya kazi vizuri;
v. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao yanayouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.
vi. Uwekezaji unaofanywa na Vyama vya msingi katika ujenzi wa maghala, ununuzi wa magari ya kubebea mazao na ujenzi wa shule ya Sekondari na ujenzi wa kiwanda cha Vifungashio

#### 6.1.2.9 Changamoto

i. Kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaopinga mfumo wa stakabadhi za ghala kwa faida binafsi.
ii. Utoroshwaji wa mazao hasa zao la soya

#### 6.1.2.10 Utatuzi wa changamoto

I. Elimu iendelee kutolewa kwa wadau mbalimbali wa mfumo
II. Kuendelea kuimarisha usimamizi katika ngazi ya Halmashauri

### 6.1.3 SEKTA YA MIFUGO

#### 6.1.3.1 Utangulizi

Katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Mifugo Mkoa wa Ruvuma umeendelea kuboresha huduma za ugani, uzalishaji wa mifugo, uendelezaji wa nyanda za malisho kwa mfumo wa ranchi ndogo, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo, uboreshaji wa

miundombinu ya mifugo, masoko ya mifugo pamoja na miundombinu ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo kama ifuatavyo:-

#### 6.1.3.2 Utekelezaji wa utoaji wa huduma za ugani

##### a) Idadi ya watumishi wa Mifugo

Mkoa wa Ruvuma una watumishi wa ugani **109** wa mifugo na uvuvi kati ya watumishi **677** wanaohitajika. Idadi hiyo ya maafisa ugani inaufanya mkoa kuwa na upungufu wa maafisa ugani mifugo **568** kwa mchanganuo wa ufuatao:-

**Jedwali Na. 31 Idadi ya Maafisa Mifugo mkoa wa Ruvuma**

| | Idadi ya Maafisa Mifugo | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Sekretarieti ya Mkoa** | **Tunduru DC** | **Nyasa DC** | **Songea DC** | **Madaba DC** | **Mbinga DC** | **Mbinga Mji** | **Namtumbo DC** | **Songea Manispaa** | **Jumla** |
| Mahitaji | 3 | 157 | 84 | 64 | 35 | 100 | 73 | 66 | 95 | **677** |
| Waliopo | 2 | 16 | 18 | 9 | 8 | 16 | 7 | 14 | 19 | **109** |
| Upungufu | 1 | 141 | 66 | 55 | 27 | 84 | 66 | 52 | 76 | **568** |
| Waliopo kwenye mpango wa kuajiriwa | 0 | 0 | 95 | 14 | 15 | 0 | 66 | 16 | 25 | **231** |

Pamoja na upungufu huo wa maafisa ugani Mkoa unaendelea kutoa huduma za ugani kwa kuwatumia maafisa ugani waliopo kuhudumia wastani wa vijiji **5** badala ya kijiji kimoja.

#### 6.1.3.3 Mashamba Darasa

##### A. Mashamba Darasa ya Ufugaji wa Kuku

Ili kuimarisha ufugaji wa kisasa wa kuku pamoja na kuongeza uzalishaji wa kuku na mayai, Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi inategemea kuwa na mashamba darasa ya kufugia kuku katika Manispaa ya Songea ambapo vikundi vitatu **(3)** vya wafugaji wa Kuku vitapokea vifaranga wa Kuku **4,000** aina ya Sasso. Vikundi hivi vitajengewa miundombinu ya kufugia kuku pamoja na kupewa vyakula na madawa ya kutunza kuku kwa mwezi mmoja, kuku watakaofugwa watatumika kwa ajili ya kujifunzia ufugaji wa kuku na kugawa kwa vikundi vingine vya ufugaji kuku.

##### B. Mashamba Darasa ya Malisho

Athari za kupungua kwa malisho zimeendelea kujitokeza mara kwa mara kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na mifugo, mabadiliko ya tabia ya nchi na mtazamo wa wafugaji kutegemea malisho ya asili tu. Athari hizo zimesababisha mifugo kudhoofika na wakati mwingine kufa kwa kukosa malisho na maji.

Katika jitihada za kukabiliana na athari hizo, Wizara imeandaa mpango wa kuwajengea uwezo wafugaji kuzalisha, kutunza na kuhifadhi malisho kupitia utaratibu wa mashamba darasa ya malisho katika maeneo ya malisho. Katika utekelezaji wa mpango huu kazi zote zitakazohitaji nguvu kazi zitafanywa na vikundi vya vijana waliopo kwenye maeneo husika. Lengo la mpango huu ni kubadili mtazamo wa wafugaji kutegemea malisho ya asili tu na kuboresha maeneo ya malisho yaliyopo. Wizara imepanga kuanzisha mashamba darasa ya malisho **9** yenye jumla ya ukubwa wa ekari **45** katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Songea, Namtumbo na Tunduru. Lengo kuu la mpango huu ni kuwajengea uwezo wafugaji kuzalisha, kutunza na kuhifadhi mbegu na malisho kwa kutumia utaratibu wa mashamba darasa.

#### 6.1.3.4 Uzalishaji wa Mifugo na Mazao Yake

Mkoa wa Ruvuma una mifugo **3,354,927** idadi hiyo inajumuisha ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, Kuku, Bata, Punda, Mbwa na mifugo mingine midogo midogo kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na 32.**

**Jedwali Na. 32 Idadi ya Mifugo**

| | TUNDURU | NAMTUMBO | MBINGA DC | NYASA | SONGEA DC | MADABA | SONGEA MC | MBINGA TC | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Ng'ombe** | 68,440 | 50,853 | 36,856 | 22,290 | 27,307 | 17,766 | 5,405 | 6,211 | **235,128** |
| **Mbuzi** | 30,235 | 54,465 | 102,563 | 39,585 | 37,665 | 6,648 | 4,992 | 17,208 | **293,361** |
| **Kondoo** | 8,206 | 4,162 | 9,481 | 4,911 | 3,651 | 576 | 107 | 2,765 | **33,859** |
| **Nguruwe** | 4,135 | 5,949 | 100,591 | 41,653 | 48,653 | 8,560 | 3,237 | 19,932 | **232,710** |
| **Kuku** | 316,355 | 199,248 | 346,660 | 160,083 | 254,841 | 79,315 | 810,229 | 264,243 | **2,430,974** |
| **Bata** | 17,386 | 2,708 | 4,105 | 3,985 | 3,867 | 2,504 | 1,125 | 2,311 | **37,991** |
| **Bata mzinga** | | - | - | - | 91 | 21 | 36 | 23 | **171** |
| **Kanga** | 2,357 | 127 | 2,391 | - | 15,041 | 29 | - | 241 | **20,186** |
| **Sungura** | 523 | 253 | 423 | - | 621 | 178 | 103 | 123 | **2,224** |
| **Njiwa** | | 1,905 | 8,408 | - | 1,142 | 1,786 | - | 251 | **13,492** |
| **Punda** | 81 | 197 | 57 | 12 | 457 | 52 | 151 | 6 | **1,013** |
| **Mbwa** | 2,725 | 5,051 | 13,781 | 6,257 | 4,642 | 4,998 | 2,296 | 3,213 | **42,963** |
| **Paka** | 359 | 1,029 | 5,898 | 1,367 | 721 | 835 | 378 | 268 | **10,855** |

Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Septemba 2022 uzalishaji wa mazao yatokanayo na Mifugo umefikia tani **3,555.41** za nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo, tani **1,732** za nyama ya nguruwe tani **2010.79** na tani **603** za nyama ya kuku. Uzalishaji

wa maziwa umefikia lita **1,120,807.2** wakati uzalishaji wa mayai umefikia mayai **29,439,196,** vipande vya ngozi za ng'ombe zilizozalishwa ni **22,572,** vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo ni **19,500.**

#### 6.1.3.5 Utoaji wa Huduma Za Mifugo

**Udhibiti wa Magonjwa**

Mkoa wa Ruvuma umeendelea na shughuli za udhibiti wa magonjwa ambapo kwa kipindi cha Mwezi Julai 2021 hadi Septemba, 2022 magonjwa yaliyojitokeza zaidi ni Ndigana kali, Ndigana baridi, Homa ya Mapafu kwa ng'ombe na mbuzi, ugonjwa wa Mapele ngozi, Kideri na homa ya matumbo kwa kuku na Ndui.

Ili kukabiliana magonjwa ya Mifugo, Mkoa umesimamia utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ambapo Ng'ombe **6,273** wamepatiwa chanjo dhidi ya Homa ya Mapafu (CBPP), mbwa **8,749** na paka **38** wamepatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha Mbwa (Rabies), Kuku **182,327** dhidi ya Ugonjwa wa Kideri, ugonjwa wa Ndui na ugonjwa wa Gumboro.

Katika utekelezaji wa zoezi la uogeshaji wa mifugo michovyo **118,590** imefanyika kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Septemba, 2022.

Matokeo ya uogeshajikatika Mkoa wa Ruvuma ni kupungua kwa vifo vya mifugo vitokanavyo na magonjwa yaenezwayo na kupe na ndorobo.

Pamoja na jitihada hizi katika zoezi la uogeshaji mifugo kuna changamoto ambazo ni pamoja na;

i) Uchache wa mifugo inayoogeshwa kwa majosho yaliyo mengi, hivyo kupelekea ugumu wa uendeshaji wa majosho kwasababu majosho yaliyo mengi yalijengwa kwa ajili ya uogeshaji ng'ombe na mbuzi wa maziwa.

ii) Kukosekana kwa majosho ya kuogeshea Mifugo katika vijiji **24** vyenye maeneo ya kuchungia kwa mfumo wa ranchi ndogo. Hali hii imepelekea kuendelea kuwepo kwa vifo vya Mifugo kutokana na magonjwa yaenezwayo na kupe na ndorobo katika ranchi hizo.

Kwa sasa Mkoa kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejenga Majosho **11** katika Halmashauri za Tunduru majosho tisa **(9),** Songea DC Josho moja **(1)** na Nyasa Josho moja **(1)** kwa thamani ya Tshs **246,000,000.00.** Hata hivyo mkoa umeendelea kushikirikiana na Wizara na kupitia bajeti ya mwaka 2022/2023 unategemea kujenga Majosho mapya **2** katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwenye Kijiji cha Njalila Kata ya Mgazini na Kijiji cha Nambendo Kata ya Ndongosi kwa thamani ya Tshs. **44,000,000.00**

**Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa**

Mkoa una mbwa **43,919** ambao wako wanaofugwa kisasa na wengine wanaofugwa kiholela. Kufuatia kuwepo kwa idadi kubwa ya mbwa wanaozurura mitaani na kuwa kero kwa ustawi na afya ya jamii inayotuzunguka, kumekuwa na jitihada za kuchanja mbwa ili kudhibiti ugonjwa huu unaoathiri wanyama na binadamu kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba, 2022 mbwa **8,749** walichanjwa. Pia kumekuwepo na matukio **172** ya mbwa kung'ata binadamu. Pamoja na juhudi hizo Mkoa unaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa, kampeni ya uchanjaji mbwa, na kuua mbwa wote wanaozurura ili kuendelea kuilinda jamii dhidi ya ugonjwa huu.

Mkoa ulipokea dozi **1000** za chanjo ya kichaa cha Mbwa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuadhimisha wiki ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa wa mbwa. Wiki hiyo iliadhimishwa kuanzia tarehe 26 Septemba 2022 hadi tarehe 02 Oktoba 2022 ambapo mbwa **2,717** walichanjwa.

### 6.1.3.6 Utekelezaji wa Uboreshaji Miundombinu ya Masoko na Biashara ya Mifugo

### i). Uongezaji Thamani Zao la Maziwa

Pia katika jitihada za kuimarisha mnyororo wa thamani wa maziwa, Mkoa umefanya uchunguzi wa ugonjwa wa kutupa mimba (brucelosis) kwa ng’ombe wa maziwa **104** katika Halmashuri ya Mbinga Mji.Mkoa unaendelea kuhamasisha wafugaji zaidi waweze kupima ng’ombe zao ili kuzuia maambukizi zaidi.

Kwa upande wa usindikaji wa Maziwa Mkoa una wasindikaji wadogo **6** wanaosindika wastani wa lita **201,600** kwa mwaka. Aidha ,ili kuimarisha lishe kwa jamii wananchi wanaendelea kuhamasishwa kunywa maziwa ili kufikia lengo la unywaji wa lita **200** za maziwa kwa kila mtu kwa mwaka.

### ii). Minada ya Mifugo na Uongezaji Thamani Zao la Nyama

Mkoa kwa kushirikiana na Bodi ya Nyama ulifanya ukaguzi wa mabucha **156** na machinjio **6** za nyama ya ng’ombe na nguruwe katika Manispaa ya Songea na Halmashauri ya Mbinga MjI ili kumlinda mlaji na kuhakikisha kuwa bucha zote zinasajiliwa na kukidhi vigezo vya kuuza nyama bora. Wafanayabishara wote walipewa muda wa miezi sita **(6)** kufikia Disemba 2022 wawe wameanza kutumia Misumeno ya kukatia nyama na magogo ya Plastiki ili kuhakikisha kuwa nyama inakuwa na ubora unaotakiwa.

Pia Mkoa una viwanda viwili vya kusindika nyama katika Abbasia ya Peramiho na Chipole Sisters Halmashauri ya Wilaya ya Songea maarufu kwa usindikaji wa ***sausages*** za nyama wastani wa tani **100** za nyama kwa mwaka.

Katika kuimarisha biashara ya Ng’ombe, Mbuzi na Kondoo Mkoa una Mnada mmoja **(01)** wa upili katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba Kijiji cha Mtyangimbole na minada sita (**06**) ya awali katika kijiji cha Ruanda (Mbinga), Lituhi Nyasa, Muhuwesi (Tunduru), Mhepai (Songea), Ligera na Lismonji (Namtumbo) kwa ajili ya kufanyia biashara ya mifugo

#### 6.1.3.7 Uendelezaji wa Nyanda za Malisho kwa Mfumo wa Ranchi Ndogo na Udhibiti wa Migogoro Baina ya Wakulima na Wafugaji

Mkoa katika kujidhatiti na upatikanaji wa malisho bora ya mifugo na kuepusha migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na kuboresha mahusiano kati ya wakulima na wafugaji Mkoa umefanya mambo yafuatayo: -

**i. Kumefanyika Mikutano ya Uhamasishaji wa Mahusiano Mazuri Baina ya Wakulima na Wafugaji.**

- Katika kuboreshwa malisho ya mifugo wafugaji **23** wamefundishwa namna ya uanzishaji wa mashamba ya malisho na mashamba ya malisho **7** yameanzishwa ili wafugaji waweze kuhifadhi malisho na kuyatumia wakati wa ukame.
- Pia katika kuimarisha mahusiano mazuri ya wafugaji na Mkoa umeendelea kuwapanga wafugaji katika Ranchi za Ngadinda na Muhukulu zenye jumla ya hekta **7,416.414.**

**ii. Kupima Maeneo ya Kuchungia na Kuandaa Vitalu kwa Mfumo wa Ranchi Ndogo**

Kwa mwaka 2021/2022 zoezi la upimaji na uandaaji wa vitalu limefanyika katika kijiji cha Litowa na Magwamila katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambapo hekta **13,110.493** zimepimwa.

Hata hivyo kumekuwepo na ongezeko la mifugo inayochungwa holela katika maeneo kadhaa ya Mkoa yakiwemo mashamba ya wakulima na katika hifadhi za Taifa na misitu ya kijamii, na waliopangiwa kwenye vitalu kutoka kwenye maeneo hayo. Hali hiyo imejitokeza zaidi katika Wilaya ya Namtumbo na Tunduru. Hii imesababisha wakulima kuamua kulinda mazao yao ili yasiharibiwe au kuliwa na mifugo na hivyo hatua hiyo inayochukuliwa na wakulima imekuwa ikileta kutoelewana baina ya wakulima na wafugaji na wakati mwingine kusababisha matukio ya kuchukua sheria mkononi na kupelekea kujeruhiana.

Aidha, kwa mifugo iliyoko kwenye hifadhi imekuwa ikisababisha tembo kukimbia kwenye hifadhi na kwenda kwenye makazi ya watu na hivyo kusababisha uharibifu wa mali za wananchi na wakati mwingine maafa yamekuwa yakitokea.

Hata hivyo Mkoa umechukua hatua za kukutana na viongozi wa wafugaji kwa ajili ya kutatua changamoto hii, ambapo moja ya maelekezo kwa wafugaji kupitia viongozi ni kuwataka wafugaji kukaa katika maeneo waliyopangiwa na kuwa na mifugo kuendana na eneo walilo nalo.

Pia kuzielekeza Halmashauri zenye wafugaji kutatua changamoto ya ukosefu wa miundombinu kwenye maeneo yaliyotengwa kwa kushirikiana na wafugaji kujenga majosho, malambo na visima vya maji ili wafugaji wabakie katika maeneo yao waliopangiwa, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilikusanya kiasi cha **Tshs**. **190,423,000.00** kupitia adhabu mbalimbali kwa wafugaji wanaokiuka taratibu ikiwa ni pamoja na kulisha kwenye vyanzo vya maji na nje ya maeneo ya kufugia.

#### 6.1.3.7 Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo.

Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo Tanzania unasimamiwa kwa Sheria ya **Usajili, Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo Na.12** ya **Mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2011** na Kwa Mkoa wetu wa Ruvuma Halmashauri ziko kwenye hatua tofauti ya kutekeleza zoezi hili. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Mkoa wametoa elimu ya kwa Wahe. Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Idara za Mifugo na Uvuvi, Maafisa Tehama na Maafisa Utambuzi wa Halmashauri.

Faida ya zoezi hili la utambuzi ni; Kusaidia Kudhibiti wizi wa mifugo, Kuthibitisha umiliki wa mifugo hiyo, Fursa ya kibiashara kimataifa kwa kukidhi viwango, ushindani, na matakwa ya soko la kimataifa, Uhakika wa usalama wa chakula kwa kuifahamu idadi ya mifugo na jinsi ya kuvuna mifugo hiyo na mazao yake, pia itasaidia kuepusha migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Aidha, kupitia matangazo ya Serikali Taarifa kwa Umma kupitia hotuba ya Mhe. Waziri Mkuu wa bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zoezi la utambuzi limesitishwa mpaka hapo Serikali itakapofanya Tathmini na kutoa maelekezo. Mpaka zoezi linasitishwa Mkoa ulikuwa umefanya utambuzi kwa mbuzi na kondoo **875**, Ng'ombe na punda **5,539 katika** Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, Namtumbo, Songea, Mbinga Mji na Manispaa ya Songea.

#### 6.1.3.8 Mikakati ya Kuboresha Sekta ya Mifugo Mkoani Ruvuma

i. Kuhimiza matumizi ya kinga zaidi kuliko tiba kwa mifugo;

ii. Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya mifugo;

iii. Kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa wenye tija; na

iv. Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vya kusindika mazao ya mifugo.

### 6.1.4 SEKTA YA UVUVI

Katika sekta ya uvuvi, Mkoa unategemea kupata samaki kutoka ziwa Nyasa, mito, mabwawa ya asili na mabwawa ya kufugia samaki. Hata hivyo tija itokanayo na vyanzo hivyo vya samaki haitoshelezi mahitaji ya Mkoa ambayo ni zaidi ya tani **18,000** kwa mwaka, hivyo tunapata samaki kutoka nje ya Mkoa wastani wa tani **55** kwa mwezi, ukilinganisha na wastani wa mavuno ya samaki kwenye maji ya asili tani **151.5** kwa mwaka. Watalaamu wanaendelea kuhamasisha ufugaji wa samaki kwenye mabwawa ili kukidhi mahitaji ya walaji. Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka **2021** Julai hadi **2022** Septemba jumla ya wavuvi **7,635** walisajiliwa, pamoja na vikundi **38** vya wavuvi na vikundi **4** vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi **(BMUs**) vilivyopo katika mialo ya Mbamba bay, Lituhi, Ndengele na Ng'ombo. Uzalishaji wa samaki katika Ziwa Nyasa ni wastani wa tani **8,411.4** kwa mwaka zenye thamani ya **Tshs. 25, 234, 200,000.00**.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya wataalamu wa kada ya uvuvi **7** ambapo katika ngazi ya Mkoa ni mmoja (**1**) na nane(**6**) wako katika ngazi ya Halmashauri za wilaya.

**Jedwali Na. 33: Wataalamu wa kada ya uvuvi kwa kila halmashauri**

| Halmashauri | Wanaohitajika | Waliopo | Mapungufu | Waliopo kwenye mpango wa kuajiriwa 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|
| Tunduru | 12 | 1 | 11 | 0 |
| Namtumbo | 21 | 2 | 19 | 8 |
| Mbinga DC | 31 | 1 | 30 | 0 |
| Nyasa | 22 | 1 | 21 | 5 |
| Songea DC | 18 | 0 | 18 | 14 |
| Madaba | 9 | 1 | 8 | 0 |
| Songea MC | 5 | 0 | 5 | 5 |
| Mbinga TC | 14 | 0 | 14 | 1 |
| **Jumla** | **132** | **6** | **124** | **33** |

### 6.1.4.1 Uzalishaji wa Samaki Kwenye Mabwawa

Mkoa una jumla ya wafugaji wa samaki **4,170** wenye jumla ya mabwawa **6,602** yenye wastani wa uzalishaji wa tani **847.9** kwa mwaka.

Hata hivyo, Ufugaji wa samaki ni shughuli ambayo wananchi wengi wamekuwa wakiifanya katika kuongeza kipato na lishe katika jamii inayowazunguka. Kutokana na kutotosheleza kwa samaki wanaotoka kwenye vyanzo vya samaki vilivyopo kwenye Mkoa, wananchi wanaendelea kuhamasishwa kufuga samaki kwa tija katika mabwawa ili kuweza kukidhi mahitaji hayo kwa ajili ya chakula na kwa biashara pia.Ndani ya Mkoa kuna kituo kimoja **(1)** cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki kwa ajili ya wafugaji,kituo hicho kipo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ,Ruhila (**RADC)** kilichopo Manispaa ya Songea.

#### 6.1.4.2 Fursa Katika Ufugaji wa Samaki

- Mwamko wa wananchi wa Mkoa kuhamasika na ufugaji wa samaki.
- Uwepo wa vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo,mito, chemchem na mabwawa ya Asili/Malambo zaidi ya kumi na nne (**14**) katika Mkoa yenye fursa ya ufugaji wa kupandikiza au kufuga kwa njia ya vizimba(Cage culture).
- Uwepo wa ziwa Nyasa linalotoa fursa ya ufugaji kwa njia ya vizimba (cage culture).
- Uwepo wa mahitaji makubwa ya samaki katika Mkoa.
- Uwepo wa wafugaji wa samaki zaidi ya **4,170** na mabwawa ya samaki zaidi ya **6,602,**wanaohitaji vyakula bora vya samaki.
- Upatikanaji wa uhakika wa malighafi za kutengenezea chakula cha samaki.

**Jedwali Na 34Idadi ya Mabwawa, Wafugaji na Wastani wa Hali ya Uzalishaji wa Samaki Katika Mabwawa Kwa Mwaka.**

| Halmashauri | Idadi ya wafugaji | Idadi ya mabwawa | Uzalishaji (tani) |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tunduru | 315 | 463 | 3.90 |
| Namtumbo | 200 | 71 | 1.3 |
| Songea M.C | 955 | 937 | 7.1 |
| Mbinga | 954 | 1,293 | 8.4 |
| Songea D.C | 1,327 | 3,227 | 96.8 |
| Nyasa | 170 | 225 | 1.4 |
| Mbinga Mji | 215 | 310 | 1.2 |
| Madaba | 34 | 56 | 1.1 |
| **JUMLA** | **4,170** | **6,602** | **121.20** |

***Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa.***

### 6.1.4.3 Matumizi ya Zana Bora Za Uvuvi.

Katika matumizi ya zana bora za uvuvi, jitihada zimewekwa ili kujenga uwezo kwa wavuvi kutambua madhara yatokanayo na matumizi ya zana haramu za uvuvi , utoaji wa elimu juu ya matumizi ya zana bora za kisasa za uvuvi zinazokubalika kisheria, kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kuhamasisha ufugaji bora wa kisasa na wenye tija. Pamoja na kuhamasisha uwanzishwaji wa vikundi vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi BMUs (**Beach Management Units)** hasa katika mwambao wa ziwa Nyasa na mto Ruvuma ili rasilimali za uvuvi zitunzwe, zilindwe na ziwe endelevu. Aidha, ujenzi wa karakana ya kuunda boti za uvuvi za kisasa katika kituo cha Mbamba Bay umefikia hatua za mwisho za kuweka mashine.

### 6.1.4.4 Mikakati ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi.

- Kuhimiza matumizi ya zana bora za uvuvi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ambapo hadi kufikia Septemba **2022** zaidi ya wavuvi **5,380,** wafugaji **4,159** na wadau **279** wamefundishwa njia bora za uvuvi,ufugaji bora wa samaki na utunzaji wa mazingira.

- Kuendeleza/kuboresha ujenzi wa miundombinu ya uvuvi hasa mialo(**Land stations**), na katika mwaka huu wa fedha **2022/2023** Wizara ya Mifugo na Uvuvi(sekta ya uvuvi) ina mpango wa kujenga mualo **1** katika kijiji cha Ng'ombo**.**
- Kutoa elimu endelevu ya uanzishaji wa vikundi vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi(**BMUs**) katika mwambao wa ziwa Nyasa.
- Kuhimiza uanzishaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki, ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba (***cage*)** katika ziwa na mabwawa ya asili ili kupata mavuno mengi ya samaki yatakayofaa kwa ajili ya viwanda.
- Kukijengea uwezo kituo cha maendeleo ya ufugaji samaki Ruhila ili kiweze kuzalisha vifaranga bora na vya kutosha, kwa sasa kituo kina uwezo wa kuzalisha vifaranga **1,000,000.00** kwa mwaka ukilinganisha na mahitaji ya vifaranga **3,000,000** kwa mwaka.
- Kila Halmashauri kuwa na kituo cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki ambapo vituo hivyo vitatumika pia kama mashamba darasa.
- Kuendeleza doria za mara kwa mara ili kuzuia utumiaji na uingizaji wa zana haramu za uvuvi katika ziwa na mito pamoja na kuvikagua vyombo vyote na kuvisajili kisheria.
- Ujenzi wa soko la samaki lililopo Mbamba bay upo katika hatua za mwisho ili liweze kutumika.
- Mradi wa ujenzi wa maboti **6** za kisasa za Halmashauri bado unaendelea,mpaka kufikia Septemba **2022,** boti **2** tayari zimeshakamilika na zinafanyakazi.

### 6.1.5 SEKTA YA MALIASILI

#### 6.1.5.1 Taarifa ya Misitu -

##### 6.1.5.1.1 Utangulizi

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya eneo la **km$^2$67,550** ambalo kati ya hizo km$^2$**63,968** ni ardhi na **km$^2$3,582** ni maji yanayojumuisha ziwa Nyasa, mito na Mabwawa. Eneo la misitu ya asili ya miombo peke yake ni **km$^2$41,567** sawa na **asilimia 65** ya eneo lote la ardhi.

Misitu ya Hifadhi ya vijiji iliyohifadhiwa katika wilaya zote tano (05) ni **39** yenye jumla ya eneo la **km$^2$30,110.7** au Hekta **311,069.47** sawa na **asilimia 7.5** ya misitu ya miombo iliyopo mkoa wa Ruvuma.

**6.1.5.2 Hali ya Ufugaji Nyuki ya Mkoa**

Mkoa una lengo la kuwa na **mizinga 80,000** angalau kila Halmashauri iwe na **mizinga 10,000** na kuwa na viwanda vya kuchakata mazao ya **nyuki 20** mpaka ifikapo **mwaka 2025**. Utekelezaji wa lengo hili utashikisha Wakala wa Huduma za Misitu, Halmashauri, Taasisi za Umma (kama Magereza, JKT, Mashule, Vyuo) na Taasisi za Kiserikali (kama CARITAS, PALMS, Vikundi mbalimbali na wananchi kupitia miradi ya FORVAC, SECAD na wakulima wa Soya, Alizeti, Ufuta, Mawese n.k.)

Mpaka sasa mkoa wa Ruvuma una jumla ya mizinga **14,426,** kati ya hiyo ya kisasa ni **10.004** na mizinga ya kienyeji ni **4,422** sawa na **asilimia 30.65.** Mizinga hiyo inazalisha asali **kilo 16,186** wastani kila mzinga unazalisha kilo **1.12** badala ya **kilo 10**, uzalishaji huu hauridhishi kabisa.

Mkoa unapendekeza juhudi za kuhamasisha wananchi kushiriki zaidi kufuga nyuki kwenye maeneo ya mashamba yao hasa kwenye maeneo ya kilimo cha mazao ya Mafuta **(Block farms)** ya Soya, Alizeti, Ufuta na Mchikichi kwa kufanya Hivyo wananchi wataongeza mazao yao kwa sababu yatachevushwa na nyuki.

Asali itakayopatikana itawasaidia wakulima kupata kipato na chakula, Hivyo kuboresha lishe kwa Watoto wao. Ili kuleta ufanisi kwenye elimu ya ufugaji nyuki, teknolojia ya uchakataji na taarifa za masoko ni vyema kila wilaya ikaanzisha Jumuiya (**Association**) ya Wafugaji na wafanyabiashara wa mazao ya Nyuki. Kwa kufanya Hivyo kutatengeneza mtiririko wa taarifa za masoko na teknolojia mpya ngazi ya Kimataifa, Kitaifa, Kimkoa, Kiwilaya hadi Kijijini.

**6.1.5.3 Hali ya Misitu na Mazao ya Misitu**

Hali ya misitu ya Hifadhi ya vijiji bado sio nzuri sana kwa sababu ya uvamizi na kufanya shughuli za kibinadamu kama kulima, kuchungia, kuvuna mazao ya misitu bila utaratibu na migogoro ya mipaka kati ya wananchi na hifadhi.

Mpaka sasa wananchi bado hawajafaidika na misitu hiyo, basi ni vyema sasa juhudi zikaogezwa za kuhakikisha mazao ya misitu kama mbao zinatumika kwenye miradi ya

mikakati ya Kitaifa kama Ujenzi wa madarasa, mabweni, zahanati, madawati na thamani za maofisini ili kupunguza gharama kwa wananchi.

Aidha, kwa upande wa Nyasa bado wavuvi wanatumia mitumbwi ya kuchonga magogo ambayo huoza haraka kwenye maji, huwa midogo na haina nafasi wala **balance** ya kutosha na kusababisha wavuvi kushindwa kuvua mbali na kuleta ajali.

Hivyo ni vyema mradi ukaelekeza nguvu Nyasa ya kutumia mbao nzuri kutengeneza maboti imara ya kudumu ili Ziwa Nyasa liweze kuleta tija.

Zao lingine linalopatikana ni mianzi ambayo kwa mkoa wetu litatumika kwa ajili ya pombe, kutengeneza makapu, matenga n.k. Sasa umefika wakati wa kutumia mianzi kibiashara ili iweze kuongeza kipato kwa wananchi kwa kupatiwa mashine ya kutengeneza njiti za meno na mishikaki, kwani njiti hizo zinatoka China na kuuzwa Mbinga na Nyasa ambako kuna mianzi mingi badala ya wananchi wetu kuzitengeneza wenyewe.

Misitu ya asili ya Ruvuma bado ina mazao mengine ya chakula kama uyoga, matunda pori, dawa za asili na baadhi ya wadudu kama kumbikumbi na senene. Mazao hayo kama yangefanyiwa utafiti na kuongezwa thamani yangeweza kutoa mchango mkubwa kwenye kuondoa umaskini na kuongeza lishe kwa wakinamama na Watoto.

Mkoa utashirikiana na wadau wengine wa ufugaji nyuki kama:
FORVAC, WWF, SUA, Chuo cha Maliasili Jamii, TFS, TAWA na TAN

**6.1.5.4 Mradi wa Panda Miti Kibiashara**

Mkoa wa Ruvuma uliainisha **hekta 80,235** kwenye maeneo kumi na moja ya kupanda miti ya biashara kwenye wilaya za Nyasa, Mbinga, Songea, Namtumbo na Tunduru. Kwenye awamu ya kwanza ya miaka kumi iliyoanzia **mwaka 2015** hadi **2025,** Mkoa ulikuwa na lengo la kupanda **hekta 40,500 (Eka 100,000**) ya biashara aina ya Misindano **(Pine),** Milingoti **(Eucalyptus)** na Misaji **(Teak).**

Utekelezaji wa mradi wa upandaji miti ya biashara mpaka sasa ni kama ifuatavyo:

- Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Hekta 7,397
- Mashule na Vyuo (SUA) Hekta 1,475
- Wananchi (TGA) Hekta 26,360
- Halmashauri (LGAS) Hekta 1,340

**Jumla Hekta 36,572**

Jumla ya **hekta 36,572** za miti ya biashara zimeshapandwa kwenye awamu ya kwanza sawa na **asilimia 90.3** ya lengo.

### Jedwali Na. 35: Idadi ya miche ya miti ya biashara na vyanzo vya maji

| Wilaya | Bustani | Idadi na aina ya Miti | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Mashamba ya MitiTFS** | **Wananchi** | **Vyanzo vya maji** |
| Songea | Wino | 600,000 | 200,000 | |
| | Mkongotema | 48,000 | | |
| | Ifinga | 200,000 | | |
| | SUA | 430,000 | 10,000 | |
| | Matogoro | | 300,000 | |
| | Ndongosi | 200,000 | 30,000 | |
| | Songea boys | | 32,000 | 200,000 |
| | Songea girls | | | |
| | Mahenge Nurseries | | | |
| | | | | 85,000 |
| Mbinga | Kinaha | | 200,000 | 95,000 |
| Nyasa | Mpepo | 150,000 | 10,000 | |
| | Liuli | 500,000 | 50,000 | 20,000 |
| Tunduru | Kazamoyo | 280,000 | 100,000 | |
| Namtumbo | | | | 150,000 |
| **JUMLA** | | **2,408,000** | **932,000** | **550,000** |

### Jedwali Na. 36 Maeneo Maalum ya Upandaji Miti na Wananchi

| Wilaya | Eneo | Matumizi | Aina ya miti | Idadi ya miti |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Songea** | Wino TGA<br><br>Mkongotema TGA<br>Ifinga TGA<br>Bonde la Luhira<br>Lihuhu Intake<br>Mlima Gumbiro<br>Kibandisi Intakes<br>Mhimbasi Intakes<br>Lihanje Intakes<br>Mashuleni | Mashamba ya miti mto nguzo<br><br>Mashamba ya miti<br><br>Vyanzo vya maji<br><br>Vyanzo vya maji<br>Vyanzo vya maji<br>Vyanzo vya maji<br>Vyanzo vya maji<br>Mashamba ya miti | Pine/Eucalyoptis<br><br>Pine/Eucalyptis<br><br>Pine/Eucalyptis<br><br>Migwina/Minyonyo | 285,000 |
| **Mbinga** | Liumbe TGA<br><br>Kihangi mauka TGA<br><br>Mikiga hill | Mashamba ya miti (Mbao, Nguzo)<br>Mashamba ya miti (Mbao, Nguzo)<br>Mashamba ya miti (Mbao, Nguzo) | Pine/Eucalyptis<br><br>Pine/Eucalyptis<br><br>Pine/Eucalyptis | 200,000 |
| **Nyasa** | Liuli escapement<br>Upolo TGA | Mashamba ya miti<br>Mashamba ya miti | Teak<br>Pine | 150,000 |

#### 6.1.5.5 Hifadhi ya Vyanzo vya Maji

**Jedwali Na. 37: Orodha ya vyanzo vya maji vinavyotakiwa kuhifadhiwa haraka**

| Halmashauri | Kijiji | Chanzo kilipo | Kazi zinazotakiwa kufanyika |
|---|---|---|---|
| 1. Mbinga DC | Kigonsera | Halale intake | Demarcation & Tree planting |
| | Lasau | Lisau intake | |
| | Kibandai Asili na Kihongo | Langiro intake | |
| | Kiyaha | Kiyaha intake | |
| | Matiri | Mtende intake | |

| Halmashauri | Kijiji | Chanzo kilipo | Kazi zinazotakiwa kufanyika |
|---|---|---|---|
| **Halmashauri** | **Kijiji** | **Chanzo kilipo** | **Kazi zinazotakiwa kufanyika** |
| | Kibanga | Kimbanga | Demarcation & Tree planting |
| | Mahilo Asili | Liwingu | Demarcation & Tree planting |
| | Miyau | Liwingu | |
| | Amanimakoro | Mikeke | |
| | Mkako | Halale | |
| | Mpapa | Likwela | |
| | Kindimbajuu | Mbugani | |
| | Ndongosi | Namswea | |
| | Wukiro | Wukiro | |
| | Ruanda | Namswea | |
| | Litoho | Liwanga/Ulolela | |
| | Kipapa na Mahilo | Kingoro A | |
| | Utili | Utili | |
| | Kagugu | Maganagana | |
| | Maganagana | maganagana | |
| | Kihungu | Kihungu | |
| | kilimani | Kilimani | |
| | Mkwaya | Mkwaya | |
| | Lupilo | Lupilo | |
| | Mateka | Mateka | |
| | Tanganazomba | Ugano | |
| | Mbangamao | Ukimo | |
| | Kikolo | Kikolo | |
| | Mpepai | Mpepai | |
| 2. Tunduru DC | Amani | Nambango | |
| | Nalasi | Kagoya | |
| | Milonde | Namalowe na Mwinda | |
| | Naluwale | Naluwale | |
| 3. Songea DC | Liula | Livengwa intake | Demarcation & Tree planting |
| | Mbingamhalule | Liula intake | Demarcation & Tree planting |
| | Mgazini | Lunyera intake | Demarcation & Tree planting |
| | Kilagano | | |
| 4. Madaba DC | Magingo | Mgombasi intake | Demarcation & Tree planting |
| **Halmashauri** | **Kijiji** | **Chanzo kilipo** | **Kazi zinazotakiwa kufanyika** |
| | Matetereka | Kitekago intake | demarcation &Tree planting |
| | Mahanje | Kibandis intake | demarcation &Tree planting |
| 5. Namtumbo DC | Luhimbalilo na Naikesi | | Tree planting |

| Halmashauri | Kijiji | Chanzo kilipo | Kazi zinazotakiwa kufanyika |
|---|---|---|---|
| | Njalamatata/Luegu | Chanzo cha Luegu | |
| | Rwinga | Chanzo cha Lwinga | |
| 6. Nyasa | Makata | Makata intake | Tree planting |
| | Litindoasili na Lumecha | Matogoro intake | Tree planting |

### 6.1.5.6 Utalii

#### 6.1.5.6.1 Vituo vya Taarifa za Vivutio vya Utalii

Ili kukuza sekta ya utalii na kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mhe. Kanali Thomas laban ameagiza kwanza, kuanzishwa kwa vituo vya taarifa za utalii kila Halmashauri.

Vituo hivyo vitakuwa chini ya Afisa maliasili na mazingira wa Halmashauri husika.

1. Kituo cha Mbinga kitakuwa kwenye Ofisi ya Maliasili iliyopo Mbiga Mjini na kitatumiwa na Halmashauri ya wilaya ya Mbinga, Mbinga mji, TFS Mbinga na Liparamba- TAWA.
   Kituo cha Namtumbo kitaanzishwa na TANAPA (Nyerere National Park) kanda ya Kusii kwa kushirikiana na Halmashauri ya Namtumbo na Tunduru kitaanzishwa na hifadhi ya mazingira asili ya Mwambesi (TFS) na vitakuwa kwenye Ofisi za Maliasili za Halmashauri za wilaya na watashirikiana na WMA zote 5 na kukianzisha (Nalika, Chingole, Mbarang'andu, Kisungule na Kibanda)

2. Kuanzishwa vituo viwili vya taarifa za vivutio vya utalii
   i. Kituo cha taarifa za vivutio vya utalii cha Mkoa wa Ruvuma
      Kituo hiki kitaanzishwa na Mkoa kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

      Kituo hiki kitaanzishwa kwenye Ofisi za maliasili mahenge na baadae itajengwa Ofisi kubwa ambayo itakuwa na ofisi zote za sekta ya maliasili na utalii (TANAPA, TAWA, TFS, Makumbusho ya Taifa na Kituo cha taarifa cha utalii).

Kituo hiki jumuishi (onestop centre) kitahudumia hata mikoa mingine ya Tanzania.

ii. Kituo kingine maalum kitakuwa Mbambabay ambacho TAWA watashirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Nyasa kukianzisha kwa sababu bandari ya Mbambabay ni lango kubwa la kuingia watalii toka Malawi, Msumbiji na nchi za SADC.

Taarifa zitakusanywa ni pamoja na utalii wa kihistoria, utamaduni, dini, hifadhi za wanyamapori, samaki, misitu na fukwe za maziwa, bahari na mito mikubwa kama Ruvuma na milima, kilimo na chakula cha asili.

#### 6.1.5.7 Wanyamapori

##### 6.1.5.7.1 Hifadhi ya Mbambabay

Hifadhi ya Wanyamapori ya Mbambabay ina jumla ya hekta 597 ikiwa ni milima miwili (Mlima Mbamba hekta 440 na Mlima Tumbi hekta 110) na visiwa viwili (Lundo hekta 20 na Mbambabay hekta 27).

Tarehe 05 Novemba, 2022 Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Thomas Elias Laban aliwakabidhi rasmi mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) hifadhi hiyo ili waiendeleze kwa kuongeza wanyama na kujenga mabanda ya kupumzikia.

Mpaka sasa jumla ya wanyamapori tisa wamewekwa ambao ni Swalapara watatu na Digidigi sita. Pamoja na wanyama hao, hifadhi hiyo ina wanyama wa asili kama Pimbi, Tumbiri, Fisimaji, Kenge, Nyoka, Mijusina Ndege wanaishi kandokando ya Ziwa (**King fisher, Fish eagle, Commorant, Gunnet, Hammer cock).**

Mchakato unaendelea wa kuongeza wanyama wengi na kulinda wanyama wa asili na Samaki wa mapambo waendelee kuongezeka. Kazi zinazoendelea kufanyika kwenye hifadhi hiyo ni:

- Kufanya tathmini ya mazingira ya makazi ya wanyama (**Habitat Assessment**);
- Mpango wa matumizi ya rasilimali zilizopo (**Resource use Zone management Plan);**
- Tathmini ya athari ya mazingira (**Environmental Impact Assessment**);
- Andiko la Kibiashara (**Business Plan**);

- Kumalizia mchakato wa kuitanga hifadhi ya Mbambabay kwenye Gazeti la Serikali (**Gazettment**).

TAWA watachangia kuandaa kituo cha taarifa za vivutio vya utalii ambacho kitakusanya taarifa zote za vivutio vya mkoa wa Ruvuma ili wageni wanaoingia kupitia bandari ya Mbambabay waweze kupata taarifa kwa urahisi na sahihi zikiwepo za Samaki Adimu wa Mapambo wa Ziwa Nyasa.

### 6.1.5.8 Mazingira

### 6.1.5.8.1 Mkakati wa Kudhibiti Taka Ngumu

i. **Hali ya Taka**

Mkoa wa Ruvuma ni moja ya mikoa ambayo ina tatizo sugu la uzoaji takataka ngumu. Taka hizi ngumu zimezagaa sana hasa kwenye Miji Mikubwa ya Wilaya ikiongozwa na Mji wa Songea, Mbinga, Tunduru, Namtumbo na Mbambabay.

Kwa mji mkubwa wa Ruvuma Manispaa ya Songea huzalisha wastani wa tani 71.5 za taka kwa siku na uwezo wa Manispaa wa kuzoa taka ni tani 55 – 60 kwa siku sawa na asilimia 77 ya taka zote.

Aina ya takataka zinazozalishwa ni mabaki ya mazao ya chakula hasa kwenye masoko ya wakulima (kama Bombambili, Mfaranyaki na Mjimwema), pumba ngumu za mpunga hupatikana kwenye mashine za kukoboa mpunga (Mtaa wa Viwanda Mjini), Maranda ya mbao hupatikana wa wingi eneo la soko la mbao Mfaranyaki, mabaki ya vifungashio (Maboksi, mifuko ya nailoni na viroba), chupa za plastiki za vinywaji (Juisi, dawa), mabaki ya nguo chakavu na taulo (Pady) na vyuma chakavu ni vichache sana.

Matatizo ya kuongezeka kwa uchafu husababiswa na kuongezeka kwa idadi ya watu, kuongezeka Wafanyabiashara, Taasisi mbalimbali (Mashule, vyuo, magereza, mafesha). Sababu zingine ni uwezo mdogo wa Manispaa wa kuzoa takataka, mpaka sasa kuna magari matatu lakini linalofanya kazi ni moja tu na kijiko (Loader) cha kupakia takataka nacho kimekufa. Mradi wa kujenga dampo la kisasa Subira nao umesimama sababu ya ukosefu wa fedha, sababu zingine ni uelewa mdogo wa wananchi na kukosa hamasa ya swala la usafi wa mazingira kwa baadhi ya wananchi kutokushiriki siku maalum ya usafi wa mazingra ya kila mwezi na kutochangia gharama za usafi kwenye mitaa yao.

i. **Mkakati wa Kupunguza Takataka**

a) **Kuanzisha vituo vya kuzalisha mboji (Composite)**

- Takataka za mabaki ya chakula (matunda, mboga za majani, mabua ya mahindi na majani ya mimea) huweza kutumika kutengeneza mboji ambayo inatumika kwenye bustani za mboga, maua na mashambani. Aina hii ya mbolea hukaa muda mrefu shambani na husaidia kutunza maji na kuboresha udongo;

- Kituo cha mfano cha kuzalisha mboji cha eneo la bustani ya kilimo Msamala Miembeni bado hakijaanza kazi. Manispaa isimamie uanzishaji wa kituo hiki kwa kushirikiana na vikundi vya vijana au wakinamama.

- Mashine za kutengeneza mkaa mbadala na majiko sanifu takataka zinazotokana na Maranda ya mbao (**sawdust**) na pumba ngumu za mpunga huweza kutumika kutengeneza mkaa mbadala (**Briqutte and Pilets**).

- Kupitia sekta binafsi tayari kuna mashine mbili, lakina inayofanya kazi ni moja iliyopo Ruhira boys. Tatizo ni ukosefu wa soko kutokana na uelewa wa aina hii ya mkaa mbadala.

- Maranda ya mbao huweza kutumika moja moja kwa kutumia majiko maalum sanifu ambayo hutumika hasa kwenye maeneo ya kitimoto. Taasisi zenye watu wengi (Mashule, vyuo, magereza, majeshi, mashirika ya dini) yahamasishwe kutumia mkaa huu mbadala au majiko maalum sanifu ya Maranda na pumba ngumu za mpunga. Teknolojia hii hutumika hata majumbani na maeneo ya kitimoto, chips na yanayotumia mkaa muda mrefu.

**i. Mashine za Plastiki**

Mashine hizi za kukusanya na kukatakata chupa za plastiki na kuzifunga pamoja kwa sasa hazipo kabisa hapa mjini Songea. Takataka hizi baadaye husafirishwa kwanye viwanda vya plastiki (Dar es Salaam au Tanga na Mbeta) na kutengenezwa bidhaa nyingine (**recycle**).

Usafirishaji taka ngumu kwa kushirikisha jamii, mkakati huu unashirikisha jamii ya mtaa mmoja kupanga kiwango cha mchango kwa ajili ya kupata fedha za kuajiri vibarua wa mtaani wa kuzoa taka na kukodi gari la kusafirisha taka hadi dampo. Mhusika mkuu ni Mwenyekiti wa Mtaa, wajumbe na wananchi kwa ujumla.

**ii. Kuchimba mashimo ya takataka**

Mkakati huu unafaa zaidi kwenye maeneo ya pembezoni na yenye viwanja vikubwa (medium na low density plots). Kwa maeneo ya katikati ya miji au ya viwanja vidogo haiwezekani na badala yake maeneo hayo yanatakiwa kuwa na vifaa vya kukusanyia taka (mapipa, ndoo za plastiki).

**iii. Kuiongezea uwezo Halmashauri wa kuzoa taka**

Manispaa ya Songea pamoja na Halmashauri zenye miji hazina magari ya kutosha ya kuzoa taka na yaliyopo ni machache na mabovu na yana kazi nyingi. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa Mafuta ya magari unaotokana na bajeti ndogo.

Kwa kushirikisha wadau wengine au taasisi zingine zilizopo kwenye Halmashauri wanaweza wakasaidia kutoa magari ya kuzoa taka japo mara moja kwa mwezi hasa siku maalum ya usafi ya kila mwezi.

## 6.2 VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NA TAARIFA YA TIMU YA KUCHAMBUA, KUANDAA NA KUAINISHA MFUMO MZURI WA UWAJIBIKAJI KWA JAMII (CSR) WA WACHIMBAJI WA MADINI MKOA WA RUVUMA

### 6.2.1 Viwanda

Mkoa wa Ruvuma una viwanda vikubwa 6 ambavyo vitatu (3) vya kukoboa kahawa (Coffee Curing) katika Wilaya ya Mbinga, kiwanda kimoja (1) kipo katika Wilaya ya Tunduru cha kubangua korosho, Kimoja (1) kipo Wilaya ya Songea cha Kufua Umeme na kimoja (1) kipo Wilaya ya Songea cha Kusindika Sembe. Mkoa pia una viwanda vya kati ishirini na tano (25) vinavyojishughulisha na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo kama unga wa sembe, mchele, Mikate na Maziwa.

Aidha Mkoa wa Ruvuma una Viwanda vidogo 190 na viwanda vidogo sana vipo 3,264 ambavyo ni viwanda vya kukoboa na kusaga nafaka mbalimbali, kukamua mafuta ya alizeti, usindikaji wa Mihogo, Chereheni, usindikaji wa nyama (sausages), sembe, juice, useremala na bidhaa zingine za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili na huchangia ajira kwa wakazi wengi wa Mkoa wa Ruvuma. Bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo huuzwa ndani ya Mkoa na kiwango kingine huuzwa mikoa ya jirani kama vile Mbeya, Lindi, Mtwara, Njombe, Dar es Salaam na Mikoa mengine katika nchi yetu na nchi jirani za Malawi na Msumbiji.

### 6.2.2 Biashara

**a) Kufanyika kwa Mabaraza ya Biashara**

Mabaraza ya Biashara ya Wilaya na Mkoa hufanyika kwa Mujibu wa waraka wa Rais Na.1 wa mwaka 2001, ikiwa ni jukwaa la Majadiliano kati ya Sekta binafsi na Sekta ya Umma ambapo Baraza la Biashara la Mkoa lilifanyika tarehe 21 Disemba, 2021 na kupitia Mabaraza ya Biashara changamoto mbalimbali huibuliwa na kufanyiwa kazi. kwa sasa hamasa inaendelea kutolewa kwa viongozi wa Wilaya na Halmashauri kuitisha mabaraza ya biashara kwa ngazi ya Wilaya kwa kuwa ni jukwaa muhimu linalokutanisha Sekta binafsi na Sekta ya Umma kwa ajili ya Majadiliano.

**b) Upangaji wa machinga katika maeneo rasmi ya kufanyia biashara**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakati ikizindua Mpango wa uelimishaji na uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022, alielekeza kuwapanga machinga na zoezi hilo, lifanyike kwa umakini kwa lengo la kuepuka vurugu, fujo na uonevu. Ambapo Mkoa wa Ruvuma kupitia maekelezo hayo tulianza kutekeleza.

**c) Hali ya utekelezaji wa maelekezo ya upangaji wa Machinga.**

I. Kuunda Uongozi wa Machinga kwa ngazi ya Mkoa na ngazi ya Halmashauri kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma haukuwa na uongozi wa machinga.

II. Kuwaunganisha Viongozi wa Machinga Mkoa na Viongozi wa Machinga Taifa na kushiriki semina mbalimbali za Viongozi wa Machinga zilizofanyika na zinazoendelea kufanyika Dodoma.

III. Halmashauri zimetenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Machinga.

IV. Kuendelea kutoa Vitambulisho vya Wajasiriamali wadogo.

V. Viongozi wa Machinga kuwezeshwa na Mkoa na Halmashauri kufanya ziara kwenye Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kujitambulisha, kutoa elimu ya Katiba na Kanuni za Shirikisho na kuhamasisha machinga kuhamia kwenye maeneo rasmi yaliyotengwa na Halmashauri.

***VI.*** Halmashauri zimeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ya masoko na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za Machinga***.***

**d) Changamoto zilizojitokeza wakati wa upangaji wa Machinga**

I. Baadhi ya Wafanyaboiashara kukataa kufanya biashara kwenye maeneo yaliyotengwa.

II. Miundombinu mbambali kwenye baadhi ya masoko ambapo Machinga wanafanyia biashara imechakaa inahitaji kufanyiwa marekebisho.

III. Baadhi ya machinga kurejea kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

IV. Baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za machinga kutokuwa na Miundombinu muhimu,

**e) Utoaji wa Leseni za Biashara**

Mkoa unaendelea na zoezi la kurasimisha Biashara na kutoa Leseni kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara kama Serikali ilivyo Agiza. Mwaka 2021/2022 jumla ya Leseni **7,815** zilitolewa na kupata jumla ya TShs **722,254,500** zilikusanywa ikiwa ni mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa Leseni za Biashara katika Mkoa wa Ruvuma. Jedwali namba 38 hapa chini linaonesha Idadi ya Leseni zilizotolewa kwa kila Halmashauri.

**Jedwali Na. 38: Idadi ya leseni zilizokatwa kwa kila halmashauri mwaka 2021/2022**

| **Na.** | **Halmashauri** | **JULAI, 2021 – JUNI, 2022** | |
|---|---|---|---|
| | | **Idadi ya Leseni** | **Thamani** |
| 1 | SONGEA MC | 2,681 | 327,737,000 |
| 2 | MBINGA TC | 1290 | 150,364,000 |
| 3 | MBINGA DC | 376 | 23,885,000 |
| 4 | MADABA DC | 383 | 24,350,000. |
| 5 | TUNDURU | 1798 | 96,594,000. |
| 6 | SONGEA DC | 213 | 21,354,000 |
| 7 | NYASA DC | 485 | 37,647,000 |
| 8 | NAMTUMBO | 589 | 40,323,500 |
| | JUMLA | **7,815** | **722,254,500** |

**f) Fursa za Uwekezaji Mkoani Ruvuma**

Mkoa wa Ruvuma una fursa za Uwekezaji katika Sekta za Kilimo, Biashara, Ufugaji, Misitu, Madini, Utalii, Mawasiliano, Umeme wa Maporomoko ya Maji, Uvuvi, Viwanda, Uendelezaji wa Makazi, Usafiri na Usafirishaji ambapo fursa

zote hizi zimeanishwa kwenye Mwongozo wa Uwekezaji uliozinduliwa tarehe 25 Julai, 2019 katika viwanja vya Majimaji mjini Songea. Mkoa unaendelea kupokea Wawekezaji mbalimbali ambao wanaonesha nia ya kuwekeza Mkoa wa Ruvuma

### 6.2.3 Taarifa ya Timu ya Kuchambua, Kuandaa na Kuanisha Mfumo Mzuri wa Uwajibikaji Kwa Jamii (CSR) wa Wachimbaji wa Madini Mkoa wa Ruvuma

#### 6.2.3.1 Utangulizi

Lengo mahususi la ripoti hii ni kuelezea hali halisi ya Uwajibikaji kwa Jamii wa wachimbaji wa Madini waliopo Mkoa wa Ruvuma. Hii ni kufuatia Timu ambayo iliundwa na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kuchambua, kuandaa na kuainisha mfumo mzuri wa Uwajibikaji kwa Jamii *(Corporate Social Responsibility),* kazi ambayo timu ilipewa kuifanya kwa muda wa wiki sita.

Lengo mahususi la kuundwa kwa Timu hiii ilikuwa ni kuhakikisha, inapata taarifa za wachimbaji wa Madini jinsi wanavyowajibika kwa jamii, pia kujifunza kwenye Mikoa yenye uchimbaji wa Madini namna wanavyotekeleza na kusimamia wachimbaji wa Madini juu ya Uwajibikaji kwa Jamii kwa kuchangia utekelezaji wa Miradi ya maendeleo. Baada ya hapo, kuchambua, kuandaa na kuainisha mfumo mzuri wa CSR ambao utatumika kwenye Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma. Kazi hii imefanyika, imekamilika na kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Ruvuma, Mheshimiwa Kanali Laban Elias Thomas

#### 6.2.3.2 Wajumbe wa timu

**Jedwali Na. 39: Wajumbe wa Timu**

| Na. | JINA | WADHIFA | TAASISI ANAYOTOKA | CHEO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Amos Samwel Lugomela | Mwenyekiti | TAKUKURU | Afisa Uchunguzi Mkuu Kiongozi |
| 2 | Joseph Martin Kabalo | Katibu | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Afisa Biashara Mkoa |
| 3 | E 9476 SGT Kheri Said Komagi | Mjumbe | Jeshi la Polisi | Askari Polisi |
| 4 | Edmund Eslom Lubinga | Mjumbe | Usalama wa Taifa | Afisa Usalama |
| 5 | Zabron Paul Walwa | Mjumbe | TRA | Afisa Mkuu Msimamizi wa Kodi |
| 6 | Dickson Francis Mbugano | Mjumbe | Ofisi ya Madini | Mhandisi Migodi |
| 7 | Frank John Chonja | Mjumbe | Ofisi ya Taifa ya Mashitaka | Wakili wa Serikali |

#### 6.2.3.3 Hadidu za Rejea

1. Kutafuta taarifa za utekelezaji wa CSR katika Mikoa na sehemu mbalimbali zenye uchimbaji na biashara ya Madini.
2. Kupata na kupitia mapato ya mwaka *(Annual turnover)* ya Makampuni yanayochimba madini/yanayofanya biashara ya madini.
3. Kupata na kuchambua Mipango ya Uwajibikaji kwa Jamii *(CSR Plans)* ya Makampuni husika.
4. Kuangalia na kulinganisha mipango *(CSR Plans)* ya Makampuni na utekelezaji wa mipango hiyo.
5. Kuanisha na kubainisha Makampuni ya uchimbaji madini yamefanya nini/yametekeleza mpango gani katika jamii hadi sasa.
6. Kupata maoni ya wadau wa madini na kujadili nao juu ya namna bora ya kutekeleza mipango ya uwajibikaji kwa jamii *(CSR Plans)* katika Mkoa wa Ruvuma.
7. Kuandaa mfumo wa utekelezaji wa mipango ya uwajibikaji kwa jamii kwa kushirikiana na Makampuni ya uchimbaji na biashara ya madini.

8. Kufanya kazi zingine zinazohusiana na zitakazosaidia kuandaa mfumo fanisi wa utekelezaji wa mipango ya uwajibikaji kwa jamii (CSR Plans).
9. Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mipango ya uwajibikaji kwa jamii.

**6.2.3.4 Namna Timu Ilivyofanya Kazi**

i. Kukutana na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na kupata maelekezo ya namna ya kufanya kazi kwa kuzingatia hadidu za rejea.

ii. Timu kukutana, kutambulishana, kupitia hadidu za rejea na kuandaa mpango kazi.

iii. Kupitia Sheria ya Madini Sura Na. 123 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019, kifungu cha 105.

iv. Kuomba taarifa za mauzo *(turnover*) za wachimbaji wote wa madini waliopo Mkoa wa Ruvuma pamoja na orodha ya wachimbaji Mkoa wa Ruvuma.

v. Timu ilikutana na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya zilizopo Mkoa wa Ruvuma pamoja na Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ili kupata maoni yao namna ya utekelezaji wa Uwajibikaji kwa jamii wa wachimbaji wa madini.

vi. Timu ilikwenda katika Halmashauri za Wilaya ya Songea, Mbinga, Nyasa, Namtumbo na Tunduru kwa lengo la kukutana na viongozi wa Halmashauri na kamati za Serikali za Vijiji na kuomba taarifa na kupata maoni yao juu ya utekelezaji wa CSR.

vii. Timu ilikwenda kujifunza katika Mikoa ya Shinyanga na Geita namna zinavyotekeleza Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) katika Halmashauri za Wilaya ya Msalala, Geita, Halmashauri ya Mji Geita na Manispaa ya Kahama.

#### 6.2.3.5 Nukuu ya Sheria

***The Mining Act Chapter 123 Revised Edition 2019***

***105.(1)****A Mineral right holder shall on annual basis, prepare a credible corporate social responsibility plan jointly agreed by the relevant local government authority or local government authorities in consultation with the Minister responsible for local government authorities and Minister responsible for Finance.*

*(2) The plan prepared under subsection (1) shall take into account environmental, social, economic and cultural activities based on local government authority priorities of host community.*

*(3) The corporate social responsibility plan referred to under subsection (1) shall be submitted by a mineral right holder to a local government authority for consideration and approval.*

*(4) Subject to the provision of this section, every local government authority shall;-*

*(a) Prepare guidelines for corporate social responsibility within their localities;*

*(b) Oversee the implementation of corporate social responsibility action plan; and*

*(c) Provide awareness to the public on projects in their areas*

*(5) In this section "host community" means inhabitants of the local area in which mining operations activities take place.*

#### 6.2.3.6 Aina za Madini Yanayopatikana Katika Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa kuwa na madini aina mbalimbali ambayo yanaweza kuunufaisha Mkoa wa Ruvuma endapo kutakuwa na usimamizi mzuri na kuhakikisha Wachimbaji wanawajibika kwa jamii kwa utaratibu mzuri.
Ifuatayo ni orodha ya aina ya madini na maeneo yanapopatikana.

**Jedwali Na.40: Orodha za Aina ya madini yanayopatikana katika Mkoa wa Ruvuma**

| Na. | Aina ya Madini | Mahali yanapopatikana |
|---|---|---|
| 1 | Dhahabu | • **Nyasa** (Darpori, Mpepo na Nindi)<br>• **Mbinga** (Mhongozi na Lukalasi)<br>• **Namtumbo** (Kitanda)<br>• **Tunduru** (Mbesa na Mbati) |
| 2. | Shaba | • **Nyasa** (Mt. Livingstone)<br>• **Mbinga** (Ndongosi)<br>• **Tunduru** ( Mbesa na Mbati) |
| 3 | Makaa ya Mawe | • **Nyasa** (Liweta na Malini)<br>• **Mbinga** (Luanda, Mbuyula na Paradiso)<br>• **Songea** (Mhukuru) |
| 4 | Chuma | • **Namtumbo** (Mtonya) |
| 5 | Urani | • **Namtumbo** (Mtonya) |
| **6** | Madini ya Ujenzi na Viwanda *(Mchanga, Kokoto, Moramu naMawe)* | • **Nyasa**<br>• **Mbinga**<br>• **Namtumbo**<br>• **Songea** (Mhukuru na Mtyangimbole) na<br>• **Tunduru** |
| **7** | **Madini ya Vito** (*Sapphire, Ruby, Alexandrite,Chrisoberly,Spinel, Ganet,Aquamarine,Tourmaline)* | • **Tunduru(**Ngapa,Muhuwesi,Majimaji,Mbuyula na Lukala)<br>• **Nyasa**( Maeneo ya Mwambao wa Ziwa)<br>• **Mbinga** (Maeneo ya Mkako, Masuguru,Ngembambili, Amani Makolo na Kuhagala) |

| | | |
|---|---|---|
| | | • **Namtumbo**(Mputa,Lusewa,Suluti,Mtwarapachani,Mkongo na Kiburungutu) |

**6.2.3.7 Hali ya Utekelezaji wa CSR Ndani ya Mkoa wa Ruvuma**

Timu ilitembelea Halmashauri za Tunduru, Mbinga, Nyasa, Namtumbo na Songea zenye uchimbaji wa Madini na kubaini mambo yafuatayo;

i. Udhaifu mkubwa katika ufuatiliaji na utekelezaji wa CSR wa Makampuni yanayochimba Madini.

ii. Halmashauri kukosa uelewa wa namna ya kusimamia CSR kutokana na wachimbaji wa Madini waliopo katika maeneo yao.

iii. Miradi ya CSR kutekelezwa katika Vijiji vinavyozunguka maeneo ya uchimbaji pekee bila kuwa na tafsiri sahihi ya neno "Local area" kwenye sheria ya madini.

iv. Halmashauri kutokuwa na mtu maalum anayehusika na CSR.

v. Halmashauri kutokuwa na Mwongozo, Hati ya Makubaliano (MoU) na Mpango wa Uwajibikaji wa wachimbaji wa Madini.

vi. Katika maeneo ambayo CSR inatekelezwa haiendani na mauzo ya Madini kutoka kwa wachimbaji. Kwa mfano Ruvuma Coal Ltd iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, ilianza uchimbaji Mwezi April, 2020 hadi kufikia Januari 2022 walikuwa wamechimba na kuuza Makaa ya Mawe tani 1,023,567.85 zenye mauzo ya Tshs 104,007,680,959.46 na endapo wangechangia CSR hata asilimia 0.5 wangechangia Tshs 520,038,404.80 lakini hadi Machi, 2022 wamechangia Tshs 35,000,000 tangu waanze uchimbaji hii ni sawa na asilimia 0.033 ya mauzo.

vii. Wachimbaji wa Madini kutoa fedha kwenye Vijiji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya CSR, lakini miradi imekuwa ikitekelezwa kwa kusuasua. Kwa

mfano Kampuni ya Ruvuma Coal Ltd ilitoa fedha kiasi cha Shilingi Milioni Kumi (10,000,000/=) tangu mwaka 2020 kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Sara kilichopo Mbinga DC lakini hadi kipindi timu inatembelea eneo hilo, mradi huo ulikuwa haujaanza kutekelezwa.

viii. Halmashauri kushindwa kusimamia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Madini kuhusiana na suala la CSR.

ix. Baadhi ya wachimbaji wa Madini kutowajibika kwa jamii kwa kuchangia Miradi ya Maendeleo.

x. Wataalam wa Halmashauri kushindwa kufika kwenye maeneo ya miradi kwa wakati kwa lengo la kutoa ushauri na kutoa maelekezo ya taratibu za utekelezaji wa miradi. Ambapo ilibainika kuwa Kijiji cha Malini kilichopo Nyasa DC kiliingiziwa fedha na Kampuni ya Godmwanga Germs Ltd kiasi cha Shilingi Milioni kumi tangu mwezi Disemba, 2020 kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati lakini wataalam kutoka Halmashauri hawajafika kwa ajili ya kutoa maelekezo ya kitaalam ya eneo la ujenzi na gharama za ujenzi.

xi. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina Madini aina ya Mchanga na Gemstones na timu ilibaini kutokuwepo kwa takwimu za mauzo ya gemstones.

xii. Halmashauri kushindwa kusimamia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Madini kuhusiana na suala la CSR.

#### 6.2.3.8 Miradi Iliyopangwa Kutekelezwa na Iliyotekelezwa na Wachimbaji wa Madini Ikiwa ni Sehemu ya Uwajibikaji kwa Jamii Ndani ya Mkoa wa Ruvuma

Timu ilitembelea Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma pamoja na baadhi ya wachimbaji kwa lengo la kuona hali ya utekelezaji na Uwajibikaji kwa Jamii katika kutekeleza miradi mbalimbali kwenye maeneo hayo. Katika hatua hii, ilibainika kwamba wachimbaji walio wengi hawana Uwajibikaji kwa Jamii na timu ilifanikiwa kupata baadhi ya wachimbaji walio na mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii na utekelezaji wake. Wachimbaji hao kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo;

**Jedwali 41: Wachimbaji Waliowajibika kwa Jamii kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Ruvuma**

| Na. | H/Shauri | Jina la mchimbaji | Mwaka | Kiasi cha CSR | Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga | Tancoal Enegy Ltd | 2020/2021 | 80,300,000 | 22,800,000 |
| | | Ruvuma Coal Ltd | 2020/2021 | 60,000,000 | 15,000,000 |
| | | | 2021/2022 | 45,000,000 | 15,000,000 |
| 2 | Songea DC | Lukolo Company Ltd | 2017- 2019 | 11,833,320 | 11,833,320 |
| 3 | Nyasa DC | Godmwanga Germs Ltd | 2019/2020 | 4,050,000 | 14,050,000 |
| 4 | Tunduru | Ruby International Ltd | 2018 | 70,000,000 | 70,000,000 |
| | | Elia Joseph Gikalo | 2018 | 20,000,000 | 20,000,000 |
| | **JUMLA** | | | **291,183,320** | **168,683,320** |

### 6.2.3.9 Wawekezaji Wengine Wanaowajibika kwa Jamii Nje ya Wachimbaji wa Madini

Timu imebaini uwepo wa Wawekezaji wengine nje ya wachimbaji wa Madini wanaochangia Uwajibikaji kwa Jamii katika maeneo waliyowekeza. Wawekezaji hao ni AVIV, Ndolela farm, Benki za NMB, CRDB, NBC na TCB.

Wawekezaji hawa kwa mujibu wa Sera za Makampuni yao wanatambua Uwajibikaji kwa Jamii kutokana na shughuli wanazozifanya katika maeneo husika na wamekuwa wakitekeleza Uwajibikaji kwa Jamii japo si kwa kiwango kinachoridhisha.

Katika utekelezaji wa CSR kwa upande wa Mabenki, kila tawi limekasimiwa madaraka ya kupokea maombi toka kwenye jamii ya maeneo ilipo Benki kwa vipaumbele vya

sekta ya Elimu na Afya, kisha maombi hayo huwasilishwa Makao Makuu kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa. Viwango vya CSR vinavyotolewa na taasisi hizo za fedha, NMB ni asilimia moja (1%) ya faida na Benki zingine hawakuwa na taarifa za viwango vya CSR kwa kuwa uratibu wake unafanywa Makao Makuu ya taasisi hizo.

**Jedwali 42: Wawekezaji wengine nje ya wachimbaji wanaowajibika kwa Jamii**

| **Taasisi** | **Mwaka** | **Kiwango cha CSR kilichotekelezwa** |
|---|---|---|
| NMB | 2019 - 2022 | 75,865,000.00 |
| CRDB | 2020/2021 | 77,000,000.00 |
| NBC | 2020/2021 | Haijatekeleza |
| TCB | 2021 | 6,480,000.00 |
| AVIV | 2017- 2022 | 93,495,000.00 |
| **JUMLA** | | **252,840,000.00** |

**6.2.3.10 Hali ya Utekelezaji wa Sheria ya Madini Sura Na. 123 Kuhusu Uwajibikaji kwa Jamii Katika Mikoa ya Shinyanga na Geita**

Timu ilifanya ziara ya kwenda kujifunza na kupata uzoefu katika Mikoa ya Shinyanga na Geita ambapo kuna uchimbaji mkubwa wa Madini ya Dhahabu. Katika Mikoa hiyo, timu ilitembelea Halmashauri ya Manispaa Kahama na Halmashauri ya Wilaya Msalala zilizopo katika Mkoa wa Shinyanga pia Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Wilaya ya Geita zilizopo Mkoa wa Geita. Katika maeneo hayo, timu ilifanikiwa kuona mafanikio ya utekelezaji wa Uwajibikaji kwa Jamii wa wachimbaji wa Madini hasa upande wa wachimbaji wakubwa. Mambo ambayo timu imejifunza katika Mikoa hiyo juu ya utekelezaji wa CSR ni kama ifuatavyo;

- Halmashauri zilianza maboresho ya CSR kuanzia mwaka 2018 kutokana na juhudi za Wakuu wa Mikoa kutaka kufanya maboresho kwenye eneo hilo.

Hili lilifanyika baada ya kuongezwa kifungu namba 105 ndani ya sheria ya Madini Sura namba 123 kinachohusu CSR.

- Halmashauri zilipitia Sheria kwa lengo la kupata ufahamu wa utekelezaji mzuri wa CSR, pamoja na maeneo mengine zilipata tafsiri ya neno "Local area" na kutanua wigo wa wanufaika wa CSR kwa mujibu wa tafsiri ya Sheria ya Madini Sura Na. 123 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019. Hivyo, utekelezaji wa CSR unahusisha maeneo yote ya Halmashauri na ngazi ya Mkoa.
- Kila Halmashauri iliandaa Mwongozo wa Uwajibikaji kwa Jamii kwa kuzingatia sheria ya madini Sura Na. 123 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019 kifungu cha 105(4)(a).
- Kila Halmashauri iliteua waratibu wa CSR watakaohusika na masuala yote ya CSR.
- Kufanya vikao vya maridhiano kati ya Halmashauri na wachimbaji wa Madini na kuwa na kiwango cha CSR cha asilimia 1 ya mauzo kwa mwaka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Mji Geita na kiwango cha asilimia 0.7 kwa Halmashauri ya Manispaa Kahama na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, Kuandaa Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR Plan), Hati ya Maridhiano (MoU) na kuunda kamati za kusimamia miradi.
- Kwa mujibu wa Miongozo ya Halmashauri zipo Kamati za Uwajibikaji kwa Jamii ngazi ya Wilaya ambazo kazi yake ni kusimamia shughuli zote za CSR na kufanya vikao vyake kila mwezi na Wakurugenziwa Halmashauri wanagharamia vikao hivyo. Vilevile, yupo mratibu wa CSR ngazi ya Mkoa anayesimamia shughuli zote za CSR kwa Halmashauri zote.
- Halmashauri za Mkoa wa Geita zinatekeleza miradi yake kwa utaratibu wa Mgodi kuingia Mkataba na watoa huduma na kuwasilisha vifaa kwenye Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Hivyo, kazi ya manunuzi na ulipaji wa fedha inafanywa na Mgodi na Halmashauri zinabaki kuwa wasimamizi wa ujenzi wa miradi na Halmashauri za Mkoa wa Shinyanga zinasimamia hatua zote za manunuzi kwa njia ya nguvu ya pamoja *(Force*

*account)* na kuwasilisha Nyaraka za madai kwa Wachimbaji kwa ajili ya malipo.

- Kazi ya ufuatiliaji wa ubora wa miradi inafanywa na Kamati za Uongozi, Wakuu wa Wilaya, Halmashauri na Wachimbaji wa eneo husika kwa lengo la kuwa na thamani ya fedha ya miradi hiyo.

**6.2.3.11 Utekelezaji wa Miradi ya CSR Kwenye Maeneo ya Halmashauri za Kahama, Msalala, Geita TC Na Geita DC**

Timu iliweza kutembelea baadhi ya miradi na kupata taarifa za utekelezaji wa CSR katika Mikoa ya Shinyanga na Geita, ambapo miradi ya CSR katika maeneo hayo imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na mfumo mzuri ulioandaliwa na Mikoa hiyo. Utekelezaji wa miradi ni kama ilivyoainishwa katika majedwali hapo chini;

**i) Halmashauri ya Mji Geita**

**Jedwali Na. 43: Miradi iliyotekelezwa na gharama zake katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2021.**

| Mwaka | Idadi ya Miradi | Kiasi cha CSR (Tshs) | Thamani ya Miradi iliyotekelezwa (Tshs) |
|---|---|---:|---:|
| 2018 | 25 | 5,004,007,955.00 | 5,310,223,409.30 |
| 2019 | 27 | 4,977,500,600.00 | 5,225,460,446.51 |
| 2020 | 47 | 4,645,000,000.00 | 4,154,307,300.00 |
| 2021 | 47 | 4,920,000,000.00 | 1,528,793,140.00 |
| **JUMLA** | **146** | **19,546,508,555.00** | **16,218,784,295.81** |

**ii) Halmashauri ya Wilaya ya Geita**

**Jedwali Na. 44: Miradi iliyotekelezwa na Gharama zake katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020-2021**

| Mwaka | Idadi ya Miradi | Kiasi cha CSR (Tshs) | Thamani ya Miradi iliyotekelezwa (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 2020 | 31 | 4,300,000,000.00 | 3,495,630,217.00 |
| 2021 | 48 | 4,900,000,000.00 | - |
| **JUMLA** | **79** | **9,200,000,000** | **3,495,630,217.00** |

**iii) Halmashauri ya Manispaa ya Kahama**

**Jedwali Na. 45: Miradi iliyotekelezwa na gharama zake katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019/2020**

| Mwaka | | Idadi ya Miradi | Kiasi cha CSR ( Tshs) | Thamani ya Miradi iliyotekelezwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 2019/2020 | Awamu ya 1 | 58 | 2,294,371,653.00 | 1,392,144,801.00 |
| | Awamu ya 2 | 8 | 344,000,000.00 | 330,584,500.00 |
| **JUMLA** | | **66** | **2,638,371,653.00** | **1,722,729,301.00** |

**iv) Halmashauri ya Wilaya Msalala**

**Jedwali Na. 46: Miradi iliyotekelezwa na gharama zake katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi 2021.**

| Mwaka | Idadi ya Miradi | Kiasi cha CSR ( Tshs) | Thamani ya Miradi iliyotekelezwa (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 2019 | 12 | 515,773,000.00 | 497,961,260.00 |
| 2020 | 30 | 900,000,000.00 | 653,103,964.91 |
| 2021 | 20 | 2,530,000,000.00 | 468,605,728.28 |
| **JUMLA** | **62** | **3,945,773,000.00** | **1,619,670,953.19** |

#### 6.2.3.12 Changamoto za Timu Wakati wa Utekelezaji wa Majukumu

i. Baadhi ya wachimbaji na Taasisi kuchelewa na wengine kushindwa kuwasilisha taarifa zao zilizohitajika kwenye timu.
ii. Timu kushindwa kufika kwenye baadhi ya maeneo ya miradi kutokana na changamoto ya miundombinu ya barabara na muda.
iii. Mjumbe mmoja wa timu kukosekana baadhi ya wiki katika utekelezaji wa majukumu ya timu kutokana na kupangiwa kazi nyingine na Mkuu wake wa Taasisi.
iv. Halmashauri hazikuwa na watu maalum wa kutoa taarifa sahihi za utekelezaji wa CSR kwenye timu.

#### 6.2.3.13 Maoni ya Timu

Suala la uwajibikaji kwa jamii kwa wachimbaji wa Madini ndani ya nchi ya Tanzania ni la kisheria, na kwa jinsi hiyo wachimbaji wote wa madini katika Mkoa wa Ruvuma wanapaswa kuendesha shughuli zao za uchimbaji na kulipa Uwajibikaji kwa Jamii ili jamii inayozunguka migodi inufaike na uwepo wa madini kutokana shughuli hizo za uchumi na athari za kimazingira.

Kwa kuwa timu hii imefanikiwa kwenda katika maeneo ya Kahama (Shinyanga) na Geita kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu, uzoefu huo toka maeneo hayo unapaswa kutumika katika Mkoa wa Ruvuma kwa wachimbaji wote waliopo. Kazi ya kuweka kiwango cha uwajibikaji kwa jamii ni ngumu, inahitaji kuwa na meza ya mazungumzo kati ya Serikali ya Mkoa, Halmashauri na wachimbaji, lakini nguvu kubwa iwekwe kwenye ushawishi na mshikamano wa pamoja (upande wa Serikali na Taasisi zake) hususani katika kuweka kiwango cha CSR na utekelezaji wake.

Halikadhalika, eneo jingine la uwajibikaji kwa jamii ambalo Timu imelibaini ni Makampuni yaliyopo ndani ya Mkoa wa Ruvuma hususani taasisi za fedha (Benki) na Wawekezaji katika Sekta ya Kilimo. Hii ni kwa mujibu wa hadidu za rejea ambazo timu ilipewa. Timu imebaini kwamba Makampuni haya yamekuwa na uwajibikaji kwa jamii, lakini bado hakuna mfumo mzuri uliowekwa ili kuwa na kiwango halisi kinachotambulika pamoja na usimamizi wa Serikali. Ni Benki moja tu ya NMB iliyoweka wazi kuwa asilimia moja ya faida inayopatikana kwa mwaka huwa inatolewa ikiwa ni uwajibikaji kwa jamii. Hivyo maeneo haya nayo, timu ina maoni ya kwamba yawekewe mfumo mzuri wa uwajibikaji kwa jamii. Japo la kupendeza ni kwamba makampuni haya yana Sera/miongozo inayobainisha uwepo wa uwajibikaji kwa jamii wa Makampuni yao ili kunufanisha jamii na kuleta mahusiano mazuri katika jamii.

#### 6.2.3.14 Mapendekezo ya Timu

i. Kuteua Waratibu wa CSR ngazi ya Mkoa na Halmashauri ambao wataratibu shughuli zote za CSR pamoja na kuanzisha mchakato wa uboreshaji wa CSR Mkoa wa Ruvuma.
ii. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iitishe kikao cha wadau wa Madini kwa lengo la kutoa elimu ya utekelezaji wa CSR kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika Mikoa ya Geita na Shinyanga.
iii. Mkoa ufanye vikao vya majadiliano na maridhiano na wachimbaji wa Madini ili kuwa na makubaliano ya pamoja ya kiwango cha CSR na namna ya utekelezaji wake.
iv. Timu inapendekeza kiwango cha CSR kiwe kati ya asilimia 0.7 hadi asilimia 1 ya mauzo ya mwaka husika.
v. Tafsiri ya jamii inayozunguka mgodi ‘’Local area’’ kwenye sheria ya madini Sura 123 (R.E 2019) iwe eneo lote la Halmashauri na Mkoa.
vi. Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae Miongozo ya Uwajibikaji kwa Jamii kama sheria ya madini inavyoelekeza.
vii. Kila mchimbaji wa Madini awe anaandaa Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR Plan) kwa kila mwaka.

viii. Halmashauri ziwe na jukumu la kusimamia mwenendo wa utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kupitia CSR bila kupokea fedha kwa miradi inayotekelezwa na wachimbaji wenye Makampuni ya kigeni. Kwa Makampuni ya ndani utaratibu uwekwe wa namna ya kuwa na Mfuko wa pamoja wa CSR utakaosimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

ix. Wakurugenzi waunde Kamati za CSR kwenye maeneo yao.

x. Zitungwe Sheria ndogo ambazo zitawabana wasafirishaji wanaomwaga Makaa ya Mawe barabarani kwa lengo la kuzuia uharibifu wa mazingira.

xi. Kuboresha mawasiliano kwenye taasisi zote za Serikali zinazosimamia Madini kama Tume ya Madini, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi.

xii. Wataalam wa Halmashauri kusimamia hatua zote za utekelezaji wa miradi ya CSR kwa kushirikiana na wachimbaji ili kuwa thamani ya fedha.

xiii. Halmashauri zenye madini zipimwe utendaji kazi wake kwa jinsi zinavyotekeleza miradi ya CSR.

xiv. MoU ibainishe hatua ambazo zitachukuliwa kwa wachimbaji watakaoshindwa kutekeleza Uwajibikaji kwa Jamii.

xv. Kamati za CSR zitoe elimu kwa wananchi na wachimbaji juu ya Sheria ya Madini na namna CSR inavyotakiwa kutekelezwa.

xvi. Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa taarifa za Madini yanayouzwa ili kuweza kutoza ushuru wa huduma (*Service Levy*), CSR na mapato mengineyo kwa uhalisia.

xvii. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ishauri Mamlaka inayohusika ili Sheria ya Madini Sura ya 123 (R.E 2019) itengenezewe kanuni itakayoonesha kiwango cha CSR.

xviii. Utaratibu wa utekelezaji wa CSR utumike pia nje ya wawekezaji wa Madini.

xix. Chombo cha uchunguzi TAKUKURU ichukue hatua za kisheria kufanya uchunguzi ili kubaini matumizi ya fedha shilingi milioni kumi (10,000,000.00) kwa Kijiji cha Sara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kilichotolewa na Kampuni ya mgodi ya Ruvuma Coal kwa mwaka 2020 kwa kuwa kuna viashiria vya ubadhirifu.

#### 6.2.3.15 Hitimisho

Timu inampongeza Mkuu wa Mkoa Ruvuma, Mheshimiwa Kanali Laban Elias Thomas kwa kusimamia kazi hii hadi kukamilika na hatimaye kufikia hatua ya kuanza kuandaa mfumo mzuri wa uwajibikaji kwa jamii wa wachimbaji wa madini Mkoa wa Ruvuma. Kazi ya timu hii imefanyika kwa weledi, uaminifu, uadilifu na kwa bidii kwa lengo la kutimiza azma ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa. Ni wajibu wa kila mdau katika Mkoa wa Ruvuma kutoa ushirikiano wa dhati ili kufikia azma hiyo.

## 6.3 AFYA, LISHE NA USTAWI WA JAMII

### 6.3.1 Sekta ya afya

#### 6.3.1.1 Huduma za Afya

Mkoa una jumla ya vituo **356** vinavyotoa huduma za afya. Kati ya vituo hivyo Hospitali ni **13** zikiwemo **6** za serikali, vituo vya afya **36** kati ya hivyo **10** ni vya mashirika ya dini, zahanati zipo **307** ambapo za serikali ni **246**, Mashirika ya dini ni **26, na 9** ni za mashirika ya umma na **26** ni za watu binafsi.

**a) Mapokezi ya Fedha za Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo**

Kwa mwaka 2020/2021 Mkoa umepokea jumla ya **Shilingi 1,700,00.000.00** kwa ajili ya kujenga/kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya ambapo **Sh. 1,200,000,000.00** zilikuwa kwa ajili ya umaliziaji wa maboma **50** ya zahanati na Sh. **500,000,000.00** kwa ya kituo cha Afya Magazini.

Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa umeendelea na ujenzi wa Hospitali tano (5) za Wilaya katika Halmashauri za Wilaya za Nyasa, Namtumbo, Madaba, Songea DC na Mbinga DC kwa gharama ya Tshs. **3,700,000,000.00.** Mkoa umepokea kiasi cha **Tshs. 7,250,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya **12** kupitia fedha za Tozo na Serikali Kuu**.** Pia Mkoa unaendelea na ujenzi wa vituo vya Afya vitatu **(3)** kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa gharama ya Tshs**. 1,500,000,000.00.** Kwa

upande wa Zahanati Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs. **1,050,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa Zahanati **21** kwenye Halmashauri saba (**7**).

Aidha, Mkoa umepokea pia kiasi cha shilingi **1,780,000,000.00** za kutekeleza Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 - (**Mradi Na. 5144 TCRP)** kama ifuatavyo:

d) **Shilingi Milioni 630,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi wa sekta ya Afya kwa Halmashauri 7 (Madaba DC, Songea DC, Mbinga DC, Nyasa DC, Mbinga TC, Namtumbo DC & Tunduru DC)

e) **Shilingi Milioni 900** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya dharura (emergency Medical Department-EMD) kwa Halmashauri za Madaba DC, Nyasa DC & Tunduru DC

f) **Shilingi 250,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa jengo la huduma za Wagonjwa mahututi (ICU) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

g) **Taarifa ya Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa**

Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs. **2,700,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa awamu ya kwanza ambao unahusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la mionzi na nyumba ya mtumishi.

#### 6.3.1.2 Hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya

Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya imeendelea kuimarika, kwani upatikanaji umeongezeka kutoka 93 (2021) hadi asilimia 96 mwezi Novemba, 2022. Upatikanaji huu umetokana na kuongezeka kwa mapato ya ukusanyaji ya mapato ya uchangiaji wa huduma za afya, ufuatiliaji na usimamizi pamoja na ruzuku ya dawa kutoka serikali kuu.

#### 6.3.1.3 Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto

Vituo vinavyotoa huduma ya Afya ya Uzazi na mtoto vimeongezeka kutoka **324** hadi **348 sawa na asilimia** (98**%)** ya vituo vyote vinavyotoa huduma katika Mkoa. Kati ya vituo vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto, Vituo **316** sawa na asilimia **92** vinatoa huduma ya chanjo. Aidha kati ya vituo vya afya 36, vituo **14** (**38.8%)** ya vituo

vya Afya (H/C) vinatoa huduma kabambe za dharura za mama wajawazito na Watoto wachanga (**CEmONC**).

Kwa upande wa huduma ya wazazi, kiwango cha akina mama waliojifungulia kituoni kimeongezeka kutoka asilimia **84.4** mwaka **2020** hadi asilimia **85.4** Desemba **2021**. Kiwango hiki ni juu ya lengo la taifa la asilimia **80.**

**Jedwali Na. 47: Kuonesha mwenendo wa vifo vya kina mama wazazi Mkoa wa Ruvuma kwa miaka minne (4)- 2019-2022**

| **Na** | **Mwaka** | **Idadi ya vifo** |
|---|---|---|
| 02 | 2019 | 34 |
| 03 | 2020 | 31 |
| 04 | 2021 | 24 |
| 05 | 2022 | 20 |

Idadi ya vifo vya wazazi vimepungua kutoka vifo **24** Disemba mwaka **2021** hadi vifo **20** sawa na vifo **39 /100,000** vizazi hai Novemba mwaka 2022. Sababu zilizochangia vifo ni Kutokwa na damu nyingi PPH, Kifafa cha mimba, mgando katika mishipa ya damu (Embolism), Upungufu wa damu na madhara ya dawa za usingizi (anaethetic complication).

Vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja kwa mwaka **2022** vimepungua kutoka **131** sawa na vifo **3 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2021** hadi vifo **88** sawa na vifo **2 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai Disemaba mwaka 2022**. Sababu zilizochangia vifo hivyo ni magonjwa ya watoto wachanga (perinatal condition). Vifo **35** sawa na asilimia **40.0** Prematurity vifo **25** sawa na asilimia **28.4**, Pneumonia vifo **13** sawa na asilimia15**.0**, Malaria vifo **7** sawa na asilimia **8.0,** Septicemia vifo **5** sawa na asilimia **6.0** na Anaemia vifo **3** sawa na asilimia **3.4** ya vifo vyote.

Takwimu za vifo vya watoto chini ya **miaka mitano** vilivyotolewa taarifa ngazi ya vituo na jamii kwa mwaka **2022** vilikuwa **124** sawa na vifo **3 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai.** Idadi ya vifo hivi imepungua ukilinganisha na vifo **204** sawa na vifo **4 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2021**. Sababu zinazoongoza kwa vifo hivyo ni Neonatal condition vifo **41** sawa na asilimia **33.0**, Pneumonia vifo **33 saw**a na asiimia **26.6** malaria vifo **24** sawa na asilimia **19.3**, Septicaemia vifo **15** sawa na asilimia **12.0** na Anaemia vifo **11** sawa na asilimia **9.0** ya vifo vyote.

**6.3.1.4 Hali ya chanjo**

Katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2022 Mkoa umekuwa na mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma za chanjo mbalimbali kama ifuatavyo;

Chanjo ya kifua kikuu (BCG) ni **141%,** chanjo ya kuzuia kupooza (Polio) **125%,** chanjo ya Donda koo, kukakamaa na kifaduro (DTP3) **123%** chanjo ya kuzuia homa ya mapafu (Pneumonia) **122%,** chanjo ya kuzuia kuharisha (Rota virus) **99.5%,** chanjo ya surua (Measles Rubella) **122%,** chanjo ya Pepopunda (Td) kwa wajawazito **117%** na chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 ni **115%.**

Mkoa umeendelea kutoa chanjo ya ugonjwa wa Korona ikiwa ni jitihada za kupambana na ugonjwa huu ambapo kwa kipindi cha kuanzia tarehe 04 Agosti, 2021 hadi tarehe 31 Oktoba, 2022 jumla ya watu **1,045,390** wamekamilisha dozi ya chanjo ya korona sawa na asilimia **109**. Mkoa uliwekewa kuchanja jumla ya watu 670,577 ambao ni sawa na asilimia 70 ya watu wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea (ambao ni 957,938).

Mkoa wa Ruvuma umeongoza Kitaifa kwa utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 na kupewa vyeti 2 na tuzo kwa vipindi tofauti tofauti kwa mwaka 2021 hadi Mei, 2022. Pia katika mazoezi ya Kitaifa ya utoaji wa chanjo ya polio Mkoa wa Ruvuma umefanya vizuri katika awamu zote 4 (awamu ya kwanza nay a pili Tuliongoza Kitaifa iliyofanyika mwezi Machi na Mei, 2022). Utoaji wa chanjo za kawaida tunaendelea kufanya vizuri tangu tutangazwe kuwa vinara 2021.

#### 6.3.1.5 Huduma za VVU na UKIMWI

Kati ya vituo **356**, vituo **328  sawa na asilimia 92** vinatoa huduma za unasihi na upimaji wa VVU (HTS); vituo **285 sawa na asilimia 80** vinatoa huduma za Kuzuia Maambuzi ya VVU toka kwa Mama kwenda kwa Mtoto (PMTCT); vituo **147 sawa na asilimia 41** vinatoa huduma za tiba na matunzo ya VVU na UKIMWI (CTC); vituo **41 sawa na asilimia 12** vinatoa huduma za Dawa Kinga ya Kuzuia Maambukizi ya VVU (PrEP) na vituo **45 sawa na asilimia 13** vinatoa huduma ya Tohara ya Kitabibu kwa Vijana Wanaume (VMMC).

Kiwango cha maambukizi ya VVU katika Mkoa wa Ruvuma **kimepungua kwa 1.4 sawa na asilimia 20 kutoka asilimia 7.0** mwaka 2011 kutokana na matokeo ya Utafiti Viashirikia vya UKIMWI na Malaria (THMIS) wa mwaka 2011/2012 hadi **asilimia 5.6** mwaka 2016  kwa matokeo ya utafiti matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI (THIS) wa mwaka 2016/2017. Kiwango cha maambukizi ya VVU kwa wanawake ni **asilimia 6.6** na wanaume ni **asilimia 4.5** (THIS 2016/2017).

Katika utekelezaji wa **malengo ya kitaifa ya kimkakati ya 95-95-95 (Tisini na Tano TaTu)** kwa mwaka 2022, Makadirio ya idadi ya Watu Wanaoishi na Maambukizi ya VVU (WAVIU) katika Mkoa ni **63,088,** ambapo wanawake ni **38,716** na wanaume ni **24,372**. Kufikia robo ya Julai - Septemba 2022, **95 ya Kwanza;** watu **60,862** kati ya WAVIU **63,088** sawa na **asilimia 96.5** wamepimwa na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU. **95 ya Pili;** watu  **60,133** kati ya WAVIU **60,862** wanaotambua hali zao za maambukizi ya VVU sawa na **asilimia 98.8,** wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs). Na **95 ya Tatu;** watu **57,367** kati ya WAVIU **60,133** wanaotumia dawa za ARV sawa na **asilimia 95.4,** wamefubaza makali ya VVU. Utekelezaji wa malengo ya Kitaifa ya Kimkakati ya 95-95-95 kwa halmashauri umeainishwa katika jedwali namba 48:

**Jedwali Na 48: kuonyesha Utekelezaji wa Malengo ya Kitaifa ya Kimkakati ya 95-95-95 kwa Halmashauri kwa mwaka 2022 kufikia Robo ya Tatu, Julai - Septemba.**

| Halmashauri | Idadi ya WAVIU | 95 ya Kwanza | 95 ya Pili | 95 ya Tatu | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| Madaba DC | **3,536** | 112.6 | 98.5 | 96.3 | Malengo yamefikiwa |
| Mbinga DC | **7,841** | 105.8 | 98.8 | 95.4 | Malengo yamefikiwa |
| Mbinga TC | **7,620** | 88.9 | 98.9 | 95.7 | 95 ya kwanza haijafikiwa |
| Namtumbo DC | **7,533** | 62.2 | 98.9 | 94.8 | 95 ya kwanza na 95 ya tatu havijafikiwa |
| Nyasa DC | **5,525** | 122.9 | 98.5 | 94.3 | 95 ya Tatu haijafikiwa |
| Songea DC | **5,730** | 105.7 | 98.6 | 95.6 | Malengo yamefikiwa |
| Songea MC | **16,776** | 99.6 | 99.6 | 96.1 | Malengo yamefikiwa |
| Tunduru DC | **8,528** | 88.8 | 97.5 | 94.5 | 95 ya kwanza na 95 ya tatu havijafikiwa |
| **Jumla Mkoa** | **63,088** | **96.3** | **98.8** | **95.4** | Malengo yamefikiwa |

**Chanzo cha Taarifa:** DHIS-2, 10 Desemba, 2022.

Pamoja na mfanikio haya, Mkoa kupitia Timu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya Mkoa (RHMT) imejipanga kuendelea kufanya yafuatayo ili kufikia adhma ya malengo ya **95-95-95** kwa kila mwaka na **0-0-0** (Sifuri Tatu) ifikapo mwaka 2030:

i. Kuimarisha hudumaza rafiki za upimaji wa VVU miongoni mwa watoto (chini ya miaka 15), vijana balehe (miaka 15 - 19), vijana (miaka 20 - 24), wanaume pamoja na watu wa makundi maalumu yenye hatari kubwa ya kupata maambukizi ya VVU (KVPs),

ii. Kuimarisha utoaji wa dawa kinga (PrEP) kwa makundi maalumu pamoja na usambazaji wa mipira ya kinga (kondomu) katika jamii katika maeneo yenye hatari kubwa ya maambukizi ya VVU kama vile nyumba za kulala wageni, baa, sokoni, machimbo, ofisi za umma na binafsi, pamoja na vituo vyote vya kutolea huduma za afya katika halmashauri,

iii. Kuimarisha ufuatiliaji kwa wakati wa watoro wa huduma za utumiaji ARVs kupitia watoa huduma za afya na wahudumu ngazi ya jamii katika vituo vya tiba na matunzo ya VVU/UKIMWI (CTCs), hasa kwa makundi ya watoto, vijana balehe, vijana, wanaume na KVPs,

iv. Kuimarisha mikakati ya utoaji elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU, ufuasi wa dawa za ARVs pamoja na kuzuia unyanyapaa kwa WAVIU katika jamii kupitia vyombo vya habari, elimu ya VVU/UKIMWI pahali za kazi, mikutano ya hadhara na vituo vya kutolea huduma za afya.

### 6.3.2 Huduma za Ustawi wa Jamii

#### 6.3.2.1 Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF)

Mkoa wa Ruvuma unatekeleza Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa kwa mujibu wa Waraka Na.1 wa Mwaka 2018 wa Maboresho ya Mfuko wa Afya ya Jamii ambao umeleta tija kubwa kwa wananchi katika kupata huduma za afya za uhakika. Hadi kufikia 30 Novemba, 2022 jumla ya kaya 25,745 (7.4%) zimeandikishwa kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF).

**Jedwali Na.49: Hali ya iCHF Mkoa wa Ruvuma hadi 30 Novemba, 2022**

| NA | HALMASHAURI | IDADI YA KAYA | KAYA ZILIZOSAJILIWA | ASILIMIA | MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MADABA DC | 12,250 | 1,636 | *13.4%* | 49,080,000.00 |
| 2 | MBINGA DC | 57,738 | 4,965 | *8.5%* | 148,950,000.00 |
| 3 | TUNDURU DC | 82,129 | 6,659 | *8.1%* | 199,770,000.00 |
| 4 | MBINGA TC | 33,256 | 2,579 | *7.8%* | 77,370,000.00 |
| 5 | NAMTUMBO DC | 45,856 | 3,488 | *7.6%* | 104,640,000.00 |
| 6 | SONGEA DC | 33,933 | 2,510 | *7.4%* | 75,300,000.00 |
| 7 | SONGEA MC | 57,640 | 2,549 | *4.4%* | 76,470,000.00 |
| 8 | NYASA DC | 37,367 | 1,359 | *3.6%* | 40,770,000.00 |
| | **JUMLA** | **360,169** | **25,745** | ***7.4%*** | 772,350,000.00 |

#### 6.3.2.2 Usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya Miaka Mitano (U5BR)

Mkoa unaendelea kutekelezwa mpango wa usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano bure ulioanza Machi, 2020 katika Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma. Usajili na utoaji vyeti hufanywa na Wauguzi kwenye vituo vyote vya huduma za afya vinavyotoa huduma za afya ya mama na mtoto. Lengo la Mkoa wa Ruvuma ni kusajili na kuwapatia vyeti watoto 242,140, ambapo hadi tarehe 30 Novemba, 2022 Mkoa umesajili na kutoa vyeti kwa watoto **242,083 (99.9%).**

#### 6.3.3 Huduma za Lishe

Katika kuendelea na kupambana na tatizo la utapiamlo nchini hususani udumavu ***(asilimia 41, TNNS 2018***), Mkoa wa Ruvuma unatekeleza viashiria mbalimbali vilivyoainishwa katika mkataba wa Lishe ulioingiwa baina ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma. Utekelezaji wa mkataba kwa mwaka 2020/2021 Mkoa wa Ruvuma ulikuwa ni mshindi wa pili kitaifa na mwaka 2021/2022 Mkoa umeshika nafasi ya 4 Kitaifa. Matokeo haya kwa kiasi kikubwa yametokana na; -

- ✓ Matumizi ya Kifungu/Lengo Y (Objective Y) katika kutekeleza shughuli zisizo za Lishe.
- ✓ Kutumia vifungu/malengo mengine (objectives) kutekeleza shughuli za Lishe.

Haya yote yaliyotajwa hapo juu yamesababisha Mkoa kutofanya vizuri katika utekelezaji wa Mkataba wa Lishe katika mwaka wa fedha 2021/2022. Hivyo, ili kutekeleza Mkataba wa Lishe kwa Kiwango kinachotakiwa tunapendekeza yafuatayo; -

- ✓ Waweka hazina wa Halmashauri wahakikishe vifungu vya Lishe (Objective Y expenditure codes) vinatumika kulipia shughuli za lishe tu
- ✓ Maafisa Mipango wahakikishe vifungu vya Lishe vinatumika kupanga shughuli za Lishe tu
- ✓ Maafisa Lishe wa ainishe vifungu sahihi vya shughuli anayokwenda kutekeleza.
- ✓ Wakaguzi wa ndani ya Halmashauri wahakikishe wanafanya uhakiki wa fedha za lishe kila robo mwaka ili kubaini changamoto mapema na kuzitatua kwa wakati.

Aidha, katika mwaka wa fedha **2022/2023** Mkoa kupitia Halmashauri zake umeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo utengaji na utoaji wa fedha kwa ajili kutekeleza afua za lishe, ambapo jumla ya **TZS. 355,274,918.3** zimepangwa na hadi kufikia Novemba, 2022 jumla ya **TZS. 122,852,599** sawa na asilimia **34.6 tu** zimetolewa

kutekeleza afua za lishe katika Halmashauri kama inavyoonesha katika jedwali namba 50.

**Jedwali Na. 50: Matumizi ya fedha zilizopangwa kutekeleza afua za lishe kwa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2022/2023**

| NA | HALMASHAURI | FEDHA ILIYOTUMIKA JULAI - NOVEMBA, 2022 IKILINGANISHWA NA FEDHA ILIYOPANGWA MWAKA 2022/2023 | | | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KWA MTOTO (PER CAPITA PLANNED) FY 2022/2023 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KILICHOPANGWA | KILICHOTUMIKA HADI NOVEMBA, 2022 | % | IDADI YA WATOTO | TZS |
| 1 | SONGEA MC | 39,860,000 | 24,404,000 | 61.2 | 32216 | 1237 |
| 2 | MBINGA TC | 23,971,068 | 7,526,000 | 31.4 | 20961 | 1144 |
| 3 | SONGEA DC | 38,729,712 | 6,570,000 | 17.0 | 21396 | 1810 |
| 4 | MBINGA DC | 92,711,750 | 37,140,000 | 40.1 | 41575 | 2230 |
| 5 | TUNDURU DC | 71,204,134 | 21,254,600 | 29.9 | 47833 | 1489 |
| 6 | NAMTUMBO DC | 39,432,000 | 5,070,000 | 12.9 | 36712 | 1074 |
| 7 | NYASA DC | 23,823,206 | 11,744,000 | 49.3 | 27023 | 882 |
| 8 | MADABA DC | 25,543,048.3 | 9,143,999 | 35.8 | 7684 | 3324 |
| **JUMLA KUU** | | **355,274,918.3** | **122,852,599** | **34.6** | **235400** | **1509** |

**NB:** - Halmashauri **saba (7)** ziliweza kupanga kwa kufuata kigezo cha kima cha chini cha **TZS. 1000** kwa kila mtoto chini ya miaka mitano, isipokuwa ***Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa*** ambayo ina jumla ya Watoto wenye umri chini ya miaka mitano **27023** lakini wamepanga **TZS. 23,823,206** badala ya kima cha chini cha **TZS. 27,023,000**. Athari ya hii itafanya Halmashauri kutofikia matumizi ya kima cha chini cha **TZS. 1000** wakati wa tathmini na mwisho wa siku itaathiri matokea ya Mkoa Kitaifa.

**Ushauri:** Tunapoelekea kwenye **re–allocation** Halmashauri ihakikishe inafanya marekebisho ili kuepuka hii changamoto kama iliyojitokeza mwaka wa fedha 2021/2022.

### 6.3.3.1 Mambo yanayosababisha lishe duni ni: -

i. Ulaji duni wa chakula unaotokana na kula milo michache na kiasi kisichotosheleza mahitaji ya virutubishi mwilini, hii pia hujumuisha kutowanyonyesha watoto ipasavyo.
ii. Magonjwa ya mara kwa mara yanayoondoa hamu ya kula na, kusababisha ufyonzaji duni wa virutubishi na huongeza mahitaji ya virutubishi mwilini.
iii. Matumizi mabaya ya chakula mfano kuuza chakula chote, kutumia nafaka kutengenezea pombe nk.
iv. Utayarishaji mbaya wa chakula unaopoteza virutubishi kama kuosha mboga za majani baada ya kukatakata.
v. Upungufu katika matunzo ya makundi maalumu (watoto wadogo, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha, wazee na wagonjwa) Makundi haya yanahitaji matunzo na huduma muhimu za kiafya kama vile chanjo, kupata vidonge vya nyongeza, kutibu maradhi na huduma za kilishe.

Utapiamlo huathiri afya, uzalishaji mali na maendeleo katika jamii. Athari hizi hujitokeza katika hali ya kuchelewa kwa hatua za ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili, kuongezeka kwa magonjwa na vifo vya watoto, kupungua kwa kinga mwili na kupungua kwa uwezo wa kufanya kazi za uzalishaji mali.

Hivyo, katika kuhakikisha jamii inaondokana na tatizo hili la lishe Halmashauri na Mkoa ni muhimu kuendelea kuelekeza nguvu katika kusimamia utekelezaji wa mikataba ya lishe ngazi ya Halmashauri, kata na vijiji / Mitaa ili jamii iweze:-

a) kubadili tabia na kuzingatia ulaji unaofaa.
b) Kupata elimu sahihi ya lishe kwa kupitia njia mbalimbali kama vyombo vya habari vilivyopo, ngoma za asili, viongozi wa dini na kimila.
c) Kupata elimu sahihi ya lishe katika kipindi cha siku 1000 za uhai wa mtoto (yaani toka mimba ilipotungwa hadi mtoto anapofikisha umri wa miaka 2) –
d) Kuimarisha maadhimisho ya siku za afya na Lishe ya Kijiji zinazofanyika kila baada ya miezi mitatu.
e) Mkoa na Halmashauri kuhakikisha fedha inayotengwa kwa shughuli za lishe inatolewa na kufanya shughuli za lishe kama zilivyotengwa.
f) Mkoa na Halmashauri kuendelea kufanya usimamizi shirikishi ili kuweza kutambua changamoto zinazojitokeza kwa wakati na kuzitafutia ufumbuzi.

## 6.4 ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Sekta ya Elimu Mkoani inafanya kazi kwa ushirikiano na Halmashauri, Idara ya uthibiti ubora wa elimu, Idara ya Tume ya utumishi wa walimu (TSC), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, vyuo vya Ualimu na Mamlaka ya vyuo vya ufundi (VETA), Chuo kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na maktaba ya Mkoa. Jedwali lifuatalo linaainisha mchanganuo wa Taasisi za elimu zilizopo Mkoa wa Ruvuma.

**Jedwali Na.51: Idadi ya taasisi za elimu katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Novemba, 2022**

| Halmashauri | Elimu ya Awali | | Elimu ya Msingi | | Elimu ya Sekondari | | Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi | | VETA | | Vyuo vya Ualimu | | Vyuo vya Elimu ya Juu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *S | *B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B |
| Madaba | 28 | 1 | 28 | 1 | 10 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mbinga dc | 164 | 3 | 164 | 3 | 31 | 16 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mbinga TC | 72 | 9 | 72 | 9 | 15 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Namtumbo | 108 | 5 | 108 | 5 | 26 | 8 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Nyasa | 111 | 0 | 111 | 0 | 16 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Songea DC | 78 | 3 | 78 | 3 | 17 | 5 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Songea MC | 82 | 14 | 82 | 14 | 25 | 18 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Tunduru | 151 | 1 | 151 | 1 | 24 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **794** | **36** | **794** | **36** | **164** | **59** | **5** | **4** | **3** | **1** | **1** | **2** | **1** | **1** |
| **Jumla Kuu** | **830** | | **830** | | **223** | | **9** | | **4** | | **3** | | **2** | |

Chanzo: *Taarifa za Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma Novemba,2022*
*S – Serikali *B – Binafsi

### 6.4.1 Elimu ya Awali na Msingi

Elimu ya Awali ni hatua muhimu ya Maandalizi katika mzunguko wa elimu. Serikali ya Tanzania imeirasmisha na kujumuisha elimu hii kwenye mfumo rasmi wa elimu na kuagiza kila shule ya msingi iwe na darasa la elimu ya awali litakaloandikisha watoto wenye umri wa miaka 5-6. Elimu ya Awali inachukua miaka miwili bila ya mitihani ya kuwapandisha watoto. Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo (ETP) ya mwaka

1995, Elimu ya Awali inakusudiwa kuhimiza maendeleo ya jumla ya haiba ya mwanafunzi, sifa za kimwili, kiakili na kimaadili na uwezo.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya shule za msingi **828**, kati ya hizo za Serikali ni **793** na zisizo za Serikali ni **35**. Mkoa umeanza zoezi la uandikishaji wa wanafunzi wa awali kwa mwaka wa masomo utakaoanza mwezi januari 2023 kama inavyoonesha hapa chini: -

**Jedwali Na. 52: Idadi ya maoteo na uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali wa mwaka 2023 hadi Novemba,2022**

| HALMASHAURI | MAOTEO | | | WALIOANDIKISHWA (WASIO WA MAHITAJI MAALUM) | | | WALIOANDIKISHWA (MAHITAJI MAALUM) | | | JUMLA WALIOANDIKISHWA | | | ASILIMIA YA UANDIKISHAJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JUMLA | WAV | WAS | JUMLA | WAV | WAS | JUMLA | WAV | WAS | JUMLA | WAV | WAS | JUMLA |
| MADABA | 645 | 1293 | 596 | 579 | 1175 | 9 | 6 | 15 | 605 | 585 | 1190 | 1775 | 91 | 92 | 91.6 |
| MBINGA DC | 3386 | 3195 | 6581 | 1114 | 1125 | 2239 | 0 | 0 | 0 | 1114 | 1125 | 2239 | 33 | 35 | 34 |
| MBINGA TC | 2255 | 2314 | 4569 | 1376 | 1297 | 2673 | 27 | 31 | 58 | 1403 | 1328 | 2731 | 46 | 57 | 60 |
| NAMTUMBO | 3875 | 3762 | 7632 | 3022 | 3097 | 6119 | 13 | 19 | 32 | 3035 | 3116 | 6151 | 78 | 83 | 81 |
| NYASA | 2798 | 2689 | 5487 | 1423 | 1400 | 2823 | 2 | 1 | 3 | 1425 | 1401 | 2826 | 51 | 52 | 52 |
| SONGEA DC | 2157 | 2162 | 4319 | 1422 | 1399 | 2821 | 4 | 6 | 10 | 1426 | 1405 | 2831 | 66 | 65 | 66 |
| SONGEA MC | 2994 | 3243 | 6237 | 1378 | 1590 | 2968 | 4 | 7 | 0 | 1382 | 1597 | 2979 | 46 | 49 | 48 |
| TUNDURU | 2972 | 3146 | 6094 | 1350 | 1433 | 2782 | 7 | 3 | 10 | 1357 | 1436 | 2792 | 46 | 46 | 46 |
| **JUMLA** | **21,082** | **21,804** | **41,515** | 11664 | 12516 | 22434 | 63 | 82 | 718 | 11727 | 12598 | 24324 | **56** | **58** | **57** |

***Chanzo: Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa Novemba, 2022***

**i) Idadi ya wanafunzi darasa la Awali-VII mwaka 2022**

Mkoa wa Ruvuma hadi kufikiaNovemba, 2022 una idadi ya wanafunzi wa darasa la Awali hadi la VII **353,509** Kati yao wavulana **175,368** na wasichana**178,141.**

**ii) Walimu wa Shule za Msingi hadi Novemba, 2022**

Hadi kufikia Novemba, 2022 mahitaji ya walimu wa shule za msingi ni **10,071**, Waliopo **6,214** hivyo upungufu ni walimu **3,857.** Mchanganuo wa idadi ya walimu imeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na. 53. Idadi ya walimu wa shule za msingi kwa kila Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Novemba,2022**

| **WALIMU WA SHULE ZA MSINGI** | | | |
|---|---|---|---|
| **Halmashauri** | **Mahitaji** | **Waliopo** | **Upungufu** |
| Madaba DC | 323 | 196 | 127 |
| Mbinga DC | 1898 | 991 | 907 |
| Mbinga TC | 1,026 | 626 | 400 |
| Namtumbo DC | 1342 | 929 | 413 |
| Nyasa DC | 1175 | 665 | 510 |
| Songea DC | 967 | 523 | 444 |
| Songea MC | 1275 | 1177 | 98 |
| Tunduru | 2065 | 1107 | 958 |
| **JUMLA** | **10,071** | **6214** | **3857** |

**iii) Hali ya ufaulu wa mtihani wa darasa la saba 2021**

Mwaka **2021** wanafunzi wa darasa la saba wapatao **39,614 walisajiliwa** kufanya mtihani wa darasa la saba. Wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi walikuwa ni **39,604** sawa na asilimia **99.9.** Wanafunzi waliofaulu mtihani walikuwa **28,356** sawa na asilimia **73.1** ambapo wanafunzi wote waliofaulu wamechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari.

**Jedwali Na. 54: Hali ufaulu wa mtihani wa darasa la saba mwaka 2021 na waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza Januari, 2022**

| NA | HALMASHAURI | WALIOFANYA MTIHANI | | | WALIOCHAGULIWA | | | % ASILIMIA | NAFASI ZA UFAULU KIHALMASHAURI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | WAS | WAV | JML | WAS | WAV | JML | | |
| 1 | SONGEA(M) | 3,058 | 2,818 | 5,876 | 2,770 | 2,402 | 5,172 | 88.019 | 1 |
| 2 | MADABA | 675 | 645 | 1,320 | 580 | 559 | 1,139 | 86.288 | 2 |
| 3 | NYASA | 2,245 | 2,284 | 4,529 | 1,768 | 1,662 | 3,430 | 75.734 | 3 |
| 4 | NAMTUMBO | 2,752 | 2,745 | 5,497 | 2,054 | 1,990 | 4,044 | 73.567 | 4 |
| 5 | MBINGA(M) | 1,809 | 1,608 | 3,417 | 1,365 | 996 | 2,361 | 69.096 | 5 |
| 6 | TUNDURU | 4,198 | 4,116 | 8,314 | 2,573 | 2,932 | 5,505 | 66.214 | 6 |
| 7 | SONGEA(V) | 1,743 | 1,721 | 3,464 | 1,128 | 1,053 | 2,181 | 62.962 | 7 |
| 8 | MBINGA(V) | 3,562 | 3,625 | 7,187 | 2,474 | 2,050 | 4,524 | 62.947 | 8 |

### iv) Hali ya samani katika shule za Msingi

Hadi kufikia Novemba, 2022 Mkoa una mahitaji ya madawati **126,248** yaliyopo ni **102,430** na upungufu ni **23,818** Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Wilaya zake umeendelea na jitihada mbalimbali ili kuweza kuondoa upungufu uliopo.

**Jedwali Na.55. Hali ya samani katika shule za msingi hadi kufikia Novemba ,2022**

| NA. | HALMASHAURI | MADAWATI | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | MAHIT. | YALIOPO | UPUNG. | ZIADA |
| 1 | Madaba | 4153 | 4524 | 0 | 371 |
| 2 | Mbinga DC | 22231 | 17872 | 4359 | |
| 3 | Mbinga Mji | 10777 | 8388 | 2389 | |
| 4 | Namtumbo | 17115 | 13867 | 3248 | |
| 5 | Nyasa | 15661 | 12325 | 3336 | |
| 6 | Songea DC | 11613 | 10455 | 1158 | |
| 7 | Songea MC | 18516 | 16771 | 1745 | |
| 8 | Tunduru | 26182 | 18228 | 7954 | |
| | **JUMLA** | **126,248** | **102,430** | **23,818** | |

*Chanzo: Sensa Elimu msingi Novemba,2022*

**v) Hali ya majengo katika shule za Msingi**

Hadi kufikia Novemba, 2022 Mkoa una mahitaji ya vyumba vya madarasa **10,003**; yaliyopo ni **6,294** na upungufu ni **3,709**. Kwa upande wa matundu ya vyoo Mkoa ulikuwa na mahitaji **17,372** yaliyopo ni **9,977** na upungufu ni **7,395**.

**Jedwali Na. 56: Hali ya majengo ya Shule za Msingi hadi kufikia Novemba ,2022**

| | | MADARASA | | | NYUMBA | | | MATUNDU YA VYOO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU |
| 1 | MADABA | 368 | 273 | 95 | 345 | 113 | 232 | 603 | 648 | -45 |
| 2 | MBINGA DC | 1760 | 1145 | 615 | 1698 | 618 | 1080 | 2923 | 1712 | 1211 |
| 3 | MBINGA TC | 921 | 567 | 354 | 874 | 209 | 665 | 1555 | 892 | 663 |
| 4 | NAMTUMBO | 1411 | 875 | 536 | 1325 | 439 | 886 | 2696 | 1583 | 1113 |
| 5 | NYASA | 1224 | 788 | 436 | 1114 | 345 | 769 | 2125 | 1171 | 954 |
| 6 | SONGEA | 914 | 650 | 264 | 863 | 264 | 599 | 1552 | 1015 | 537 |

| | | MADARASA | | | NYUMBA | | | MATUNDU YA VYOO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU |
| | DC | | | | | | | | | |
| 7 | SONGEA MC | 1453 | 962 | 491 | 1224 | 119 | 1105 | 2667 | 1436 | 1231 |
| 8 | TUNDURU | 1952 | 1034 | 918 | 1840 | 548 | 1292 | 3251 | 1520 | 1731 |
| **JUMLA KUU** | | **10003** | **6294** | **3709** | **9283** | **2655** | **6628** | **17372** | **9977** | **7395** |

*Chanzo: Sensa Elimumsingi Novemba,2022*

### 6.4.2 Elimu ya Sekondari

Mkoa una jumla ya shule za sekondari **218** zikiwemo **160** za Serikali na **58** ni shule za binafsi. Kati ya shule **160** za Serikali, shule tano **(5)** ni za bweni na shule **155** ni za kutwa. Kati ya shule **218** zenye kidato cha tano na sita ni **35** (Serikali **23** na zisizo za Serikali **12**).

**Jedwali Na. 57: Idadi ya Shule za Sekondari**

| **Halmashauri** | **Elimu ya Sekondari** | |
|---|---|---|
| | **Serikali** | **Binafsi** |
| Madaba DC | 8 | 3 |
| Mbinga DC | 31 | 16 |
| Mbinga TC | 15 | 5 |
| Namtumbo DC | 25 | 8 |
| Nyasa DC | 16 | 1 |
| Songea dC | 17 | 5 |
| Songea MC | 24 | 18 |
| Tunduru DC | 24 | 2 |
| **Jumla** | **160** | **58** |
| **Jumla kuu** | **218** | |

***Chanzo: Sensa Elimu msingi Novemba, 2022***

**Jedwali Na. 58: Idadi ya wanafunzi Kidato cha Kwanza hadi Sita Oktoba,2022**

| SN | Halmashauri | Wavulana | Wasichana | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Madaba | 1747 | 2226 | 3973 |
| 2 | MBINGA DC | 6732 | 8024 | 14756 |
| 3 | Mbinga Tc | 3614 | 4401 | 8015 |
| 4 | Namtumbo | 5412 | 5712 | 11124 |
| 5 | Nyasa | 4125 | 4706 | 8831 |
| 6 | Songea Dc | 3024 | 4316 | 7340 |
| 7 | Songea Mc | 9465 | 10589 | 20054 |
| 8 | Tunduru | 6793 | 5634 | 12427 |
| | **Jumla** | **40,912** | **45,608** | **86,520** |

***Chanzo: Sensa Elimu msingi Novemba ,2022***

**i) Walimu wa Shule za Sekondari hadi Novemba ,2022**

Hadi kufikia No vemba ,2022 mahitaji ya walimu wa shule za sekondari ni **4,041**, Waliopo **3,523** hivyo upungufu ni walimu **518** Mchanganuo wa idadi ya walimu kwa masomo imeoneshwa katika majedwali yafuatayo:

**Jedwali Na.59:1Idadi ya Walimu kufikia Novemba, 2022 Kwa masomo ya Sanaa na lugha**

| NA | **1.Mahitaji ya walimu wa masomo ya sanaa na Lugha** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Halmashauri** | **Mahitaji** | **Waliopo** | **Upungufu** |
| 1 | Madaba DC | 118 | 132 | -14 |
| 2 | Mbinga DC | 426 | 149 | 277 |
| 3 | Mbinga TC | 218 | 245 | -27 |
| 4 | Namtumbo DC | 290 | 296 | -6 |
| 5 | Nyasa DC | 250 | 174 | 76 |
| 6 | Songea MC | 585 | 772 | -187 |
| 7 | Songea DC | 254 | 219 | 35 |
| 8 | Tunduru DC | 332 | 310 | 22 |
| | **JUMLA** | **2473** | **2297** | **176** |

**Jedwali Na.60: Idadi ya Walimu kufikia Novemba ,2022 kwa masomo ya sayansi**

| Na | 2.Walimu wa Sayansi | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Halmashauri** | **Mahitaji** | **Waliopo** | **Upungufu** |
| 1 | Madaba DC | 70 | 64 | **6** |
| 2 | Mbinga DC | 290 | 235 | **55** |
| 3 | Mbinga TC | 144 | 120 | **24** |
| 4 | Namtumbo DC | 167 | 153 | **14** |
| 5 | Nyasa DC | 191 | 88 | **103** |
| 6 | Songea DC | 96 | 142 | **-46** |
| 7 | Songea MC | 361 | 260 | **101** |
| 8 | Tunduru DC | 249 | 168 | **81** |
| | **JUMLA** | **1,568** | **1230** | **338** |

### ii) Walimu wa Ajira Mpya

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi **Juni, 2022** ilitoa ajira kwa walimu katika Mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo Mkoa wa Ruvuma ulipangiwa jumla ya walimu **389 (Me 279, Ke 110)** kwa shule za Msingi na Sekondari. Aidha, walimu **213 (Me 175, Ke 38)** walipangwa katika shule za Sekondari ambapo kati yao walimu **212 (Me 174**, **Ke 38**) tayari wameripoti katika shule walizopangiwa. Kwa upande wa shule za Msingi walipangwa walimu **176 (Me 104, Ke72)** na wote wameripoti.

**Jedwali Na. 61 : Idadi ya Walimu wa ajira mpya walioripoti Mkoa wa Ruvuma Juni, 2022**

| **Na.** | **Halmashauri** | **Msingi** | **Sekondari** | | | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Sanaa** | **Sayansi** | **Jumla** | |
| 1 | MADABA | 2 | 2 | 4 | 6 | 8 |
| 2 | MBINGA DC | 40 | 11 | 37 | 48 | 88 |
| 3 | MBINGA TC | 5 | 4 | 21 | 25 | 30 |
| 4 | NAMTUMBO | 24 | 4 | 25 | 29 | 53 |
| 5 | NYASA | 24 | 7 | 12 | 19 | 43 |
| 6 | SONGEA DC | 25 | 4 | 15 | 19 | 44 |
| 7 | SONGEA MC | 0 | 1 | 36 | 37 | 37 |
| 8 | TUNDURU | 56 | 5 | 24 | 29 | 85 |
| **JUMLA** | | **176** | **38** | **174** | **212** | **388** |

**iii) Hali ya ufaulu wa kidato cha nne**

Mkoa wa Ruvuma kitaaluma unaendelea kufanya jitihada za makusudi ili kuweza kupata matokeo mazuri zaidi. Mwaka 2021 Mkoa ulikuwa na ufaulu wa asilimia **90.1**% Juhudi za kupandisha ufaulu na kudhibiti udanganyifu ziliendelea kufanyika.

**Jedwali Na.62: Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne kwa miaka mitatu (CSEE 2019-2021)**

| MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) | |
|---|---|
| **MWAKA** | **ASILIMIA YA UFAULU** |
| 2019 | 86.06 |
| 2020 | 89.4 |
| 2021 | 90.1 |

*Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania 2021*

**iv) Ufaulu wa kidato cha Sita 2022**

Mkoa umeendelea kufanya jitihada kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika matokeo ya kidato cha Sita. Mwaka 2022 Mkoa umepandisha ufaulu na kupata wastani wa ufaulu wa 99.9.

**Jedwali Na.63: Jedwali Na.11.1 Matokeo ya mtihani wa kidato cha sita kwa miaka mitatu (ACSEE 2018-2022)**

| MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (ACSEE) | | |
|---|---|---|
| **MWAKA** | **WALIOFANYA** | **% YA UFAULU** |
| 2019 | 3582 | 99.7 |
| 2020 | 3282 | 99.8 |
| 2021 | 3482 | 99.9 |
| 2022 | 3488 | 100 |

***Chanzo: Baraza la Mitihani la Tanzania,2022***

### v) Miundombinu ya shule za sekondari

Miundombinu ya shule za sekondari imekuwa ikijengwa ili kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia yakiwemo madarasa, majengo ya utawala, nyumba za walimu, Mabweni, Maktaba, maabara na vyoo. Hadi kufikia Novemba ,2022 miundombinu ya shule za sekondari ilikuwa kama ifuatavyo;

**Jedwali Na.64: Miundombinu ya shule za Sekondari hadi kufikia Novemba ,2022**

| | MADARASA | | | MABWENI | | | NYUMBA | | | MATUNDU YA VYOO | | | MAABARA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU |
| MADABA | 127 | 151 | -24 | 17 | 15 | 2 | 190 | 74 | 116 | 188 | 172 | 16 | 36 | 33 | 3 |
| MBINGA DC | 484 | 556 | -72 | 114 | 63 | 51 | 726 | 216 | 510 | 837 | 746 | 91 | 143 | 108 | 35 |
| MBINGA TC | 240 | 254 | -14 | 4 | 3 | 1 | 351 | 42 | 309 | 400 | 385 | 15 | 60 | 44 | 16 |
| NAMTUMBO | 323 | 320 | 3 | 99 | 48 | 51 | 484 | 165 | 319 | 645 | 437 | 208 | 91 | 61 | 30 |
| NYASA | 274 | 256 | 18 | 48 | 9 | 39 | 349 | 90 | 259 | 442 | 260 | 182 | 54 | 36 | 18 |
| SONGEA DC | 258 | 299 | -41 | 72 | 34 | 38 | 357 | 98 | 259 | 455 | 419 | 36 | 66 | 55 | 11 |
| SONGEA MC | 546 | 522 | 24 | 138 | 96 | 42 | 804 | 115 | 689 | 1176 | 915 | 261 | 127 | 94 | 33 |
| TUNDURU | 357 | 406 | -49 | 84 | 38 | 46 | 496 | 159 | 337 | 612 | 526 | 86 | 78 | 53 | 25 |
| **Jumla Kuu** | **2609** | **2764** | **-155** | **576** | **306** | **270** | **3757** | **959** | **2798** | **4755** | **3860** | **895** | **655** | **484** | **171** |

*Chanzo: Sensa Elimumsingi Novemba ,2022*

### vi) Samani

Hadi kufikia Novemba, 2022 hali ya samani katika shule za sekondari kwa ajili ya wanafunzi ni, mahitaji ya meza ni **88,350,** zilizopo zikiwa ni **83,346** na Upungufu ni **5,004**. Mahitaji ya viti ni **88,506**, vilivyopo ni **82,766** upungufu ni viti **5,740**.

**Jedwali Na.65: Samani katika shule za sekondari kufikia Novemba ,2022**

| | | MEZA | | | VITI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU | MAHITAJI | YALIYOPO | UPUNGUFU |
| 1 | MADABA | 3975 | 4227 | -252 | 3972 | 4240 | -268 |
| 2 | MBINGA DC | 15597 | 15559 | 38 | 15597 | 15264 | 333 |
| 3 | MBINGA TC | 8043 | 7751 | 292 | 8043 | 7761 | 282 |
| 4 | NAMTUMBO | 11102 | 9992 | 1110 | 11094 | 9808 | 1286 |
| 5 | NYASA | 9146 | 8695 | 451 | 9146 | 8602 | 544 |
| 6 | SONGEA DC | 7638 | 7160 | 478 | 7648 | 6474 | 1174 |
| 7 | SONGEA MC | 20281 | 16947 | 3334 | 20281 | 17668 | 2613 |
| 8 | TUNDURU | 12568 | 13015 | -447 | 12725 | 12949 | -224 |
| **JUMLA KUU** | | **88350** | **83346** | **5004** | **88506** | **82766** | **5740** |

***Chanzo: Sensa Elimumsingi Novemba ,2022***

**vii) Maabara**

Maabara za sayansi hadi kufikia Novemba, 2022 ni kama ifuatavyo; mahitaji ni **655,** zilizopo ni **484** pungufu ni **171**.

**Jedwali Na.66: Maabara za sayansi katika shule za sekondari**

| MAABARA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **HALMASHAURI** | **MAHIT.** | **YALIOPO** | **UPUNG.** |
| 1 | MADABA | 36 | 33 | 3 |
| 2 | MBINGA DC | 143 | 108 | 35 |
| 3 | MBINGA TC | 60 | 44 | 16 |
| 4 | NAMTUMBO | 91 | 61 | 30 |
| 5 | NYASA | 54 | 36 | 18 |
| 6 | SONGEA DC | 66 | 55 | 11 |
| 7 | SONGEA MC | 127 | 94 | 33 |
| 8 | TUNDURU | 78 | 53 | 25 |
| **JUMLA** | | **655** | **484** | **171** |

***Chanzo: Sensa Elimumsingi Novemba,2022***

**6.4.3 Utekelezaji wa Programu ya Elimu Bila Malipo**

Sera ya utoaji wa Elimu Bila Malipo inaendelea kutekelezwa ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Oktoba 2022 Mkoa umepokea kiasi cha **5,090,198,358.75** ambazo zimesaidia katika uendeshaji wa shule na kuboresha na kuimarisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi na sekondari ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada. Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri unaendelea kufuatilia na kutekeleza kwa ufanisi utoaji wa elimu bila malipo ili fedha ya Serikali inayowekezwa iweze kutoa Matokeo chanya katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika Mitihani ikiwemo kuimarisha taaluma na elimu kwa ujumla na hivyo kujenga jamii yenye uelewa na kujiletea maendeleo

### 6.4.4 Mapokezi ya Fedha za Miradi ya Mendeleo Sekta ya Elimu

**i. Ujenzi wa Shule mpya za Sekondari kupitia Mradi wa SEQUIP**

Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa ulipokea kiasi cha shilingi Bilioni **7,700,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya **11** za Sekondari katika Halmashauri zote 8 za Mkoa wa Ruvuma.ujenzi huu unajumuisha ujenzi wa shule ya Mkoa ya Wasichana inayojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa gharama ya shilingi bilioni **3,000,000,000.00.** Ujenzi wa shule hizi upo katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwa ni maandalizi ya kupokea wanafunzi mwezi Januari 2023.

**ii. Ukamilishaji wa Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa na Maabara kupitia Fedha za Tozo na Serikali Kuu,**

Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa ulipokea fedha kiasi cha Tshs. **2,152,500,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa **128** ya shule za Msingi na Sekondari na Maabara **23** za Shule za Sekondari kupitia fedha za Tozo na Serikali Kuu. Pia tulipokea Tshs. **540,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa na mabweni Shule Sekondari ya Wasichana Songea na Shule ya Sekondari ya Wavulana Songea na kama mchanganuo wake unavyoonekana kwenye jedwali 67.

**Jedwali Na. 67: Fedha za Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa na Maabara kupitia Fedha za Tozo na Serikali Kuu,**

| HALMASHAURI | MADARASA | | MAABARA | | MABWENI | KIASI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | IDADI | KIASI | IDADI | KIASI | | |
| MADABA DC | 12 | 362,500,000.00 | 4 | 120,000,000.00 | | |
| MBINGA DC | 9 | 112,500,000.00 | 0 | 0 | | |
| MBINGA TC | 18 | 225,000,000.00 | 0 | 0 | | |
| NAMTUMBO DC | 21 | 262,500,000.00 | 5 | 150,000,000.00 | | |
| NYASA DC | 12 | 37,500,000.00 | 0 | 0 | | |
| SONGEA DC | 0 | 0 | 0 | 0 | | |
| SONGEA MC | 28 | 402,500,000.00 | 4 | 100,000,000.00 | 4 | 400,000,000.00 |
| TUNDURU DC | 28 | 350,000,000.00 | 10 | 30,000,000.00 | | |
| **JUMLA YA MKOA** | **128** | **1,752,500,000** | **23** | **400,000,000.00** | **4** | **400,000,000.00** |

### i. Ujenzi wa Madarasa ya Sekondari Mwaka 2022/2023

Aidha mwezi Oktoba, 2022 Serikali ilitoa kiasi cha sh. **3,120,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya wanafunzi wa Kidato cha kwanza kwa mwaka 2023

**Jedwali Na 68: Fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Madarasa ya Kidato cha Kwanza 2023**

| HALMASHAURI | IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA | KIASI CHA FEDHA KWA DARASA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Madaba | 10 | 20,000,000.00 | 200,000,000.00 |
| Mbinga DC | 10 | 20,000,000.00 | 200,000,000.00 |
| Mbinga TC | 11 | 20,000,000.00 | 220,000,000.00 |
| Namtumbo | 17 | 20,000,000.00 | 340,000,000.00 |
| Nyasa | 12 | 20,000,000.00 | 240,000,000.00 |
| Songea DC | 10 | 20,000,000.00 | 200,000,000.00 |
| Songea MC | 76 | 20,000,000.00 | 1,520,000,000.00 |
| Tunduru | 10 | 20,000,000.00 | 200,000,000.00 |
| **JUMLA** | **156** | | **3,120,000,000.00** |

### 6.4.5 Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

Utoaji wa elimu unahusisha Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ambayo ni Elimu Endelevu inayotekelezwa katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma. Elimu Nje ya Mfumo Rasmi inayojumuisha Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA), Mpango wa Elimu ya Sekondari kupitia Ujifunzaji huria (Open Learning) unaojumuisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa mtihani wa Maarifa (QT). Elimu ya Watu Wazima inahusisha utoaji wa stadi za Kisomo (KKK) kwa watu wazima na Kisomo cha kujiendeleza kwa kupiga vita Umasikini, Maradhi na Ujinga ili kumudu mazingira na kujiletea maendeleo kupitia Elimu ya Ufundi Stadi na shughuli za kijamii na za uzalishaji mali (shughuli za kiuchumi).

Hadi kufikia Novemba, 2022 kuna vituo **109** katika shule za msingi vinavyotekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA). Utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya sekondari katika vituo **125** vinavyoaandaa wanafunzi wa mtihani wa Maarifa **(QT)** na utekelezaji wa elimu ya ufundi stadi katika vituo vya ufundi stadi **24**.

Utekelezaji wa **elimu maalum** unafanyika katika shule zote za msingi na sekondari. Kwa sasa kuna vituo **302** katika shule zilizobainisha watoto wenye mahitaji maalum. Ubainishaji kwa ajili ya usajili wa wanafunzi wenye mahitaji maalum hufanyika kila mwaka kwa ajili ya uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa mwaka wa masomo unaofuata.

### 6.4.6 Elimu ya Ufundi Stadi

Eneo hili linajumuisha utoaji wa elimu katika vyuo vya ufundi (VETA) na vyuo vya ufundi stadi vya kati. Kwa sasa Mkoa una vyuo 3 vya Serikali vya ufundi stadi kati ya hivyo 2 vinatoa huduma ya ufundi ambavyo ni VETA Songea na VETA Namtumbo. Chuo cha VETA Nyasa ujenzi umekamilika. Aidha kuna chuo cha VTC Kiuma kilichopo Tunduru ambacho kinamilikiwa na taasisi ya dini.

### 6.4.7 Michezo

Mkoa wa Ruvuma unaendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Kwa Kuhakikisha kuwa Michezo Inaendelea kufanyika na Kushiriki Katika Mashindano Mbalimbali. Mwaka 2022 ushiriki katika mashindano ya shule za Msingi (UMITASHUMITA), na Mashindano ya UMISSETA kitaifa, Mkoa ulifanikiwa kutoa wachezaji wanne walioshiriki mashindano ya FEASSSA Jijini Arusha.walio chaguliwa kujiunga na timu ya mpira wa wavu Iliyoshiriki katika mashindano ya wanafunzi ya Afrika Mashariki ambao ni kutoka wilaya ya **Namtumbo.**

**d) Michezo kwa shule za msingi na Sekondari**

Mwaka 2022 Mkoa umeshiriki katika mashindano hayo yaliyofanyika Mkoani Tabora ambapo timu moja iliingia hatua ya robo fainali kwa UMISSETA ambayo ni timu ya mpira wa Kikapu wasichana, na kwa upande wa UMITASHUMTA timu ya Mpira wa Wavu ndiyo iliyoingia hatua ya robo fainali. Na kutolewa katika hatua ya robo na hivyo kushindwa kupata ushindi katika UMITASHUMTA Mkoa ulikuwa wa **26** kati ya **28** na katika UMISSETA Mkoa ulikuwa nafasi ya **22**. Kati ya timu **30**

**Jedwali Na. 69: Orodha ya wanafunzi Waliochaguliwa Kujiunga na timu ya mpira wa wavu 2022 Katika Mashindano ya FEASSSA**

| Na | Jina La Mchezaji | Halmashauri Anayotoka | Alikochaguliwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Proscovia Condrad Libundi | Namtumbo | Timu ya Mpira Wa Wavu |
| 2 | Bonita Daniel Exavery | Namtumbo | Timu ya Mpira Wa Wavu |
| 3 | Ratifa Seiph Amiri | Namtumbo | Timu ya Mpira Wa Wavu |
| 4 | Witness Maiko Almasi | Namtumbo | Timu ya Mpira Wa Wavu |

**e) Mashindano ya SHIMIWI**

Mashindano haya huhusisha watumishi wa serikali wa wizara na idara za serikali mwaka 2022 Mkoa wa Ruvuma ulipata umeshiriki kuptia michezo ya Karata, Darts, Bao, ushindi wa kwanza katika mchezo wa bao.

**f) Tamasha la Utamaduni la Taifa**

Mashindano haya Yalifanyika jijini dar es salamu ambapo jumla ya washiriki 13 wa fani ya Ngoma walishiriki na kushika nafasi ya sita. Lengo la mashindano haya yalikuwa ni kuenzi utamaduni wa Mtanzania. Vikundi mbalimbali toka Tanzania bara na visiwani walishiriki katika mashindano. Aidha, vijana wawili wa sanaa ya Muziki wa kizazi kipya wamepata ufadhili wa masomo katika chuo cha Sanaa Bagamoyo kwa muda wa Mwezi mmoja na kuhitimu mafunzo yao.

**Ligi zinazosimamiwa na shirikisho la mpira wa miguu Tanzania (TFF)**

Mkoa wa Ruvuma unatimu zinazoshiriki ligi hizo kama ifuatavyo:

i. Majimaji ligi daraja la pili (2)
ii. Tunduru korosho ligi daraja la pili (2)

**Hatua za kuboresha michezo**

i. Kila Halmashauri imeagizwa kuwana vitalu ambavyo vitawaandaa wanamichezo kuepuka maandalizi ya zimamoto.
ii. Shule ya sekondari ya Mahanje ya Halmashauri ya Madaba kuwa shule inayopokea wanafunzi wenye vipaji vya michezo mbalimbali kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma ili kukuza vipaji vyao. Wanafunzi hawa ni wale waliofika ngazi ya taifa na kufaulu mitihani yao ya elimu ya msingi.
iii. Kuendelea kuwashirikisha wananchi katika shughuli za kuchangia na kuendeleza Michezo katika Mkoa wetu wa Ruvuma
iv. Kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika jogging na michezo mbalimbali ya asili ya Mtanzania
v. Timu ya majimaji kuwa katika mchakato wa kuwa kampuni ili kuboresha mwenendo wake

### 6.4.8 Changamoto Katika Sekta ya Elimu

i. Wazazi kuhamia mashambani mbali na shule na kuwaacha wanafunzi peke yao hivyo kusababisha baadhi yao kuwa watoro na kuacha masomo.
ii. Baadhi ya wazazi kutokuchangia chakula cha mchana shuleni kwa ajili ya wanafunzi

iii. Upungufu wa Walimu hasa katika shule za Msingi
iv. Kutokuwa na shule za bweni zinazokidhi mahitaji
v. Upungufu wa miundombinu, samani na hosteli

### 6.4.9 Mikakati ya Kuinua Ubora wa Elimu Kuongeza Taaluma

i. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala wa elimu katika ngazi za elimu za Halamshauri na shule.
ii. Kuhimiza na kufuatilia ufanyikaji wa mtihani ya upimaji wa mara kwa mara kwenye madarasa yote.
iii. Kutoa ushauri kwa Halmashauri kufanya urekebishaji wa ikama ya walimu.
iv. Kuhimiza utoaji wa motisha kwa wanafunzi, walimu, shule na Halmashauri zinazofanya vizuri kwenye taaluma.
v. Kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa utoaji wa chakula kwa wanafunzi wawapo shuleni wakati wa mchana.
vi. Kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwemo ujenzi wa shule maalum ya Kitaifa ya wasichana inyojengwa Kijiji cha Migelegele katika wilaya ya Namtumbo.

## 6.5 UTUMISHI NA UTAWALA

### 6.5.1 Taarifa ya Hali ya Watumishi Mkoa wa Ruvuma

Mkoa wa Ruvuma mpaka kufikia Juni, 2022 una jumla ya watumishi **13,021** kati ya watumishi **21,259** wanaohitajika na Ofisi ya Mkuu wa mkoa na Halmashauri zote nane (8). Aidha, Mkoa una upungufu wa watumishi **8,238** kama mchanganuo unavyoonyesha kwenye jedwali namba 70:

**Jedwali Na. 70: idadi ya watumishi waliopo na upungufu**

| NA | JINA LA TAASISI | IDADI YA WATUMISHI HITAJIKA | IDADI YA WATUMISHI WALIOPO | UPUNGUFU | ASILIMIA YA WATUMISHI WALIOPO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 346 | 158 | 188 | 46% |
| 2 | Halmashauri ya wilaya Tunduru | 3,349 | 2,180 | 1,169 | 65% |
| 3 | Halmashauri ya wilaya Namtumbo | 3,528 | 1759 | 1769 | 50% |
| 4 | Halmashauri ya Manispaa Songea | 3,028 | 2498 | 530 | 83% |
| 5 | Halmashauri ya wilaya Songea | 2208 | 1186 | 1022 | 54% |
| 6 | Halmashauri ya wilaya Madaba | 1014 | 545 | 469 | 54% |
| 7 | Halmashauri ya mji Mbinga | 1838 | 1371 | 467 | 75% |
| 8 | Halmashauri ya wilaya Mbinga | 3800 | 1999 | 1801 | 53% |
| 9 | Halmashauri ya wilaya Nyasa | 2148 | 1325 | 823 | 62% |
| | **Jumla kuu** | **21,259** | **13,021** | **8,238** | **61.24%** |

### 6.5.2 Watumishi waliopandishwa Madaraja

Mkoa wa Ruvuma, umeidhinishiwa kupandisha madaraja jumla ya watumishi 1740 kwa ikama ya mwaka 2021/2022, kati ya hao watumishi **1,726** wameshapandishwa madaraja na kubadilishiwa mishahara. Aidha watumishi **14** hawajapandishwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukosa sifa za kimuundo.

### 6.5.3 Idadi ya watumishi waliopandishwa madaraja

**Jedwali Na. 71: Idadi ya watumishi waliopandishwa madaraja**

| NA | JINA LA TAASISI | IDADI YA WATUMISHI WALIOHIDHINISHWA KUPANDISHWA/ KUBADILISHWA VYEO | IDADI YA WATUMISHI WALIOPANDISHWA /BADILISHWA VYEO | IDADI YA WATUMISHI WALIOPANDISHWA MADARAJA NA KUBADILISHWA MISHAHARA | IDADI YA WATUMISHI AMBAO BADO HAWAJABADILISHIWA MISHAHARA |
|---|---|---|---|---|---|

| NA | JINA LA TAASISI | IDADI YA WATUMISHI WALIOHIDHINISHWA KUPANDISHWA/ KUBADILISHWA VYEO | IDADI YA WATUMISHI WALIOPANDISHWA /BADILISHWA VYEO | IDADI YA WATUMISHI WALIOPANDISHWA MADARAJA NA KUBADILISHWA MISHAHARA | IDADI YA WATUMISHI AMBAO BADO HAWAJABADILISHIWA MISHAHARA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya mkuu wa Mkoa | 11 | 11 | 11 | 0 |
| 2 | Tunduru DC | 174 | 174 | 174 | 0 |
| 3 | Namtumbo DC | 106 | 106 | 106 | 0 |
| 4 | Songea MC | 525 | 525 | 525 | 0 |
| 5 | Songea DC | 266 | 266 | 266 | 0 |
| 6 | Madaba dc | 63 | 62 | 62 | 1 |
| 7 | Mbinga TC | 131 | 128 | 128 | 3 |
| 8 | Mbinga DC | 244 | 244 | 234 | 10 |
| 9 | Nyasa DC | 220 | 220 | 220 | 0 |
| | **JUMLA** | **1740** | **1736** | **1726** | **14** |

### 6.5.4 Ajira Mpya

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kuletewa jumla ya Watumishi **787** kwa kada za elimu, afya, utawala na miundombinu kutoka Serikali Kuu, Jedwali hapo chini linaonyesha mchanganuo wa watumishi hao:

**Jedwali Na 72: Idadi ya watumishi walioajiriwa kwa mwaka 2020/21 na 2021/2022**

| Na | JINA LA TAASISI | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 4 |
| 2 | H/W Tunduru | 127 |
| 3 | H/W Namtumbo | 35 |
| 4 | Songea MC | 28 |
| 5 | Songea DC | 141 |
| 6 | Madaba dc | 13 |
| 7 | Mbinga TC | 71 |
| 8 | Mbinga DC | 276 |
| 9 | Nyasa | 92 |
| **Jumla** | | **787** |

## 7.0 TAARIFA ZA TAASISI NA MASHIRIKA

### 7.1 WAKALA WA HIFADHI YA CHAKULA KANDA YA SONGEA (NFRA)

**Taarifa ya utekelezaji wa kazi za wakala wa hifadhi ya chakula – NFRA kuanzia Julai 1, 2022 hadi 30 Novemba 2022**

**i. Ununuzi Msimu wa 2022/2023**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kupitia kanda ya Songea ilipangiwa kununua jumla ya tani 25,000 za mahindi. Kutokana na upatikanaji mdogo wa nafaka kwa msimu huu wa 2022/2023 kanda ilipewa idhini ya kununua tani 6000 kwa kuanzia. Aidha, kuanzia tarehe 21 Septemba, 2022 kanda ilipewa idhini ya kununua tani 3000 za nyongeza ili kuendelea na zoezi la kuongeza akiba ya chakula kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali.

**ii. Njia za Ununuzi Zilizopagwa**

Kutokana na ushindani katika soko kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala ulipanga kutumia njia kuu tatu za ununuzi ambazo ni:-

i) Kununua kwa njia ya vituo vya ununuzi

ii) Kununua kwa njia ya vikundi vya wakulima vya ushirika.

iii) Kununua kwa kutumia mawakala.

**iii. Mpango wa Ununuzi**

Wakala ulipanga kiwango cha ununuzi kwa Halmashauri saba zilizopo Mkoa wa Ruvuma kwa kuzingatia uwiano wa taarifa za matarajio ya uzalishaji wa ziada ya mahindi. Aidha, kutokana na upatikanaji mdogo wa nafaka kwa mwaka huu, mgawanyo huo haukufuatwa.

**iv. UNUNUZI**

Kanda ya Songea ilianza ununuzi katika maeneo yote ya Mkoa wa Ruvuma kuanzia tarehe 05/08/2022 na mpaka kufikia tarehe 30/11/2022, kanda ilikuwa imenunua tani 7,098.283 zenye thamani ya shilingi 5,168,367,960/= kutoka katika vituo vya ununuzi vya kudumu 11 na vile vya muda 5 pia ununuzi ulifanyika kupitia mawakala 6 na kuleta jumla ya vituo 22.

**V. Bei za Ununuzi**

Mahindi yalinunuliwa kwa bei kati ya shilingi 650 na 780. Mabadiliko ya bei za kununulia zilibadilika mara kwa mara kutokana na ushindani wa bei zilizokuwa sokoni. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulifanya mabadiliko ya bei ili kuongeza akiba ya Taifa ya chakula kwa lengo la kuihakikikishia Nchi inakuwa na uhakika wa chakula kukabiliana na majanga mbalimbali hasa ukame uliojitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi.

**vi. Mafanikio**

a) Hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2022, NFRA ilikuwa imefanikiwa kununua tani 7098.283 za mahindi sawa na asilimia 28.4 ya tani 25,000 zilizopangwa kununuliwa katika msimu wa 2022/2023.

b) Serikali kupitia NFRA iii nufaisha wakulima kwa kuongeza bei ya kununulia mahindi kadri wafanyabiashara walivyoongeza bei sokoni hadi kufikia kikomo cha bei ya shilingi 780 kwa kila kilo hivyo kuwasaidia wakulima kujiingizia kipato cha kununulia p na kurudi shambani.]

c) Kutengeneza ajira kwa vijana takribani 450 waliotumika kwenye zoezi la ununuzi

d) Kusaidia serikali kukusanya kodi ya zuio yenye jumla ya shilingi 103,367,359.20 ambapo hadi Novemba 30 2022 kiasi cha shilingi 69,997,898 kilikuwa kimelipwa kwa kamishina wa TRA. Aidha jumla ya shilingi 155,051,038.80 Kitalipwa kwa Halmashauri kama ushuru wa mazao (crop ces).

### vii. Changamoto

i) Ufinyu wa nafaka ya mahindi sokoni kwa msimu huu wa 2022/2023 kulikosababishwa na mahitaji ya nafaka ya mahindi kuwa kubwa sana.

ii) NFRA kutumia muda mrefu kununua tani 7098.283 tu ukilinganisha na misimu mingine hivyo, kuongeza gharama za uendeshaji

iii) Baadhi ya wakulima/ wafanyabiashara kuleta vituoni nafaka ambazo hazikizi viwango vya ubora.

### viii. Hitimisho

Mwisho, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula unaishukuru Serikali kwa ujumla kuwezesha kutekeleza jukumu la ununuzi wa mahindi kwa kutenga fedha za kutosha kununua mahindi ya wakulima kwa njia mbalimbali.

## 7.2 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) MKOA WA RUVUMA

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA MAMLAKA YA MAPATO (TRA) MKOA WA RUVUMA.

**1. UTANGULIZI:**

Kuwasilisha taarifa inayoelezea utendaji kazi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Ruvuma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na kipindi cha JULAI mpaka NOVEMBA kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**2. MAKUSANYO JULAI 2021- JUNI 2022**

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 tulikua na lengo la kukusanya **TZS 19,553,627,572.74** tuliweza kukusanya **TZS 19,850,805,877.61** sawa na asilimia **101.52%,** mchanganuo wa lengo na makusanyo kwa kila mwezi ni kama ifuatavyo: -

**Jedwali Na. 73. Lengo na Makusanyo ya Mapato 2021/2022**

| Mwezi | Mwaka | Lengo la Mwezi | Makusanyo Mwezi | Utendaji |
|---|---|---|---|---|
| JULAI | 2021 | 1,430,800,000.00 | 991,300,000.00 | **69.28%** |
| AGOSTI | 2021 | 1,459,900,000.00 | 1,846,300,000.00 | **126.47%** |
| SEPTEMBA | 2021 | 1,829,000,000.00 | 1,612,200,000.00 | **88.15%** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| OKTOBA | 2021 | 1,718,200,000.00 | 1,384,900,000.00 | **80.60%** |
| NOVEMBA | 2021 | 1,684,000,000.00 | 1,142,590,000.00 | **67.85%** |
| DISEMBA | 2021 | 2,260,500,000.00 | 2,238,320,000.00 | **99.02%** |
| JANUARI | 2022 | 1,723,300,000.00 | 1,284,940,000.00 | **74.56%** |
| FEBRUARI | 2022 | 1,644,700,000.00 | 1,383,750,000.00 | **84.13%** |
| MACHI | 2022 | 1,514,860,000.00 | 1,843,450,000.00 | **121.69%** |
| APRILI | 2022 | 1,243,400,000.00 | 1,845,720,000.00 | **148.45%** |
| MEI | 2022 | 1,267,000,000.00 | 1,643,800,000.00 | **129.74%** |
| JUNI | 2022 | 1,778,200,000.00 | 2,633,600,000.00 | **148.11%** |
| **JUMLA** | | **19,553,860,000.00** | **19,850,870,000.00** | **101.52%** |

**3. MAKUSANYO JULAI 2022- NOVEMBA 2022**

Kwa kipindi cha JULAI mpaka NOVEMBA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 tulikua na lengo la kukusanya **TSHS. 8,674,550,000/=** tumefanikiwa kukusanya **TSHS. 8,891,310,000/=** sawa na asilimia **102.5%,** mchanganuo wa lengo na makusanyo kwa kila mwezi ni kama ifuatavyo: -

**Jedwali Na. 74. Lengo na Makusanyo ya Mapato Julai 2022 – Novemba 2022**

| Mwezi | Mwaka | Lengo la Mwezi | Makusanyo Mwezi | Utendaji |
|---|---|---|---|---|
| JULAI | 2022 | 1,671,900,000.00 | 1,556,900,000.00 | **93.12%** |
| AGOSTI | 2022 | 1,652,200,000.00 | 1,616,000,000.00 | **97.81%** |
| SEPTEMBA | 2022 | 1,874,500,000.00 | 2,151,100,000.00 | **114.76%** |
| OKTOBA | 2022 | 1,765,900,000.00 | 1,966,360,000.00 | **111.35%** |
| NOVEMBA | 2022 | 1,710,050,000.00 | 1,600,950,000.00 | **93.62%** |
| **JUMLA** | | **8,674,550,000.00** | **8,891,310,000.00** | **102.50%** |

**4 MIKAKATI NA MALENGO**

i. Kuwatembelea walipakodi na kuwahimiza ulipaji wa malimbikizo ya madeni ya kodi wanazodaiwa;

ii. Kuendelea na zoezi **(KAMATA WOTE)** kwa dhumuni la kuwakamata wanunuzi wote ambao hawadai risiti kwa manunuzi mbalimbali watakayoyafanya na wauza bidhaa wote wasiotoa risiti;

iii. Kuhamasisha na kusimamia matumizi ya Stempu za kielektroniki kwa kutembelea maeneo ya mauzo ya vimiminika kuhakiki uhalali wa stempu maeneo hayo kama, Baa, Majumba ya Starehe, Maduka ya viywaji;

iv. Kutembelea maeneo mbalimbali kama, songea vijijini, songea wilayani ili kuongeza wigo wa walipakodi;

v. Kusimamia ukaguzi wa bidhaa zote zinazoingia nchini, kwa kufuata utaratibu mujibu wa sheria za forodha na ushuru, ikiwa pamoja na kuthaminisha thamani ya mizigo hiyo;

vi. Kusimamia ubadilishaji umiliki wa vyombo vyote vya moto kutoka kwa wanufaika wa misamaha kwenda kwa wasio wanufaika wa misamaha;

vii. Kufanya doria katika sehemu mbalimbali ndani ya mkoa ili kudhibiti mianya yote ya bidhaa kuingizwa kwa njia ya magendo;

viii. Kutambua idadi ya majengo na mabango kwa kushirikiana na watendaji wa mitaa kwaajili ya utekelezaji wa kukusanya kodi za pango Pamoja na ushuru wa mabango;

ix. Kuwaleta karibu washikadau wa Mamlaka ya Mapato kama TCCIA na JWT, kuwakusanya wamiliki wa biashara ili wahudhurie semina stahiki za kodi.


***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

## 7.3 OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU (NBS) MKOA WA RUVUMA - MATOKEO YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA 2022.

### MGAWANYO WA WATU


Matokeo ya awali ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yanaonyesha kuwa idadi ya watu imeongezeka kutoka 1,376,891 kwa mwaka 2012 hadi kufikia watu 1,848,794 kwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 2.9.

**Kielelezo Na. 1: Ongezeko la idadi ya watu Mkoa wa Ruvuma kwa Sensa ya watu na Makazi ya mwaka 2012 na 2022.**





Kati ya watu 1,848,794 waliohesabiwa mwaka 2022 katika Mkoa wa Ruvuma wanaume ni 902,298 sawa na asilimia 49 ya watu wote Mkoani Ruvuma na wanawake ni 946,496 sawa na asilimia 51

**Kielelezo Na.2: Idadi ya Watu kwa Jinsi Mkoani Ruvuma.**




**Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa Watu kwa Jinsi katika Asilimia**




**UWIANO WA KIJINSI**

Uwiano wa idadi ya watu kijinsi kwa Mkoa wa Ruvuma ni wanaume 95 kwa kila wanawake 100

**WASTANI WA KASI YA ONGEZEKO LA IDADI YA WATU KWA MWAKA.**

Wastani wa kasi ya ongezeko la watu katika Mkoa wa Ruvuma kwa mwaka imeongezeka kutoka asilimia 2.1 mwaka 2012 hadi asilimia 2.9 mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 4: Wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2012 na 2022.**




**IDADI YA MAJENGO**

Matokeo ya Sensa ya Majengo Mwaka 2022 yanaonesha kuwa, idadi ya majengo yote Mkoa wa Ruvuma ni 448,328 ambapo majengo 408 ni ya ghorofa, majengo 434,989 sio ya ghorofa na majengo 12,931 yapo katika hatua ya ujenzi.

**Jedwali Na 74: Idadi ya Majengo**

| ENEO | JUMLA | AINA YA JENGO | | |
|---|---|---|---|---|
| | | GHOROFA | YASIYO YA GHOROFA | YANAENDELEA NA UJENZI |
| RUVUMA | 448,328 | 408 | 434,989 | 12,931 |

**Kielelezo Na. 5: Idadi ya Majengo**




## FAIDA ZA TAKWIMU ZA IDADI YA MAJENGO

1. Kutambua majengo yaliyopo kwenye eneo na matumizi yake (Mfano biashara, Makazi, n.k)
2. Kupeleka huduma mbalimbali kama vile umeme, Maji, vituo vya polisi, n.k.
3. Kuweza kufanya Makadirio ya Kodi ambazo zinakusanywa katika eneo
4. Kujua aina ya Majengo yaliyoko kwenye eneo na hudumu zinazopatikana kama barabara, umeme, n.k.

## MAJENGO YENYE ANWANI ZA MAKAZI

Kati ya majengo 448,328 yaliyohesabiwa wakati wa Sensa ya watu na Makazi, majengo yenye anwani za makazi 370,620 sawa na asilimia 82.7 ya majengo yote Mkoani; wakati majengo 77,708 sawa na asilimia 17.3 hayana anwani za makazi.

**Kielelezo Na. 6 Majengo yenye anwani za Makazi na yasiyo na anwani za Makazi**



**Faida za Takwimu za Anwani za Makazi**

1. Kutambua majengo ambayo yana Anwani za Makazi na Kuhakisha yale ambayo hayana yanawekwa;
2. Kupunguza gharama za kupata huduma;
3. kuboresha makusanyo ya mapato;
4. Kuwezesha kufanyika kwa Biashara;
5. Kutengeneza ajira;
6. Kuimarisha ulinzi na usalama;
7. Kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kama vile Zimamoto, n.k.


## MATOKEO YA SENSA YA WATU NA MAKAZI KWA HALMASHAURI MKOANI RUVUMA

Mkoa wa Ruvuma una Halmashauri nane (8). Kutokana na matokeo ya Mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 idadi ya watu kwa Mkoa wa Ruvuma ni 1,848,794

**Jedwali Na. 75: Mlinganisho wa idadi ya watu kwa Matokeo ya Sensa ya Mwaka 2012 na 2022 kwa kila Halmashauri Mkoani Ruvuma.**


| | Mwaka 2012 | | | | | | Mwaka 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Kaya | Ukubwa wa Kaya | Uwiano Kijinsi | Wanaume | Wanawake | Jumla | Kaya | Ukubwa wa Kaya | Uwiano Kijinsi |
| Halmashauri | 668,684 | 708,207 | 1,376,891 | 300,005 | 4.6 | 94 | 902,298 | 946,496 | 1,848,794 | 466,823 | 4.0 | 95 |
| Tunduru DC | 143,660 | 154,619 | 298,279 | 69,525 | 4.3 | 93 | 201,668 | 210,386 | 412,054 | 110,208 | 3.7 | 96 |
| Songea DC | 62,645 | 63,402 | 126,047 | 28,049 | 4.5 | 99 | 89,943 | 88,258 | 178,201 | 45,198 | 3.9 | 102 |
| Mbinga DC | 115,589 | 120,380 | 235,969 | 49,982 | 4.7 | 96 | 141,271 | 144,311 | 285,582 | 69,775 | 4.1 | 98 |
| Songea MC | 96,347 | 106,962 | 203,309 | 47,092 | 4.3 | 90 | 134,920 | 151,365 | 286,285 | 76,927 | 3.7 | 89 |
| Namtumbo DC | 98,335 | 103,304 | 201,639 | 39,206 | 5.1 | 95 | 132,035 | 139,333 | 271,368 | 63,274 | 4.3 | 95 |
| Nyasa DC | 71,392 | 74,768 | 146,160 | 30,808 | 4.7 | 95 | 93,494 | 97,699 | 191,193 | 44,737 | 4.3 | 96 |
| Madaba DC | 23,903 | 23,871 | 47,774 | 10,466 | 4.6 | 100 | 33,085 | 32,130 | 65,215 | 16,725 | 3.9 | 103 |
| Mbinga TC | 56,813 | 60,901 | 117,714 | 24,877 | 4.7 | 93 | 75,882 | 83,014 | 158,896 | 39,979 | 4.0 | 91 |

**Kielelezo Na. 7: Idadi ya Watu kwa Halmashauri kwa Mwaka 2012 na 2022**





Kutokana na Matokeo ya Mwanzo ya Sensa ya watu na Makazi kwa Mkoa wa Ruvuma, Halmashauri ya wilaya ya Tunduru ina idadi kubwa ya watu wapatao 412,054 ukilinganisha na Halmashauri nyingine za Mkoa wa Ruvuma. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha idadi ya watu kwa kila Halmashauri.

**Kielelezo Na. 8: Idadi ya Watu kwa Halmashauri (Sensa ya Mwaka 2022)**




**Kielelezo Na. 9: Idadi ya Kaya kwa Halmashauri (Sensa ya Mwaka 2022)**




**FAIDA ZA TAKWIMU ZA IDADI YA WATU NA KAYA KATIKA HALMASHAURI NA KATA**

i). Kupanga bajeti kwa idadi ya Watu, Kupanga mipango ya Muda mrefu kulingana na mahitaji ya watu;

ii). Kujua ni maeneo gani yanahitaji huduma mbalimbali kutokana na wingi wa watu kama vile Shule, Hospitali, Masoko, Maji, mawasiliano, biashara, Miundombinu

iii). Kugawana Rasilimali kwa idadi ya Watu na Kaya na Kugawa Majimbo ya Uchaguzi kulingana na idadi ya watu

iv). Idadi ya Watu na Umri wao inasaidia kujua kukadiria kiasi cha huduma inayohitajika mfano - Idadi ya watoto wanaostahili kupata chanjo, idadi ya vyandarua, n.k.

## 7.4 SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SHIRIKA LA UMEME (TANESCO)

### 7.4.1 TAARIFA YA MKOA

Mkoa wa Ruvuma una wilaya tano (5) ambazo makao makuu ya Wilaya zote tayari yamepatiwa umeme, wilaya hizo ni Songea, Namtumbo, Tunduru, Mbinga na Nyasa. Mkoa wa Ruvuma unapata umeme wa gridi kupitia vituo vikubwa vya kupoza umeme vilivyopo Madaba na Songea.

**Usambazaji**

Mkoa wa Ruvuma una mtandao mkubwa wa usambazaji wa umeme wenye mashine umba (Transformers) **762** na urefu wa jumla ya kilomita **2,463.18** kwa msongo wa kilovoti 33, kilomita **154.12** kwa msongo wa kilovoti 11 na kilomita **2,230.98** kwa msongo wa kilovoti 0.4/ 0.23 (LT). Pia Mkoa una jumla ya wateja **96,383** mpaka kufikia tarehe 30/11/2022 kwa mchanganuo ufuatao; wateja wa mtumizi ya kundi la chini (D1) ni **27,869** wateja wa matumizi ya kawaida (Tarifu 1) ni **68,485** na wateja wakubwa maumizi ya kati (Tarifu 2) ni **20** na kundi la mwisho ni la wateja wakubwa wa matumizi ya juu (Tarifu 3) ni **9.**

- **Makusanyo**

Mkoa una wastani wa makusanyo ya **Tsh.1.5 Bill** kutoka kwenye umeme uliouzwa kwa mwezi kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23.

- **Madeni**

Mpaka sasa Mkoa una deni linalofikia Shs **454,633,793.13** linalojumuisha tasisi za serikali na watu binafsi mchanganuo wa deni la Mkoa ni kama inavofafanuliwa kwenye vielelezo hapa chini: -

**Jedwali Na. 76: Madeni ya Taasisi za Serikali**

| **Na** | **Jina la Tasisi** | **Tarifu ya matumizi** | **Deni** |
|---|---|---|---|
| 1 | TPDF | T2 | **192,757,180.13** |
| 2 | MAMLAKA YA MAJI(SOUWASA) | T2 | **101,780,902.74** |
| | **Jumla la Deni** | | **294,538,082.87** |

**Jedwali Na. 77: Madeni ya Tasisi binafsi**

| | **Jina la Mdaiwa** | **Tarifu ya matumizi** | **Deni** |
|---|---|---|---|
| 1 | Mr Ramadhani. N. Kayombo | T2 | **98,668,665.97** |
| 2 | M/s Andoya Minhydro Electrical | T3 | **61,427,044.29** |
| | Ju**mla la Deni** | | **160,095,710.26** |

- **Wafanyakazi**

Mkoa una jumla ya wafanyakazi wa kudumu **134 (**93 mafundi na 41 wasio mafundi**)** na wale wa mkataba wa mwaka mmoja ni **35 (**19 mafundi na wasio

mafundi 16**)** mpaka kufikia mwezi Novemba 2022 kwa mchanganuo ufuatao:
-

**Jedwali Na. 78. Mchanganuo wa wafanyakazi kwa jinsia**

| **Wilaya** | **Waliopo** | | **Wanaohitajika (Idadi)** |
|---|---|---|---|
| | **Jinsia** | **Idadi** | |
| Songea | ME | 67 | 38 |
| | KE | 16 | |
| Tunduru | ME | 19 | 13 |
| | KE | 5 | |
| Namtumbo | ME | 12 | 12 |
| | KE | 4 | |
| Mbinga | ME | 18 | 13 |
| | KE | 5 | |
| Nyasa | ME | 17 | 15 |
| | KE | 6 | |
| **Jumla** | ME | 154 | **101** |
| | **KE** | **169** | |

### 7.4.2 HALI YA UPATIKANAJI WA UMEME

Hali ya upatikanaji wa umeme kwa mkoa wa Ruvuma kwa sasa ni nzuri na ya kuridhisha baada ya kuunganishwa na Gridi ya Taifa tarehe **15/09/2018** katika wilaya nne (4) za Songea, Namtumbo, Mbinga na Nyasa kupitia ujenzi wa laini ya msongo wa Kilo volti 220 kutoka Makambako na vituo viwili vikubwa vya kupoza na kusambaza umeme vya Songea na Madaba.

Wakati huohuo wilaya ya Tunduru iliunganishwa na gridi ya Taifa tarehe **22/12/2019** na kuzima mitambo ya mafuta. Pia mkoa unapata umeme kutoka kwa mwekezaji binafsi wa kampuni ya **TULILA** ambao wana uwezo wa kufua Megawati **5.** na kuingiza kwenye Gridi ya Taifa.

**Jedwali Na. 79: Njia kuu za umeme**

| Na | Jina la njia | Uwezo (voltage) | Jumla ya nguzo | Umbali (km) | Aina |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Makambako-Songea | 220kV | 711 | 245 | Nguzo za chuma |

**Jedwali Na 80: Vituo vya kupoza umeme**

| Na | Maelezo | Madaba | Songea | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uwezo wa kituo(MVA) | 30 | 60 | 90 |
| 2 | Uwezo wa kituo (MW) | 24 | 48 | 72 |
| 3 | Idadi-ya transfoma( vituo vya gridi) | 1 | 2 | 3 |
| 4 | Matumizi ya juu yaliyofikiwa | 1.7 | 17 | |
| 5 | Laini za usambazaji 33kV | 3 | 4 | |
| 6 | Reactor zilizofungwa 220KV, 15MVar | 1 | 0 | |
| 7 | Reactor zilizofungwa 33KV, 5MVar | 2 | 2 | |

- **Kituo cha madaba**

Kituo cha kupoza, kusambaza na kusafirisha umeme cha Madaba kiliwashwa rasmi tarehe 08 Septemba 2018.

Kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Madaba kinapokea umeme kutoka Makambako wenye msongo wa kilo volt 220 ambapo kiliwashwa rasmi tarehe 08 Septemba 2018 kikiwa na transfoma zenye uwezo wa 30MVA. Kituo kina reactor mbili za 5MVar na Auxiliary transformer moja ya 250kW. Pia kituo hiki kinatoa huduma mkoa wa Njome wilaya yote ya Ludewa kupitia njia ya umeme ya Ludewa kwa msongo wa kilovoti 33 na sehemu ya wilaya ya njome kupitia njia ya umeme ya njombe msongo wa kilovoti 33.

Kiwango cha matumizi cha juu kilichofikiwa katika njia za umeme tokea wakati wa kuwashwa mpaka sasa ni kama yanavyojionesha kwenye Jedwali namba 81 hapo chini: -

**Jedwali Na. 81: Kiwango cha matumizi cha juu kilichofikiwa katika njia za umeme Kituo cha Madaba**

| Na | Jina la laini ya Umeme | Tarehe ya kuwasha | Matumizi (MW) wakati wa kuwasha | Matumizi ya juu (MW) iliyofikiwa wakati wa sasa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Njombe | 03-04-19 | 0.274 | 1.1 |
| 2 | Ludewa | 12-09-18 | 0.12 | 1.2 |
| 3 | Songea | 19-11-18 | 0.032 | 0.09 |
| 4 | Laini ya ziada-2 | | | |

Reactor ya 220kv, 15MVAR iliweza kuwashwa tarehe 22/09/2019 na kuondoa tatizo la njia kuu ya msongo wa 220kv kutoka kwa “Over voltage”.

- **Kituo cha songea**

Kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Songea kinapokea umeme kutoka Madaba wenye msongo wa kilo volt 220 ambapo kiliwashwa rasmi tarehe 15 Septemba 2018 kikiwa na uwezo wa 60MVA ambayo ni sawa 48MW. Kituo kina transformer mbili za 30MVA kila moja, reactor mbili za 5MVar na Auxiliary transformer moja ya 250kW.

Kiwango cha matumizi cha juu kilichofikiwa katika njia za umeme tokea wakati wa kuwashwa mpaka sasa ni kama yanavyojionesha kwenye Jedwali namba 82 hapo chini: -

**Jedwali Na. 82: Kiwango cha matumizi cha juu kilichofikiwa katika njia za umeme Kituo cha Songea**

| Na | Laini ya Umeme | Tarehe ya kuwasha | Matumizi (MW) wakati wa kuwasha | Matumizi (MW) ya juu iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea Interconnector | 15-09-18 | 4.83 | 9.27 |
| 2 | Mbinga | 15-09-18 | 2.21 | 8.23 |
| 3 | Madaba | 15-09-18 | 0.006 | 0.47 |

| Na | Laini ya Umeme | Tarehe ya kuwasha | Matumizi (MW) wakati wa kuwasha | Matumizi (MW) ya juu iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Namtumbo | 15-09-18 | 0.39 | 7.53 |
| 5 | Spare feeder -2 | | | |

Mkoa wa Ruvuma una mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya dizeli ambayo imezimwa baada ya kuunganishwa na Gridi ya Taifa, uwezo wa vituo vilivyozimwa ni kama inavyofafanuliwa kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 83: Vituo vya kufua umeme vilivyozimwa Mkoa wa Ruvuma**

| Na. | Wilaya | Kituo | Ufuaji (MW) |
|---|---|---|---|
| 1 | Songea | Songea PP (3 M/C) | 4.8 |
| 2 | Mbinga | Mbinga PP (1 M/C) | 1 |
| 3 | Tunduru | Tunduru PP (3 M/C) | 1.75 |
| | | | |
| | **JUMLA** | | **7.55** |

Pamoja na hayo mkoa wa Ruvuma una jumla ya vijiji **vipatavyo 554, kati ya hivyo 320 vina umeme** sawa na **58%** ya vijiji vyote **na vijiji 234 vinaendelewa kuwekewa umeme kupitia REA III mzunguko wa pili** kama jedwali namba 84 linavyojieleza hapo chini: -

**Jedwali Na. 84: Idadi ya Vijiji vilivyo kwenye mpango wa mradi**

| Wilaya | Idadi ya vijiji kwa wilaya | Majimbo | Idadi ya vijiji kwa jimbo | Vijiji vyenye umeme | Vijiji visivyo na umeme | Vijiji vilivyo kwenye R3R2 | % ya vijiji vyenye umeme | % ya vijiji visivyo na umeme |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Madaba** | 22 | Madaba | 22 | 21 | 1 | 1 | 95.45% | 4.55% |
| **Mbinga** | 169 | Mbinga Mjini | 49 | 26 | 23 | 23 | 53.06% | 46.94% |
| | | Mbinga Vijijini | 120 | 56 | 64 | 64 | 43.33% | 56.67% |
| **Namtumbo** | 66 | Namtumbo | 66 | 54 | 12 | 12 | 81.82% | 18.18% |
| **Nyasa** | 84 | Nyasa | 84 | 50 | 34 | 34 | 59.52% | 40.48% |
| **Songea DC** | 56 | Peramiho | 56 | 32 | 24 | 24 | 57.14% | 42.86% |
| **Tunduru** | 157 | Tunduru Kaskazini | 92 | 67 | 25 | 25 | 72.83% | 27.17% |
| | | Tunduru Kusini | 65 | 14 | 51 | 51 | 21.54% | 78.46% |
| | **554** | | **554** | **320** | **234** | **234** | **60.59%** | **39.41%** |

### 7.4.3 MIRADI MIKUBWA (MAJOR PROJECTS)

Mkoa wa Ruvuma kwa sasa hauna Mradi mkubwa unaotekelezwa kwenye mwaka wa fedha 2021/22, hata hivyo, Mkoa wa Ruvuma ni mojawapo ya Mikoa iliyofaidika na **Miradi ya Gridi Imara** inayotazamiwa kutekelezwa kuanzia **mwaka wa fedha 2022/23**.

Mradi huu unategemewa kujenga laini ya msongo wa 220kV kutoka Songea hadi Tunduru umbali wa **Kilomita 265** na kujenga kituo cha kupozea umeme **katika mji wa Tunduru chenye ukubwa wa 180MVA**.Mradi unatazamia kujenga njia mpya kumi (10) za msongo wa kati zitakazosambaza umeme kwenye Wilaya ya Namtumbo, Tunduru, Nanyumbu na Masasi. Mradi wa Gridi imara upo kwenye hatua za awali za utekelezaji.

### 7.4.4 MIRADI INAYOFADHILIWA NA TANESCO

#### 7.4.4.1 Miradi ya kusongea miundombinu (New extension projects)

Mkoa wa Ruvuma umetekeleza miradi ya kusambaza umeme maeneo mbalimbali ambayo bado yalikuwa hayajafikiwa na huduma hiyo. Kwa mwaka huu wa fedha wa **2021/22** jumla ya shilingi **TZS 2,071,809,025.20 zilitengwa** kwa kazi hiyo ili kufikisha umeme **maeneo 92** Mkoani na Wilayani.

Kwa mwaka wa fedha wa **2020/21**, mkoa ulifanikiwa kujenga laini za msongo wa kati (33&11kV) zenye jumla ya kilomita **52** laini za msongo wa 0.4kV zenye jumla ya kilomita **83** na transfoma **31** zilifungwa

Miradi hii imefanikiwa kufikia maeneo **92** ambayo hayakuwa na huduma ya umeme mwanzoni. Utekelezaji wa miradi hii umewezesha kuunganisha wateja zaidi ya **1800**

#### 7.4.4.2 Miradi ya kuimarisha umeme (Voltage improvements projects)

Katika mwaka wa fedha 2021/22 jumla ya **miradi 54** ya kuondoa tatzo la umeme hafifu imetekelezwa katika **maeneo 47** katika mkoa wa Ruvuma.Miradi hii imetekelezwa kwa gharama ya Shs **1,169,510,335.00.**

Utekelezaji wa miradi hii umefanikiwa kuwanufaisha wananchi zaidi ya 500 na viwanda vidigo (mashine za kusaga na kukoboa) 4 hivyo kuongeza tija zaidi katika uzalishaji na matumizi ya umeme.

#### 7.4.4.3 Miradi ya Matengenezo (Repair and Maintenance)

Miradi ya ukarabati wa miundombinu chakavu imetekelezwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma.Miradi hii ilihusisha kazi za kubadilisha nguzo takribani 950 kukata miti inayokaribia laini kwa umbali wa kilomita 1200 na. kufanya matengenezo ya vituo vidogo vya kupoozea umeme (sabstations) 150. Gharama iliyotumika katika kufanikisha marekeisho haya ni TShs **1,221,830,998.87**

Maboresho haya yaliyofanyika yamesaidia kupunguza kukatika kwa umeme kutoka mara 11 hadi mara 4 kwa mwezi kwa laini za Mbinga, Namtumbo na Madaba, na kutoka mara 9 Hadi mara 2 kwa laini za Ludewa, Songea na Njombe.

Kwa ujumla maboresho haya yameboresha hali ya upatikanaji umeme na kupunguza kadhia ya kukatia umeme kwa kiwango kibubwa na kuchangamsha shughuli za uzalishaji mali.

#### 7.4.4.4 Kuunganisha wateja

Kwa mwaka wa fedha wa **2022/2023** mpaka novemba mkoa ulifanikiwa kuwaunganishia umeme wateja **9,489** sawa na asilimia **96.4%** ya lengo la Mkoa la kuunganisha wateja wapatao **9,845.** Kwa kiasi kikibwa upatikanaji wa meme wa uhakika umechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la wateja.

### 7.4.5. MIRADI YA UMEME VIJIJINI INAYOFADHILIWA NA WAKALA WA UMEME

**A: Mradi wa umeme unaofadhiliwa na wakala wa umeme vijijini (REA) awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza**

- **Lengo la Mradi**

Lengo la mradi ni kuunganisha umeme katika vijji **177** katika wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma (baada ya kuongezewa vijiji 39).

- **Gharama halisi za mradi**

Gharama za mradi ni Fedha za kitanzania **(TZS) 43,869,003,071.89 (VAT Inclusive)** na Fedha za Kimarekani **(USD) 7,483,076.98 (VAT Inclusive)** Jedwali namba 85 hapo chini linaonesha mchanganuo wa wigo na kazi iliyofanyika

**Jedwali Na. 85: Mchanganuo wa wigo na kazi iliyofanyika**

| Wilaya | Songea | Mbinga | Tunduru | Nyasa | Namtumbo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wigo wa Laini ya Msongo wa kati (MV Line) (KM) | 192.91 | 211.1 | 81.1 | 329.52 | 274 | 1088.63 |
| Wigo wa Msongo wa kati zilizojengwa (KM) | 192.91 | 211.1 | 81.67 | 328.06 | 273.99 | 1087.73 |
| Utekelezaji katika % | 100.00% | 100.00% | 100.70% | 99.56% | 100.00% | 99.92% |
| Idaid yaTrasfoma katika Wigo | 51 | 72 | 35 | 40 | 39 | 237 |
| Idadi ya transfoma zilizofungwa | 50 | 69 | 34 | 40 | 39 | 232 |
| Utekelezaji katika % | 98.04% | 95.83% | 97.14% | 100.00% | 100.00% | 97.89% |
| Wigo wa laini ya msongo wa 0.4kV (KM) | 100 | 147 | 77.5 | 74.9 | 71.6 | 471 |
| Laini ya msongo 0.4kV zilizojengwa(KM) | 100 | 147 | 77.5 | 74.9 | 71.6 | 471 |
| Utekelezaji katika % | 100.00% | 100.00% | 100.00% | 100.00% | 100.00% | 100.00% |
| Idadi ya Vijiji katika wigo | 33 | 505 | 25 | 36 | 28 | 177 |
| Vijiji vilivyowasha | 33 | 55 | 25 | 36 | 28 | 177 |
| Utekelezaji katika % | 100% | 100% | 100% | 100% | 100% | 100% |
| Idadi ya wateja katika wigo wa kazi | 3248 | 2204 | 1534 | 1277 | 1515 | 9778 |
| Idadi ya wateja waliounganishwa | 2644 | 1537 | 1360 | 1060 | 1212 | 7813 |
| Utekelezaji katika % | 81.40% | 69.74% | 88.66% | 83.01% | 80.00% | 79.90% |

Mradi umekamilika tangu juni 2022, na sasa mkandarasi anendelea na kazi ya kuwaunganishia wateja umeme pamoja na kumalizia kazi ndogondogo katika kipindi hiki cha matazamio.

**B: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA USAMBAZAJI UMEME MAENEO YA VIJIJINI (REA) MKOA WA RUVUMA KUFIKIA TAREHE 04/07/2022**

Mradi huu unatekelezwa na Wakandarasi wawili ambao ni JV Guangdong Jianneng Electric Power Engineering Co. LTD and White City International Contractors LTD (ambaye atatekeleza mradi katika Wilaya za Tunduru na Namtumbo Kwa gharama ya Shilingi Bilioni 31.60 Pamoja na Mkandarasi Namis Corporate LTD ambaye atetekeleza mradi katika Wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa Kwa gharama ya Shilingi Bilioni 41.67. Mradi utajenga mkondo wa kati wa umeme (MV Line) wa 1,542.3km, mkondo mdogo wa usambazaji wa umeme (LV lines) 260.6km ukiwa na mashine umba 261 zenye ukubwa wa 50kVA na kufanikisha kuunga wateja 5,658. Taarifa za kina zinafafanuliwa na jedwali namba 86 hapa chini: -

**Jedwali Na. 86: Taarifa za Miradi**

| Na | Maelezo | LOT 25 | LOT 26 |
|---|---|---|---|
| 1 | Namba ya Mkataba | AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 25 | AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 26 |
| 2 | Eneo la utelelezaji Wilaya | Songea,Mbinga na Nyasa | Tunduru na Namtumbo |
| 3 | Jina la Mkandarasi | **M/s Namis Corporate Ltd** | **M/s Whitecity Guangdong JV** |
| 4 | Gharama za Mradi zinazojumisha kodi ya Ongezeko la thamani | 35,281,367,752.46 | 36,678,446,302.59 |
| 5 | Muda wa kutekeleza Mkataba miezi | 18 | 18 |
| 6 | Muda wa Kuanza Mkataba | 28/08/2021 | 15/07/2021 |
| 7 | Muda wa kumaliza Mkataba | 7/3/2023 | 14/01/2023 |
| 8 | Idadi ya Vijiji Nufaika | 168 | 99 |

Utelezaji wa mradi wa kupeleka umeme awamu ya tatu mzunguko wa pili nia kama ifuatavyo: -

a) Kwa Lot 25 kupitia mkataba-**AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 25** unaotekelezwa na Mkandarasi **M/s Namis Corporate Ltd**, katika Wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa mpaka sasa vijiji 25 kati ya 168 vimeshawashwa na mradi **umeshafikia asilimia 20%** mkandarasi bado yupo eneo la mradi na ufuatiliaji wa karibu unaendelea na mkandarasi ameongeza kasi ya kuleta vifaa vya ujenzi.
b) Kwa Lot 26 kupitia mkataba namba **AE/008/2020-21/HQ/W/31 LOT 26** unaotekelezwa na Mkandarasi **M/s Whitecity Guangdong JV** katika Wilaya za Tunduru na Namtumbo mpaka sasa vijiji 13 Vimeshwashwa kati ya vijiji 99. **Utekelezaji wa mradi umeshafikia 32.34 %** na mkandarasi bado yupo eneo la mradi na amefanikiwa kusimamisha nguzo katika vijiji 48 kati ya 98. Mkandarasi pia ameongeza kasi ya kuleta vifaa vya utekelezaji wa mradi.

Hata hivyo utekelezaji wa mardi uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa gharama za vifaa lakini majadiliano kati yake na REA yamekamilika na sasa wanaendelea na utekelezaji. Mradi utakapokamilika utakuwa umewezesha kufikia vijiji vyote vya mkoa wa Ruvuma.

**C: MIRADI MINGINE YA UMEME VIJIJINI ITAKAYO TEKELEZWA KARIBUNI**

Serikali kupitia Wakala wa Nishati vijijini, umepanga kutekeleza miradi mbalimbali ya kuhamasisha matumizi ya nishati bora vijijini kuanzia mwaka wa fedha 2022/23. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**i. Mradi wa ujazilizi 2C (Densification 2C)**

Wakala umepanga kutekeleza mradi wa Ujazilizi 2C katika Mkoa wa Ruvuma. Lengo la mradi huu nikuongeza wigo wa miundombinu ya umeme kwenye maeneo na vitongoji ambavyo havijafikiwa na miundombinu hiyo. Mradi huu utahusisha ujenzi wa 664km za mkondo mdogo wa umeme, transifoma 241 na kuunganisha wateja wa awali 13,744. Gharama za mradi huu zinatarajia kufika

**shilingi Bilioni 26.64**. Mchanganuo wa idadi ya vitongoji kwa kila Wilaya ni kama ifuatavyo;

**Jedwali Na. 87: Idadi ya Vitongoji vitafikishiwa miundombinu ya umeme kwa ujazilizi**

| Na | WILAYA | IDADI YA VITONGOJI |
|---|---|---|
| **1.** | Songea DC | **50** |
| 2. | Mbinga | 42 |
| 3. | Nyasa | 19 |
| 4. | Namtumbo | 46 |
| 5. | Tunduru | 89 |
| **JUMLA** | | **272** |

Mradi upo katika hatua za mwisho za manunuzi na utekelezaji utaanza ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/23.

### 7.4.6 UTOAJI WA HUDUMA (SERVICE DELIVERY)

- **Nikonekt**

Kwa Mkoa wa Ruvuma unatekeleza mfumo mpya wa kuhudumia wateja kwa njia mbalimbali za kidigitali kama, kutumia njia ya mtandao wa kijamii (Nikonekt App), njia ya tovuti, na kiswaswadu (USSD). Mfumo ulizinduliwa tarehe **13/06/2022** katika kanda ya kusini na umepokelewa kwa kishindo katika Mkoa wa Ruvuma na hadi kufikia novemba 30,2022, Mkoa ulikuwa umefanikiwa kuwanganisha **wateja 10,127**. Mfumo huu umeboresha kwa kiasi kikubwa ungnaishaji umeme kwa wateja kwa haraka na kurahisisha mchakato wa uunganishaji wateja nakuongezenga uwajibikiaji kwa wafanyakazi.

- **Huduma ya Kituo cha miito ya simu cha pamoja (Unified call centre)**

Mkoa pia umeunganishwa na kituo cha miito cha pamoja, wateja wameweza kuhudumiwa kwa wakati na kutatuliwa changamoto zao pamoja na kupatiwa

majibu na majawabu ya maswali yao. Pamoja na hayo, pia wateja wamefurahia huduma hii kwa sababu wanapiga simu bure bila kutozwa gharama yoyote.

- **Mfumo wa huduma kwa wateja (Customer Relation Management System – CRM)**

Mkoa wa Ruvuma katika kusogeza huduma za shirika karibu na Wananchi umeanzisha vituo vidogo vya huduma (viunga) karibu na wananchi. Viunga hivi vimewezesha kuwafikia wanchi kwa karibu na kutatuta matatizo yanayojitokeza kwenye mifumo ya usambazaji kwa haraka. Mkoa wa Ruvuma una jumla ya viunga 18, katika mgawanyo ufuatao: -

a) Wilaya ya Songea –Kuna viunga vitano (6) katika maeneo yafuatayo, Peramiho, Mkuzo, Mshangano, Magagula, Matomondo na Wino
b) Wilaya ya Namtumbo-kuna viunga vitatu (3) katika maeneo ya Hanga, Lusewa na Mkongo gulioni.
c) Wilaya ya Tunduru –Kuna viunga vitatu (3) katika maeneo ya Nandembo, Mkowela na Milonde.
d) Wilaya ya Mbinga-Kuna viunga vitatu (3) katika maeneo ya Luanda, Litembo na Matiri
e) Wilaya ya Nyasa-Kuna viunga vitatu (3) katika maneo ya Lituhi, Pingi na Kingerikiti.

Unazishwaji wa mfumo wa mahusiano kwa wateja (Customer Relation Management System –CRM) katika Mkoa wa Ruvuma unaofanya sambamba na viunga umeongeza tija zaidi ya kuwahudumia wateja ndani ya muda mfupi na kuongeza uwajibikaji wa watumishi katika kutatua matatizo ya mifumo ndani ya muda mfupi. Mfumo umepokelewa chanya na wafanyakazi kwani wanapokea taarifa moja kwa moja kwenye simu zao za kiganjani na kuwahudumia wateja kwa wakati.

### 7.4.7 BAJETI TULIYOPEWA KWA MWAKA FEDHA 2022/23

Kwa mwaka wa fedha huu 2022/23, Mkoa umetengewa fedha kwa ajili ya kutekekela miradi na kuboresha miundombinu pamoja na kuwaunganishia wateja kama ifutavyo; -

- Mkoa umetengewa Sh 276,049,940 kumalizia miradi ambayo haikukamilika katika mwaka wa fedha 2021/22.

- Mkoa umetengewa juma ya Shiling 2,074,119,468 kutekeleza miradi mipya 43 ya kusogeza huduma kwa wananchi.

- Miradi 22 ya matengenezo ya miundo mbinu imetengewa jumla Sh 2,240,776,359 ili kuboresha hali ya upatikanaji umeme katika Mkoa wa Ruvuma.

- Miradi ya 24 kuboresha upatikanaji wa umeme na kuimarisha nguvu ya umeme (Voltage improvements) imetengewa Shilingi **1,886,924,672.**

- Mkoa umetengewa jumla ya Shillingi **3,159,039,340 maalum** kwa ajili ya kuwaunganishia wateja wote wapya wanaohitaji kuunganishiwa huduma ya umeme**.**

### 7.4.8 MIPANGO YA UTENDAJI KAZI KWA MWAKA FEDHA 2022/23

Mkoa umejipanga kuhakikisha unatekeleza miradi yote iliyo kwenye mwaka huu wa fedha 2022/23 lengo kuu ikiwa ni: -

- Kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la kukatika umeme mara kwa mara ili kuongeza mapato na karaha kwa wananchi wanayopata kwa kukatika kwa umeme.
- Kuondoa kabisa au kupunguza hitilafu zinazojitokeza kwenye mifumo ya laini ndogo za msongo 0.4kV, zinasosambaza umeme kwa wananchi kwa kuboresha maungio yote ya nyaya.
- Kuboresha mifumo ya usambazaji umeme ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la umeme hafifu linaathiri wananchi.
- Kusogeza huduma ya umeme maeneo ambayo yamejitokeza ambayo hayakuwa na umeme.
- Kuwaunganishia umeme wananchi kwa haraka kupitia mifumo mipya ya utendaji (Nikonekt).
- Kutatua matatizo yanayoripotiwa kwenye mfumo wa pamoja wa Miito (unified call center) kwa haraka kupitiwa mifumo ya uboreshaji uwajibikaji iliyoanzishwa (CRM-Customer Relation management).

### 7.4.9 MAFANIKIO

Mkoa wa Ruvuma baada ya kuunganishwa na grid umepata mafanikio mengi ikiwemo yafuatayo:

- Mwitikio mkubwa wa wananchi kulipia huduma ya umeme ili waunganishwe na huduma hii muhimu

- Ongezeko kubwa la wateja baada ya kuwa na umeme wa uhakika na kuridhisha
- Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya umeme, kutoka wastani wa bilioni moja (1) mwaka 2018 hadi billioni 1.5 mwaka 2022.
- Kuokoa gharama za uendeshaji baada ya kuzima vituo vine (4) vya kuzalisha umeme kutumia mafuta baada ya Mkoa kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa.

### 7.4.10 CHANGAMOTO

Mkoa wa Ruvuma unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Madeni sugu ya Taasisi za serikali na watu binafsi ambapo **67%** ya deni lote linatokana na akaunti za jeshi (TPDF).

ii. Uchomaji wa mashamba ambao unaathiri miundombinu ya shirika.

iii. Matukio ya wizi wa waya za kwenye transfoma na vyuma vya kushikilia nguzo isianguke (base plate)

iv. Upungufu wa wafanyakazi katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kwa ujumla uliosababishwa na baadhi yao kuhamishwa au kustaafu

### JINSI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

i. Kwa kukabiliana na madeni sugu ya Taasisi, tunaendelea na ufungaji wa mita za LUKU ili kuzuia ukuaji wa deni na kurahisisha ukusanyaji wake. Mpaka sasa Polisi, Magereza, FFU na Hospitali zimefungiwa mita za LUKU, Pia sehemu kubwa ya vikosi viwili vya jeshi kati ya vikosi vitano tayari tumefunga mita za LUKU na tunaendelea na vikosi vilivyobaki.
ii. Tumeendelea na zoezi la kupalilia visahani kwa kutumia wanavijiji na kuendelea kutoa elimu pamoja na mwaka huu tutaanza kutumia nguzo za zege kwa Mkoa wa Ruvuma
iii. Tunaendelea kushirikiana na jeshi la Polisi pamoja na viongozi wa serikali ili kuwabaini wanaofanya uharibifu huo na kuchukuahatua za kisheria.
iv. Juu ya upungufu wa wafanyakazi tumeshapeleka mahitaji makao makuu kitengo cha rasilimali watu pia tumeendelea kutumia wafungwa na wanakijiji kwa kazi ambazo sio za kiufundi.

### 7.4.11 HITIMISHO

**Mwisho,** napenda kushukuru kwa dhati Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kipaumbele katika kutekeleza miradi mikubwa ya Umeme itakayochochea ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

## 7.5 WAKALA MAJI MIJINI NA VIJIJINI (RUWASA)

**TAARIFA YA HALI YA UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI MKOA WA RUVUMA HADI KUFIKIA NOVEMBA, 2022 - RUWASA**

### 7.5.1 UTANGULIZI

Kulingana na Sensa ya mwaka 2022, Mkoa wa Ruvuma una jumla ya watu 1,848,794. Hadi kufikia Novemba, 2022 jumla ya watu 1,257,180 walikuwa wanapata huduma ya maji safi na salama ikiwa ni asilimia 70 ya wakazi wote wa Mkoa**.**

Vyanzo vya maji vinavyopatikana katika Mkoa wa Ruvuma ni mito, chemchemi, na visima virefu na vifupi. Lengo la Mkoa ni kufikia asilimia 85 kwa wakazi waishio vijijini na 95 kwa wakazi washio Mjini ifikapo mwaka 2025.

### 7.5.2 HALI YA HUDUMA YA MAJI

i. **Huduma ya Maji Mijini.**

Mkoa wa Ruvuma unayo miji sita ambayo ni makao makuu ya Halmashauri ambazo ni Songea, Mbinga, Tunduru, Namtumbo na Mbambabay. Hadi kufikia Oktoba, 2022 huduma ya maji safi na salama katika Makao Makuu ya Miji na Halmashauri ilikuwa ni asilimia 72.7. Jedwali Na. 88 linaonyesha hali halisi ya upatikanaji wa huduma ya Maji Mjini hadi kufikia Novemba,2022.

**Jedwali Na.88: Hali ya upatikanaji wa maji mijini kufikia Novemba, 2022**

| NA | MJI | IDADI YA WATU | | ASILIMIA YA WANAOPATA |
|---|---|---|---|---|
| | | WALIOPO | WANAOPATA MAJI | |

| | | | | MAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea MC | 230,684 | 206,000 | 89.3 |
| 2 | Mbinga | 52,381 | 26,295 | 50.2 |
| 3 | Namtumbo | 47,988 | 13,220 | 27.5 |
| 4 | Tunduru | 48,784 | 35,500 | 72.8 |
| 5 | Mbambabay | 12,847 | 10,068 | 78.4 |
| | **Jumla /Wastani** | **392,684** | **291,083** | **72.7** |

***Chanzo:*** *Mamlaka za Maji Mijini mkoa wa Ruvuma*

### ii. Huduma ya Maji vijijini.

Kulingana na Sensa ya mwaka 2022, Mkoa wa Ruvuma una jumla ya watu 1,848,794 ambapo inakadiliwa watu 1,479,036 wanaishi vijijini**, 68**% ambayo ni sawa na watu 1,005,745 wanaishio vijijini wwanapata huduma ya maji safi na salama. Lengo la Mkoa ni kufikia asilimia 85 kwa wakazi washio vijijini.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya vijiji 551, vijiji 525 kati 551 vinahudumiwa na RUWASA. Vijiji 355 kati ya vijiji 525 vinavyohudumiwa na RUWASA vinapata huduma ya maji na vijiji 170 havina huduma ya maji kama Jedwali Na. 89 hapa chini linavyosomeka.

**Jedwali Na. 89. Vijiji vyenye huduma ya maji na visivyo na huduma ya maji**

| Idadi ya vijiji vyenye Huduma ya Maji na visivyo na huduma ya Maji Mkoa wa Ruvuma | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Jina la Wilaya** | **Jina la Halmashauri** | **Idadi ya Vijiji** | **Idadi ya vijiji vyenye Huduma** | **Idadi ya Vijiji visivyo na Huduma** |
| 1 | Songea | Songea DC | 56 | 32 | 24 |
| 2 | Songea | Madaba DC | 22 | 15 | 7 |
| 3 | Nyasa | Nyasa DC | 84 | 45 | 39 |
| 4 | Tunduru | Tunduru | 131 | 116 | 15 |
| 5 | Namtumbo | Namtumbo DC | 66 | 47 | 19 |
| 6 | Mbinga | Mbinga DC | 117 | 62 | 55 |
| 7 | Mbinga | Mbinga TC | 49 | 38 | 11 |
| **Jumla** | | | **525** | **355** | **170** |

***Chanzo:*** *Ofisi za RUWASA Wilaya katika Mkoa wa Ruvuma kufikia Novemba, 2022*

### 7.5.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mkoa wa Ruvuma ulitengewa jumla ya **TSh 16,523,488,640.94** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji. Mchanganuo wa fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kila Halmashauri ni kama inavyosomeka kwenye jedwali Na.90

**Jedwali Na.90: Mchanganuo wa Fedha zilizotengwa kwenye bajeti 2022/2023**

| NA | HALMASHAURI | FEDHA ZILIZOTENGWA 2022/2023 |
|---|---|---|
| 1 | Songea DC | 2,082,240,096.13 |
| 2 | Mbinga DC | 2,500,060,315.00 |
| 3 | Namtumbo DC | 2,952,957,504.00 |
| 4 | Tunduru DC | 3,890,260,884.13 |
| 5 | Nyasa DC | 2,691,104,466.68 |
| 6 | Madaba DC | 1,789,344,108.00 |
| 7 | Mbinga TC | 617,521,267.00 |
| | **Jumla** | **16,523,488,640.94** |

#### a) HALI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

Hadi kufikia Novemba 30,2022, Mkoa wa Ruvuma ulikuwa unatekeleza jumla ya miradi **32** yenye Jumla ya Tsh. **51,252,361,503.71,** Miradi hii ikikamilika itakuwa inahuduhumia zaidi ya wananchi 264,000 na vijiji 81**.** Orodha ya miradi inayotekelezwa kwa kila Halmashauri ni kama inavyosome ka kwenye jedwali Na.91 hapa chini

**Jedwali Na.91. Orodha ya Miradi inayotekelezwa kwa mwaka 2022-2023**

| Na | HALMASHAURI | JINA LA MRADI |
|---|---|---|
| 1 | Mbinga TC | Mradi wa Maji Ruvuma Chini |
| 2 | | Mradi wa Maji Mbangamao |
| 3 | | Mradi wa Maji Utiri |
| 4 | | Mradi wa Maji Kitanda |
| 5 | | Mradi wa Maji Tanga |
| 7 | | Mradi wa Maji Myangayanga |
| 8 | | Mradi wa Maji Luwaita |
| **8** | | |
| 1 | Mbinga DC | Mradi wa Maji Kihuruku na Luhagara |
| 2 | | Mradi wa Maji Mabuni |
| 3 | | Mradi wa Maji Maguu |
| 4 | | Mradi wa Maji Ruanda |
| **4** | | |
| 1 | Namtumbo DC | Mradi wa Maji Luhimbalilo Naikesi |
| 2 | | Mradi wa Maji Litola Kumbara |
| 3 | | Mradi wa Maji Mgombasi |
| **3** | | |
| 1 | Nyasa DC | Mradi wa Maji Lituhi |
| 2 | | Mradi wa Maji Liuli |
| 3 | | Mradi wa Ngumbo |
| 4 | | Mradi wa Maji Nangombo -Kilosa |
| 5 | | Mradi wa Maji Malungu |
| 6 | | Mradi wa Maji Puulu Songambele |
| **6** | | |
| 1 | **Tunduru DC** | Mradi wa Ndaje - Mbesa Hatua ya pili |
| 2 | | Mradi Maji Masuguru-Mchoteka |
| 3 | | Mradi wa maji semeni na muhuwesi |
| 4 | | Mradi wa maji Ligoma, Makoteni, na Imani, Majimaji na Chalinze |
| **4** | | |
| 1 | Songea DC | Mradi wa Maji Matimira |
| 2 | | Mradi wa Maji Kizuka, Lipaya na Lipokela |
| **2** | | |
| 1 | | Mradi wa maji Mahanje |
| 2 | | Mradi wa maji Kipingo |
| 3 | | Mradi wa Maji Ndelenyuma na Lutukira |
| 4 | | Mradi wa Maji Mbangamawe |
| 5 | | Mradi wa Maji Mtangimbole |

**b) UENDESHAJI WA MIRADI YA MAJI**

Huduma ya maji safi na salama katika Mkoa wa Ruvuma inatolewa na Jumuiya za watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSOs) ambapo mpaka sasa Mkoa una jumla ya (CBWSOs) 116 zilizoundwa kwa mjibu wa Sheria Na. 92 ya mwaka 2019. Orodha ya CBWSOs kwa kila Halmashauri ni kama inavyosomeka kwenye jedwali Na 4 hapa chini

**Jedwali Na.92. Orodha ya CBWSOs kwa kila Halmashauri**

| MKOA | WILAYA | DADI YA COWSOs | IDADI YA CBWSOs KWA MJIBU WA SHERIA NA 5/2019 | IDADI YA CBWSOs ZILIZOUNGANISHWA |
|---|---|---|---|---|
| Ruvuma | Songea DC | 0 | 16 | 2 |
| | Madaba DC | 0 | 9 | 2 |
| | Namtumbo DC | 0 | 26 | 2 |
| | Nyasa DC | 0 | 19 | 0 |
| | Tunduru DC | | 28 | 16 |
| | Mbinga DC | 0 | 18 | 6 |
| | **JUMLA** | | **116** | **28** |

***Chanzo: RUWASA Wilaya katika Mkoa wa Ruvuma kufikia Octoba, 2022***

### c) MPANGO WA UENDELEVU WA MIRADI YA MAJI

Ili miradi iweze kuwa endelevu kwenye maeneo ya huduma ya maji na kuongeza mapato Mkoa kwa kushirikiana na makao makuu ya taasisi una mpango wa kufanya yafuatayo; -

i. Kuajiri kampuni/vikundi kwa ajili ya uendeshaji wa miradi ya maji

ii. Kuendelea kuimarisha CBWSOs kwa kuajiri watumishi wenye sifa

## 7.5.4 VYANZO VYA MAJI.

Huduma ya maji na usafi wa mazingira inategemea kwa kiasi kikubwa uendelevu wa vyanzo vya maji ambavyo vinasimamiwa na Mabonde. Mkoa wa Ruvuma unahudumiwa na mambonde 3 amabyo ni Nyasa, Ruvuma na Rufiji.

i. **Bonde la Ziwa Nyasa**

Bonde la ziwa Nyasa ninahumia Wilaya ya Mbinga, Nyasa na sehemu ya Wilaya ya Songea. Bonde limefanikiwa kuweka mipaka kwenye jumla la vyanzo vine (4) ambavyo ni Lupembe A, Lupembe B, Lupembe C na Lupembe D ambazo zimefanyika kwenye eneo la jumla ya heckta 43 katika Kijiji cha Tukizi Wilaya ya Mbinga.

ii. **Bonde la Ruvuma na Pwani ya kusini**

Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini linahudumia Wilaya ya Tunduru, sehemu ya Wilaya za Songea na Namtumbo. Bonde limefanya kazi ya ukarabati wa vituo vya mito kwa ajili ya ufuatiliaji wa mtiririko wa maji kwenye vituo vya Ruvuma Mkenda, Litapwasi na Muhiga katika Wilaya ya Songea Vijijini na Likonde at Ligowonga katika Wilaya ya Namtumbo, Msinjewe at Chiungo na Muhuwesi at Muhuwesi katika Wilaya ya Tunduru.

Pia kutoa elimu juu ya utunzaji wa rasilimali za maji kwenye shule za msingi kama vile shule ya msingi MajiMaji, Mashujaa na Msamala zilizopo katika halmashauri ya Manispaa ya Songea.

### 7.5.5 HALI YA UBORA WA MAJI MKOA WA RUVUMA

Huduma ya Ubora wa huduma ya Maji kwa Mkoa wa Ruvuma inatolewa na Maabara ya huduma za ubora wa maji Mkoa. Ubora wa maji umeendelea kusimamiwa kwa kukusanya sampuli za maji, kupima pamoja na kuangalia hali ya mazingira ya vyanzo vya maji ili kutoa ushauri wa kitaalamu kwa vitengo vinavyo husika na hifadhi ya mazingira ya vyanzo vya maji.

Pia kutoa ushauri wa kitaalamu kwa mamlaka zinazo husika na ugawaji wa huduma ya maji kwa walaji (Mamlaka za maji, RUWASA, watu binafsi pamoja na taasisi mbalimbali) hasa katika kuweka dawa za kutibu maji, kuzuia vyanzo vya uchafuzi wa maji kibailojia, kikemikali na kifizikia.

Kazi zilizo fanyika;

i). Watu binafsi, sampuli zilizo kusanywa na kupimwa zilikuwa 6 (kibailojia, kifizikia na kikemia)
ii). Taasisi (za kIgeni na za ndani) zilikusanywa na kupimwa sampuli 73 (kibailojia, kifizikia na kikemia)
iii). Mamlaka za maji zilikusanywa sampuli 30 kibailojia, kifizikia na kikemia)
iv). RUWASA zilikusanywa sampuli 268 (kibailojia, kifizikia na kikemia)

Baadhi ya sampuli hizi matokeo yake yalionyesha kuwa maji yamechafuliwa na wadudu wa kinyesi cha wanyama wenye damu joto pamoja na vumbivumbi ambalo husababishwa na shughuli za kibinadumu hasa kilimo karibu na vyanzo vya maji pamoja na kuchimba visima karibu na vyoo.

Ufumbuzi wa matatizo haya.

a. Kuweka mipaka ya shughuli za kibinadamu zinazo fanyika kwenye vyanzo vya maji (Mabonde)
b. Kuweka dawa maeneo yote yenye miradi ya maji ya mtiiriko (Wataalamu wa huduma za ubora wa maji)
c. Kutoa elimu ya matumizi bora ya maji pamoja na matumizi bora ya vyanzo vya maji (Mabonde)

### 7.5.6 CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA MAJI KWA MKOA WA RUVUMA

#### i. Changamoto

Sekta ya maji Mkoa wa Ruvuma inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Uharibifu wa mazingira unachangia kwa kiasi uharibifu wa vyanzo vya maji na kupelekea kuwa na upungufu wa maji katika vyanzo vingi vya maji hasa wakati wa kiangazi,
b) Uendeshaji wa miradi ya maji hasa kwenye eneo la kuchangia huduma ya maji, wananchi kuwa na mwitikio mdogo wa kuchangia huduma ya maji hasa kulipia.

#### ii. Mikakati ya kukabiliana na changamoto

Sekta inaendelea kuchukua hatua zifuatazo: -

a) Kuelimisha wananchi kuacha shughuli za kibinadamu karibu na maeneo ya vyanzo vya maji.

b) Kuendelea kuelimisha jamii juu ya uchangiaji wa huduma ya maji hasa kwa kulipia gharama za matumizi ya maji kulingana na bei elekezi (ukomo)

## 7.6 MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA SONGEA (SOUWASA)

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 – NOVEMBA 2022 KWA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) - SOUWASA

### SEHEMU A: HALI YA HUDUMA KWA SASA

- Manispaa ya Songea ina wakazi wapatao **203,309** kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Taifa iliyofanyika mwaka 2012. Ongezeko (*Growth rate*) kwa mwaka ni 4.4%, hivyo kwa mwaka 2022 Manispaa inakadiriwa kuwa na Wakazi **262,567**. Wakazi **236,936** wanapata huduma ya maji sawa na asilimia **88**
- Vyanzo vya maji vinavyotumika ni vya aina ya chemchem pamoja na maji ya bwawa kama ifuatavyo;-
  - Maji yanayozalishwa kutoka kwenye chemchemi ni wastani wa Lita **1,750,000** kwa siku wakati wa kiangazi na Lita **12,300,000** kwa siku wakati wa masika.
  - Wakati wa kiangazi kikali Bwawa la Ruhila hutumika kuongeza uzalishaji kwa wastani kiasi cha Lita **6,400,000** kwa siku
- Mahitaji ya maji ni wastani wa meta za ujazo **20,366** kwa siku mwaka **2022** katika katika maeneo yote ya Manispaa.
- Wastani wa upatikanaji wa huduma ya Majisafi ni saa **22.62** kwa siku
- Mtandao wa Majisafi una urefu wa kilomita **524.95**

- Huduma ya Majitaka ina mtandao wa bomba zenye urefu wa km **37.7** na maunganisho ya wateja **1,574.** Huduma hii inawafikia wananchi wapatao **16,020** ambao ni asilimia **6** ya wakazi wote wanaoishi katikati ya mji na wasiounganishwa wanahudumiwa na Gari la kuondoa majitaka.

**MPANGO WA KUBORESHA HUDUMA KATIKA MANISPAA YA SONGEA**

Manispaa ya Songea ni miongoni mwa miji **28** nchini Tanzania ambayo itanufaika na mradi wa maji kwa ufadhili wa Serikali ya India na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara ya Maji imekamilisha zoezi la kumpata Mkandarasi na utaratibu wa kusaini mkataba unaandaliwa ili kazi ianze mara moja.

Mradi huo utawezesha ujenzi wa miundombinu ifuatayo;

- Bwawa la Mahilo lenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo **4,800,000**
- Ujenzi wa mtambo wa kuchuja na kutibu maji wenye uwezo wa kutibu maji Lita **16,000,000** kwa siku
- Matanki manne yenye uwezo wa kuhifadhi maji Lita **9,000,000**
- Upanuzi wa mtandao wa bomba za usambazaji kilomita **190.40** katika Manispaa ya Songea.
- Kubadili bomba chakavu zenye urefu wa Kilomita **50** katika maeneo mbalimbali ya Manispaa

**SEHEMU B: TAARIFA YA HUDUMA YA MAJI MJI WA MBINGA**

- Mji wa Mbinga una wakazi wapatao 52,674 ambao wanapata huduma ya maji safi ni 44,089 sawa na asilimia 83.7
- Idadi ya wateja ni 4,152 ambao wote wamefungiwa dira

- Mahitaji ya maji ni mita za ujazo 5,668 kwa siku wakati uzalishaji ni mita za ujazo 3,400 kwa siku.
- Mamlaka ina bomba za usambazaji km 109.9km
- Kiwango cha huduma ni saa 12.5 kwa siku

**MIPANGO YA KUBORESHA HUDUMA KATIKA MJI WA MBINGA**

- Upanuzi wa bomba za usambazaji maeneo ya pembezoni mwa mji ambako hawajafikiwa na huduma ya maji kilomita 15
- Ukarabati wa bomba kuu la usafirishaji kutoka chanzo cha maji cha Ndengu kwa kuondoa bomba la Kipenyo cha nchi 6 na kuweka bomba la kipenyo cha nchi 8 umbali wa Kilomita 1, lengo kuongeza uzalishaji wa maji Mjini Mbinga
- Kuongeza wateja wapya 1,000 wa maji safi.
- Kubadili dira za Maji zinazofanya kazi chini ya kiwango kwa wateja 500
- Kufanya utafiti na usanifu wa vyanzo vipya vya maji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa maji Mji wa Mbinga kwa mahitaji ya sasa na ya baadae.

**SEHEMA C: TAARIFA YA HALI YA MAJI MJINI TUNDURU**

- Mji wa Tunduru una wakazi 68,340 kwa mwaka 2022 na wakazi wanaopata huduma ya maji safi ni 46,040 Sawa na asilimia 67
- Mahitaji ya maji ni mita za ujazo 4,100 kwa siku na uzalishaji ni mita za ujazo 2,390
- Mamlaka ina bomba za usambazaji km 82
- Kiwango cha huduma ni saa 12 kwa siku

**MIPANGO YA KUBORESHA HUDUMA KATIKA MJI WA MBINGA**

Mpango uliopo ni kupanua mtandao katika maeneo yasiyofikiwa na huduma ya maji utakaogharimu Tsh 596,972,005.50. Hadi Novemba 2022 Tsh 89,545,800.80 zimepokelewa kwa ajili ya kuanza utekelezaji huo na km 21.10 za bomba za usambazaji zitaongezwa. Pia Tsh 355,080,000.00 kupitia dirisha la (*Quick win*) zinatarajiwa kwa ajili ya kuongeza chanzo cha maji na bomba za usambazaji km 6.

**SEHEMU D: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI MANISPAA YA SONGEA, MJI WA MBINGA NA MJINI TUNDURU**

Mamlaka inatekeleza miradi ya maji katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Mji wa Mbinga na Mjini Tunduru kama inavyoonyesha katika jedwali namba 93 lifuatalo.

**Jedwali Na. 93: Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Manispaa ya Songea, Mji wa Mbinga na Mjini Tunduru**

| Na | Jina la Mradi | Kazi zilizopangwa na Kazi zilizofanyika | Gharama za Mradi | Fedha zilizotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | **A. MANISPAA YA SONGEA** | | | | |
| 1 | Mradi wa Maji Lilambo eneo la Viwanda | **a) Kazi zilizopangwa**<br>i) Manunuzi ya vifaa vya Ujenzi, Pump na Bomba za usambazaji<br>ii) Ujenzi wa nyumba ya Mtambo (Pump house)<br>iii) Ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji<br>iv) Uchimbaji wa kisima kirefu<br>**b) Kazi zilizofanyika**<br>i) Manunuzi ya vifaa vya Ujenzi,<br>ii) Ujenzi wa nyumba ya Mtambo<br>(*Pump house*) na<br>iii) Uchimbaji wa kisima kirefu | **415,980,885.00** | **100,000,000.00** | **35%** |
| 2 | Mradi wa maji Mwengemshindo | **a) Kazi zilizopangwa** | **547,521,500.00** | **200,000,000.00** | **25%** |

| Na | Jina la Mradi | Kazi zilizopangwa na Kazi zilizofanyika | Gharama za Mradi | Fedha zilizotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | eneo la Hospitali ya Rufaa | i) Manunuzi ya Bomba za usambazaji km 26.5 na Viungio | | | |
| | | ii) Ujenzi wa bomba za usambazaji km 26.5 | | | |
| | | **B) Kazi zilizofanyika** | | | |
| | | i) Manunuzi ya bomba za usambazaji na viungio. | | | |
| | | | | | |
| 3 | Mradi wa Maji Safi mtaa wa Pambazuko katika Manispaa ya Songea | **A) Kazi zilizopangwa** | **546,104,822.18** | **546,104,822.18** | **100%** |
| | | | | | |
| | | i) Ujenzi wa nyumba ya pampu mbili katika vituo vya kusukuma maji | | | |
| | | ii) Kufunga pampu mbili katika vituo vya kusukuma maji | | | |
| | | iii) Kufunga mfumo wa umeme katika vituo vya kusukuma maji. | | | |
| | | iv) Ujenzi wa tanki moja (1) la juu la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 150,000 | | | |
| | | v) Ujenzi wa uzio katika nyumba za pampu | | | |
| | | vi) Kujenga uzio katika tanki la kuhifadhi maji. | | | |
| | | vii) Kuchimba mtaro na kulaza bomba za kusafirisha maji kutoka kwenye vyanzo hadi kwenye tanki kilometa 3.5 | | | |
| | | viii) Kuchimba mtaro na kulaza bomba za kusambaza maji kilometa 15.2 | | | |
| | | ix) Ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji | | | |
| | | | | | |
| | | **B) Kazi zilizofanyika** | | | |
| | | | | | |
| | | i) Kazi zote zilizopangwa | | | |
| | | Zimekamilika | | | |
| | | | | | |
| | **B. MJI WA MBINGA** | | | | |
| 4 | Mradi wa maji | **A) Kazi zilizopangwa** | **322,633,300.00** | **322,633,300.00** | **100%** |

| Na | Jina la Mradi | Kazi zilizopangwa na Kazi zilizofanyika | Gharama za Mradi | Fedha zilizotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | katika mji wa Mbinga kupitia quickwin | i) Manunuzi ya bomba (*HDPE 6"*) mita 6,900 Viungio vya bomba na Vifaa vya ujenzi<br>ii) Ujenzi wa Kidaka maji (*Intake*)<br>iii) Uchimbaji mitaro na ulazaji bomba za usafirishaji mita 6,600<br>**B) Kazi zilizofanyika**<br>i) Kazi zote Zilizopangwa Zimekamilika | | | |
| | **C. MJINI TUNDURU** | | | | |
| 5 | Mradi wa upanuzi wa bomba za usambazaji Maji safi katika Mji wa Tunduru | **A) Kazi zilizopangwa**<br>i) Ununuzi wa bomba za usambazaji maji safi Kilomita 21<br>ii) Uchimbaji mitaro na ulazaji wa bomba za usambazaji majisafi Kilomita 21<br>**B) Kazi zilizofanyika**<br>i) Ununuzi wa bomba za usambazaji maji safi Kilomita 6<br>ii) Uchimbaji mitaro na ulazaji wa bomba za usambazaji majisafi Kilomita 6 | **596,972,005.50** | **89,545,800.80** | **27%** |

| Na | Jina la Mradi | Kazi zilizopangwa na Kazi zilizofanyika | Gharama za Mradi | Fedha zilizotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| 6 | Mradi uboresho wa uzalishaji maji katika mji wa Tunduru | **A) Kazi zilizopangwa**<br>i) Ununuzi wa Pampu ya kusukuma maji na vifaa vya ujenzi<br>ii) Uchimbaji wa kisima kirefu cha maji (Kufanya Pump test, kufunga pampu)<br>iii) Ukarabati wa Nyumba ya Pampu<br>iv) Ukarabati wa tanki la maji<br>**B) Kazi zilizofanyika**<br>i) Ukarabati wa Nyumba ya Pampu | 355,080,000.00 | 53,262,000.00 | **5%** |

## 7.7 WAKALA WA MISITU (TFS) - TAARIFA YA SHAMBA LA MITI WINO NA MPEPO

### 7.7.1 Taarifa ya Shamba la Miti Wino

**Utangulizi**

Hifadhi ya msitu wa Wino ni miongoni mwa mashamba 23 ya miti ya kupandwa yanayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Hifadhi hii kwa sasa ina ukubwa wa hekt 39,718 zinazoundwa na safu tatu (Wino 2,259ha, Ifinga 29,000ha na Mkongotema 8,459ha).

Hifadhi ya msitu wa Wino ulianza kuendelezwa na TFS mwaka 2010 ikihusisha eneo dogo la msitu wa asili wenye ukubwa wa hekta 2,259 (ambayo ndio safu ya Wino) na baadae mwaka 2014 na 2016 tulipata maeneo kutoka vijiji vya Mkongotema na Ifinga kama ilivyobainishwa hapo juu. Tangu tumeanza upandaji wa miti mpaka sasa jumla ya hekta 5,495 zimepandwa miti ya jamii mbalimbali lakini sehemu kubwa ikiwa ni misindano.

Shamba la miti Wino limeendelea kuboresha mahusiano na wananchi, Halmashauri, Wilaya pamoja na Ofisi yako katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya maendeleo. Aidha katika kutekeleza hayo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kupitia Shamba la miti Wino uliridhia na kufadhili mradi wa maji kijiji cha Ifinga uliogharimu shilingi milioni mianne themanini na mbili miamoja ishirini na sita miatano tisini na tisa (482,126,599/=) ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Shamba la miti Wino linapenda kutoa rai kwa wananchi na jamii kutunza mradi huu na maeneo yote ya vyanzo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji unakuwa endelevu.

Aidha mchango wa Shamba kwa jamii inayolizunguka ni kama inavyoonekana kwenye jedwali na. 94, ingawa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 bado tunaendelea kwa kuwa tumeahidi kuwapatia waalimu wa shule ya sekondari Wino viti na meza za waalimu pamoja na kukarabati mfumo wa maji kutoka kwenye chanzo hadi mabweni ya wasichana.

**Jedwali Na. 94: Mchango wa shamba la miti kwa jamii inayolizunguka kipindi ha mwaka wa fedha 2018/2019 – 2022/2023.**

| Na | Jamii | Mwaka wa fedha | Mchano | Kipimo | kiasi | Gharama kwa kipimo (Tsh) | Jumla (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Shule ya msingi Turiani na Lilondo | 2018/2019 | Cement 32.5R | Mifuko | 100 | 14,500 | 1,450,000 |
| 2 | Kanisa la Turiani na Lilondo | 2018/2019 | Cement 32.5R | Mifuko | 100 | 14,000 | 1,400,000 |
| 3 | Shule ya sekondari Wino | 2018/2019 | Mabati 28G | Kipande | 100 | 24,500 | 2,450,000 |
| 4 | Kijiji cha Mkongotema | 2018/2019 | Cement 32.5R | Mifuko | 100 | 14,500 | 1,450,000 |
| 5 | Halmashauri ya Madaba | 2018/2019 | Simtank 3000Ltr | Namba | 1 | 650,000 | 650,000 |
| 6 | K.K.K.T Lilondo | 2019/2020 | Cement 32.5R | Mifuko | 30 | 15,500 | 465,000 |
| 7 | Shule ya sekondari Wino | 2020/2021 | Madirisha ya Aluminiam | Namba | 14 | 165,000 | 2,725,800 VAT imejumuishwa |
| 8 | T.A.G Church | 2020/2021 | 97.5*147 cement | Mifuko | 40 | | 896,800 VAT imejumuishwa |
| 9 | Shule ya sekondari Wino | 2020/2021 | Cement 32.5R, | Mifuko | 80 | 19,000 | 2,472,100 VAT imejumuishwa |
| | | | Cement 42.5R, | Mifuko | 20 | 20,000 | |
| | | | Rangi | Ndoo | 5 | 35,000 | |
| 10 | Kijiji cha Mkongotema | 2020/2021 | Cement 32.5R | Mifuko | 100 | 19,000 | 2,242,000 VAT imejumuishwa |
| 11 | Kanisa la Turiani | 2020/2021 | Cement 32.5R | Mifuko | 50 | 19,000 | 1,242,000 VAT imejumuishwa |
| 12 | Kanisa la Wino | 2020/2021 | Cement 32.5R | Mifuko | 100 | 19,000 | 1,242,000 VAT imejumuishwa |
| 13 | Wanavijiji 91 wa Wino, Ifinga, Mkongotema na Lilondo | 2020/2021 | Miche ya Miti | Namba | 132,10 | - | - |
| 14 | Kanisa la Turiani | 2020/2021 | Rangi 20Ltr | Ndoo | 10 | 140,000 | 1,652,000 VAT imejumuishwa |
| 15 | Shule ya Sekondari Wino | 2021/2022 | Cement 42.5R | Mifuko | 100 | 175,000 | 2,065,000 VAT imejumuishwa |
| 16 | Kijiji cha Mkongotema | 2021/2022 | “Tiles” 40*40 | Boksi | 40 | 35,000 | 1,652,000 VAT imejumuishwa |

| Na | Jamii | Mwaka wa fedha | Mchano | Kipimo | kiasi | Gharama kwa kipimo (Tsh) | Jumla (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 17 | Kijiji cha Mkonhgotema | 2021/2022 | Madirisha ya Aluminiam | Namba | 9 | 276,645 | 2,489,800 VAT imejumuishwa |
| 18 | Kanisa la Lilondo (RC) | 2021/2022 | Cement 32.5R | Mifuko | 100 | 16,500 | 1,947,000 VAT imejumuishwa |
| 19 | Kijiji cha Lituta – Madaba | 2021/2022 | Viriba"4" | Kilogram | 30 | 6,550 | 196,500 VAT imejumuishwa |
| 20 | Kijiji cha Ifinga (Mradi wa Maji) | 2018/2019 | | | | | 482,126,599.35 VAT imejumuishwa |
| 21 | Kijiji cha Igawisenga | 2021/2022 | Mizinga ya Nyuki | Namba | 30 | 100,000 | 3,000,000 |
| 22 | Kijijii cha Wino | 2022/2023 | Cement 42.5R | Namba | 150 | 16,000 | 2,400,000 |
| 23 | Kijiji cha Matetereka | 2022/2023 | Cement 42.5R | Namba | 100 | 16,000 | 1,600,000 |
| 24 | Kituo cha Afya Matetereka | 2022/2023 | Cement 42.5R | Namba | 500 | 16,000 | 8,000,000 |
| **JUMLA** | | | | | | | **526,693,599.35/=** |

**Malengo ya Uanzishwaji wa Shamba**

**Mh. Mkuu wa Mkoa;** Malengo makuu ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya msitu wa Wino ni pamoja na:

1. Kuhifadhi maliasili zinazotaka kutoweka na vyanzo vya maji, Vyanzo vya mto lupahila – lutukila-luhuhu-Ziwa Nyasa, Mnywa masi – Pitu-Ruhuji-ifakara-Rufiji, Mwesa – Ruhuji…,Lutukila – Luhuhu…., Mgombezi – Lutukila…, Kineneka – Lutukila…, Kipilili – Pitu…., Balali – Pitu…., Mapancha – Chechengu-pitu…, Mbega – Chechengu…, Chechengu – Pitu….

2. Ajira, Watumishi wa kudumu 15, mkataba 10, vibarua wa msimu wanakadiriwa kufikia 4,000.

3. Mazao ya biashara kama mbao na nguzo za umeme kwa siku za usoni ili kuongeza mapato ya serikali; na

4. Kuboresha mazingira na mandhari.

Hali nzuri ya hewa (Carbon sink / Sequenstration) na mazingira ya kuvutia

**Upandaji Miti**

Shughuli za upandaji miti katika Shamba la miti Wino zimeendelea kufanyika kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji vinatunzwa vizuri kwa upatikanaji maji na mazao ya Misitu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Takwimu za upandaji miti ndani ya Shamba la miti Wino ni kama zinavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

Aidha, baada ya upandaji miti kazi mbalimbali za kuhudumia miti iliyopandwa hufanyika. Miongoni mwa kazi hizo ni usafi wa mashamba (Spot weeding, sanitary slashing, singling); Kupogoa matawi; doria /ulinzi wa msitu; Ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja ambapo kazi hizo hutumia wananchi wanaozunguka shamba na hata kutoka maeneo mbalimbali na hivyo kuongeza kipato na mzunguko wa fedha.

**Jedwali 94: Taarifa ya miche kwa kipindi cha miaka 11 (2012-2022).**

| MWAKA | MICHE ILIYOKUZWA | MICHE ILIYOPANDWA/ITAKAYOPANDWA | ILIYOGAIWA/ITAKAYOGAIWA |
|---|---|---|---|
| 2012 | 291,000 | 285,083 | - |
| 2013 | 378,000 | 371,437 | - |
| 2014 | 676,000 | 670,600 | - |
| 2015 | 518,000 | 512,593 | - |
| 2016 | 307,000 | 303,525 | - |
| 2017 | 908,000 | 904,576 | - |
| 2018 | 1,042,000 | 1,039,007 | - |
| 2019 | 507,000 | 503,283 | 132,100 |
| 2020 | 690,000 | 543,279 | 132,100 |
| 2021 | 600,000 | 459,065 | 135,000 |
| 2022 | 717,119 | 565,499 | 93,535 |
| 2023 | 1,000,000 | 800,000 | 200,000 |
| **Jumla** | **6,634,119** | **6,957,947** | **692,735** |

## Changamoto

Matukio ya moto kwa kiasi kikubwa hupunguza jitihada za usimamizi endelevu wa shamba. Vyanzo vikuu vya moto ni uandaaji wa mashamba msimu wa kilimo kwa kutumia moto ambapo kwa mwaka 2016 ziliungua hekta 600 na 2021 hekta 1,623 ukisababishwa na uaandaaji wa mashamba maeneo ya mabonde yanayopakana na Shamba. Vyanzo vingine ni radi, sigara, vichaa, n.k

Katika kukabiliana na tatizo hili, Uongozi wa Shamba la miti wino umekuwa ukifanya yafuatayo: -

a) Kutoa elimu na vifaa vya kuzimia moto kwa jamii/ vijiji

b) Kutoa msaada wa vitendea kazi vinavyotumika kuzimia moto kwa jamii

c) Kujenga mahusiano mema na vijiji vinavyozunguka Shamba kwa kuwapatia vifaa vya ujenzi mbalimbali.

d) Kufanya kazi za kinga dhidi ya moto (kusafisha Fire lines na kufungua barabara, Kufyekea miti, uwepo wa vituo 3 vya mawasiliano, doria ya msituni mwaka mzima, kuimarisha ulinzi wa kupambana na moto kipindi chote cha kiangazi, kuweka gari standby kwa kiangazi na mfumo wa satelaiti wa kuangalia matukio ya moto uliopo makao makuu ya Wakala.

Shamba la miti Wino linaendelea kuwaomba wananchi kuepuka kuanzisha moto maeneo hatarishi wakati wa uandaaji wa mashamba na kuwataka kufanya maandalizi mazuri ya barabara za kinga moto.

Pamoja na changamoto pia Shamba la Miti Wino limeweza kufanikiwa katika maeneo yafuatayo; -

i) Uhifadhi wa eneo hili umehimarika sana.
ii) Miti iliopandwa imestawi vizuri.
iii) TFS kupitia shamba hili imeimarisha ushirikiano wake na jamii na uongozi katika ngazi mbalimbali.
iv) Aidha kupitia shamba hili tumekuwa wadau wakubwa wa maendeleo katika Nyanja za afya, elimu, maji na usalama.
v) Shamba limetoa ajira miaka yote kwa makundi mbalimbali. Kwa wastani wananchi 4,000 hujipatia ajira za mda mrefu na mfupi katika shamba hili kwa mwaka.
vi) Uwepo wa shamba hili umevutia wawekezaji wengine kuja eneo hili.

    Mf Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ambapo pia wamepewa ardhi na kijiji cha Ifinga.

vii) Tunawashirikisha wananchi katika usimamizi na uendelezaji wa mashamba yao. Mara kadhaa pia tunatoa miche kwa jamii inayozunguka ili kuongeza chachu ya uhifadhi.

**Malengo ya Shamba**

Wakala wa huduma za misitu Tanzania kupitia shamba la miti ya kupandwa la Wino tunatekeleza maagizo mbalimbali ya Viongozi pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzwa ipasavyo na upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya misitu na watumiaji wengine unakua endelevu kwa kizazi kilichopo na kijacho.

Yafuatoyo tumepanga kuyatekeleza kwa kipindi mpaka ifikapo 2025

I. Kuendelea kuongeza bajeti kwenye eneo la upandaji kutoka hekta 500 kwa sasa kwa mwaka mpaka kufikia hekta 3,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.

II. Kuendelea kuongeza bajeti kwenye maeneo ya miundombinu, vyombo vya usafiri na nyumba za makazi ya watumishi ili kuongeza ufanisi katika malengo ya taasisi.

III. Kuendelea kushirikiana na taasisi zote, vikundi na watu binafsi wanaojihusisha na upandaji miti katika kuhakikisha kwamba tunalitokomeza tatizo la moto wa msituni.

IV. Uongozi wa shamba utaendelea kutoa elimu ya utunzaji mazingira kwa jamii ya vijiji vinavyouzunguka msitu pamoja na kuzisaidia shule za msingi na sekondari vifaa na mbegu za miti ili waanzishe vitalu vyao wenyewe na kuwajengea uwezo.

V. Kuendelea kushirikiana na jamii za vijiji vinavyozunguka msitu katika shughuli mbalimbali za maendeleo

#### 7.7.2 Taarifa ya Shamba la Miti Mpepo

1. **Utangulizi**

**Shamba** la Miti Mpepo ni miongoni mwa Mashamba 24 ya Miti yanayosimamiwa na kuhudumiwa na **Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS),** chini ya **Wizara ya Maliasili na Utalii**.

Shamba la Miti Mpepo lilianza mwaka wa fedha 2017/2018 likiwa na ukubwa wa Hekta 2,017 Ha, kisha zikafika hekta 3,905ha ambazo zote zipo Wilayani Nyasa.Kutokana na juhudi mbalimbali za Menejimenti ya Shamba kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji, Wilaya na Mkoa zinazofanyika za kupata maeneo mapya toka kwa wananchi na maeneo ya hifadhi yaliyokuwa yamevamiwa na wananchi, Eneo la Shamba kwa sasa ni takribani hekta 20,905ha ambazo zipo Wilaya za Nyasa, Songea na Namtumbo kwa mchanganuo ufuatao:

**Jedwali Na. 95: Eneo la Shamba la miti Mpepo**

| **Jina la Eneo** | **Ukubwa (Ha)** | **Wilaya** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| Mpepo | 3,905 | Nyasa | Limepatikana kijijini |
| Luekei/Liuli | 2,000 | Nyasa | Hifadhi/Vijijini |
| Lihanje | 6,000 | Songea | Hifadhi |
| Ndongosi | 8,000 | Songea | Limepatikana kijijini |
| Kipiki | 1,000 | Namtumbo | Hifadhi |
| **Jumla** | **20,905** | | |
| | | | |

Hali kadhalika Shamba limefanikiwa kupata eneo lenye jumla ya hekta 50,000 wilayani Tunduru kwaajili ya uanzishwaji wa Shamba jipya la Miti mara baada ya kukamilisha taratibu kadhaa za umilikishaji wa eneo hilo kisheria. Eneo hilo lote limepatikana toka katika vijiji

vilivyoridhia uanzishwaji wa mradi wa upandaji miti katika wilaya ya Tunduru na Tayari kwa Mwaka wa Fedha huu 2022/2023 Serikali imetenga Bajeti ya kuanza na Upandaji wa Hekta 100 na hivi sasa tupo kwenye maandalizi ya mwisho ya Kuandaa Shamba kwa ajili ya Upandaji Miti January 2023.

**2. Utekelezaji mipango kazi ya shamba**

Shamba la Miti Mpepo hadi sasa limeshapanda jumla ya hekta 2240ha ambapo hekta 1440ha zimepandwa miti jamii ya Misindano (*Pines*) katika tarafa ya Mpepo wilayani nyasa na Liwilikitesa Wilayani Mbinga na hekta 400ha imepandwa miti jamii ya Misaji (Mitiki) katika hifadhi ya Kipiki, Wilayani Namtumbo na 400ha zimepandwa misaji (teak) Liuli Wilaya ya Nyasa pia miundombinu ya bustani tayari imesimikwa kwa ajili ya uzalishaji wa miche aina ya misaji (teak) kwa maeneo ya Liuli na Ndongosi.

Aidha serikali inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara Ya 69 (g) ya mwaka 2020-2025 inayoelekeza kuendeleza programe ya upandaji miti na ufugaji nyuki ili kutunza mazingira na kuongeza kipato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

**Jedwali Na. 95 Taarifa ya Upandaji Miti**

| NA | AINA YA MITI | UKUBWA (ENEO)(Ha) | MAHALI |
|---|---|---|---|
| 1. | PINE(MISINDANO) | 1200 | MPEPO |
| | | 240 | LIWILIKITESA |
| 2. | TEAK (MISAJI) | 400 | LIULI |
| 3. | TEAK(MISAJI) | 400 | KIPIKI |
| | **JUMLA** | **2240** | |

Hali kadhalika Shamba linaendelea na kazi mbalimbali za utunzaji wa Miti ikiwemo Palizi (weeding/sanitary slashing), kupogolea miti (pruning), ulinzi wa Shamba (Forest protection), kufungua barabara (Forest Roads) na ujenzi wa Mkalavati(culverts) kwa maeneo yenye shida ya kupitika hasa kipindi cha masika kwa kuzingatia mwongozo (**Technical order**) wa TFS 2021 pamoja uboreshaji wa Miundombinu ikijumuisha ujenzi wa majengo manne (4) yaani Ofisi Kuu ya Shamba 1, Nyumba ya Mhifadhi Mkuu 1, Nyumba za watumishi 2.

Shamba lina Bustani Nne, Mpepo, Ndongosi, Tunduru na Liuli yenye jumla ya miche ya Miti 1,130,000 ikijumuisha miche aina ya misindano (pine) pamoja na misaji (teak) kama ilivyoainishwa kwenye jedwali Namba 96 hapo chini;

**Jedwali Na. 96 Bustani za Miti katika Shamba la Miti Mpepo**

| NA. | MAHALI | AINA YA MICHE | IDADI YA MICHE |
|---|---|---|---|
| 1. | MPEPO | MISINDANO(PINE) | 150,000 |
| 2. | TUNDURU | MISINDANO (PINE) | 280,000 |
| 3. | LIULI | TEAK(MISAJI) | 500,000 |
| 4. | NDONGOSI | TEAK (MISAJI) | 200,000 |
| | **JUMLA** | | **1,130,000** |

Kati ya miche hii 700,000 ni aina ya miti ya misaji (Teak) na 430,000 ni aina ya miti ya Misindano (Pines)**..**

### 3. Fidia ya ardhi na mali za wananchi

Shamba limeshalipa Fidia Jumla ya Tshs. 318,223,778/= kwa wananchi 115 waliopisha mradi wa upandaji miti katika kata ya Mpepo pamoja na Liuli baada ya kufanyiwa uthamini na Mthamini Mkuu wa Serikali.

Hali kadhalika shamba la miti mpepo limewafanyia uthamini kupitia ofisi ya Mthamini Wilaya ya Nyasa Jumla ya wananchi 8 katika Kata ya Mpepo ambao bado Wanasubiria Malipo yao na kwa kuwa Tayari Bajeti imetengwa kwa ajili yao hadi kufikia Desemba Mwaka 2022 Shamba litamaliza rasmi Malipo yao ambayo ni **Tsh 83,843,749.**

**4. Faida za uanzishwaji wa shamba la miti Mpepo.**

**Uanzishwaji wa shamba la Miti Mpepo una faida nyingi kwa wananchi na Taifa kwa ujumla; miongoni mwa faida hizi ni pamoja na;**

i. Chanzo cha mapato ya serikali kuu (Royality), Halmashauri za wilaya na vijiji (CESS 5%).

ii. Kutoa ajira kwa wananchi wanaozunguka shamba kupitia kazi mbalimbali zinazofanyika shambani. Takribani ajira za muda 3,000 kwa mwaka.

iii. Halmashauri ya vijiji kupata tozo mbalimbali pindi miti itakapouzwa.

iv. Kuwezesha upatikanaji wa elimu ya upandaji na miche kwa wananchi bure.

v. Kuwezesha upatikanaji wa nguzo, mbao na kuni kwa matumizi ya biashara na nyumbuni na hivyo kupunguza utegemezi wa misitu asilia.

vi. Upatikanaji wa Malighafi za viwanda vya mbaona kukuza ajira kwa wananchi na uchumi wa Taifa.

vii. Kuboresha mazingira na hali ya hewa kwa kufyonza Hewa ukaa na kutoa Hewa Safi kwa Viumbe vyote, udongo na ikolojia.

**viii.** Kusaidia huduma za kijamii zinazozunguka Shamba, Milioni 10 inatengwa kwa mwaka ili kusaidia Huduma mbalimbali za Jamii zinazozunguka Shamba**.**

**5. Ujenzi wa Ofisi Mpepo pamoja na nyumba tatu za watumishi**

Ujenzi wa ofisi Mpepo pamoja na nyumba tatu za watumishi umetekelezwa na NHC na jumla ya majengo manne yaani Ofisi kuu ya Shamba moja,nyumba ya Mhifadhi moja na nyumba mbili za watumishi zina thamani ya shilingi **968,634,587/=** na fedha zimetolewa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuboresha mazingira bora ya kufanyia kazi na kuishi watumishi wa umma nchini.

Kwa sasa nyumba hizi nne kwa maana ya Ofisi na nyumba tatu za watumishi zipo tayari kwa 95% kwani kuna maboresho na marekebisho machache ambayo NHC waliagizwa na TFS kumalizia mapungufu yaliyojitokeza ili ziwe tayari kwa matumizi.

Na lengo letu ni kuhamia Mpepo muda wowote pindi miundo msingi ya mtandao yaani Internet pamoja na umeme vikikamilika kwani shughuli nyingi za kiofisi zinahitaji Mtandao wa Internet. Hivyo mchakato wa kuweka mtandao unaendelea kupitia kampuni ya TTCL.

**6. Changamoto**

Pamoja na kufanikisha kazi mbalimbali zilizotajwa hapo juu bado Shamba la Miti Mpepo linakabiliwa na changamoto kadhaa zifuatazo:

1. Ubovu wa barabara kutoka Nyoni hadi Mpepo inayopitika kwa taabu hasa kipindi cha masika .

2. Ukosefu wa umeme Mpepo kwa ajili ya shughuli za kiofisi za kila siku.

3. Moto wa mara kwa mara hususan kipindi cha Kiangazi unaosababishwa na Wananchi kuandaa Mashamba kwa kutumia Moto na hivyo kusababisha hasara kwa Mashamba ya Miti

**Shukrani**

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), shamba la miti Mpepo tunapenda kutoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi mbalimbali anazozifanya katika kuhakikisha Sekta ya Misitu na Nyuki kupitia Wakala Wa Huduma Za Misitu Tanzania (TFS) inafanya vizuri kiutendaji katika Kulinda,Kutunza na Kuhifadhi Misitu kwa manufaa ya Kizazi cha sasa na cha Baadae.

## 7.8 CHUO CHA MAFUNZO YA UHIFADHI WA MALIASILI KWA JAMII – LIKUYU SEKAMAGANGA

## TAARIFA YA CHUO CHA MAFUNZO YA UHIFADHI WA MALIASILI KWA JAMII (CBCTC) - LIKUYU SEKAMAGANGA

### 1. UTANGULIZI

Chuo cha mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kilianzishwa mnamo mwaka 1995 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii - Idara ya Wanyamapori na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani chini ya Shirika lake la ufundi (GTZ).

Awali Chuo hiki kilipoanzishwa mwaka 1995, kililenga kutoa mafunzo tajwa kwa wananchi wanaoishi kuzunguka pori la akiba la Selous pekee. Lakini kutokana na mahitaji ya elimu hiyo kila mahali, kwa sasa washiriki wa mafunzo wanatoka nchi nzima hususani jamii zinazoishi kando kando ya maeneo yaliyohifadhiwa. Chuo hiki kina majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

i) Kutoa mafunzo ya uhifadhi wa maliasili na utalii
ii) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa jamii kuhusu masuala ya uhifadhi wa maliasili
iii) Kushirikiana na wadau mbalimbali wa uhifadhi ili kuhakikisha rasilimali zamaliasili na utamaduni zinalindwa na kuhifadhiwa ipasavyo .

### 2. MAHALI CHUO KILIPO

Mkoani Ruvuma, Wilayani Namtumbo, katika kata na kijiji cha Likuyu Sekamaganga. Kinapatikana umbali wa kilometa 110 kutoka Songea mjini na 40 kutoka Namtumbo mjini. Kinamiliki eneo mojawapo ya iliyokuwa kambi ya wakimbizi kutoka Msumbiji kwa miaka ya 1985. Kimepakana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere Kusini, Jumuiya ya hifadhi ya Mbarang'andu (WMA) na Ushoroba wa Selous Niassa. Chuo kina usajili wa kudumu kutoka katika Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

## 3. MAFUNZO YATOLEWAYO

**Jedwali Namba 96: Mafunzo yatolewayo na Chuo**

| S/N | AINA YA KOZI | MUDA | SIFA ZA KUJIUNGA | ADA (TSH) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Astashahada ya awali ya Utalii na Uongozaji Watalii | Mwaka mmoja | i) Mhitimu wa kidato cha nne mwenye ufaulu katika masomo manne kwa kiwango cha "D" isipokuwa masomo ya dini<br>ii) Mhitimu wa Chuo cha VETA katika fani za Utalii na uhifadhiwanyamapori | 2,406,000 (Inagharamia chakula, malazi , mafunzo ya nadhariana vitendo) |
| 2 | Astashahada ya Utalii na UongozajiWatalii | Mwaka Mmoja | i) Mhitimu wa kidato cha sita mwenye ufaulu katika masomo mawili (Principal pass and Subsidiary Pass)<br>ii) Mhitimu wa Astashahada ya Awali ya kozi zinazoendana na masuala ya utalii , waongoza watalii, uhifadhi, ukarimu na huduma kwa wateja kutoka<br>katika Chuo chochote kilichosajiliwa na NACTVET | 2,800,000 (Inagharamia chakula, malazi , mafunzo ya nadhariana vitendo) |
| 3 | Diploma ya Utalii na Uongozaji Watalii (**Kozi tarajiwa)** | Mwaka mmoja | Mhitimu wa Astashahada ya Utalii na Uongozaji Watalii kutoka katika Chuo chochotekilichosajiliwa na NACTVET | 3,100,000 (Inagharamia chakula, malazi , mafunzo ya nadharia<br>na vitendo) |
| 2 | Mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) | Miezi mitatu | i) Kujua kusoma na kuandika<br>ii) Utimamu wa akili na mwili<br>iii) Wachaguliwe na vijiji husika | 1,800,000 (Inagharamia chakula, malazi , mafunzo ya nadharia<br>na vitendo) |
| 3 | Mafunzo kwa viongozi na wajumbe wa<br>kamati za maliasili za Vijiji | Mwezi mmoja | i) Kujua kusoma na kuandika<br>ii) Utimamu wa akili na mwili | 600,000 (Inagharamia chakula, malazi , mafunzo ya nadharia na ziara za mafunzo) |

| S/N | AINA YA KOZI | MUDA | SIFA ZA KUJIUNGA | ADA (TSH) |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Mafunzo maalum kulingana na mahitaji ya wateja (Himasheria, Mbinu za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, ujasiliamali ambao ni rafiki wa mazingira n.k) | Wiki moja – Mwezi mmojai | i) Kujua kusoma na kuandika<br>ii) Utimamu wa akili na mwili | 250 ,000 – 1,000,000 |

## 4.0 IDADI YA WANAFUNZI WALIOPO CHUONI KWA SASA

Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi takriban 136 wanaoendelea na mafunzo mbalimbali kama inavyochanganuliwa katika jedwali namba 97 hapa chini:

**Jedwali Na.97: Idadi ya wanafunzi waliopo Chuoni**

| S/N | AINA YA KOZI | IDADI YA WANAFUNZI | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JUMLA |
| 1 | Astashahada ya Utalii na UongozajiWatalii | 3 | 3 | 6 |
| 2 | Astashahada ya Awali ya Utalii na Uongozaji watalii | 69 | 29 | 98 |
| 2 | Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) | 26 | 6 | 32 |
| **JUMLA** | | **98** | **38** | **136** |

## 5.0 MAFANIKIO

Tangu kuanzishwa kwa Chuo hiki kimeshafanikiwa kufanya yafuatayo;

**5.1 Mafunzo**: Kutoa mafunzo kwa takriban wananchi 5000 katika kozi mbalimbali kama inavyooneshwa katika jedwali Namba 98.

**Jedwali Na. 98: Idadi ya wahitimu**

| S/N | JINA LA KOZI | IDADI YA WANAFUNZI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | |
| 1 | Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) | 2047 | 139 | 2186 |
| 2 | Viongozi na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji | 1238 | 499 | 1737 |
| 3 | Himasheria | 729 | 27 | 756 |
| 4 | Mbinu za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu | 73 | 6 | 79 |
| 5 | Ujasiliamali ambao ni rafiki wa mazingira | 24 | 6 | 30 |
| 6 | CBNRM | 55 | 36 | 91 |
| 7 | Uhifadhi wa misitu na mbinu za doria | 221 | 92 | 313 |
| 5 | Astashahada ya awali ya Waongoza watalii | 32 | 9 | 41 |
| | **Jumla** | **4419** | **814** | **5233** |

**5.2 Uboreshaji wa mafunzo na miundombinu**

- Uanzishaji wa kozi ya Astashahada ya waongoza watalii (NTA LEVEL 5)
- Uboreshaji wa majengo ya kujifunzia (Ujenzi wa maktaba na chumba cha kompyuta, bwalo na jiko na vyoo vya wanafunzi na watumishi)

pamoja na ukarabati wa baadhi ya majengo ikiwemo vyoo, nyumba ya watumishi na bweni la wanafunzi wa kike.

- Kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi wa kozi ya Utalii na waogoza watalii ( Kutoka 11 mwaka 2020/21 – 104 mwaka 2022/23)
- Kuongeza vifaa vya mafunzo ikiwemo vifaa vya maktaba na magari mawili (Bus na Hardtop)
- Kupata usajili wa kudumu na Ithibati ya muda (Accreditation Candidacy)kutoka NACTVET.

## 6.0 CHANGAMOTO NA NAMNA YA KUKABILIANA NAZO

Pamoja na mafanikio yaliyobainishwa Chuo pia kina changamoto kadhaa kama ikiwemo;

### 6.1 upungufu na uchakavu wa majengo

Chuo kina ukosefu wa majengo kama mabweni na upungufu wa nyumba za watumishi. Pia majengo yaliyopo ni chakavu na hasa ikizingatiwa kuwa mengi ya majengo haya ni yale yaliyorithiwa kutoka kwa wakimbizi wa Msumbiji miaka ya 1985, hivyo yanahitaji ukarabati.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo Chuo kinaendelea kuwasiliana na Wizara pamoja na wadau wengine wa maendeleo ili kuweza kujenga majengo mapya na kukarabati yaliyopo. Tunaishukuru sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kujenga na kukarabati baadhi ya majengo na hivyo kurahisisha utendaji kazi. Itihada Zaidi zinaendelea ili kuweza kuboresha miundombinu hasa majengo.

### 6.2 Uhafifu wa mfumo wa umeme

Kwa sasa Chuo kinatumia mfumo wa umeme jua ambao ni hafifu na hautoshelezi kuendesha shughuli za kiofisi kwani umeshakuwa ni wa muda mrefu. Hali hiihupelekea Chuo kulazimika kutumia jenereta ambapo ni gharama kubwa kujiendesha na hasa ikizingatiwa kuwa kwa sasa idadi ya wanafunzi inaongezekakila mwaka.

### 6.3 Gharama kubwa za upatikanaji wa Maji

Chuo kinatumia maji ya kisima yanayosukumwa kwa kutumia jenereta na mashine. Hali hii inafanya Chuo kitumie gharama kubwa sana ya mafuta (Diesel) na hasa kunapokuwa na wanafunzi wengi. Japokuwa mfumo wa maji tayari umeshafika Chuoni kupitia mradi wa maji unaoendelea katika kijiji cha Likuyu Sekamaganga, lakini maji bado hayafiki Chuoni kwa sababu ya msukumo kuwa mdogo.

## 7.0 MAOMBI;

Naomba nitumie fursa hii kuiomba ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikisaidie Chuo katika yafuatayo:

i. Upatikanaji wa umeme wa uhakika kupitia mradi wa umeme wa REA unaoendelea katika Kata ya Likuyu Sekamaganga kwani wataalamu tayari walishafika Chuoni na kufanya tathmini.

ii. Upatikanaji wa maji ya uhakika kupitia mradi wa maji ulioko katika kijiji cha Likuyu Sekamaganga kwa kuongeza msukumo wa maji ili yaweze kufikaChuoni.

Upatikanaji wa umeme na maji ya uhakika utaboresha huduma kwa wanafunzi na kuwafanya wasome katika mazingira stahiki. Pia utakipunguzia Chuo gharama kubwa ya mafuta inayotumika kwenye kuwasha majenereta kwa ajili ya umeme na maji na hasa ikizingatiwa kuwa kwa sasa gharama za mafuta (Diesel) ziko juu sana na idadi ya wanafunzi inaongezeka mwaka hadi mwaka.

## 8.0 SHUKRANI

Kwa niaba ya watumishi wa Chuo, Natoa shukrani za dhati kwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa ushirikiano wa hali na mali inaokipatia Chuo na hivyo kukiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Chuo kinaahidi kuendelea kutoa huduma bora na kwa weledi wa hali ya juu ili kuweza kuchangia katika maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa Ujumla.

## 7.9 OFISI YA KAMISHNA MSAIDIZI WA ARDHI MKOA WA RUVUMA.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ARDHI MKOA WA RUVUMA

### 1. UTANGULIZI

Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Ruvuma ilianzishwa mnamo mwezi Machi, 2020. Uanzishwaji waOfisi hizi ni moja ya mikakati ya Serikali kusogeza huduma karibu na wananchi ili kukabiliana na changamoto za Sekta hii na kukidhi mahitaji ya huduma za ardhi za Kupanga miji na vijiji, Uthamini,Upimaji, Umilikishaji na Usajili wa Hati na Nyaraka mbalimbali. Awali huduma hizi zilikuwa zinatolewa katika Ofisi ya ardhi Kanda ya Kusini (Mtwara) hivyo, wananchi walilazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita mia sita kufuata huduma hizi ambazo kwa sasa zinatolewa Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma.

### KAZI ZILIZOFANYIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KUANZIA TAREHE 1 JULAI HADI TAREHE 30 NOVEMBA

Ofisi ya Ardhi Mkoa inaendelea kusimamia na kutekeleza kazi za upangaji, upimaji, umilikishaji, uthamini, usajili wa Hati na nyaraka mbalimbali, utatuzi wa migogoro ya Ardhi na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kama ilivyoainishwa hapo chini;

### UPIMAJI WA VIWANJA NA MASHAMBA

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya viwanja **16,614** na mashamba **08** yamepimwa katika maeneo ya mijini na vijijini kwa ajili ya makazi na matumizi mengine kwa mchanganuo ufuatao:

**Jedwali Na. 99: Viwanja na Mashamba yaliyopimwa 2021/22**

| | | VIWANJA | MASHAMBA |
|---|---|---|---|

| NA | HALMASHAURI | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA | IDADI | GHARAMA ILIYOTUMIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Songea Manispaa | 3,967 | 396,700,000.00 | 0 | 0 |
| 2 | Songea DC | 332 | 33,200,000.00 | 5 | 3,225,000.00 |
| 3 | Mbinga Mji | 4,695 | 469,500,000.00 | 0 | 0 |
| 4 | Mbinga DC | 3,937 | 393,700,000.00 | 0 | 0 |
| 5 | Tunduru DC | 1,738 | 173,800,000.00 | 1 | 645,000 |
| 6 | Madaba DC | 511 | 51,100,000.00 | 1 | 645,000 |
| 7 | Nyasa DC | 847 | 84,700,000.00 | 0 | 0 |
| 8 | Namtumbo DC | 587 | 58,700,000.00 | 1 | 645,000 |
| **JUMLA** | | **16,614** | **1,661,400,000.00** | **8** | **5,160,000.00** |

Pia kuanzia Julai hadi Novemba 2022, jumla ya viwanja **5,429** na mashamba **03** yamepimwa katika maeneo ya mijini na vijijini kwa ajili ya makazi na matumizi mengine kwa mchanganuo ufuatao:

**Jedwali Na. 100: Viwanja na Mashamba yaliyopimwa Julai – Novemba 2022**

| NA | HALMASHAURI | VIWANJA | | MASHAMBA | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | IDADI | GHARAMA | IDADI | GHARAMA |
| 1 | Songea Manispaa | 3,398 | 339,800,000.00 | 0 | 0 |
| 2 | Songea DC | 128 | 12,800,000.00 | 1 | 645,000.00 |
| 3 | Mbinga Mji | 1 | 100,000.00 | 0 | 0 |
| 4 | Mbinga DC | 277 | 27,700,000.00 | 1 | 645,000.00 |
| 5 | Tunduru DC | 1,452 | 145,200,000.00 | 0 | 0 |
| 6 | Madaba DC | 144 | 14,400,000.00 | 1 | 645,000.00 |
| 7 | Nyasa DC | 27 | 2,700,000.00 | 0 | 0 |

| NA | HALMASHAURI | VIWANJA | | MASHAMBA | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | IDADI | GHARAMA | IDADI | GHARAMA |
| 8 | Namtumbo DC | 2 | 200,000.00 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | | **5,429** | **542,900,000.00** | **3** | **1,935,000.00** |

**MIPANGO MIJI NA VIJIJI**

Jumla ya michoro 47 yenye jumla ya viwanja 15,253 vya matumizi mbalimbali kutoka Mamlaka za upangaji imepokelewa, kukaguliwa na kuidhinishwa kwa mchanganuo ufuatao:-

**Jedwali Na 101: Michoro iliyopokelewa**

| Na | Halmashauri | Idadi ya Michoro ya Mipango Miji | Idadi ya viwanja |
|---|---|---|---|
| 1 | Mbinga Mji | 09 | 3,196 |
| 2 | Mbinga DC | 02 | 1,597 |
| 3 | Songea DC | 02 | 26 |
| 4 | Nyasa DC | 03 | 710 |
| 5 | Madaba DC | 05 | 2,788 |
| 6 | Songea Manispaa | 21 | 6,298 |
| 7 | Namtumbo DC | 02 | 92 |
| 8 | Tunduru DC | 03 | 546 |
| | **JUMLA** | **47** | **15,253** |

Aidha, Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika Idara ya Maendeleo ya Makazi ni kusimamia na kuhakikisha Halmashauri za Mbinga Mji na Tunduru wanaanza mchakato wa kuandaa Mpango Kabambe (Masterplan) katika miji hiyo, pia malengo tuliyopangiwa na Wizara kwa mwaka huu wa fedha ni pamoja na kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro 40 na kurasimisha makazi

holela mijini viwanja 1,200.Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2022 jumla ya michoro ya mipango miji 4 imeidhinishwa, ikiwa na jumla ya viwanja 1,620 vya matumizi mbalimbali.

**UMILIKISHWAJI ARDHI NA USAJILI WA HATI**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya miamala **831** ikiwemo ya rehani na uhamisho wa milki imesajiliwa pamoja na Hati Milki **1,191** zimeandaliwa na kusajiliwa. Pia kuanzia Julai 2022 hadi Novemba 2022 jumla ya miamala **454** ikiwemo ya rehani na uhamisho wa milki imesajiliwa pamoja na Hati Milki **554** zimeandaliwa na kusajiliwa. Jedwali hapo chini linatoa mchanganuo wa utekelezaji Hatimiliki kwa mwaka 2021/2022 pamoja na mwaka wa fedha 2022/2023 kuanzia tarehe 1 Julai hadi Novemba 2022.

**Jedwali Na. 102: Utekelezaji wa hati milki**

| NA | HALMASHAURI | IDADI YA HATI | |
|---|---|---|---|
| | | 2021/2022 | JULAI-NOVEMBA 2022 |
| 1 | Mbinga DC | 70 | 44 |
| 2 | MbingaTC | 275 | 76 |
| 3 | Songea MC | 479 | 295 |
| 4 | Namtumbo DC | 20 | 27 |
| 5 | Madaba DC | 45 | 13 |
| 6 | Songea DC | 86 | 16 |
| 7 | Nyasa DC | 129 | 38 |
| 8 | Tunduru DC | 87 | 45 |
| | **JUMLA** | **1,191** | **554** |

**UTHAMINI**

Taarifa za Uthamini 505 za madhumuni mbalimbali zenye thamani ya Tshs. 76,550,228,850 /= zimeidhinishwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Novemba 2022 kwa mchanganuo ufuatao:-

**Jedwali Na. 103: Taarifa za Uthamini**

| NA. | HALMASHAURI | JULAI 2021 HADI JUNI 2022 | JULAI 2022 HADI NOVEMBA 2022 |
|---|---|---|---|
| 1. | Songea Manispaa | 96 | 42 |
| 2. | Songea DC | 6 | 3 |
| 3. | Mbinga Mji | 32 | 15 |
| 4. | Mbinga DC | 4 | 3 |
| 5 | Tunduru DC | 5 | 5 |
| 6 | Madaba DC | 4 | 3 |
| 7 | Nyasa DC | 7 | 8 |
| 8. | Namtumbo DC | 4 | 2 |
| 9. | Makampuni Binafsi | 190 | 76 |
| **JUMLA** | | **348** | **157** |

**MIGOGORO YA ARDHI**

Ofisi ya Ardhi Mkoa imepokea na kushughulikia migogoro ya Ardhi mbalimbali inayohusu mipaka ya Kijiji na Kijiji, mipaka ya Vijiji na maeneo ya Uhifadhi, migogoro inayotokana na ucheleweshwaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi, migogoro kati ya wamiliki wa ardhi na Halmashauri pamoja na migogoro kati ya Taasisi na Taasisi. Miongoni mwa migogoro hiyo kwa sehemu kubwa imeshughulikiwa na kumalizika.

**MAKUSANYO YA MADUHULI YA SERIKALI**

Tumeendelea kuhamasisha ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kwa kushirikiana na Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma. Katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Mkoa

waRuvuma ulipangiwa lengo la kukusanya jumla ya **Tshs. 3,000,000,000/=** ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022, jumla ya **Tshs. 1,450,244,369/=** zilikusanywa sawa naasilimia **48** ya lengo.

Aidha katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mkoa umepangiwa kukusanya jumla ya **Tshs. 3,000,000,000/=**. Hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2022, jumla ya **Tshs. 767,008,107.82/=** zimekusanywa kutokana na Kodi ya pango la Ardhi na tozo mbalimbali za Ardhi sawa na asilimia 25.6%. Mikakati ya kuongeza makusanyo ya kodi ya Ardhi pamoja na maduhuli mengine yatokanayo na Ardhi ikiwemo kutoa elimu ya ulipaji kodi, kuandaa na kusambaza ankara za umilikishaji na kutoa Hati za madai ya kodi inaendelea katika Halmashauri zote kama ilivyoelekezwa na Wizara.

## 3.0 HITIMISHO

Kwa namna ya pekee tunatoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuendelea kutupa ushirikiano tangu Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Ruvuma ianzishwe. Tunawashukuru pia, Wakuu wote wa Wilaya na Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), wadau mbalimbali, Taasisi mbalimbali pamoja na watumishi wote wa Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma pamoja na watu binafsi kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia tangu kuanzishwa rasmi kwa Ofisi ya Ardhi Mkoa, tunawashukuru sana. Tunaomba tuendeleena ushirikiano huu.

## 7.10 IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI MKOA WA RUVUMA - WIZARA YA MAMBO YA NDANI

### TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI MKOA WA RUVUMA - WIZARA YA MAMBO YA NDANI

### 1.0 UTANGULIZI

**Idara ya Huduma za Uangalizi** chini ya **Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi** inasimamia na kuratibu utekelezaji wa Adhabu Mbadala ya Gereza kupitia **Sheria ya Huduma kwa Jamii Na.6/2002, (The Community Service Act, No.6 of 2002)** ambapo mfungwa anatumikia adhabu yake kwenye jamii kwa kufanya kazi za kijamii katika ofisi ya serikali atakayopangiwa kwa **masaa manne (04) kwa siku kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa**. Pia Idara inasimamia **Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia Sura 247, Marejeo ya Mwaka 2002 (The Probation Act, CAP. 247 RE: 2002)**

Lengo ni kupunguza msomangano Magerezani na kuipunguzia serikali gharama za kuwahudumia wafungwa wakiwa gerezani. Pia kuimarisha mahusiano ya kifamilia kwa kupunguza madhara ambayo familia ingeweza kupata pale mtu anayetegemewa na familia (breadwinner) anapofungwa gerezani.

### 2.0 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA IDARA

Mpaka sasa katika utekelezaji wa kazi za Idara katika mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kuzifikia Wilaya zifuatazo ni: -

- Wilaya ya Songea Vijijini,
- Manispaa ya Songea,
- Wilaya ya Mbinga
- Wilaya ya Madaba
- Wilaya ya Namtumbo

Wilaya ambayo hatujaifikia ni Tunduru.

Katika kipindi cha Julai 2021 mpaka Novemba 2022, Idara ya Huduma za Uangalizi Mkoa wa Ruvuma imetekeleza majukumu yake kwa kuratibu na kusimamia adhabu ya kifungo mbadala ya Gereza kupitia **Sheria ya Huduma kwa JamiiNa.6/2002, (The Community Service Act, No.6 of 2002) ambapo jumla ya wafungwa mia moja themanini na mmoja (181)** wameingizwa kwenye programu:

- Wanaume wakiwa **mia moja arobaini na wawili (142)**, kati yao wanne wametokea Magereza na waliobaki wametokea mahakamani
- Wanawake **thelathini na tisa (39)** wawili wametokea gerezani na waliobaki wametokea mahakamani.

Idadi taarifa za uchunguzi wa kijamii zilizoandaliwa ni **198**

Zilizofanikiwa ni **181**

Zinazosubiri maamuzi ni **0**

Zilizofanikiwa ni **17**

Idadi ya wafungwa waliorudishwa kwenye Jamii baada ya kumaliza adhabu zao:

Wanaume = **104**

Wanawake = **28**

**Jumla = 132**

Idadi ya wafungwa wanaoendelea na kifungo katika taasisi mbalimbali za serikali:

Wanaume = **39**

Wanawake= **09**

**Jumla ya wafungwa wote = <u>48</u>**

## USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA WAFUNGWA KWENYE MAENEO YA KAZI/ WANAYOISHI.

Idara inandelea kuwafuatilia wafungwa katika taasisi mbalimbali za serikali ilizowapangia, kwaajili ya kujua mwenendo wao kitabia na kuendelea kutoa ushauri nasaha na nasihi ili waweze kurekebishika kitabia na kuwa watu wema katika jamii zao

Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Novemba 2022

- Idadi ya Wafungwa waliokiuka masharti na kupewa onyo –wanne, wote wanaume
- Idadi ya wafungwa waliorudishwa gerezani kwa kukiuka masharti - Hakuna.
- Idadi ya wafungwa waliotoroka – Watatu, wanaume 2 na mwanamke, ambao bado wanaendelea kutafutwa
- Idadi ya wafungwa waliofariki - Hakuna.
- Idadi ya wafungwa waliohama kwenda Wilaya nyingine - Hakuna

## UHAMASISHAJI WA KUITANGAZA IDARA YA HUDUMA ZA UANGALIZI MKOA WA RUVUMA.

Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Huduma za Uangalizi kupitia Maafisa Probesheni walishiriki shughuli mbalilmbali ikiwemo kushiriki Wiki ya SHERIA nchini.

## 2.0 MAFANIKIO.

Katika utekelezaji wa kazi wa Programu ya Huduma kwa Jamii, matokeo chanya yamepatikana katika Idara

- Wafungwa kubadilika kitabia na kimatendo na hasa kutambua haki wajibu wao katika jamii
- Familia zimeimarika, watoto wamepata fursa ya kutunzwa na wazazi wote wawili na kupata huduma zote muhimu toka kwa wazazi wao

- Pia maafisa wameweza kutoa ushauri nasaha kwa wafungwa na kuwaunganisha wafungwa na taasisi zinazotoa huduma hasa kwa wale wenye mahitaji maalumu, pamoja na kuwaunganisha wafungwa na familia zao pindi wanapomaliza vifungo vyao.

- Taasisi za serikali zimefanikiwa kupata wahudumu hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi.

Kupitia utekelezaji wa Programu ya Huduma Kwa Jamii serikali imeokoa kiasi cha Tsh.**79, 000,000.00** kwa wafungwa 181 kufanya kazi za usafi wa mazingira kwenye Taasisi za serikali. Ikiwa kibarua mmoja angekuwa analipwa Kiasi cha Tsh 5,000 kwa siku. Pia serikali imeokoa kiasi cha Tsh.**39, 500,000.00** za kuwahudumia wafungwa hao tajwa endapo wangekaa gerezani. Hivyo jumla ya Tsh. **118,500,000.00** zimeokolewa.

## 3.0 MATARAJIO.

Katika kuendelea kuitangaza Idara yetu tunatarajia kuomba vipindi vya redio, kwa redio zilizopo mkoa Ruvuma ili kutoa elimu kwa kazi tunazozitekeleza. Pia kuzifikia Wilaya za Mkoa huu ambayo bado hatujazitembelea kwa lengo la kuitambulisha Idara yetu na kuongeza uelewa kwa jamii inayotuzunguka, vilevile kuongeza ufanisi wa kazi katika Mkoa.

### 4.0 CHANGAMOTO

i. Hali ya Kijiografia ya Mkoa inasababisha kutowafikia wananchi kwa wakati katika kutoa Huduma ya Kifungo mbadala ya Gereza, hivyo kusababisha jamii kutokua na uelewa wa kutosha wa namna ya utekelezaji wa vifungo mbadala kupitia Sheria ya Huduma kwa Jamii Na. 6/2002 na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia Sura ya 247, Marejeo ya Mwaka 2002.

ii. Ushirikiano mdogo wa Magereza katika kutekeleza programu za adhabu mbadala kwenye kupendekeza wafungwa ambao wana sifa za kutumikia adhabu zao chini ya Programu ya Huduma kwa Jamii.

iii. Uhaba wa Watumishi ambapo kwa sasa kuna Watumishi wawili wanaofanya kazi Mkoa mzima hivyo kupunguza ufanisi hasa kwenye ukaguzi, ufuatiliaji na usimamizi wa wafungwa wanaopatikana ambapo ukaguzi unafanyika mara chache.

### 5.0 MAPENDEKEZO

kuongezawa rasilimali fedha na rasilimali watu kwa ajili ya kuzifikia wilaya ambazo hazina Afisa Probesheni ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa wafungwa na mahusiano na wadau wengine kama Magereza, Mahakama na Polisi katika Wilaya hizo.

## 7.11 TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMABA NA RUSHWA (TAKUKURU)

## TAARIFA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA KWA MAENDELEO YA MKOA WA RUVUMA.

### 1. UTANGULIZI

Mapambano dhidi ya rushwa yanaendelea kuwa ni agenda ya kudumu katika shughuli za maendeleo Mkoani Ruvuma. Adhma hii inatokana na Rushwa kuendelea kuwa kikwazo kikubwa katika maendeleo ya nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania kwani rushwa inadhuru uwezo wa mtu

Rushwa ni matokeo ya uozo wa kimaadli (a moral decay) inayomsukuma mtu kufanya jambo lenye sura ya uhalifu na ni kosa kiimani. Matendo haya yote maovu yanadhibitiwa na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 chini ya Usimamizi wa Taasisi ya Kuzuia Na kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

### 2. UCHUNGUZI NA MASHTAKA.

TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imeendelea kupambana na vitendo vya rushwa ambapo kwa kipindi cha kutoka Januari 2022 hadi kufikia Novemba 2022, taarifa /malalamiko yaliyopokelewa yalikuwa ni **168** ambapo taarifa zote zilifanyiwa kazi,

kati ya hizo taarifa **77** hazikuhusu rushwa kabisa na walalamikaji walishauriwa kwenda mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao, pia kati ya taarifa hizo taarifa zilizohusu rushwa ni **91** ambapo zote zilichunguzwa na majalada **33** kati ya hayo uchunguzi wake ulikamilika, kesi mpya **7** zilifunguliwa na **3** zinaendelea mahakamani, Aidha uchunguzi kwa kipindi hicho ulihusu zaidi ubadhilifu kwenye manunuzi ya umma, na ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa njia ya POS.

1. **UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.**

Serikali kupitia TAKUKURU hapa mkoani Ruvuma imefanya kazi ya uchambuzi wa mifumo pamoja kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma kwenye miradi **31** yenye thamani ya shilingi **5,439,978,723.72 Bilioni tano milioni mia nne thelathini na tisa laki tisa sabini na nane mia saba ishirini na tatu na senti sabini na mbili** kazi hizo zilifanyika katika sekta zaelimu, barabara, maji ujenzi na miundombinu. Katika miradi hiyo iliyofuatiliwa/kaguliwa mradi miwili imefunguliwa majalada ya uchunguzi, na miradi iliyokuwa na kasoro ndogondogo kupitia vikao kazi pamoja na kuelimishwa, wahusika walishauriwa namna ya kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo ili ikamilike bila kuwa na mapungufu yoyote.

2. **ELIMU KWA UMMA**

Pia Serikali kupitia TAKUKURU mkoa wa Ruvuma imeendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ambapo kwa kipindi hicho imeweza kuimarisha klabu 216 za wapinga Rushwa mashuleni, imetoa semina **67** kwa makundi mbalimbali, imefanya mikutano **89** ya hadhara kwa wananchi sehemu mbalimbali, imefanikiwa kufanya maoneshao **4** kurusha vipindi **9** redioni na kuandaa press 4 kwa wamahabari za mapambano dhidi ya Rushwa.

**Uwezo wa kuidhibiti Rushwa tunao kinachokosekana ni utashi wetu wa kupambana na adui huyu rushwa. Siku zote tukumbuke kuwa, rushwa ni Adui wa Haki na ni Adui wa Maendeleo yetu.**

## 7.12 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA MKOA WA RUVUMA

## TAARIFA FUPI YA UENDESHAJI WA KIWANJA CHA NDEGE CHA SONGEA KWA KAMATI YA USHAURI YA MKOA WA RUVUMA DISEMBA, 2022.

### 1.0 UTANGULIZI.

#### 1.1 Historia Fupi ya Kiwanja:

Kiwanja cha ndege cha Songea ni mmojawapo ya viwanja vya ndege vipatavyo 59 vinavyosimamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania (TAA) kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kiwanja hiki cha ndege, kilijengwa kati ya mwaka 1974 hadi 1980, kikiwa na barabara ya kutua na kurukia ndege ya changarawe iliyokuwa na urefu wa mita 1600 na upana wa mita 30. Lengo kuu la ujenzi wa kiwanja hiki yalikuwa ni kwa ajili ya kuhudumia ndege ndogo na abiria wachache na hata miundo mbinu yake ilikuwa ni kwa ajili ya kuhudumia abiria wachache kwa mfano hata jengo la abiria tunalolitumia hivi sasa lilijengwa mwaka 1980 halikidhi matakwa ya sasa ya kisheria kwa matumizi ya kukagulia abiria, kwa kuwa linachukua abiria wachache.

Ilipofika mwaka 2018, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitenga kiasi cha fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Songea. Uwanja huu kwa sasa umeshakarabatiwa barabara ya kurukia na kutulia ndege na kufikia urefu wa mita 1860 na upana wa meta 30 na kwa sasa unaruhusu ndege za saizi ya kati aina ya Bombardier Q400 kutua pia, kuna matarajio makubwa ya kupata mashirika mengine ya ndege ilhali, jengo tunalolitumia kuhudumia abiria limebakia ni lile lile la mwaka 1974/1980 hivyo halitoshelezi wingi wa abiria wanaojitokeza kupanda ndege kwa sasa.

#### 1.2 Jiografia ya Kiwanja:

Kijiografia, kiwanja cha ndege Songea kiko umbali wa kilomita 09 upande wa magharibi mwa mji wa Songea. Eneo la Kijiografia liko kwenye '*Coordinates*' 104055.01S 0353455.62E; Hali ya mwinuko ni futi 3480 kutoka usawa wa bahari na hali ya hewa ni nyuzi joto 25.9$^{0}$C.

Kiwanja cha ndege cha Songea kinapakana na Mtaa wa Lupapila upande wa Magharibi, upande wa Kusini kinapakana na Mtaa wa Namanditi, Kaskazini kimepakana na Mtaa wa Lilambo na Mashariki kimepakana na Mtaa wa Ruhuwiko.

## 2.0 UENDESHAJI WA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KIWANJANI (OBJECTIVES C& D)

Katika Mpango Mahususi wa utekelezaji wa mwaka wa fedha 2021/2022, kiwanja cha Ndege cha Songea kimejikita katika kutekeleza Malengo Mkakati C and D kama ilivyo elekezwa katika Mpango Mkakati wa Mamlaka wa miaka mitano 2021/2022- 2025/2026 na lengo hili linahusu:

a) Uimarishaji usalama (*safety*) na utunzaji mazingira kulingana na miongozo ya Shirika la kimataifa (*ICAO*) linalosimamia usafiri wa anga kwa kufuata miongozo yake (*Annex 14 na Annex 16*).
b) Kuimarisha ulinzi na usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Songea kwa Mwongozo wa usalama wa kimataifa "*ICAO Annex 17"* na sehemu ya "*Annex 9"* inayotolewa na shirika la usafiri wa anga la "ICAO" pamoja na Miongozo ya kiusalama ya kitaifa *"The National Civil Aviation Security Programme"* inayotolewa na Mamlaka ya usafiri wa Anga Nchini (*TCAA*).
c) Uwezeshaji wa abiria, ndege na mizigo kwa kufuata Miongozo ya "*ICAO Annex 9"* na ya kitaifa *"The National Civil Aviation Facilitation Programme"* inayotolewa na kusimamiwa na Mamlaka ya Usafiri wa anga (*TCAA*).
d) Utunzaji na Utumiaji wa rasiliamali bora (fedha na watu) kwa kujali utoaji huduma bora kwa watumiaji wa kiwanja cha ndege Songea.

### 2.1 Utendaji Kazi wa Kiwanja cha Ndege:

Kiwanja cha Ndege cha Songea kinafanya kazi kwa saa 12 (Mawio hadi Machweo). Kazi za kila siku za Mamlaka ya Viwanja Ndege ambazo Meneja wa Kiwanja kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu huhakikisha zinafanyika na kuendelea vizuri kwa taratibu na miongozo ya Shirika la usafiri wa anga duniani (***ICAO*)** na zinazosimamiwa hapa nchini na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (***TCAA*)** ni kama ifuatavyo:-

a) Kuratibu na kudhibiti shughuli mbalimbali za usafiri wa anga zinazotekelezwa na taasisi na makampuni mbalimbali, ya kiserikali na yale ya sekta binafsi.

b) Kuhakikisha miundo mbinu yote inafanya kazi vizuri na iko katika viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

c) Kusimamia ulinzi na usalama wa kiwanja, miundombinu yake, ndege zilizopo, abiria na wafanyakazi.

d) Kuratibu na kusimamia mipango ya kuzuia ajali kutokea na pindi inapotokea kudhibiti madhara yake na kuokoa mali na maisha ya wahanga.

e) Kuweka miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa kiwanja (*Standard Operating Procedures*) na kuhakikisha inatekelezwa.

f) Kukusanya mapato ya Serikali kwa niaba ya TAA na mamlaka nyingine tunazotoa huduma pamoja yaani TCAA na TMA.

g) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa maazimio yanayofikiwa na kamati mbalimbali za uendeshaji wa kiwanja kwa lengo la kuboresha huduma bora kwa wateja.

h) Pamoja na shughuli hizi Meneja wa Kiwanja cha ndege cha Songea, anawajibika na usimamizi na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Mbamba Bay na Liuli, vilivyopo katika wilaya ya Nyasa.

**2.2 Hali ya Miundo Mbinu ya kiwanja cha ndege cha Songea:**

Kiwanja cha Ndege Songea kina barabara moja ya kutua na kuruka ndege "*Runway*". Barabara hiyo ina urefu wa mita 1860 na upana wa mita 30, yenye uimara wa *"PCN 50/F/A/Y/T",* njia hii huitwa "14/32", njia hii ya kuruka/kutua ndege ndio inayotumika hivi sasa. Kwa kuwa kiwanja hiki hakina taa za kuongozea ndege nyakati za usiku; hivyo huduma za kiwanja hiki ni muda wa mchana pekee yaani "*sunrise & sunset operations"*.

Pia, kiwanja kina jengo la abiria "*Terminal Building*" moja la kuhudumia abiria waondokao na kuwasili kiwanjani na ukumbi wa watu mashuhuri "*VIP*". Jengo la abiria lina uwezo wa kubeba abiria 50 tu kwa wakati mmoja.

Katika majukumu yetu ya kila siku ya uendeshaji wa kiwanja tunawajibika kuhakikisha kuwa wakati wote miundombinu yote ya kiwanja; i.e barabara ya kutua/kuruka ndege, maegesho ya ndege "*apron*", barabara ya maungio "*taxway*" jengo la kuhudumia abiria, ukumbi wa watu mashuhuri (*VIP Lounge*), na kituo cha Jeshi la zimamoto na uokoaji

yako katika hali nzuri na ya usalama, hivyo tunawajibika kuhakikisha kuwa inafanyiwa matengenezo (*Maintenance*) ya mara kwa mara.

### 2.3 Ukarabati na Upanuzi wa Miundombinu ya Kiwanja cha Ndege Songea

Kwa sasa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia wakala wa barabara nchini (*TANROADS*) ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ukarabati na upanuzi wa miundombinu mbalimbali ya kiwanja cha ndege cha Songea. Ukarabati huo unajumuisha maeneo yafuatayo;

- Kurefusha njia ya kuruka/kutua ndege "*runway*" kutoka mita 1625 za awali mpaka mita 1860,
- Ujenzi wa barabara mpya ya kuingia na kutoka kiwanjani ijulikanayo kama "*taxway*"
- Ujenzi wa jengo la kuongozea abiria yaani "*Control Tower*" Building
- Ujenzi wa maegesho mapya ya ndege "*apron*" yenye ukubwa wa 139m kwa 126m,
- Kuweka taa na alama za kuongozea ndege "*Airfield Ground Lighting & Signages*"
- Manunuzi ya gari la Zimamoto na Uokoaji "Fire Tender" lenye ujazo wa Maji – Lita 10,000 na Foam – 1,200 Kg linaloendana na ukubwa wa ndege inayofanya safri zake katika kiwanja cha ndege cha Songea yaani (Bombardier -Q400)
- Ujenzi wa barabara ya ukaguzi "*Perimeter road*" upande wa ndani na nje ya uzio
- Ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la kutua na kuruka ndege "*Perimeter Inner fence*"
- Ujenzi wa mfumo wa mitaro "*Drainage system*"
- Usimikaji wa mitambo ya kuongozea ndege "*Installation of Navigation Aids and Communication equipments*."

### 2.4 Uendeshaji wa Shughuli za Kiwanja:

Uendeshaji wa kila siku wa kiwanja cha ndege unatekelezwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali kutoka taasisi za umma na sekta binafsi kwa kupitia kamati za kudumu za kiwanja ambazo zimeundwa kisheria. (Sheria na kanuni za TCAA na mkataba wa *ICAO Chicago Convetion*).

Kamati za uendeshaji wa kiwanjani kama zifuatazo:

1. Kamati ya ulinzi (*Aviation Security committee*).
2. Kamati ya uwezeshaji (*Airport Facilitation Committee*)
3. Kamati ya dharura na Uokoajiki wanjani (*Aerodrome Emergency Committee*).
4. Kamati ya usalama katika Eneo la uendeshaji (*Airside Safety Committee*).
5. Timu ya kuboresha Huduma bora kwa wateja (*Customer Service Joint Improvement Team Committee)*.
6. Kamati ya kudhibiti Wanyama na ndege (*Wildlife Management Committee*).
7. Timu ya Menejimenti ya kiwanja (*Management Team*).

Kiwanja cha ndege Songea kiko kwenye daraja la 3C (*Aerodrome Category*) na kina leseni ya uendeshaji kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) katika kutekeleza kanuni za uendeshaji wa viwanja vya ndege (*Civil Aviation (Aerodrome) Regulation of 2007*). Leseni hii ilipatikana baada ya maandalizi ya miongozo na "*program*" mbalimbali ambazo huridhiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA). Miongozo hii ni kama vile "*Airport Security Programme, Air Facilitation Manual, Airport Aerodrome Manual, Airport Emergency Plan na Wildlife Hazards Management Manual"* kwa mujibu wa taratibu hizo leseni hii huhuishwa kila baada ya miaka miwili.

## 2.5 Taasisi na Idara Zilizopo Katika Kiwanja cha Ndege cha Songea

Katika kukamilisha shughuli mbalimbali za huduma ya kiwanja cha ndege cha Songea, kuna taasisi, Idara mbalimbali zikiwemo za Serikali, Makampuni ya watu binafsi ambazo kwa pamoja hushirikiana kwa namna moja au nyingine katika utendaji wa kazi za kila siku kiwanjani. Miongoni mwa Taasisi na Idara hizo ni kama zifuatazo:-

**Jedwali Na. 103: Taasisi na Idara Zilizopo Katika Kiwanja cha Ndege cha Songea**

| NA | JINA LA TAASISI/KAMPUNI | AINA/MMILIKI |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania (TAA) | Wakala wa Serikali |
| 2 | Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) | Wakala wa Serikali |
| 3 | Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) | Wakala wa Serikali |
| 4 | Jeshi la Polisi (Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi) | Serikali |
| 5 | Kampuni binafsi ya Ulinzi ya "M/S 94 Security Services". | Binafsi |
| 6 | Idara ya Usalama wa Taifa | Serikali |
| 7 | Idara ya Uhamiaji | Serikali |
| 8 | Kampuni ya ndege (ATCL) | Serikali |

Jumla ya Watumishi wote wa Umma, Makampuni na Mashirika Binafsi, Waajiriwa wa muda na wale wa mikataba ni 80.

**2.5 Idadi ya Abiria na Safari za Ndege kwa Kipindi cha Mwaka 2011 hadi 2022.**

a) Idadi ya safari za ndege kwa kipindi cha miaka kumi na moja (11) iliyopita, kuanzia mwaka 2011 hadi 2022. Idadi ya safari za ndege imeongezeka kutoka ndege 150 zilizorekodiwa mwaka 2011 hadi kufikia ndege 205 kwa mwaka 2022.

b) Idadi ya abiria waliotumia kiwanja cha ndege cha Songea katika kipindi cha miaka kumi na moja (11) iliyopita imeongezeka kutoka idadi ya abiria 1,620 waliorekodiwa mwaka 2011 hadi kufikia abiria 15,385 waliorekodiwa mwaka 2022; Kama inavyosomeka kwenye jedwali hapo chini.

**Jedwali Na. 104: Idadi ya Abiria na Safari za Ndege kwa Kipindi cha Mwaka 2011 hadi 2022**

| Mwaka | Idadi ya miruko ya Ndege | Idadi ya Abiria |
|---|---|---|
| 2011 | 150 | 1,620 |
| 2012 | 570 | 4,310 |
| 2013 | 544 | 4,075 |
| 2014 | 594 | 4,251 |
| 2015 | 562 | 4,394 |
| 2016 | 592 | 3,961 |
| 2017 | 450 | 9,703 |
| 2018 | 374 | 4,849 |
| 2019 | 418 | 2,905 |
| 2020 | 229 | 1,345 |
| 2021 | 214 | 5,293 |
| 2022 | 205 | 15,385 |
| ***JUMLA*** | **4,902** | **58,231** |

c) Kwa sasa kampuni inayofanya safari zake za ratiba maalumu (*Scheduled flight*) katika kiwanja cha ndege cha Songea ni kampuni ya ndege ya *ATCL* inayofanya safari zake mara tatu kwa wiki kwa siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa.

## 3.0 ULINZI NA USALAMA KIWANJANI:

### 3.1 Mitambo ya ulinzi na elimu kwa watumiaji

Ili ndege na abiria waweze kutumia kiwanja chochote cha ndege, ulinzi na usalama ni suala la muhimu sana. Kwa kutambua hili, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imeimarisha usalama wa kiwanja kwa kununua mitambo ya kisasa ya kukagua abiria na mizigo. Tunayo mashine moja ya *"X-Ray Machine"* na *"Walk through Metal Detectors"* mbili (02) na mitambo ya mkononi yaani; *"Hand Held Metal Detectors"* sita (06). Sambamba na uwekaji wa mitambo hii pia tunawapatia Maafisa Usalama mafunzo maalumu ya jinsi ya kutumia mitambo hii na wamekuwa wakifanyiwa mitihani ya kuwa na leseni maalumu *"Recertification"* ambazo

hutolewa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*). Kutokana na kuwepo kwa mitambo hii ya kudhibiti usalama wa abiria pamoja na umakini wa wana usalama hapa kiwanjani tumefanikiwa kudhibiti matukio yanayoweza kuhatarisha usalama wa abiria na ndege kupitia kiwanja hiki.

Kwa sasa kitengo hiki cha usalama kina wafanyakazi wapatao tisa (09) kati yao watano (05) ni kutoka Jeshi la Wananchi (*JWTZ*) na wanne (04) ni kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*).

### 3.2 Huduma ya Zimamoto na Uokoaji Kiwanjani.

Kiwanja cha ndege Songea kinatoa huduma za zimamoto katika kiwango cha zimamoto (Fire Service Cat. 3). Tunalo gari la zimamoto (*Fire Tender*) lenye ujazo wa maji (*1,000 Litres*) na madawa (*100Kg*) pia lina *dry powder* (*250 Kgs*). Katika kitengo hiki kuna jumla ya askari wa zimamoto wapatao tisa (09) wenye ujuzi na mafunzo stahiki. Aidha, kiwanja kina mfumo wa majisafi yaliyounganishwa na SOUWASA ambayo yanatumika kwa shughuli za usafi wa mazingira yanayozunguka kiwanja hiki.

## 4.0 MTAZAMO WA MAENDELEO YA KIWANJA

### 4.1 Fursa za uwekezaji:

Mara baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa ukarabati na upanuzi "*Rehabilitation & Upgrading of Songea airport*" kiwanja cha ndege cha Songea kitakuwa na fursa za kipekee kabisa kwa kushirikisha sekta binafsi na makampuni katika kukiendeleza kibiashara kama vile: -

- Ujenzi wa eneo la kibiashara (*Business center*)
- Uendeshaji wa maduka (*Duty free shops*)
- Majengo ya kutengenezea ndege (*Aircraft maintenance hangars*)
- Jengo kubwa la kuhifadhia mizigo (*Cargo Terminal*)
- Ujenzi wa maduka ya bidhaa mbali mbali (*Trade centre/shopping complex*)

- Ujenzi wa migahawa ya kisasa.
- Ujenzi wa visima vya mafuta ya ndege (*fuel farms*)

Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inawakaribisha Wafanyabiashara na wadau wote wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza kwenye nyanja zilizo tajwa hapo juu. Tunatoa rai kwa wafanyabiashara wote wa mkoa wa Ruvuma na mikoa ya jirani kutumia fursa kubwa za uwepo wa Kiwanja cha ndege cha Songea kwa usafiri wa anga, pamoja na kusafirisha bidhaa za kilimo n.k.

## 4.2 Matarajio ya baadae ya kiwanja.

- Baada ya kukamilika kwa mradi wa ukarabati na upanuzi wa kiwanja unaoendelea, kiwanja kitapandishwa hadhi kutoka kiwanja kidogo cha ndani (*Small Domestic Airport*) na kuwa Kiwanja kikubwa cha ndani (*Major Domestic Airport*) na hivyo idadi ya safari za ndege za ndani zitaongezeka, hasa kutokana na ukweli kuwa kiwanja kitaweza kutoa huduma zake kwa masaa 24 (Usiku na mchana) baada ya kufungwa taa za kuwezesha ndege kutua hata usiku.
- Sekta ya Utalii itakua zaidi kwani Watalii wengi watatumia Kiwanja hiki kwa ajili ya kutembelea mbuga za wanyama za Nyerere (Selous), fukwe za Mbambabay zilizoko katika ziwa la Nyasa, Makumbusho ya vita vya maji maji yaliyopo mjini Songea.
- Kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji wa madini mbalimbali kutachangia kwa kiasi kikubwa zaidi ukuaji wa uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.
- Kukuza pato la mkoa kutokana na mapato mbalimbali yatakayo tokana na huduma za usafiri wa anga.
- Fursa za ajira zitaongezeka kwa wakazi wa mkoa wa Ruvuma na mikoa ya jirani.
- Maisha ya mkazi mmoja mmoja yataboreka kufuatia kuongezeka kwa Mzunguko wa pesa.
- Pia, mkoa wa Ruvuma utazidi kujitangaza kimataifa kufuatia uwepo wa kiwanja cha ndege cha Songea.

- Kwa kuwa hali ya hewa ya mkoa wa Ruvuma inaruhusu ustawishaji wa maua, mbogamboga na matunda hivyo basi uwepo wa kiwanja hiki utatoa fursa ya usafirishaji wa mazao hayo kwa urahisi zaidi.
- Kutakuwa na fursa zaidi kwa Wafanyabiashara kuwekeza kwenye kiwanja cha ndege cha Songea.

## 5.0 CHANGAMOTO MBALIMBALI ZA KIWANJA CHA NDEGE CHA SONGEA.

### 5.1 Kuongezeka kwa Abiria kunapelekea kuibua kwa Changamoto ya kutotosheleza abiria katika ukumbi wa Kuondoka na kuwasili hapa kiwanja cha ndege Songea.

Tangu kuanza kwa Safari za Shirika la Ndege za ATCL katika kiwanja Cha Ndege cha Songea, kumekuwa na ongezeko kubwa la abira wanaotumia kiwanja hiki, wakati mwingine abiria hufikia hadi 72 wanao Ondoka na 74 wanao Wasili kwa wakati mmoja ambapo kwa sasa Shirika la Ndege la ATCL limeongeza Safari zake kutoka mara Mbili kwa wiki hadi mara Tatu kwa wiki kwa siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa.

Kuongezeka kwa abiria hao kunapelekea kuibua kwa Changamoto ya kutotosheleza abiria katika ukumbi wa Kuondoka na kuwasili abiria hapa kiwanjani. Ukumbi wa kuwasili abiria kwa sasa umekuwa Finyu sana hasa kutokana na idadi hiyo kubwa ya abiria iliyoongezeka, hivyo hupelekea abiria kusimama Nje ya Ukumbi pindi wanapo subiria mizigo yao.

Pia, pindi msimu wa Mvua unapo anza kama ilivyo sasa, huongeza Changamoto na usumbufu hasa kwa abiria wanaowasili kwa kuwa eneo la ukumbi wa kuwasili abiria ni dogo mno ambalo huweza kuchukua abiria 10 kwa wakati mmoja ikiwa ndege huweza kushusha hadi abiria 50-72. Pia eneo la kusubiri “Waiting area” kwa abiria na wasindikizaji liko finyu sana pia ni sumbufu wakati wa mvua kwa abiria wanaokaa eneo hilo kabla ya ukaguzi (Check in) wa abiria kuanza.

### 5.2 Umbali wa Kutoka Jengo la Abiria na Eneo la Maegesho Mapya ya Ndege “Apron”.

Ukarabati na upanuzi wa miundombinu mbalimbali ya kiwanja cha ndege cha Songea, umehusisha pia ujenzi wa eneo jipya la maegesho ya Ndege “Apron” yenye ukubwa wa Mita za Mraba 17577 lenye uwezo wa kuegesha ndege zipatazo sita (06) aina ya Bombardier Q-400 kwa wakati mmoja.

Ujenzi wa eneo jipya la maegesho ya ndege ni mbadala wa eneo la zamani la maegesho ya Ndege ambalo limechakaa kwa sasa na halitumiki tena kwa shughuli za kuegesha ndege kwani njia yake

inayounganisha Njia ya Miruko imefungwa hii ni kutokana na “Design” ya ujenzi unao endelea. Hivyo ndege zote kwa sasa zinatumia eneo jipya la maegesho ambalo lipo umbali wa takribani 150m kutoka kwenye jengo la abiria (Depatrure Lounge), umbali huu husababisha usumbufu mkubwa kwa abiria hasa wazee na wagonjwa.

Kuharakishwa kubadilishwa kwa jengo jipya analotumia Mhandisi mshauri kwa sasa “*Conversion of Engineer’s Office into Temporary Terminal/Passenger’s Building*” kutasaidia sana kuondoa changamoto ya umbali na Usumbufu kwa abiria kwani eneo jipya la maegesho lipo jirani sana na jengo analotumia Mhandisi mshauri ambalo linategemewa kutumika kama jengo la abiria kwa siku za usoni.

### 5.3 Ufinyu wa eneo la maegesho ya Magari.

Eneo la maegesho ya magari lililopo katika kiwanja cha ndege cha Songea ni finyu sana, kwani maegesho haya kwa sasa yana uwezo wa kuegesha magari yapatayo 15 tu kwa wakati mmoja ikiwa mahitaji ya sasa ni magari 40 - 45 kwa wakati mmoja kwa siku za ujio wa ndege hapa kiwanjani, hivyo hupelekea msongamano mkubwa wa magari kwenye eneo la maegesho hayo.

## 6.0 Hitimisho.

Changamoto nyingi zilizo ainishwa hapo juu kwa sasa, utatuzi wake ni kuharakishwa upatikanaji wa jengo jipya la abiria ambalo kwa sasa linatumiwa na Mhandisi mshauri kutokana na sababu zifuatazo:

a) Jengo hili litakuwa na eneo kubwa kwa ajili ya abiria wanaoondoka na kuwasili kutokana na mtiririko wa abiria ulivyo kwa sasa ambao 50-72.

b) Jengo jipya litasaidia kuondoa changamoto ya ukarabati wa mara kwa mara kutokana na uchakavu wa majengo uliopo sasa, lakini si hilo tu pia utabadilisha muonekano mzima wa mandhari ya kiwanja cha ndege cha Songea.

c) Upatikanaji wa Jengo jipya kutaondoa changamoto ya umbali wa kutoka kwenye jengo hadi katika eneo la maegesho ya ndege (Apron) ambapo abiria hupanda na kushuka kwani jengo hili halipo mbali sana na eneo hilo.

d) Jengo Jipya linalotumiwa na Mhandisi mshauri kwa sasa tayari lina Vyumba kadhaa ambavyo kwa “*Design*” vitatumika kama vyumba vya biashara baada ya kukamilika kwake.

e) Hata Ufinyu wa eneo la maegesho ya magari utaisha kabisa kutokana na mahitaji ya sasa kwani mbele ya jengo hili kuna eneo kubwa ambalo linaweza fanyiwa matengenezo na kuweza kutumika kama eneo la maegesho ya magari.

Hivyo, uongozi wa kiwanja cha Ndege Songea na wadau mabalimbali wanaotumia kiwanja hiki wanaiomba Serikali, kuharakisha upatikanaji wa jengo hilo na kufanyiwa matengenezo kutokana na mahitaji yetu ya sasa na baadae ili kuondoa kadhia mbalimbali zinazojitokeza hapa kiwanjani katika shughuli za kiusalama na uendeshaji wa kiwanja.

## 7.13 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA) – OFISI YA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI

## CHIMBUKO LA UDHIBITI, MAJUKUMU YA EWURA NA NYENZO ZA UDHIBITI KAZI ZILIZOFANYIKA MKOA WA RUVUMA KATI YA JANUARI 2022 MPAKA DISEMBA 2022

### 1. CHIMBUKO LA UDHIBITI NA EWURA

- Chimbuko la Udhibiti nchini Tanzania ni mageuzi ya uchumi na Sera ya Ushindani na Udhibiti ya 1999. Sera hiyo inatambua kwamba:
    - **sekta binafsi** inatoa mchango mkubwa kwenye uchumi;
    - taasisi za Umma **zijiendeshe kibiashara**;
    - **ushindani** ndio **utakaochochea uwekezaji** na uangalizi wa uchumi huru wa soko.
- Kuanzishwa kwa Mamlaka za udhibiti: **EWURA** (Nishati na Maji), **TCRA** (Mawasiliano), **LATRA** na **TASAC** (Usafiri nchi kavu na majini; zamani **SUMATRA**), **TCAA** (Usafiri wa anga), **FCC** (Tume ya Ushindani) na **FCT** (Mahakama ya Ushindani)
- EWURA ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 4 ya **Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania** na ilianza kufanya kazi Septemba 2006;
- EWURA inadhibiti sekta kuu mbili, ambazo ni **Sekta ya Nishati** na **Sekta Maji**.

- Kwenye sekta ya **Nishati** kuna sekta ndogo ya **Gesi Asilia, Sekta ndogo ya Umeme** na **Sekta ndogo ya Mafuta jamii ya Petroli**.

- Katika **Sekta ya Maji**, Mamlaka ya EWURA ipo katika kudhibiti Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zilizopo katika **Miji/Majij**i ya Makao Makuu ya **Mikoa**, **Wilaya** na **Miji Midogo** ya Wilaya.

## 2. MAJUKUMU YA EWURA

- Majukumu ya Mamlaka yameainishwa katika Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania kuwa ni:
- Kutoa leseni kwa watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa
- Kupanga au kuidhinisha bei na tozo katika sekta zinazodhibitiwa
- Kuweka viwango vya bidhaa na huduma kwa kushirikiana na TBS
- Kusimamia utoaji huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo husika
- Kuzingatia usalama na uhifadhi wa mazingira wakati wa kutoa huduma
- Kuelimisha wananchi kuhusu masuala yanayodhibitiwa na Mamlaka.
- Kutatua migogoro kati ya mtoa huduma na mpokea huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka.

## 3. OFISI YA KANDA YA NYANDA ZA JUU

- Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inapatikana Jijini Mbeya, Mtaa wa Karume kwenye jengo la NHIF, Ghorofa ya sita.
- Ofisi hiyo inahudumuia Mikoa sita (6):
    - i. Mbeya (Wilaya 5)
    - ii. Songwe (Wilaya 4)
    - iii. Rukwa (Wilaya 3)

iv. Katavi (Wilaya 3)
v. Njombe (Wilaya 4)
vi. Ruvuma (Wilaya 5)

## 4. UDHIBITI KATIKA SEKTA YA UMEME

- ❑ EWURA inasimamia shughuli ya Kiufundi na Kiuchumi katika Sekta ya Umeme katika Mikoa yote sita ya kanda hii.

- ❑ Katika **Mkoa wa Ruvuma** mtoa huduma mkubwa wa nishati hiyo ni TANESCO.

- ❑ Mkoa wa Ruvuma pia una wazalishaji wengine wadogo wa Umeme kama vile **Tulila** ambae huzalisha **megawati 5**, **Andoya** huzalisha **megawati 1**, **Madaba Electrical group** ambae huzalisha kilowati zisizozidi **200.**

- ❑ Hawa wazalishaji wadogo wa umeme hufanya biashara ya kumuuzia umeme TANESCO pamoja na wananchi wanaoishi karibu na maeneo yanayozunguka wazalishaji hao.

- ❑ TANESCO na wazalishaji hao wengine hufanyiwa **ukaguzi** wa kila mwaka kwa kuangalia kuwa anazingatia viwango vya kiufundi kwenye miundo mbinu yake na pia viwango vya utoaji huduma kwa wateja wake

- ❑ EWURA katika kipindi cha Januari mpaka Novemba 2022 imefanya ukaguzi wa waleseni wake:

    i. Ukaguzi wa miundombinu ya TANESCO Mkoa wa Ruvuma (15 to 24 Machi 2022).

    ii. Ukaguzi wa Miundombinu ya Wazalishaji Umeme ya TULILA waliopo MBINGA (Machi 2022).

    iii. Ukaguzi wa Miundombinu ya Wazalishaji na wasambazaji umeme ya ANDOYA waliopo MBINGA (Machi 2022).

- ❑ EWURA pia inatoa leseni kwa mafundi umeme wa kazi mbalimbali.

- ❑ Kwa Mkoa wa Ruvuma kuna jumla ya mafundi umeme **109 wenye leseni *(ikilinganishwa na 35 mwaka uliopita).***

i. Daraja A - 2

ii. Daraja B - 3

iii. Daraja C - 62

iv. Daraja D - 41

v. Daraja W – 1

- **CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA UMEME**

  Uwepo wa kundi kubwa la mafundi umeme (vishoka) ambao hawana vyeti vya kitaaluma vitakavyowawezesha kuomba leseni zinazotolewa na Mamlaka.

## 5. UDHIBITI SEKTA YA MAFUTA YA PETROLI

- EWURA inadhibiti Sekta ya mazao ya mafuta ya petrol (diseli, **petrol**, mafuta ya taa pamoja na gesi za LPG).

- Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ina jumla ya Vituo vya Wauzaji mafuta wa rejareja (***Retail outlets***) **301** hadi kufikia November 2022.

- Idadi hiyo inajumuisha Watumiaji binafsi wa mafuta (***Consumer Installation***), Viwanda vidogo vya kujazia gesi ya kupikia majumbani (***LPG refilling***) na Wasambazaji wa gesi ya kupikia majumbani (***LPG distributors)***

- Katika Mkoa wote wa Ruvuma, kuna **vituo (facilities) 52** kama ifuatavyo:

  i. Vituo vya Wauzaji mafuta wa **rejareja** (***Retail outlets***): **46**

  ii. Watumiaji **binafsi** (***Consumer installation***): **2**

  iii. Viwanda vidogo vya kujazia gesi ya majumbani (***LPG refilling plants***): **1**

  iv. Wasambazaji wa gesi ya kupikia majumbani (***LPG distributors***): **3**

- Katika kipindi cha kuanzia January mpaka November 2022, EWURA ilifanya **ukaguzi wa kawaida** (**Compliance monitoring**) kwenye mkoa wa Ruvuma na **kukagua vituo vya mafuta 15**.

- Kati ya hivyo:

    v. **Vituo 9** havikuwa na makosa yoyote;

    vi. **Vituo 3** vilikuwa na *makosa mbalimbali*;

    vii. **Vituo 3** vilikuwa havifanyi kazi (under construction)

- **Muhtasari wa Vituo na Ukaguzi uliofanyika**

- **Jedwali Na. 104: Muhtasari wa Vituo na Ukaguzi uliofanyika**

| Na. | Maelezo | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Jumla ya vituo Mkoani Ruvuma | **52** |
| | Wauzaji mafuta wa rejareja | 46 |
| | Watumiaji binafsi | 2 |
| | Kujaza gesi ya majumbani (LPG) | 1 |
| | Wasambazaji wa gesi (LPG) | 3 |
| 2 | Vituo vilivyokaguliwa ukaguzi wa kawaida (**compliance monitoring**) | **16** |
| 3 | Vituo vilivyokaguliwa ukaguzi wa kabla ya leseni (pre-licence inspection) | **7** |
| 4 | Leseni zilizotolewa kati ya Januari na Novemba 2022 | **9** |
| 5 | Vibali vya Ujenzi vilivyotolewa na EWURA (**construction approval**) | **3** |

- Katika kipindi cha kuanzia Januari mpaka November 2022, EWURA ilifanya **ukaguzi wa VINASABA** (**Fuel Marker**) na **kukagua vituo vya mafuta 7**. Kati ya hivyo:

    i. **Vituo 6** havikuwa na makosa yoyote;

    ii. **Kituo kimoja (1)** kilikuwa na makosa na hivyo kuadhibiwa

- Pia, EWURA ilifanya ukaguzi wa ubora wa mafuta (Fuel quality) kwenye mkoa wa Ruvuma na **kukagua vituo vya mafuta 14**. Kati ya hivyo: **Kituo kimoja (1)** kilikuwa na makosa na hivyo kuadhibiwa

- **CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA MAFUTA**

i. Baadhi ya Vituo vya mafuta **kujengwa bila kufuata utaratibu wa ujenzi** na baadhi kutokidhi mahitaji ya leseni.

ii. Ushauri wa EWURA ni kwamba Halmashauri / Manispaa husika ziangalie namna bora ya kushirikiana na EWURA na wadau wengine katika kuhakikisha ujenzi unakuwa na vibali husika (EWURA, NEMC na Manispaa / Halmashauri wanaotoa hati ya umiliki wa ardhi)

## 6. UDHIBITI SEKTA YA MAJI

- Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inasimamia **Mamlaka za Maji 20**.
- Kati ya Mamlaka hizo 20, **Mamlaka 6** ni Mamlaka za Maji zilizoko kwenye Makao Makuu ya Mikoa,
- Mamlaka moja ni Mamlaka ya **Mradi wa Kitaifa** (Wanging'ombe) na
- **Mamlaka 13** ni za Makao Makuu ya Wilaya na Miji midogo.
- Mkoa wa Ruvuma una Jumla ya Mamlaka za Maji na Usafi wa mazingira **nne (4).**
- Kati ya Mamlaka hizo, Mamlaka moja ni Mamlaka iliyopo Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma (yenye makao yake makuu hapa Manisapa ya Songea)
- Mamlaka nyingine tatu ni zilizopo katika miji ya Wilaya za Mbinga, Namtumbo na Tunduru.
- Kwa Wilaya ya Nyasa, huduma ya Maji hutolewa na RUWASA kwa kuwa Wilaya hiyo bado haina Mamlaka kwa sasa
- Katika sekta ya Maji kuna UKAGUZI aina nne:

  i. Ukaguzi maalum (**special inspection**) - utendaji usioridhisha wa Mamlaka,

  ii. Ukaguzi wa kawaida wa utendaji (**compliance monitoring**) - ukaguzi unahusisha kuangalia miuodombinu, ikiwemo uunganishaji wa wateja wapya na ubora wa huduma kwa mteja),

iii. Ukaguzi wa kuhakiki taarifa (**data verification**) – kama sehemu ya maandalizi ya kuandika Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka

iv. Ukaguzi wa ubora wa maji (**water quality monitoring**)

Katika kipindi cha Januari mpaka Novemba 2022 ukaguzi ulifanyika kama ifuatavyo:

- Ukaguzi **wa kawaida** wa utendaji wa Mamlaka (**compliance monitoring**) – kwa Mamlaka ya Maji ya **Songea**
- **Ukaguzi wa ubora** wa maji (**water quality monitoring**) kwa Mamlaka za maji za **Songea**, **Mbinga** na **Tunduru**.
- **Ukaguzi wa kuhakiki taarifa** (**data verification**) kwa Mamlaka za **Tunduru**, **Namtumbo** na **Mbinga**
- Pia Mchakato wa **kuidhinisha bei** ulifanyika kwa **Mamlaka ya Songea** ***(matokeo yatatangazwa karibuni)***

- **CHANGAMOTO SEKTA YA MAJI**

i. Uzalishaji wa Maji wa Mamlaka zote hizo Nne (4) ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya Maji kwa maeneo hayo, hususani wakati wa kiangazi.

ii. Pia, kuna tatizo la baadhi ya Mamlaka kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha ili kutoa huduma ipasavyo.

## 7. USULUHISHI WA MIGOGORO

- Mamlaka ya EWURA katika kutatua migogoro yanatoka katika **Kifungu cha 34 cha sheria ya EWURA, Sura na. 414 ya sheria za Tanzania;**
- Sheria hiyo inaipa mamlaka EWURA kusuluhisha malalamiko / migogoro kati ya Mlaji na Mtoa huduma;
- Kifungu hiki kinasema kwamba; Walaji peke yao ndio wanaoweza kuleta malalamiko yao EWURA;

- ❑ Malalamiko ***LAZIMA*** yahusiane na utoaji wa huduma au bidhaa zinazodhibitiwa na EWURA.

- ❑ Miongoni mwa malalamiko ni bili za maji, kuuziwa mafuta yasio na ubora, malalamiko mbalimbali ya umeme, malalamiko ya bei za bidhaa na malalamiko ya huduma nk.

- ❑ Mamlaka ya EWURA katika kutatua migogoro yanatoka kwenye **sheria ya EWURA, Sura na.414, sheria za sekta husika, Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro, Tangazo la Serikali Na. 428 of 2020**

- ❑ Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 mpaka Oktoba 2021, Ofisi ya EWURA ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilipokea jumla ya malalamiko **13**,

- ❑ Kati ya hayo, sita (**6)** ni ya umeme, Lalamiko moja (**1)** ni la kuhusu maji na malalamiko sita (**6)** ni kuhusu Mafuta.

- ❑ Ofisi ya Kanda iliweza kuyapatia ufumbuzi malalamiko tisa (**9**), kati ya hayo manne (**4)** ni ya umeme na matano (**5)** ni ya Mafuta.

- ❑ Katika malalamiko manne (**4)** yaliyobakia, Lalamiko moja (1) liko kwenye ngazi ya kesi (**Hearing**) na malalamiko matatu (**3)** yanasubiri vikao vya muafaka au usuluhishi (**Mediation**).

- ❑ EWURA ndio inashughulikia malalamiki kati ya Mteja na Mtoa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA.

- ❑ Pale panapotokea malalamiko basi Wananchi waeleweshwe kwamba wayawasilishe EWURA kupitia fomu ya malalamiko inayopatikana katika ukurasa wa Mamlaka kupitia tovuti (www.ewura.go.tz) au

- ❑ Kufika Ofisi ya EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliyopo Jijini Mbeya, Mtaa wa Karume kwenye jengo la NHIF, Ghorofa ya sita.

## 8. MFUMO WA MAAMUZI

- ❑ EWURA inatumia mfumo shirikishi kwa kuwahusisha wadau wote kabla ya kufanya maamuzi ya kiudhibiti;

- ❑ **Sheria ya EWURA** inaunda Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na **EWURA *(EWURA CCC);***

- Baraza lina **wawakilishi kutoka makundi** mbalimbali ya kijamii: **Viwanda**, Wafanyabiashara, **Watumiaji majumbani**, na linazingatia jinsia.

- **Serikali Kuu** inashirikishwa na kutoa maoni na ushauri wa Kisera katika mchakato wa Udhibiti kupitia Baraza la Ushauri la Serikali **(EWURA GCC*).*** Muundo huu unarahisisha mawasiliano baina ya EWURA na Serikali wakati wa mchakato wa udhibiti;

- **EWURA GCC** inajumuisha wajumbe kutoka: ***Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara za Maji, Wizara ya Nishati, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha, Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali***;

- MDAU YEYETO ASIYERIDHIKA NA UAMIZI WA MDHIBITI (EWURA-QUAS JUDICIAL FUNCTIONS) ATAKWENDA FCT KWANI HII NDIYO COURT YA MASUALA YA KIUDHIBITI

## 9. NYENZO ZA UDHIBITI

- Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania;

- **Sheria za Sekta husika: Sheria ya Umeme, 2008; Sheria ya Mafuta 2015; Sheria ya Maji, 2019**;

- **Kanuni (*Regulations*)** zinazoandaliwa na Waziri wa Sekta husika;

- **Mikataba mbalimbali** (*PPA, Lease Contracts* na *Project Agreements*); Viwango vya Ubora (TBS),

- **Leseni**, **Taratibu *(Rules) na*** **Miongozo** (**Guidelines**) zinazoandaliwa na EWURA.

## 10. MAFANIKIO YA UDHIBITI

- **Upatikanaji wa maji** kwa Mamlaka unaendelea kuongezeka kwa wananchi wanaotumia huduma;

- **Kuimarika ukaguzi** katika miundombinu ya uzalishaji na usambazaji kwa watoa huduma;

- Tangu kuanzishwa kwa Kanda mwaka 2017, kumekuwa na **utatuaji wa haraka wa migogoro** na malalamiko;

- Weledi katika kuandaa na kuwasilisha Ripoti unaongezeka (***taratibu!***)

## 11. CHANGAMOTO YA UDHIBITI

- **Ukosefu wa mikopo** yenya masharti nafuu husababisha wawekezaji wengi kushindwa kuendeleza maeneo waliyokusudia **kuwekeza** katika utoaji huduma;

- Ukosefu wa **rasilimali fedha kwa wakati** kwa ajili ya **matengenezo** ya miundo mbinu ya usambazaji maji;

- Uwekezaji katika **Sekta ya Maji** bado imebaki kuwa **changamoto** kubwa kwa EWURA

- 4. Baadhi ya Mamlaka nyingi za Maji zina changamoto ya uandaaji wa **Mipango ya Kibiashara**. EWURA itaendelea kuweka mkazo katika uandaaji wa Mipango hiyo

- **5. Utendaji** wa Mamlaka za Maji za Miji ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa **bado ni changamoto** kwa EWURA. Mamlaka hizo hazijaweza kufikia viwango vya kiutendaji - ***ukosefu wa fedha na watumishi wenye sifa*****.**

- **6. Taarifa zinazotolewa na Mamlaka** nyingi za Maji zina kasoro kwani hazijengwi katika **takwimu zilizokusanywa na kurekodiwa kwa usahihi**.

## 7.14 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA BANDARI KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI JUNI 2022

### 1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania katika Bandari za Ziwa Nyasa inasimamia Bandari 15 na Bandari ya Itungi ni makao makuu ya bandari zote upande wa Tanzania. Bandari hizo zinazopatikana katika mikoa mitatu ya Mbeya, Njombe na Ruvuma. Mkoani Mbeya katika Wilaya ya Kyela kuna Bandari tatu (3) za Itungi, Kiwira na Matema, Mkoani Njombe katika Wilaya ya Ludewa kuna Bandari sita (6) za Lumbila, Ifungu, Nsisi, Makonde, Lupingu na Manda, na Mkoani Ruvuma katika Wilaya ya Nyasa kuna Bandari sita (6) za Ndumbi, Lundu, Nkili, Njambe, Liuli na Mbamba Bay.

Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kupitia Bandari za Ziwa Nyasa licha ya kujishughulisha na huduma za kibandari za kupakia na kupakua mizigo, pia inasimamia uendeshaji wa vyombo vya usafirishaji kwa njia ya maji ikiwemo meli mbili za mizigo yaani Mv Njombe na Mv Ruvuma pamoja na moja ya abiria na mizigo Mv Mbeya II.

### 2. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA BANDARI

Shughuli za Bandari zimekuwa zikitekelezwa kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha kwa kuhusisha shughuli mbali mbali ikiwemo;

#### 2.1. KUPAKIA NA KUPAKUA MIZIGO

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kupitia Bandari za Ziwa Nyasa kwa kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022 ilitekeleza shughuli za kibandari za kupakia na kupakua mizigo pamoja na kuhudumia abiria wanao safari katika Ziwa Nyasa.

Aidha, kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022 kituo kimeweza kuhudumia mizigo tani

5,484 ambapo kati ya hizo tani 892 mzigo wa nje ya nchi uliokuwa ukisafirishwa kwenda nchini Malawi. Sambamba na hilo, pia kituo kimehudumia abira 1,343 na wote ni abiria wa ndani ya nchi.

### 2.2. UENDESHAJI WA MELI

Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imehudumia meli za mizigo mbili na moja ya abiria kwa kusafirisha mizigo na abiria ndani ya mwambao wa Ziwa Nyasa.

Kwa upande wa meli za Mizigo yaani Mv Njombe na Ruvuma zimeweza kufanya safari mbili za kufarisha makaa ya mawe kati ya bandari ya Mbamba Bay na Kiwira. Hii ni kutokana na uchache wa mizigo mikubwa ya kusafirisha katika Ziwa Nyasa ambapo mteja mkubwa ni "Mbeya Cement Co Ltd"

Aidha, meli ya abiria na Mizigo Mv Mbeya II kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022 ilifanikiwa kufanya safari moja (1) mwezi Februari 2022. Hii ilitokana na hitilafu iliyotokea kwenye mtambo wa kulia wa meli hiyo na kupelekea kushindwa kuendelea na huduma ya usafirishaji. Kwa kipindi chote baada ya hitilafu, Mamlaka imekuwa ikisimamia kwa ukaribu matengenezo ya mtambo uliopata hitilafu ambapo mpaka kufikia Julai 2022 matengenezo yalikamilika.

### 2.3. MIRADI YA UBORESHAJI WA BANDARI

Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imekuwa ikiendelea kutekeleza miradi miwili;

#### 2.3.1 UJENZI WA GATI, RAMP, SAKAFU NGUMU BANDARI YA NDUMBI

Mradi huu utekelezaji wake ulianza mwezi Desemba 2019 ambao unatekelezwa na

Mkandarasi Ms China Hainan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) na kusimamiwa na Mkandarasi mshauri Ms Unitec Civil Consultant Ltd. Mradi huu kwa hatua za awali umekamilika lakini kuna marekebisho ambayo Mkandarasi ameelekezwa kuyafanya na hivyo mradi bado unaendelea hadi mwezi Desemba 2022.

### 2.3.2 UPEMBUZI YAKINIFU WA UBORESHAJI WA BANDARI ZA ITUNGI, KIWIRA, MATEMA, LUPINGU, MANDA, NDUMBI, LIULI NA MBAMBA BAY

Upembuzi yakinifu bado unaendelea ambapo mradi huu unatekelezwa na kampuni ijulikanayo Royal Hanskoning. Taarifa ya awali ilishawasilishwa na kurejeshwa kwa ajili ya maboresha. Hatua inayofuata ni kuhusisha wadau wote wa bandari na Viongozi kwa ajili ya mapitio na kupokea ushauri.

## 3. CHANGAMOTO

Mamlaka katika bandari za Ziwa Nyasa imekuwa ikikabiliana na changamoto zifuatazo;

### 3.1 UCHAKAVU WA MIUNDOMBINU YA BARABARA

Bandari ya Ndumbi ndio ilitengwa mahususi kwa ajili ya kuhudumia makaa ya mawe pamoja mizigo mingine mikubwa "Dirt Cargo". Kutokana na changamoto ya barabara inayounganisha bandari hiyo wateja wameshindwa kutumia bandari hiyo kwani haipitiki. Hivyo ipo haja Serikali kuliangalia hili kwa koboresha barabara hiyo ili kufanya bandari iweze kutumika

## 4. HITIMISHO

Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

(TPA) katika Bandari za Ziwa Nyasa inaendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo na abiria katika mwambao wa Ziwa Nyasa na kuendelea juhudi za kimasoko kutafuta wateja wakubwa wa usafirishaji ili kuongeza idadi ya mizigo. Pia, ili kuiwezesha bandari pamoja na meli kufanya kazi kwa ufanisi, ipo haja ya Serikali hususani kwa upande wa Mikoa kuelekeza kuwa makaa yate yanayosafirishwa kwenda Mkoani Mbeya, nchini Congo na Zambia kutumia usafiri wa Maji badala ya barabara. Hii ni kwa kuwa gharama zimeendelea kupunguzwa na pia unapunguza uharibifu wa Miundombinu ya barabara.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA BANDARI KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI SEPTEMBA 2022

### 1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania katika Bandari za Ziwa Nyasa inasimamia Bandari 15 na Bandari ya Itungi ni makao makuu ya bandari zote upande wa Tanzania. Bandari hizo zinazopatikana katika mikoa mitatu ya Mbeya, Njombe na Ruvuma. Mkoani Mbeya katika Wilaya ya Kyela kuna Bandari tatu (3) za Itungi, Kiwira na Materna, Mkoani Njombe katika Wilaya ya Ludewa kuna Bandari sita (6) za Lumbila, Ifungu, Nsisi, Makonde, Lupingu na Manda, na Mkoani Ruvuma katika Wilaya ya Nyasa kuna Bandari sita (6) za Ndumbi, Lundu, Nkili, Njambe, Liuli na Mbamba Bay.

Aidah, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania {TPA) kupitia Bandari za Ziwa Nyasa licha ya kujishughulisha na huduma za kibandari za kupakia na kupakua mizigo, pia inasimamia uendeshaji wa vyombo vya usafirishaji kwa njia ya maji ikiwemo meli mbili za mizigo yaani Mv Njombe na Mv Ruvuma pamoja na moja ya abiria na mizigo Mv Mbeya II.

### 2. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA BANDARI

Shughuli za Bandari zimekuwa zikitekelezwa kwa kipindi chote cha kuanzia Julai 2022 hadi Septemba 2022 kwa kuhusisha shughuli mbali mbali ikiwemo;

#### 2.1. KUPAKIA NA KUPAKUA MIZIGO

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kupiti~ Bandari za Ziwa

Nyasa kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Septemba 2022 ilitekeleza shughuli kibandari za kupakia na kupakua mizigo pamoja na kuhudumia abiria wanao safari katika Ziwa Nyasa.

Aidha, kwa kipindi hiki kituo kimeweza kuhudumia mizigo tani 344 ambapo kati ya hizo tani 120 ni mzigo wa nje ya nchi uliokuwa ukisafirishwa kwenda nchini Malawi. Sambamba na hilo, pia kituo kimehudumia abira 4,079 na wote ni abiria wa ndani ya nchi.

### 2.2. UENDESHAJI WA MELI

Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Septemba 2022 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imehudumia meli za mizigo mbili na moja ya abiria kwa kusafirisha mizigo na abiria ndani ya mwambao wa Ziwa Nyasa.

Kwa upande wa meli za Mizigo yaani Mv Njombe na Ruvuma kituo kimeweza kufanya safari ya meli moja (1) ya kufarisha "gypsum" kati ya bandari ya Mbamba Bay na Kiwira.

Aidha, kwa upande wa meli ya abiria na Mizigo Mv Mbeya II kituo kimefanikiwa kufanya safari saba (7). Hii ni baada ya kukamilika kwa matengenezo ya hitilafu iliyokuwepo kwenye injini ya upande wa kulia.

### 2.3. MIRADI YA UBORESHAJI WA BANDARI

Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Septemba 2022 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imekuwa ikiendelea kutekeleza miradi miwili ambayo imekuwa ikitekelezwa mwaka wa fedha za 2021/2022;

#### 2.3.1 UJENZI WA GATI, RAMP, SAKAFU NGUMU BANDAR! YA NDUMBI

Mradi huu utekelezaji wake ulianza mwezi Desemba 2019 ambao unatekelezwa na Mkandarasi Ms China Hainan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) na kusimamiwa na Mkandarasi mshauri Ms Unitec Civil Consultant Ltd. Mradi huu kwa hatua za awali umekamilika lakini kuna marekebisho ambayo Mkandarasi ameelekezwa kuyafanya na hivyo mradi unatarajiwa kukabidhiwa rasmi mwezi Desemba 2022.

#### 2.3.2 UPEMBUZI YAKINIFU WA UBORESHAJI WA BANDAR! ZA ITUNGI, KIWIRA, MATEMA, LUPINGU, MANDA, NDUMBI, LIULI NA MBAMBA BAY

Upembuzi yakinifu bado unaendelea ambapo mradi huu unatekelezwa na kampuni ijulikanayo Royal Hanskoning. Taarifa ya awali ilishawasilishwa na kurejeshwa kwa ajili ya maboresha. Hatua inayofuata ni kupitia taarifa ya mwisho na kuhusisha wadau wote wa bandari na Viongozi kwa ajili ya mapitio na kupokea ushauri.

## 3. CHANGAMOTO

Mamlaka katika bandari za Ziwa Nyasa imekuwa ikikabiliana na changamoto zifuatazo;

### 3.1 UCHAKAVU WA MIUNDOMBINU YA BARABARA

Bandari ya Ndumbi ndio ilitengwa mahususi kwa ajili ya kuhudumia makaa ya mawe pamoja mizigo mingine mikubwa "Dirt Cargo". Kutokana na changamoto ya barabara inayotokea kitai hadi bandari ya Ndumb wateja wameshindwa kutumia bandari hiyo. Hivyo ipo haja Serikali kuliangalia hili kwa koboresha barabara hiyo ili kufanya bandari iweze kutumika.

## 4. HITIMISHO

Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Septemba 2022 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) katika Bandari za Ziwa Nyasa inaendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo na abiria katika mwambao wa Ziwa Nyasa na kuendelea juhudi za kimasoko kutafuta wateja wakubwa wa usafirishaji ili kuongeza idadi ya mizigo. Pia, ili kuiwezesha bandari pamoja na meli kufanya kazi kwa ufanisi, ipo haja ya Serikali hususani kwa upande wa Mikoa kuelekeza kuwa makaa yate yanayosafirishwa kwenda Mkoani Mbeya, nchini Congo na Zambia kutumia usafiri wa Maji badala ya barabara. Hii ni kwa kuwa gharama zimeendelea kupunguzwa na pia unapunguza uharibifu wa Miundombinu ya barabara.

## 8.0 TAARIFA ZA KAMATI ZA USHAURI ZA WILAYA (DCC)

### 8.1 WILAYA YA SONGEA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI (DCC) WILAYA YA SONGEA KILICHOFANYIKA TAREHE 21.11.2022 KATIKA UKUMBI WA MANISPAA SONGEA**

**MAHUDHURIO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Pololet K. Mgema | Mhe. Mkuu wa Wilaya | Mwenyekiti |
| 2 | Sajidu Idrisa .M. | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3 | Pendo Daniel | Katibu Tawala Wilaya | Mjumbe |
| 4 | Thomas s. Masolwa | M/Kiti CCM SDC | Mjumbe |
| 5 | Mwinyi .A. Msolomi | Mwenyekiti CCM Songea Mjini | Mjumbe |
| 6 | Alto A. Liwelelu | Ag. MD Songea MC | Mjumbe |
| 7 | Neema M. Maghembe | Mkurugenzi Songea DC | Mjumbe |
| 8 | Michael Mbano | Mstahiki Meya Manispaa | Mjumbe |
| 9 | Teofanes T. Mlelwa | M/Kiti H/W Madaba | Mjumbe |
| 10 | Capt. David Yamawasa | CO Mlale 842 KJ | Mjumbe |
| 11 | Amos Lugomela | DBC - Takukuru Wilaya | Mjumbe |
| 12 | SSP. W.M. Siwa | OCD Wilaya | Mjumbe |
| 13 | SP. Dickson D | DPO Wilaya | Mjumbe |
| 14 | Insp. Baraka Mtae | Uhamiaji Wilaya | Mjumbe |
| 15 | A/Insp Jackson Mahali | DFO Wilaya | Mjumbe |
| 16 | Abushehe Nondo | DSO Wilaya | Mjumbe |
| 17 | Capt. Victoria Mtega | MJA Wilaya | Mjumbe |
| 18 | Dismas A. Komba | A/Tarafa Songea Mjini Mashariki | Mjumbe |
| 19 | Flowin K. Nyoni | A/Tarafa Ruvuma | Mjumbe |
| 20 | Alkwin Ndimbo | A/Tarafa Songea Mjini Magharibi | Mjumbe |
| 21 | Showing Mapunda | A/Tarafa Madaba | Mjumbe |
| 22 | Ernest Nombo | Ag. Maliasili – Madaba | Mjumbe |
| 23 | Nico Oscar Charles | M/Kiti UWABIMASO | Mjumbe |
| 24 | Gabriel E. Kirigiti | Ag. DMO Madaba | Mjumbe |
| 25 | Yahaya Mudhihir | RM - NSSF | Mjumbe |
| 26 | Kombo JM. | HRO – Madaba DC | Mjumbe |
| 27 | Simon Hyera | DSCAO – Madaba | Mjumbe |
| 28 | Aleni F. Ngole | Soko la Mjimwema | Mjumbe |
| 29 | Zuber M. Tindwa | Katibu – CHADEMA ‘W” | Mjumbe |
| 30 | Elias Nchimbi | Chama Siasa TLP (W) | Mjumbe |
| 31 | Hamisi H. Kaisi | Katibu CUF | Mjumbe |
| 32 | Juma M. Haule | NCCR – Mageuzi | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 33 | Frank Kilanga | Meneja NBC – Songea | Mjumbe |
| 34 | Daniel Zake | Meneja - Songea | Mjumbe |
| 35 | Jafari Yahaya | Ag. Mkurugenzi SOUWASA | Mjumbe |
| 36 | Jane Shitindi | Songea MC | Mjumbe |
| 37 | Furaha J. Mwangakala | Songea MC | Mjumbe |
| 38 | Joel Mairo | Songea MC | Mjumbe |
| 39 | Zawadi H. Nyoni | Songea DC | Mjumbe |
| 40 | Consolatha Komba | MKT UDP | Mjumbe |
| 41 | Athuman Likungumwike | Songea DC | Mjumbe |
| 42 | Paulo Mpira Geho | M/Kiti ADA TADEA | Mjumbe |
| 43 | Godfrey Mngale | Tarura Songea | Mjumbe |
| 44 | Johnson Kweka | Tarura Songea | Mjumbe |
| 45 | Andrew A. Mwafalo | Songea MC | Mjumbe |
| 46 | Betram Njelelekela | Songea MC | Mjumbe |
| 47 | Rozina R. | Songea MC | Mjumbe |
| 48 | Amos Mwenda | Songea MC | Mjumbe |
| 49 | Malibe J. Boniphace | TANESCO | Mjumbe |
| 50 | Christina Chabruma | Songea MC | Mjumbe |
| 51 | Triphon Mwanangwa | RUWASA | Mjumbe |
| 52 | Onesmo Mbano | Madaba | Mjumbe |
| 53 | Godfrey Luhimbo | Songea MC | Mjumbe |
| 54 | Joseph J. Mrimi | Madaba | Mjumbe |

## AGENDA ZA KIKAO

1. Kufungua kikao
2. Utambulisho
3. Kuridhia agenda
4. Kusoma Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya cha tarahe 15.11.2021
5. Yatokanayo na Kikao cha tarehe 15.11.2021
6. Taarifa ya Utekelezaji wa miradi katika kipindi cha 2021/2022
   - Halmahsauri ya Manispaa Songea
   - Halmashauri ya Wilaya ya Songea
   - Halmashauri ya Wilaya ya Madaba
7. Taarifa ya Miradi ya TARURA
8. Taarifa ya Miradi ya RUWASA

9. Taarifa ya TANESCO
10. Taarifa ya SOUWASA
11. Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kuomba eneo la Tanroad lililopo Kijiji cha Mtepa – Madaba litumike kama Soko la Mazao
12. Taarifa ya Nanenane
13. Utunzaji wa Mazingira
14. Maombi ya kubadilisha eneo la maonyesho ya Nanenane kutoka Kata ya Msamala kwenda Kata ya Mwengemshindo
15. Mengineyo
16. Kufunga kikao

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/3/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha Wajumbe wote wa kikao hiki cha Kamati ya Ushauri Wilaya (DCC). Pia alitarajia Wageni wa kikao hiki ambao ni Wenyeviti na Makatibu CCM Wilaya, Watu wa Madhehebu ya Dini, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Wageni waalikwa. Baada ya hapo Mwenyekiti wa kikao aliwakaribisha Wajumbe wote wa kikao kwa Nyadhifa zao kutoka Kamati ya Ulinzi na Usalama, Vyama vya Siasa, Madhehebu ya Dini na Wageni waalikwa kutoka Taasisi mbalimbali baada ya hapo Mwenyekiti alifungua kikao mnamo tarehe 6.20 mchana.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/4/2022 UTAMBULISHO**

Katibu wa kikao alifanya utambulisho wa Wenyeviti wa CCM kutoka Songea Mjini, na pia aliwatambulisha Meya wa Manispaa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Madaba.

Pia aliwatambulisha Wakurugenzi kutoka Manispaa, Madaba DC na Songea DC, pia aliwatambulisha Kamati ya Ulinzi na Usalama, Viongozi wa Vya Siasa, Madhebu ya Dini, Wakuu wa Idara kutoka Halmashauri ya Madaba, Songea DC na Songea Manispaa pia aliwatambulisha Sekretarieti ya kikao hiki.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/5/2022 KUIDHINISHA AGENDA**

Mwenyekiti wa kikao alisoma Agenda hii ili kuleta maridhio katika Agenda zote zilizopo. Baada ya hapo Wajumbe kupitia Agenda zote zilizopo waliridhia kuwa Agenda za Kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya (DCC) cha tarehe 21.11.2022.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/6/2021 KUSOMA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI WILAYA CHA TARAHE 15.11.2021**

Katibu wa kikao alisoma muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 15.11.2021, baada ya kusoma aliuwasilisha. Mwenyekiti wa kikao aliwaongoza Wajumbe na Wageni waalikwa kupitia muhtasari ikiwa pamoja na kufanya marekebisho mbalimbali ya uandishi na uchapaji. Baada ya mapitio ya muhtasari Wajumbe walifanya marekebisho sehemu ya Majina na mwisho waliridhia kuwa taarifa sahihi ya kumbukumbu ya shughuli za Serikali.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/7/2022 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 15.11.2021**

Muhtasari haukuwa na yatokanayo hivyo kikao kiliendelea katika Agenda inayofuata.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/8/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI KATIKA KIPINDI CHA 2021/2022**

Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ziliwasilishwa kama ifuatavyo:-

- **HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA**

Taarifa ya utekelezaji kwa Halmashauri ya Manispaa, taarifa ilisomwa na Wajumbe kwa pamoja waliipokea kama ilivyo na kuikubali.

- **HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA**

Taarifa ya utekelezaji kwa Halmashauri ya Songea, taarifa ya Halmashauri ilisomwa na Wajumbe kwa pamoja wariridhia taarifa hiyo na kuipokea na kuikubali

- **HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA**

Taarifa ya utekelezaji kwa Halmashauri ya Madaba, taarifa ilisomwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Madaba na Wajumbe wa Kikao kwa pamoja walipokea taarifa na kuiridhia taarifa hiyo

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/9/2022 TAARIFA YA MIRADI YA TARURA**

Taarifa ya utekelezaji kwa Tarura ilisomwa na Meneja wa Tarura wa Wilaya na Wajumbe kwa pamoja waliipokea taarifa hiyo na kuiridhia taarifa hiyo.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/10/2022 TAARIFA YA RUWASA**

Taarifa ya Ruwasa ya utekelezaji wa kazi za maendeleo katika Miradi mbalimbali ya Maji ilisomwa na Meneja wa Ruwasa Songea. Katika taarifa hiyo Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuridhia taarifa hiyo. Pia Mwenyekti alisema kuwa mradi wa Maji Mtyangimbole leo tarehe 21.11.2022 tayari umesainiwa na pia kuendelea na utekelezaji. Wajumbe walipongeza harua za Serikali katika utekelezaji wa miradi katika Wilaya ya Songea.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/11/2022 TAARIFA YA TANESCO**

Taarifa ya Tanesco katika utekelezaji wa Miradi ya REA na TANESCO kwa ujumla ilisomwa na mwakilishi kutoka TANESCO ambaye ni Meneja wa TANESCO aliwasilsihwa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Wajumbe kwa pamoja waliipokea taarifa hiyo na kuridhia.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/12/2022 TAARIFA YA SOUWASA**

Taarifa ya Souwasa ilisomwa na Technical Meneja wa Mamlaka ya Maji Souwasa. Wajumbe kwa pamoja waliipokea taarifa hiyo na kuiridhia kwa pmaoja.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/13/2022 HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA KUOMBA ENEO LA TANROAD LILILOPO KIJIJI CHA MTEPA – MADABA LITUMIKE KAMA SOKO LA MAZAO**

Taarifa hii ilikuwa ni ombi la Halmashauri ya Wilaya ya Madaba juu ya eneo la Tanroad lililopo Kijiji cha Mtepa - Madaba litumike kama Soko la Mazao. Mwenyekiti alielezea kuwa hilo ni ombi hivyo taratibu zifanyike ili mchakato wa maombi haya uendelee. Hivyo Wajumbe walipokea ombi hilo, na kuridhia kwa hatua zinazofuatiwa ili kupanua maeneo ya utoaji huduma za kimasoko kwa mazao ya Wananchi na kukuza uchumi wa jamii.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/14/2022 UTUNZAJI MAZINGIRA**

Mmwenyekti wa kikao alielezea kuwa Utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya vyote ni jukumu la kila mmoja na ni suala la Taifa na Dunia nzima. Hivyo alisisitiza utunzaji wa vyanzo vya maji ufanyike na uendelee.

Kamati ya Mawaziri na hupitia maeneo yote ya Nchi kukagua na kusisitiza utunzaji wa Mazingira. Pia aliwaelekeza Maafisa Bonde wote wa Songea na Meneja TFS kuwa wanalo jukumu la kusimamia na kutunza vyanzo vya Maji. Pia alizitaka Taasisi zote zinazofanya kazi katika Eneo la Wilaya kufanya kazi kwa Ushirikiano ili kuleta ufanisi katika utunzaji wa Mazingira.

Pia Mwenyekiti wa Kikao alisisitiza Taasis zote kushirikiana na Wananchi katika Utunzaji wa Mazingira , pia aliagiza Taasis zote ziwajibike ipasavyo katika utunzajo wa Vyanzo vya Maji. Mwenyekiti alisisitiza kufanya ukarabati wa mazingira yetui ikiwa pamoja na kupanda Miti katika Mazingira yetu.

Wakuu wa Taasis wakae na Wafanyakazi wao wote ili kila Mtumishi wa Taasisi aweze kupanda miti mitano ili kuboresha mazingira. Kupanda miti huko kuendane na usimamizi wa upandaji wa miti hiyo.

**KUMB.NA:SO/DIST/C.C/15/2022 MAOMBI YA KUBADILISHA ENEO LA MAONYESHO YA NANENANE KUTOKA KATA YA MSAMALA KWENDA KATA YA MWENGEMSHINDO**

Mkurugenzi wa Manispaa alitoa maombi ya kubadilisha matumizi ya eneo la Nanenane kujengwa Ofisi za Serikali zikiwemo Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Mkuu wa Wilaya, Mahakama Kuu ya Songea, TMDA eneo la nanenane Msamala. Hivyo aliomba kutokana na ujenzi huo Halmashauri ya Manispaa

inaomba eneo hilo la nanenane lihamie Kata ya Mwengemshindo ili kupisha ujenzi eneo la Msamala kwa kuwa Taasisi za Serikali.

Mwenyekiti wa kikao alieleza kuwa eneo hilo kuwa ni eneo jumuishi kwa Taasisi mbalimbali za Kiserikali. Hivyo kutokana na hilo Wajumbe kwa pamoja waridhia agenda na kuikubali, na kuruhusu mchakato uendelee.

## KUMB.NA:SO/DIST/C.C/16/2022 MENGINEYO

Mjumbe wa kwanza aliipongeza Serikali kwa eneo la Nanenane kuwa kujenga eneo la Serikali. Aliashauri kuhusu Masoko ya Manzese kuhusu ujenzi kuanza Janurai 2023, kuwa ni mzuri na hivyo alisisitiza na kuomba ujenzi uanze mapema. Pia alisisitiza eneo la Mliyayoyo kuwa na Mitaa mchanganyiko kwa maana kuwa ni eneo la Halmashauri ya Namtumbo, Madaba na hivyo aliomba meneo hayo yawe ya Manispaa ili kuboresha Manispaa kuwa Jiji.

Mjumbe mmoja aliuliza Kata ya Subria eneo la Kisiwani C maji ya eneo hilo linatumia maji ya kisima wakata mabomba yapo hovyo

Mjumbe wa aliuliza mradi wa Maji Ruvuma hautoi maji na mambomba kuvuja nini suluhisho lake.

**MAELEZO YA MSTAHIKI MEYA MANISPAA**

Mstahiki Maye alitoa maelekezo kuwa fedha ya ujenzi wa masoko ya Manzese ipo tayari na mradi unatarajia kuanza karibuni . pia alielekeza changamoto ya fedha katika miradi ya barabara. Mstahiki Meya alieleza changamoto ya Tarura kuwa ni eneo gani kumekwama katika uamishaji wa Barabara mpya.

**MAELEZO YA MHANDISI MAJI SOUWASA**

Ni kweli kuwa subira, Mwengemshindo na Pambazuko ni miradi iliyoanishwa na Manispaa ya Songea. Souwasa baada ya kupima kina cha maji katika miradi hiyo ni visima viwili tu vilivyokidhi, kibali cha kuendelea na mradi kutoka Wizara ya Maji kinasubiliwa. Hivyo miradi ya Subira hiyo miwili itafanyiwa kazi.

Mwengemshindo mradi utaunganishwa kutoka Mkuzo kutokana na Maji yaliyopo Kata ya Mwengemshindo katika Visima hivyo hayatoshi.

Mwenyekiti wa kikao alitoa agizo kuwa kesho tarehe 22.11.2022 Souwasa wawe Ruvuma ili kupata ufumbuzi katika kutengeneza miradi hiyo.

**MAELEZO YA MWENYEKITI WA KIKAO**

Maeneo ya pembeni yapimwe ili kuweka maeneo ya Manispaa vizuri na Mji uonekane katika ubora. Hivyo alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa apime maeneo yote ya pembeni. Baada ya hapo Mwenyekiti aliruhusu Wenyeviti wa CCM Wilaya kuongea machache.

## MWENYEKITI WA CCM MADABA

Alimpogeza Mwenyekiti wa Kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya (DCC) kwa kazi nzuri lakini pia aliongelea kila Mkuu wa Taasis na Viongozi wote kwa ujumla kila mmoja awajibike ipasavyo. Pia alisisitiza eneo la utumishi kuwa Watumishi ni wachache na hivyo kumwomba Mwenyekiti kupambana kupata Watumishi wengine ili kukidhi ikama ya Watumishi.

## MWENYEKITI WA CCM MJINI

Alipongeza kikao kuwa kikao kimafanyika vizuri kwa demokrasia nzuri. Alipongeza kwa miradi mingi iliyopo Songea, pia alipendekeza kuwa Kata ya Ruvuma iangaliwe upya ili kutengeneza mchanganyiko katika uboreshaji wa Mji ili kupunguza vibaka na wahalifu katika Mji

## KUMB.NA:SO/DIST/C.C/17/2022 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao kwa kusisitiza utunzaji wa Mazingira na jukumu la kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni jukumu la kila Mtumsihi katika Taasisi zote. Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe wote wa kikao na kufunga kikao mnamo saa 01.47 mchana

## UMETHIBITISHWA NA

**……………………………………..** **…………………………………..**

**MWENYEKITI WA KIKAO** **KATIBU WA KIKAO**

**TAREHE: -……………………………**

## 8.2 WILAYA YA TUNDURU

### MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA WILAYA (DCC) KILICHOFANYIKA TAREHE 19/12/2022 KWENYE UKUMBI WA KLASTA

#### 1. MAOMBI YA KUANZISHA HALMASHAURI MPYA WILAYANI TUNDURU

Kamati ya Ushauri ya wilaya ya Tunduru imejadili hoja ya kuanzisha Halmashauri mpya wakikumbusha na kutaka kujua utekelezaji wa azimio hili baada ya kuwalishwa Mkoani.

Mwenyekiti wa Kikao aliwajulisha Wajumbe kwamba Kamati ya Ushauri ya Mkoa ilisharidhia na kupitisha ombi hili. Hata hivyo halikupelekwa mbele tukisubiri matokeo ya Sensa iliyofanyika tarehe 23 Agosti 2022 ambayo itaonyesha idadi ya watu kwenye majimbo yote mawili, ndipo Mkoa utawasilisha maombi haya Serikalini.

Kamati ya Ushauri ya wilaya ya Tunduru inaiomba tena Kamati ya Ushauri Mkoa wa Ruvuma kwenye kikao hiki kuendelea kuzingatia maombi ya Wananchi wa wilaya ya Tunduru kuongeza Halmashauri ili kusogeza huduma karibu na wananchi wanaohudumiwa na kupunguza gharama kubwa za usimamizi wa shuguhli za maendeleo wilayani Tunduru.

#### 2. HOJA YA WAFUGAJI WA NG’OMBE HOLELA

Kamati ya Ushauri ya wilaya ya Tunduru imejadili hoja hii kwa masikitiko makubwa kutokana na changamoto zinazojitokeza kwa sasa. Wilaya ya Tunduru ina wafugaji wengi sana wahamiaji kutoka maeneo mbalimbali ya nchi. Kuna wale walioingia kwa kufuata taratibu lakini pia kuna wengi ambao wameingia bila ya kufuata taratibu.

Kinachoendelea kwa sasa ni kuongezeka kwa migogoro kati ya wafugaji na wakulima na wakati mwingine kati ya makundi tofauti ya wafugaji. Wafugaji Waliowekwa kwenye vitalu nao wanatoka na kufugia kwenye maeneo yasiyo rasmi hivyo kusababisha migogoro na wakulima/Wakazi wenyeji.

Kutokana na changamoto hii inayoendelea, Kamati ya Ushauri ya wilaya ya Tunduru imeazimia kuendelea na zoezi la kutumia vyombo vyake mbalimbali kufanya zoezi la kuwakamata wafugaji wote wanaofuga kwenye maeneo yasiyo rasmi ili kuwatambua wafugaji halali waliolipia vitalu ambao watatozwa adhabu na watarejeshwa vitaluni na ambao hawajasajiliwa watatozwa adhabu na pia watatakiwa kuhama wilayani Tunduru. Lengo ni kuhakikisha wafugaji wilayani Tunduru wanafuga kwa kufuata sheria na taratibu zinazotakiwa. Kamati imeelekeza Wafugaji wote watakaokuwepo kwenye vitalu vilivyopo watapewa elimu ya kutosha kuhusu ufgaji wa kisasa ili waweze kuweka mazingira rafiki ya ufugaji ikiwa ni pamoja kujiandalia nyasi za malipo pamoja na kuandaa ya kuhifadhia maji. Ukosefu wa chakula na maji wakati wa kiangazi husababisha wafugaji wote kuhama kwenye vitalu na kusambaa maeneo mbalimbali hivyo kusababisha migogoro miongoni yao na wakulima pia.

### 3. CHANGAMOTO YA TEMBO

Wilaya ya Tunduru ni Wilaya inayopakana na hifadhi za wanyama kwa upande wa kusini na kaskazini, hivyo kusababisha kuwa na Tembo wengi. Katika kipindi cha miaka ya karibuni kumekuwa na changamoto kubwa ya makundi ya Tembo wanaovamia makazi ya wananchi na kuathiri mazao ya wakulima pamoja na kusababisha vifo kwa wananchi. Tayari kwa mwaka 2022 kufikia Desemba hii, wananchi kumi nan ne (14) walivamiwa na Tembo na kati yao sita (6) walijeruhiwa na wanane (8) wamepoteza maisha yao kutokana na uvamizi ya Tembo.

Wilaya ya Tunduru imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuwasogeza Tembo wavamizi kurejea kwenye maeneo yao kwa kutumia vikosi vilivyopo, hata hivyo kutokana na ukubwa wa eneo, kuna maeneo hushindwa kufika kwa wakati na hivyo kukuta uharibifu umeshafanyika.

Kamati ya Ushauri ya wilaya ya Tunduru inaomba Serikali kusaidia namna ya kupambana na Tembo hawa wanaovamia makazi ya wananchi. Hata hivyo tayari kituo kimoja cha Askari wanyamapori kimejengwa kwenye kijiji cha Chingulungulu ili waweze

kusaidia pale inapotokea changamoto waweze kuwasogeza Tembo hifadhini. Wilaya inaomba Serikali kuongeza jitihada za kuhakikisha vituo hivi vinajengwa kwenye maeneo yote ambayo misafara ya Tembo huathiri jamii iishiyo jirani hasa kwenye maeneo ya Tarafa za Lukumbule, Nalasi, Nampungu, Nakapanya na Matemanga.

**4. UPATIKANAJI WA MBOLE YA RUZUKU**

Kamati ya Ushauri ya wilaya ya Tunduru imeipongeza serikali kwa kuwezesha kupatikana mbolea ya ruzuku hivyo kupatikana kwa bei nafuu kwa wakulima. Kutokana na maelezo ya wataalam na wafanyabiashara wanaouza mbolea wilayani Tunduru, ni dhahiri mfumo wa ununuaji na uuzaji wa mbolea unaoendelea wa kuuzwa mjini Tunduru pekee unawaathiri sana wakulima ambao wengi wao wapo zaidi ya kilomita 50 huko vijiji ambako kuna uzalishaji mkubwa.

Kamati ya Ushauri ya wilaya ya Tunduru inaomba Serikali kuwezesha upatikanaji rahisi wa mbolea kwa kufanya yafuatayo:

- Wasambazaji wakubwa wa Mbolea waekelezwe kusambaza mbolea kwenye wilaya zote zenye uhitaji
- Serikali ipunguze masharti kwa wasambazaji wa mbolea ili waweze kusambaza mbolea hadi vijijini badala makao makuu ya wilaya
- Kutokana na wakulima wengi kukosa uwezo wa kununua kwa wakati Fulani, kamati inashauri Zoezi la usambazaji mbolea liwe ni endelevu ili wakulima waendelee kunufaika na ruzuku katika msimu wote wa kilimo

## 8.3 WILAYA YA MBINGA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA WILAYA YA MBINGA (DCC) KILICHOFANYIKAKATIA UKUMBI WA FDC – MBINGA TAREHE 14/06/2022**

**MAHUDHURIO**

| | |
|---|---|
| Mh.Aziza A. Mangossongo | Mkuu wa wilaya -M/kiti |
| Juma H. Juma | Mkurugenzi -Katibu |
| Grace S. Quintine | Mkurugenzi wa Mji – Mjumbe |
| Beda G. Hyera | M/Kiti wa CCM (W) |
| Insp George T. Buberwa | Ag. DIO |
| Asp. Edward J. Mwabulambo | Mkuu wa gereza mkwaya |
| Mh. Fredrick J. Msae | DBC – Mbinga |
| Saidi Majidu | Shekhe (W) |
| A/Insp Ally S. Alijai | For OCD |
| WO II Hassan H. Mbedo | K / Mshauri wa mgambo (W) |
| Sp Aloyce A. Mbongo | O/C Mbinga |
| INSP John Lupondije | DFO Mbinga |
| Ndg. Tariq Mohamed | For DSO |
| Ndg. Mwanaid M. Mang'uru | Ag DAS |
| Dr. Patrick P. Banzi | DLFO Mbinga |
| Ndugu. Kelvin Mpiluka | DFC – Mbinga |
| Eng. Mashaka Sirikaka | Meneja – RUWASA |
| Ndugu. Said Farahani | TEOP – Mbinga TC |
| Ndugu. Kassim A. Kassim | Mwanasheria – MTC |
| Ndugu. Job A. Mwalukosya | Mwanasheria – MDC |
| Ndugu. Pisii A. Nassoro | Afisa uvuvi– Mbinga DC |
| Ndugu. Martina Ngahy | A / Biashara – Mbinga DC |
| Ndugu. Kenedy Lyakurwa | A/Biashara - Mbinga TC |
| Ndugu. Mariam Sadala | WEO - Luhuwiko |
| Ndugu. Hasna Adam Malinzanga | WEO – bethlehem |

| | |
|---|---|
| Ndugu. John Kabada | Ag.DCTD – Mbinga DC |
| Ndugu. Christopher R. Ntandu | Ag. DPLO – Mbinga DC |
| Ndugu. Catherine Millinga | Mthibiti ubora shule DC |
| Ndugu. Gaudence C. Mbunda | WEO – Matiri |
| Ndugu. Mpoki Nsyeka | TIA-Mbinga TC |
| Ndugu. Samwel M. Komba | DEO (P) Mbinga DC |
| Dr. Louis K. Chomboko | DMO – Mbinga DC |
| Ndugu. Neema Mbilinyi | Ag. DE – Mbinga DC |
| Eng. Evance Haule | DAICO -Mbinga DC |
| Ndugu. Enock P. Ndunguru | TAICO – MTC |
| Ndugu. Neema O. Mwisho | WEO – Matarawe |
| Ndugu. Gilbert M. Gotifrid | Ag TBO |
| Ndugu Cecilia Mbata | TCDO Mbinga TC |
| Ndugu. Avelinius Rwegasira | Ag. DCDO – Mbinga DC |
| Ndugu. Fausta Sabiyanka | Tceec – Mbinga TC |
| Ndugu. Wilybroad G. Ngongi | Ag. THRO – MbingaTC |
| Ndugu. Backlay A. Mwarabu | WEO - Utiri |
| Ndugu. Noel Ngailo | A/Ushirika– Mbinga DC |
| Ndugu. Erick T. Kangalawe | WEO – Mbinga TC |
| Ndugu Elias L Bulonga | WEO_ Nyoni |
| Ndugu. Asante B. Luambano | Mratibu TASAF |
| Ndugu. Grace P. Mbena | Katibu msaidizi TSC |
| Ndugu. Calistus A. Hyera | Mkulima Mahenge AMCOS |
| Ndugu. Prosper F. Nchimbi | WEO – Linda |
| Ndugu. Hatibu F. Idd | WEO – Mapera |
| Ndugu. Amon N. Sangana | EO – Mbinga TC |
| Ndugu. Andrew L. Mbunda | EO – Mbinga DC |
| Ndugu. Peter L. Mtalamka | DSEO – Mbinga DC |
| Ndugu. Hillary M. Joseph | Ag. DIA – Mbinga DC |
| Ndugu. Anord Gabinus Ngonyani | WEO – Mbambi |
| Ndugu. Dady Ismail Hussein | WEO – Lusonga |
| Ndugu. Deodatus D. Mbata | A/Mazingira TC |

| | |
|---|---|
| Ndugu. Shanel Mbunda | PCDO Mbinga TC |
| Ndugu. Edward J. Aluko | WEO – Kipapa |
| Ndugu. Mary Y. Ndunguru | Ag. TLFO MbingaTC |
| Ndugu. Christian G. Makanury | A/Habari |
| Ndugu. Simon C. Ponera | Ofisi ya mbunge |
| Ndugu. Nasibu V. Mapunda | WEO – Ruanda |
| ndugu. gaudensia e. kapinga | D/V/Maalum Mapera |
| Ndugu. Dickson Mbungano | RMO – Ruvuma |
| Ndugu. Thomas H. Nombo | WEO - K/ mahuka |
| Ndugu. Narzis G. Mwitumba | WEO – Ukata |
| Ndugu. David A. Hyera | TFO – Mbinga TC |
| Ndugu. Anthony Bingwa | Katibu wa Mbinga |
| Ndugu. Cecilia M. Sasigwa | Afisa Utumishi |
| Ndugu. Lukas Hadrian Mapunda | WEO Kigonsera |
| Ndugu. Dominikus S. Komba | WEO Mpapa |
| Ndugu. Victor N. Lyimo | WEO Ngima |
| Ndugu. Wilson S. Mwasakutonka | WEO Mhongozi |
| Ndugu. Joakim Ngaponda | WEO - Amani makolo |
| Ndugu. Osward F. Ndunguru | WEO -Kitura |
| Ndugu. Owen R. Liholili | WEO- Kipololo |
| Ndugu. Sostenes C. Mkawala | WEO- Litumbandyosi |
| Ndugu. Joseph V. Ndunguru | WEO -Lukarasi |
| Ndugu. Manufreda R. mhagama | WEO- Mbuji |
| Ndugu. Oliva E. Kapanga | WEO -Mkako |
| Ndugu. Ditram E. Ndonde | WEO- wukiro |
| Ndugu. Haleluya Msimba | WEO -Maguu |
| Ndugu. Jenista P. Ngonyani | WEO- Kitumbalomo |
| Ndugu. Abel T. Malika | WEO- Kambarage |
| Ndugu. Cosma N. Justine | WEO Litembo |
| Ndugu. Festo M. Komba | Kitanda TC |
| Ndugu. Ivo E. Msuha | Luwaita TC |
| Ndugu. Mariam Sadala Rajab | Luhuwiko MTC |

| | |
|---|---|
| Ndugu. John A. Makoyola | Kagugu TC |
| Ndugu. Alphonce C. Mnyenyelwa | WEO – Mikalanga |
| Ndugu. Ambrose E. Mbunda | WEO - Muungano |
| Ndugu. Elizabeth O. Mapunda | WEO -Myangayanga |
| Ndugu. Emanuel P. Mbilinyi | WEO Masumuni |
| Ndugu. Barongo Wilfred Mfunjo | WEO – Mpepai |
| Ndugu. January M. Manji | WEO- Kilimani |
| Ndugu. Bosco E. Luoga | WEO – Mbangamao |
| Ndugu. Mohamed A. Hassan | WEO - Kikolo |
| Ndugu. Edward J. Aliko | WEO – Kipapa |
| Ndugu. Daniel R. Komba | WEO – Langiro |
| Ndugu. Andrea John Mhagama | WEO – Mbinga mjini TC |
| Ndugu. Bahati G. Mbele | Makamu Mbinga DC |
| Ndugu. Francis N. Kawahi | Mkuu wa chuo FDC |
| Ndugu. Osmund O. Mbunda | Kaimu/meneja mbifacu |
| Ndugu. Kitaliu Mwakyuma Angelik | Meneja TRA – Mbinga |
| Eng. Oscar Mussa | Meneja TARURA |
| Ndugu. Oscar Mussa | Meneja TANESCO |
| Eng. Zabron Malima | TARURA |
| Ndugu. Paulo D. Mawala | A/Tarafa – Hagati |
| Ndugu. Salma A. Kipande | A/Tarafa – Mbuji |
| Ndugu. Charles O. Njovu | A/Tarafa – Mkumbi |
| Ndugu. Focus J. Mgeni | A/Tarafa – Kigonsera |
| Ndugu. Enhard C. Ndunguru | A/Tarafa TC+DC |
| Ndugu. Kanisius B. Mwela | M/Kiti Kikundi Litembo |
| Ndugu. Makarius G. Kinunda | Katibu wa kikundi Litembo |
| Ndugu. David B. Mapunda | Mwandishi wa habari |
| Ndugu. Joseph Mhagama | AgTPW |
| Ndugu. Mlomi V | TI |
| Ndugu. Samwel J. Marwa | DT Mbinga DC |
| Ndugu. Maurus B. Hyera | DLNRO Mbinga DC |
| Ndugu. Stephano A. Chipangapole | Kaimu TPNRO |

| | |
|---|---|
| Ndugu. Hassan A. Mlupilo | WEO – Namswea |
| Ndugu. Andrea John Mhagama | WEO - Mbinga Mjini |
| Ndugu. Enea Stephen Inyekule | WEO – Mkumbi |
| MH. Evelin Alanus Mwitumba | Diwani – Ukata |
| MH. Tiem Kayombo | Diwani – Namswea |
| MH. Anna L. Kapinga | Viti Maalam/Mhongozi |
| MH.Bruno L. Kapinga | Diwani – Mkumbi |
| Ndugu. Shukuru A. Msimbe | THS |
| Dr. Kunge K. Nyamuryekunge | TMO |
| Ndugu. Alex Watson | M/Habari |
| Ndugu. Mfaume Cassim | DHRO Mbinga DC |
| Ndugu. Charles C. Yapesa | PLO - MTC |

**KUTHIBITISHA AGENDA**

Kikao kilithibitisha Agenda 16 zifuatazo.

1. Kufungua kikao
2. Utambulisho
3. Kupitia Muhtasri wa kikao cha tarehe 17.11.2021
4. Yatokanayo na kikao cha taehe 17.11.2021
5. Taarifa za utekelezaji wa mpango na Bajeti za Halmasahuri
    - Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga
    - Halmashauri ya Mji wa Mbinga
6. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TARURA
    - Viambatanisho
7. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TRA
8. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TANESCO
9. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za RUWASA

10. Taarifa ya chama kikuu cha ushirika Mbinga (MBIFACU)
11. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wakala wa Misitu
12. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za MBIUWASA
13. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TANROAD
14. Taarifa ya mapato ya Halmashauri
    - Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga
    - Halmashauri ya Mji wa Mbinga
15. Mengineyo
16. Kufunga kikao

**HWM/DCC/01/2020-21 : KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5 :28 asubuhi kwa kuwajulisha wajumbe kuwa walichelewa kwa sababu ya mwingiliano wa majukumu, hivyo aliwasihi wajumbe watumie muda vizuri ili kikao kifikie malengo kwa majadiliano yenye ufanisi.

**HWM/DCC /02/2020-21 : UTAMBULISHO**

Wajumbe wote walipewa nafasi ya kujitambulisha kwa makundi.

**HWM/DCC/03/2020-21 : KUPITIA MUHTASRI WA KIKAO CHA TAREHE 17.11.2021**

Muhtasari huo ulipitiwa kwa kuongozwa na Mwenyekiti kwa kupitia ukurasa kwa ukurasa, kisha ulisainiwa kuwa kumbukumbu muhimu ya Halmashauri.

**HWM/DCC/04/2020-21 : YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 17.11.2021**

Wajumbe walishauri kuwe mgawanyo wa kata umepitishwa isipokuwa wahusika watendaji kata waandike barua za kujieleza kwa nini waliandika muhtasari tarehe

16.11.2021 kwa kata ya Kilimani na tarehe 10.11.2021 kwa kata ya Mpepai wakati kikao cha kamati ya ushauri kiliketi 08.01.2021. Ilijibiwa Mtendaji wa kata ya Mpepai ameandikiwa barua ya kujieleza yenye kumb. N. MTCC/L.10/03.VOLII/98 YA TAREHE 25.11.2021 na Mtendaji wa Kata ya Kilimani naye ameandikiwa barua ya kujieleza Kumb.Na.L.10/03/VOL.III.98 ya Tarehe 25.11.2021

Wajumbe walishauri kuwa kikako kijachoTANROADS waalikwe kwenye kikao. Ilijibiwa kuwaTANROADS walialikwa

Wajumbe walishauli kuwa TANESCO iwasilishe majibu kikao kijacho ya kupeleka umeme kwenye shule zote za sekondari za serikari ili wanafunzi waweze kujisomea. Ilijibiwa taarifa itatolewa kikaoni

Fedha miradi ya maji inayofikia SUWASA fedha hiyo iletwe moja kwa moja MBIUWASA kukamiisha mradi. Ilijibiwa miradi iliyokuwa inatekelezwa na mamlaka ya mjini Songea ya Luwaita,Mnyangayanga,na Amanimakoro imekabidhiwa RUWASA hivyo fedha ya milradi hiyo inaingia mojakwa moja RUWASA

ushauri ulitolewa kuwa vituo vya Rasilimali kilimo (ward resource center) hivyo vifanye kazi iliyokusudiwa na Halmashauri zitenge fedha kwaajili ya ukarabati mathalani kituo cha Mkako Ilijibiwa kuwa Ushauri umezingatiwa majengo ya mkako yanatumika kama ofisi za halmashauri pindi ofisi zikikamilika kazi kusudiwa itafanyika

Aidha kwa kituo cha maguu kiasi cha Tsh 25,000,000.00 zimetengwa katika bajeti ya 2022/2023.

**HWM/DCC/05/2020-21 : TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI NA MATUMIZI WA HALMASHAURI MBINGA MJI**

Kaimu mkuu wa idara ya mipango wa Halmashuri ya Mji aliwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2020/2021.Aidha alielezea fedha idhinishwa kuwa ni Tsh.20,402,459,529,fedha pokelewa ambazo zilikuwa ni Tsh.15,812,071,147.85 na fedha zilizotumika ambazo ni Tsh15,812,071,147.85 sawa asilimia 100.Taarifa yake ilielezea mafanikio ya utekelezaji kwa mwaka

2020/2021.Mwenyekiti aliwapitisha wajumbe kurasa kwa kurasa na hakukuwa na majadiliano.

Mheshimiwa mwenyekiti kwa muhtasari huu kila idara na vitengo waliweza kutoa mafanikio na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 katika kipindi cha julai 2020 juni 2021 kupitia shughuli mbalimbli zilizotekelezwa kama ifuatavyo;

Kupitia utawala halmashauri imefanikiwa shughuli zote mfano vikao

**HWM/DCC/06/2020-21 : TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI ZA HALMASAHURI HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango aliwasilisha tarifa yake na kuelezea maeneo yafuatayo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021 ilikadiria kukusanya jumla ya Tsh.39,526,810,551.97 kwa ujumla. Kati ya hizo fedha Tsh.4,691,336,000 ni mapato ya ndani na fedha Tsh.34,835,474,551.97 ni za ruzuku kutoka serikali kuu kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi. Wajumbe walipitishwa ukurasa kwa ukurasa kuanzia ukurasa wa 47 hadi 71 na hakukuwa na mchango.

**HWM/DCC/07/2020-21 : TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TARURA**

Meneja wa TARURA aliwasilisha taarifa yake na kuelezea mtandao wa barabara wanaouhudumia wenye jumla ya km 2,037.15 ambapo km 1,063.51 zipo mbinga mjini na km 973.64 zipo mbinga vijijini. Taarifa yake ilielezea hali za barabara kwa wilaya nzima. Aidha alielezea idadi ya madaraja, maboksi kalavati, makalavati, na madrifti. Taarifa ilipokelewa. Aidha wajumbe walipitishwa ukurasa kwa ukurasa na hakukuwa na mjadala.

**HWM/DCC/08/2020-21 : TAARIFA ZA UTEKELEZAJI SHUGHULI ZA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

Meneja wa TRA aliwasilisha taarifa yake na kuelezea vipengele a hadi e vikielezea mambo yafuatayo ;-

Malengo ya kodi mwezi Novemba 2021 hadi mei 2022

Idadi ya wafanyabiashara waliopewa namba ya utambulisho ya mlipa kodi kwa kipindi cha mwezi Novemba 2021 mpaka mei 2022 kuwa ni 462

Idadi ya wafanyabishara waliotozwa adhabu kwa kutotumia mashine za kutolea risiti za kielektroniki kwa usahihi ambao jumla walikuwa ni 36.

Idadi ya wafanyabiashara wealiokaguliwa mahesabu ambao ni 23

Vijiji na mitaa vilivyotembelewa kwa ajili ya makadirio ya kodi na elimu kwa kipindi cha mwezi novemba 2021 mpaka mei 2022.

Aidha alielezea changamoto wanazokabiliana nazo ikiwa ni pamoja na wananchi kutokuwa na elimu kuhusu kutoa na kudai risiti kwa kila mauzo na manunuzi.

Taarifa ilipokelewa na hakukuwa na mjadala

**HWM/DCC/09/2020-21 : TAARIFA ZA UTEKELEZAJI SHUGHULI TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY(TANESCO)**

Meneja wa TANESCO aliwasilisha taarifa yake na kuelezea vipengele vikieleza mambo yafuatayo ; -

Matengenezo ya miundombinu.

Uthibiti mapato ya shirika na kazi zilizofanyika

Uunganishaji wa wateja wapya Idadi wateja waomba ni 1005 na idadi ya maombi yaliyofanyiwa kazi ni 1041

Miradi iliyofanyika kusogeza miundombinu ya umeme kwa wateja.

Utekelezaji wa miradi ya REA III Mzunguko II

Aidha alieleza changamoto wanazokutana nazo ikiwa ni pamoja na umeme uhaba wa wafanyakazi na uhaba wa vifaa vya kuunganishia umeme wananchi.

Taarifa imepokelewa na hakukuwa na mjadala.

**HWM/DCC/10/2020-21: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI SHUGHULI WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA)**

Meneja wa RUWASA aliwasilisaha taarifa yake na kuelezea vipengele vifuatavyo ; -

Hali ya upatikanaj wa maji ambapo jumla ya Vijiji 166 vinahudumiwa na RUWASA.

Vyanzo vya Maji vinavypatikana katika wilaya ya Mbinga ambapo alisema jumla yavyanzo vipatavyo 835 vilivyotambuliwa

Utekelezaji wa miradi ya Bajeti 2021/2022

Ukamilishwaji wa miradi ya maji ambapo alisema jumla ya miradi 8 yenye vituo vyakuchotea maji vipatavyo 62 vitakavyohudumia watu wapatao 29469 vimekamilishwa

Kufanyika ujenzi /Ukarabati wa miradi maji ambapo alisema jumla ya miradi 8 vimefanyiwa ukarabati

Mapokezi ya fedha na utekelezaji wa miradi hiyo

Kufanya uendelevu wa miradi ya maji

Mpango wa utekelezaji wa bajeti ya 2022/2023

Aidha pamoja na utekelezaji huo alisema wamekutana na changa moto zifuatazo wananchi kutochangia Ankara za Maji kupelekea kufa kwa miradi, Kupungua kwa maji tabaka la juu na Uhaba wa vitendea kazi hususani Magari

Wajumbe walipokea taarifa na hakukua na majadiliano

**HWM/DCC/11/2020-21: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI SHUGHULI CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA MBINGA (MBIFACU LTD)**

Meneja wa chama kikuu cha ushirika aliwasilsha taarifa yake ikiwa na vipengele vifuatavyo ;-

Utangulizi ambapo alisema chama kilianzishwa tarehe 14/08/2000 na kupewa namba za usajili 5556.

Shughuli za MBIFACU

Usimamizi wa makusanyo, mauzo na malipo ya zao la kahawa

Usuluhishi wa migogoro wa migogoro wa vyama vya msingi

Elimu ya Ushirika

Michango ya maendeleo

Upatikanaji wa pembejeo

Utekelezaji wa miradi ya chama ambapo alisema kuna miradi miwili ambapo alisema kuna shamba la miti kitelea na MBICU HOTEL

Mafanikio ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

Aidha pamoja na utekelezaji huo alisema wamekutana na changamoto zifuatazo ambapo alisema ukosefu wa sheria ndogo ndogo na upatikanaji wa mitambo ya kisasa na matumizi kidogo ya pembejeo

Wajumbe walipokea na hakukuwa na wajumbe walijadili kama ifuatavyo Mshiriki toka mahenge alihoji kuhusu chama cha ushirika Litembo aliomba kibadilishiwe uongozi kutokana na migogoro kati yao na wanachama kutokana na mgogoro. Mwenyekiti aliunda kamati kwakushirikiana na mshiriki toka Litembo ambaye ni Kalistus A Hyera

**HWM/DCC/12/2020-21: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI SHUGHULI WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU (TFS)**

Mhifadhi misitu mkuu Mbinga aliwasilisha taarifa yake ikiwa na vipengele vifuatavyo ;-

Utangulizi

Doria ambapo amesema jumla ya doria 33 zimefanywa nakupata jumla ya hifadhi tatu walizifanyia patro

Kuimarisha na kuhakiki mipaka ya misitu ambapo alisuma jumla ya mipaka 25 imehakikiwa

Uzalishaji na ugawaji wa miche kwa ajli ya wananchi na tasisi mbalimbali ambapo jumla ya miche 1,333,518. Ilizalishwa na jumla ya miche 566,652.

Ukusanyaji wamaduhuli ambapo alisema TFS walipewa mgao wa kukusanya Tsh 75,178,150. Fedha hizo hukusanywa kwa mazao na faini mbalimbali ya misitu na wamefanikiwa kukusanya jumla ya Tsh 109,868,016. Sawa na asilimia 139.5.

Utoaji wa Elimu ya kuzuia na kupambana na moto katika misitu

Aidha pamoja na utekelezaji huo wa kazi wamekumbana changamoto zifuatazo ambazo ni uchache wa watumishi na upungufu wa vitendea kazi.

Wajumbe wa lipokea taarifa hiyo na hakukuwa na majadiliano.

**HWM/DCC/13/2020-21 : MENGINEYO**

Hakukuwa na mengineyo

**HWM/DCC/14/2020-21 : KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga kikao mwenyekiti alisema kutakuwepo na Rayol Tours ambayo imeletwa Mh Rais wa Tanzania hivyo nivema watu wote wakashiriki Kikao kilifungwa saa 07 ;39 mchana

**= UMETHIBITISHWA=**

**MWENYEKITI…......................... KATIBU...........................................**

**TAREHE:......................................**

## 8.4 WILAYA YA NAMTUMBO

### HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO

### MUHTASARI WA KIKAO CHA WATAALAM OFISI YA MKUU WA WILAYA NA WATAALAM OFISI YA MKURUGENZI KILICHOFANYIKA OFISI YA MKUU WA WILAYA YA NAMTUMBO TAREHE 22/12/2022.

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA,**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Dr Julius K Ningu | Mkuu wa Wilaya Namtumbo | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Hamis Mkelle | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3. | Bw. Aden Nchimbi | Katibu Tawala (W) | Mjumbe |
| 4. | Mh. Juma Alfan Pandu | Diwani Kata ya Mkongo Gulioni | Mjumbe |
| 5. | Bw. Acheni S. Maulidi | Katibu CCM (W) | Mjumbe |
| 6. | Bw. Seleman Ismail | Kaimu DSO | Mjumbe |
| 7. | CAPT AP Kisava | Mshauri Jeshi la Akiba (W) | Mjumbe |
| 8. | A/INSP O. Mapunda | Mkaguzi – Magereza | Mjumbe |
| 9. | Bw. Claus S. Mdemu | DIO . Namtumbo | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIO HUDHURIA KWA TAARIFA:-**

1. Hakuna

SEKRETARIETI:

2. Bw. Solomon Hyera Mwandishi wa Kikao.

**DONDOO NA.NMT/DC/01/2022/2023: KUFUNGUA KIKAO**.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe katika kikao hicho muhimu akiwasihi kuchangia ili kuleta Maendeleo ya Wilaya. Mwenyekiti pia aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano katika kuleta maendeleo. Mwisho alitamka kufunguliwa kikao saa 06:00 mchana.

**DONDOO NA.NMT/DC/02/2022/2023: KURIDHIA AGENDA.**

Wajumbe waliwasilishiwa agenda za kikao na waliridhia jumla ya agenda 5 zilizo wasilishwa kujadiliwa katika Mkutano huo ambazo ni:-

1. Kufungua kikao.
2. Kusoma na kuridhia agenda za kikao.

3. Mapendekezo ya uundaji wa maeneo mapya ya Kiutawala, kitarafa, kikata, na vijiji pamoja na mapendekezo ya kugawa jimbo la Namtumbo. Ombi maalum la kuongezewa eneo la utawala mamlaka ya mji mdogo wa Lusewa na pendekezo la kuligawa jimbo la Namtumbo.
4. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
5. Kufunga kikao

**DONDOO NA.NMT/DC/03/2022/2023: MAPENDEKEZO YA UUNDAJI WA MAENEO MAPYA YA KIUTAWALA,KITARAFA,KIKATA,NA VIJIJI OMBI MAALUM LA KUONGEZEWA ENEO LA UTAWALA MAMLAKA YA MJI MDOGO WA LUSEWA PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA KUGAWA JIMBO LA NAMTUMBO.**

Taarifa iliwasilishwa ikieleza kuwa katika kuimarisha utawala bora, Kikao cha kamati yua Ushauri Wilaya ya Namtumbo (DCC) kiliwasilisha mapendekezo ya uundaji wa maeneo mapya ya kiutawala ngazi ya Tarafa, Kata, Vijiji na Ombi Maalum la kuongezewa eneo la utawala mamlaka ya Mji Mdogo wa Lusewa pamoja na mapendekezo ya kugawa jimbo la Namtumbo katika Kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya (DCC) cha tarehe 17/11/2021 ambapo kikao kilipitia mapendekezo mbalimbali ya maombi ya kuomba kugawa Tarafa mpya 4, **Tazama Jedwali Namba 105**, Kata mpya 11 **Tazama Jedwali Namba 106**, Vijiji vipya 21 **Tazama Jedwali Namba 107** na kuongeza eneo la utawala la Mamlaka ya Mji wa Lusewa **Tazama kiambatisho: A**, Pia kikao kimetoa mapendekezo ya kugawa jimbo la Namtumbo na kuwa na Majimbo mawili Namtumbo Kusini na Namtumbo Kaskazini. **Tazama Jedwali Namba 108**,

Agenda hii ilipitishwa kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya cha tarehe 16/11/2016 na ilirudia tena kupitishwa katika kikao cha kamati ya ushauri Wilaya cha tarehe 28/12/2020 pia kikao cha Kamati ya ushauri Wilaya cha tarehe 17/11/2021 kilipitia tena mapendekeo hayo tena kwa umuhimu wake.

Taarifa hiyo ilipitiwa tena na Viongozi toka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na wataalam Ofisi ya Mkurugenzi ili kuweza kuwasilishwa tena Katika Kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa RCC kutokana na umuhimu wake.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walitoa maoni ushauri na maagizo kama ifuatavyo

- Wajumbe walishauri Maeneo yanayogawika yahakikishwe yanaangaliwa vizuri kabla ya kugawa hususani katika kuangalia kaya na eneo la utawala takwimu ziwe na uhalisia na mipaka ya eneo husika ibainishwe vizuri
- Wajumbe walishauri kuhakikisha maeneo ya kiutawala yanayogawika yanazingatia mambo muhimu ikiwemo huduma za kijamii kama shule na huduma za afya
- Wajumbe walishauri katika kugawa maeneo ya kiutawala maeneo ya hifadhi yahakikishwe hayaingiliwi na kama yamependekezwa yaondolewe.
- Wajumbe walishauri kuhakikisha maeneo yanayo gawika kuangaliwa idadi ya watu na eneo la kijiografia ili kuwa na uwiano mzuri pale eneo litakapogawika.

**DONDOO NA.NMT/DCC/04/2022/2023: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hakukuwa na mengineyo

**DONDOO NA.NMT/DCC/05/2022/2023: KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao, kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri alihimiza yaliyojadiliwa na kuazimiwa katika kikao kutekelezwa kwa wakati .Mwisho kikao kilifungwa saa 07:32 Mchana.

UMETHIBITISHWA,

…………………… ………………………………

SAINI YA MWENYEKITI SAINI YA KATIBU

TAREHE 22/12/2022.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO**

**MAPENDEKEZO YA UUNDAJI WA MAENEO MAPYA YA KIUTAWALA KI TARAFA, KIKATA NA VIJIJI OMBI MAALUM LA KUONGEZEWA ENEO LA UTAWALA MAMLAKA YA MJI MDOGO WA LUSEWA PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA KUGAWA JIMBO LA NAMTUMBO**

**KWENYE KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC)**

## 1. UTANGULIZI

Katika kuimarisha utawala bora, Kikao cha kamati yua Ushauri Wilaya ya Namtumbo (DCC) cha tarehe 17/11/2021 kinawasilisjha mapendekezo ya uundaji wa maeneo mapya ya kiutawala kitarafa, kikata na vijiji ombi maalum la kuongezewa eneo la utawala mamlaka ya mji mdogo wa lusewa pamoja na mapendekezo ya kugawa jimbo la namtumbo.

Kikao cha Kamati ya ushauri Wilaya (DCC) cha tarehe 17/11/2021 kimepitia mapendekezo mbalimbali ya maombi ya kuomba kugawa Tarafa mpya 4, **Tazama Jedwali Namba 105**, Kata mpya 11 **Tazama Jedwali Namba 106**, Vijiji vipya 21 **Tazama Jedwali Namba 107** na kuongeza eneo la utawala la Mamlaka ya Mji wa Lusewa **Tazama kiambatisho:A**, Pia kikao kimetoa mapendekezo ya kugawa jimbo la Namtumbo na kuwa na Majimbo mawili Namtumbo Kusini na Namtumbo Kaskazini. **Tazama Jedwali Namba 108**,

Agenda hii ilipitishwa kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya cha tarehe 16/11/2016 na ilirudia tena kupitishwa katika kikao cha kamati ya ushauri Wilaya cha tarehe 28/12/2020 pia kikao cha Kamati ya ushauri Wilaya cha tarehe 17/11/2021 kilipitia tena mapendekeo hayo.

Kwa kuzingatia umuhimu wake naomba kuwasilisha kwenye kikao cha Kamati ya ushauri wa Mkoa (RCC) mapendekazo hayo kwa ajili ya kutoa maamuzi.

Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya kimepitia mapendekezo ya kuomba kuongeza idadi ya Tarafa kutoka 3 zilizoko sasa hadi kufikia tarafa 7. Mchanganuo wa mapendekezo ya mgawanyo wa Tarafa ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 105

**MAPENDEKEZO YA MAOMBI YA KUPANUA ENEO LA UTAWALA KATIKA MAMLAKA YA MJI MDOGO WA LUSEWA na MAPENDEKEZO YA KUGAWA JIMBO LA UCHAGUZI**

Aidha Kamati ya ushauri wilaya iliwasilisha mapendekezo ya kuongeza maeneo ya kiutawala katika Mamlaka ya mji mdogo wa Lusewa ili iweze kupanga mipango yake, kata ambazo zinaombewa kuongeza eneo la utawala ni kata za **Magazini** ,**Msisima Lisimonji**, **Limamu** na **Ligera.**

**Pia** Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo iliomba kugawa jimbo jimbo la Namtumbo na kuwa na majimbo mawili jimbo la Namtumbo KUSINI na Namtumbo KASKAZINI Kwa kuzingatia umuhimu wake, majimbo haya yataundwa na Kata mama na kata mpya kama zinavoonekana katika jedwali. Jedwali Na. 106 **Mapendekezo ya Kata mpya** Jedwali Na. 107 **Mapendekezo ya maombi ya Vijiji vipya**

## 7. HITIMISHO

Naomba kuwasilisha Mapendekezo haya ili wajumbe waweze kupitia ili kutoa maamuzi kulingana na vigezo na uwezo wa Serikali katika kuwezesha kukamilika kwa zoezi hili muhimu kwa kuharakisha maendeleo ya Wananchi wa Namtumbo.

Naomba kuwasilisha,

Dr.Julius K. Ningu

Mwenyekiti wa kamati ya ushauri ya Wilaya,

**NAMTUMBO – RUVUMA**

**JEDWALI NA. 105: MAPENDEKEZO YA UUNDAJI WA TARAFA MPYA KATIKA WILAYA YA NAMTUMBO.**

| NA | TARAFA MAMA | TARAFA MPYA | KATA MAMA | KATA MPYA | VIJIJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MKONGO | NAMABENGO | Namabengo | - | Namabengo, | Hakuna mabadiliko |
| | | | | | Nambalama | |
| | | | | | Mdwema, | |
| | | | | | Utwango | |
| | | | | | **Kanjele** | **Kijiji Kipya** |
| | | | Hanga | - | Hanga | |
| | | | | | Ruvuma | |
| | | | | **Mlilayoyo** | Mlilayoyo, | **Kata Mpya** |
| | | | | | Mawa | |
| | | | | | Mageuzi | |
| | | | Msindo | - | Msindo<br>Nambehe | |
| | | | | **Lumecha** | Lumecha | |
| | | | | | Mtakanini | |
| | | | | | **Kidugaro** | **Kijiji Kipya** |
| | | | Litola | - | Litola , Kumbara | |
| | | | | | Ngwinde na Mbimbi | |
| 2 | MKONGO | LIGERA | Ligera | - | ligera | |
| | | | | | Muungano | |
| | | | | | Mterawamwahi | |
| | | | | | Namahoka | |
| | | | | | Njoomlole | |
| | | | Lismonji | - | Matepwende | |
| | | | | - | Namali | |
| | | | | - | Ulamboni | |
| | | | | -<br>- | **Jiungeni** | **Kijiji Kipya** |
| | | | Limamu | | Limamu | |
| | | | | | Mtakuja | |
| | | | | | **Tumaini** | **Kijiji Kipya** |
| | | | | | **Mkomaindo** | **Kijiji Kipya** |
| 3 | UNDENDEULE | NAMTUMBO | Namtumbo | - | - | Ipo ndani ya Mji wa Namtumbo |
| | | | | Libango | - | |
| | | | | Suluti | - | |
| | | | Rwinga | - | - | Ipo ndani ya Mji wa Namtumbo |
| | | | | Mandepwende | - | |
| | | | | Minazini | - | |
| | | | Mchomoro | - | Kilimasera | - |
| | | | | | **Mingwea** | **Kijiji Kipya** |
| | | | | | Mchomoro | |
| | | | | | Masuguru | |
| | | | | | Songambele | |

| NA | TARAFA MAMA | TARAFA MPYA | KATA MAMA | KATA MPYA | VIJIJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Luegu | - | Luegu | - |
| | | | | | Nahoro | |
| | | | | | Ukiwayuyu | |
| | | | | | Mtwarapachani | |
| 4 | SASAWALA | MAGAZINI | Magazini | | Amani | |
| | | | | | Magazini | |
| | | | | | Sasawala | |
| | | | | **Likusanguse** | **Mji Mwema** | **Vijiji vipya na Kata Mpya** |
| | | | | | **Kilolelo** | |
| | | | | | Likusanguse | |

## 1. MAPENDEKEZO YA KATA MPYA NA VIJIJI VIPYA

Katika kuboresha utoaji wa huduma za kiutawala inapendekezwa Kata 11 na Vijiji 20 viongezwe. Mchanganuo Majedwali Na. 106 na 107 hapa chini umefafanua.

**Jedwali Na. 106: Mapendekezo ya Kata mpya**

| NA | TARAFA MAMA | TARAFA MPYA | KATA MAMA | KATA MPYA | IDADI YA KAYA | HUDUMA ZA KIJAMII |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UNDENDEULE | NAMTUMBO | Namtumbo | **Suluti** | 1201 | Shule 2 za Msingi, Kituo kidogo cha utafiti cha Kilimo, Zahanati, Kituo cha Kibiashara, eneo lenye ushawishi mkubwa wa Kisiasa |
| | | | | **Libango** | **788** | Zahanati, Shule 2 za Msingi na Barabara, Maghala ya Mazao 2, Vyanzo vya Maji ya Mtiririko ya Bomba, Misikiti 4 Makanisa 2 maeneo ya makazi na kilimo ya kutosha Ramani imeambatishwa |
| | | | Rwinga | **Minazini** | **1050** | Shule za Msingi 2, Shule za Sekondari 2, Machinjio ya Kisasa 1, Chuo cha Kanisa la Upendo, Maghala 2, Ofidsi ya Kijiji, Misikiti 3, Makanisa 2, Huduma za Maji, Barabara zinazopitika, Mawasiliano ya simu za Mkononi. Ramani imeambatishwa |
| | | | | **Mandepwende** | **1277** | Shule za Msingi 2, Sekondari 1, Hospitali ya Wilaya, Maghala 2, Ofisi za vijiji 2, Majengo ya Kampuni ya Barabara, Misikiti 3, Huduma za maji, Barabara zinazopitika na ramani imeambatishwa |

## JEDWALI NA. 106: MAPENDEKEZO YA KATA MPYA

| NA | TARAFA MPYA | TARAFA MAMA | KATA MAMA | KATA MPYA | IDADI YA KAYA | HUDUMA ZA KIJAMII |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | SASAWALA | Lusewa | **Milonji** | **990** | Zahanati, Ofisi, Huduma ya maji, Shule ya Msingi 1 Msikiti, Ardhi inayofaa kwa kilimo na ufuagaji, Maduka ya biashara.Ramani imeambatishwa |
| | | | | **Ligunga** | **830** | Shule za Msingi 2, Makanisa 2, Ofisi, Soko, Zahanati, Chuo cha VTC, Huduma ya maji na Barabara. Ramani imeambatishwa. |
| | | | Magazini | **Likusanguse** | **933** | Shule 2 za Msingi, Zahanati 1, Ofisi a Kijiji 1 Ofisi ya Jumuiya ya Hifadhi 1 na Barabara. Kanisa la Biblia na Msikiti.Ramani imeambatishwa |
| **2** | | **UNDENDEULE** | Mgombasi | **Nambecha** | **971** | Shule za Msingi, Zahanati na Barabara inayopitika Maghala makubwa ya Mazao |
| | | | Kitanda | **Mbunga** | **959** | Shule za Msingi, Shule ya Sekondari, Barabara ya lami na maeneo ya kutosha kwa ajili ya Ofisi. |

## JEDWALI NA. 107: MAPENDEKEZO YA MAOMBI YA VIJIJI VIPYA

| NA. | KATA | KIJIJI MAMA | IDADI YA KAYA | KIJIJI KIPYA | IDADI YA KAYA | HUDUMA ZA KIJAMI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kitanda | Kitanda | 893 | **Mkomanile** | 277 | Shule ya Msingi 1, Shule ya Sekondari 1 maeneo kwa ajili ya Ofisi yametengwa |
| | | | | **Kipiki** | 262 | Maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu yapo |
| 2 | Mputa | Luhimbalilo | 757 | **Maputo** | 303 | Shule ya Msingi 1 na maeneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi pia kina eneo la hifadhi |
| 3 | **Nambecha** | Mgombasi | 810 | **Mliwasi** | 329 | Shule ya Msingi ipo na eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi |
| | | Nambecha | 921 | **Mkuyuni** | 209 | Shule ya Msingi Shule ya Msingi ipo na eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi |
| 4 | Likuyuseka | Mtonya | 691 | **Muungano** | 276 | Maeneo ya kujenga shule na ofisi yapo ya kutosha |
| | | Likuyuseka | 817 | **Mfuate** | 289 | Shule ya Msingi, Eneo la ujenzi wa Ofisi, wazalishaji wa mazao kwa wingi kikata |
| | | Likuyumandela | 624 | **Miembeni** | 205 | Shule ya Msingi Shule ya Msingi ipo na eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi |
| 5 | Namabengo | Utwango | 427 | **Kanjele** | 299 | Shule ya Msingi, Huduma za Simu, Maeneo ya kujenga |

| NA. | KATA | KIJIJI MAMA | IDADI YA KAYA | KIJIJI KIPYA | IDADI YA KAYA | HUDUMA ZA KIJAMI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | zahanati na barabara inayopitika |
| 6 | **Lumecha** | Lumecha | 496 | **Kidugaro** | 260 | Shule ya awali, Msikiti, na Barabara. Ramani imeambatishwa |
| 7 | Luchili | Chengena | 389 | **Liyuni** | 256 | Mkondo 1 wa Shule ya Msingi, Barabara inayopitika |
| 8 | Mkongo | Njalamatata | 286 | **Mitoronji** | 263 | Shule ya Msingi 1 Kanisa 1 huduma ya maji, mawasiliano ya simu maeneo ya ujenzi wa ofisi na barabara |
| 9 | Mkongo Gulioni | Mkongo Gulioni | 298 | **Litete** | 261 | Shule ya Msingi 1 maeneo ya ujenzi wa ofisi na barabara |
| | | | | **Mlindimila** | 257 | Maeneo ya ujenzi wa Shule, ofisi na barabara |
| **10** | Magazini | Likusanguse | 943 | | 261 | Shule ya Msingi , Ofisi ya Kijiji,na Jumuiya, Huduma za maji Barabara na Kanisa Ramani imeambatishwa |
| | | | | **Mjimwema** | 262 | Msikiti, Huduma za Maji na Barabara |
| | | | | **Majengo** | 260 | Barabara huduma za maji |
| | | | | **Semeni** | 160 | Shule ya Msingi 1 Maeneo ya hifadhi |
| **11** | Limamu | Limamu | 611 | **Tumaini** | 321 | Makao makuu ya Chama cha Msingi, Shule ya Msingi na maeneo ya kujenga ofisi yametengwa |
| | | | | **Mkomaindo** | 262 | Meneo ya kujenga Ofisi yametengwa |
| **12** | Lismonji | Matepwende | 261 | **Jiungeni** | 253 | Shule ya Msingi na barabara inapitika |
| **13** | Msindo | Msindo | 601 | **Pacha nne** | 327 | Meneo ya kujenga Ofisi yametengwa |

## MAPENDEKEZO YA MAOMBI YA KUPANUA ENEO LA UTAWALA KATIKA MAMLAKA YA MJI MDOGO WA LUSEWA

Kamati ya ushauri wilaya inaomba kuwasilisha mapendekezo ya kuongeza maeneo ya kiutawala katika Mamlaka ya mji mdogo wa Lusewa ili mamlaka hiyo iweze kuanza kuongeza ukusanyaji wa mapato yake ya ndani na kupanga mipango yake kata ambazo zinaombewa kuongeza eneo la utawala ni kata za **Magazini** ,**Msisima Lisimonji**, **Limamu** na **Ligera.**

### 4.0 MAPENDEKEZO YA KUGAWA JIMBO LA UCHAGUZI

Katika kuimarisha Utawala Bora, mwaka 2019 Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo iliomba kugawa jimbo jimbo la Namtumbo na kuwa na majimbo mawili jimbo la Namtumbo KUSINI na Namtumbo KASKAZINI

### JEDWALI NAMBA 108 KUONESHA MGAWANYO WA JIMBO LA NAMTUMBO NA KATA ZAKE

| NA | JIMBO | TARAFA MAMA | TARAFA MPYA | | KATA MAMA | KATA MPYA | KIJIJI MAMA | KIJIJIKIPYA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **JIMBO LA NAMTUMBO KUSINI** | **SASAWALA** | **MAGAZINI** | **1** | **MAGAZINI** | LIKUSANGUSE | | MJIMWEMA |
| | | | | | | | | KILOLELO |
| | | | | | | | | **LIKUSANGUSE** |
| | | | | | | | AMANI | |
| | | | | | | | MAGAZINI | |
| | | | | | | | SASAWALA | |
| | | | | **2** | **LUSEWA** | **MILONJI** | | |
| | | **MKONGO** | **LIGERA** | **3** | **LIGERA** | | **LIGERA** | |
| | | | | | | | **MUUNGANO** | |
| | | | | | | | **MTELAWAMWAHI** | |
| | | | | | | | **NAMAHOKA** | |
| | | | | | | | **NJOMLOLE** | |
| | | | | **4** | **LISIMONJI** | | **MATEPWENDE** | **JIUNGENI** |
| | | | | | | | **NAMALI** | |
| | | | | | | | **ULAMBONI** | |

| NA | JIMBO | TARAFA MAMA | TARAFA MPYA | | KATA MAMA | KATA MPYA | KIJIJI MAMA | KIJIJIKIPYA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 5 | LIMAMU | | LIMAMU | |
| | | | | | | | MWANGAZA | |
| | | | | | | | MTAKUJA | TUMAINI |
| | | | | | | | | MKOMAINDO |
| | | | | 6 | MSISIMA | | MATEPWENDE | |
| | | | | | | | MLALAWIMA | |
| | | | | | | | MSISIMA | |
| | | | | | | | MNALAWI | |
| | NAMTUMBO KASKAZINI | UNDENDEULE | | 7 | MCHOMORO | | | MINGWEA |
| | | | | | | | | MINGWEA |
| | | | | | | | MCHOMORO | |
| | | | | | | | MASUGURU | |
| | | | | | | | SONGAMBELE | |
| | | MKONGO | | | | | KILIMASERA | |
| | | | | 8 | LUEGU | | UKIWAYUYU | |
| | | | | | | | NAHORO | |
| | | | | | | | MTWARA PACHANI | |
| | | | | 9 | NAMABENGO | | UTWANGO | KANJELE |
| | | | | | | | NAMABENGO | |
| | | | | | | | NAMBALAMA | |
| | | | | | | | UTWANGO | |
| | | | | | | | MDWEMA | |
| | | UNDENDEULE | | 10 | MPUTA | | MPUTA | |
| | | | | | | | LUHANGANO | |
| | | | | | | | LUHIMBALILO | |
| | | | | 11 | KITANDA | | KITANDA | |
| | | | | | | | NAIKESI | |
| | | | | | | | MHANGAZI | |
| | | NKONGO | NAMABENGO | 12 | HANGA | | HANGA | |
| | | | | | | | RUVUMA | |
| | | | | | | | MAWA | |
| | | | | | | | MAGEUZI | |
| | | | | | | MLILAYOYO | MLILAYOYO | |
| | | | | 13 | MSINDO | | LUMECHA | KIDUGARO |
| | | | | | | | MSINDO | |
| | | | | | | | MTAKANINI | |

| NA | JIMBO | TARAFA MAMA | TARAFA MPYA | | KATA MAMA | KATA MPYA | KIJIJI MAMA | KIJIJIKIPYA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | NAMBEHE | |
| | | **UNDENDEULE** | | **14** | **LIKUYUSEKA** | | MTONYA | MUUNGANO |
| | | | | | | | LIKUYUSEKA | MFUATE |
| | | | | | | | LIKUYUMANDELA | MIEMBENI |
| | | | **NAMTUMBO** | **15** | **RWINGA** | MANDEPEWENDE | | |
| | | | | | | MINAZINI | | |
| | | **UNDENDEULE** | | **16** | **NAMTUMBO** | LIBANGO | | |
| | | | | | | SULUTI | | |
| | | | | **17** | **MGOMBASI** | NAMBECHA | MGOMBASI | MLIWASI |
| | | | | | | | NAMBECHA | MKUYUNI |
| | | | | | | | MTUMBATI MAJI | |
| | | | | | | | NANGERO | |
| | | **MKONGO** | | **18** | **LUCHILI** | **CHENGENA** | | **LIYUNI** |
| | | | | | | | KILANGALANGA | |
| | | | | | | | NAMANGULI | |
| | | | | | | | MISUFINI | |
| | | | | **19** | **MKONGO GULIONI** | | **MKONGO GULIONI** | **LITETE** |
| | | | | | | | | **MLINDIMILA** |
| | | | | | | | **NAHIMBA** | |
| | | | | **20** | **MKONGO NAKAWALE** | | **NJALAMATA** | |
| | | | | | | | **MKONGO NAKAWALE** | |
| | | | | | | | **MWINUKO** | |
| | | | | **21** | **LITOLA** | | **LITOLA** | |
| | | | | | | | **KUMBARA** | |
| | | | | | | | **MBIMBI** | |
| | | | | | | | **NGWINDE** | |

## 8.5 WILAYA YA NYASA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI WILAYA YA NYASA (DCC) KILICHOFANYIKA TAREHE 08/12/2022 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA WILAYA YA NYASA

### NDC/DCC/2021-2022/001: MAHUDHURIO

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Aziza A. Mangosongo | Mkuu wa Wilaya Nyasa | Mwenyekiti |
| 2. | Ephrem H. Kawonga | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3. | Paul Lugongo | kaimu Katibu Tawala | Mjumbe |
| 4. | Eng Thomas Kitus | Meneja TARURA | Mjumbe |
| 5. | Abdallah Habibu | Kaimu Mweka Hazina (W) | Mjumbe |
| 6. | Chirstopher Ngonyani | Afisa mipango (W) | Mjumbe |
| 7. | Shanery Mbunda | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) | Mjumbe |
| 8. | Augustino Kapinga | KaimuAfisa Elimu Msingi (W) | Mjumbe |
| 9. | Pacific .I.Mhapa | Afisa kilimo | Mjumbe |
| 10. | Victory Kinunda | Kaimu Mtendaji Kata- Mabamba bay | Mjumbe |
| 11. | Eng Emmanuel Ndongole | kaimu meneja RUWASA | Mjumbe |
| 12. | Saidi Mailon | Mtendaji Kata- Liuli | Mjumbe |
| 13. | Michael Swati | DRO - NIDA | Mjumbe |
| 14. | Hairu Mchora | Kaimu menejea TANESCO | Mjumbe |
| 15. | Charles Chikuni | Mtendaji Kata- Chiwanda | Mjumbe |
| 16. | Martin Turuka | Mtendaji Kata- kihagara | Mjumbe |
| 17. | Onesphor Mwakatobe | Kaimu Afisa Usalama | Mjumbe |
| 18. | Dickson Nyoni | Mtendaji Kata- Kilosa | Mjumbe |
| 19. | Anzigar Lyimo | Kaimu Mhifadhi – liparamba | Mjumbe |
| 20. | John Mrina | Mganga mkuu (W) | Mjumbe |
| 21. | Mashalo Matola | Kaimu Afisa Biashara | Mjumbe |
| 22. | Eng Lulu Chilumba | Principal-VETA | Mjumbe |
| 23. | Frank Chintawi | Kaimu Mtendaji Kata- Mtipwili | Mjumbe |
| 24. | Allen Mshiu | Kaimu Muhandisi wa ujenzi | Mjumbe |
| 25. | Henry Youndey | Kaimu Afisa Manunuzi | Mjumbe |
| 26. | Zamoyoni Mpagike | Kaimu Afisa utumishi Wilaya | Mjumbe |
| 27. | Bernard Semwaiko | Afisa Mifugo, Kilimo na Uvuvi | Mjumbe |
| 28. | Bugingo Bugingo | Afisa uhifadhi Maliasili | Mjumbe |
| 29. | Dennis Mroki William | Kaimu Afisa Mazingira | Mjumbe |
| 30. | Said.O.Mailoni | Mtendaji Kata Liuli | Mjumbe |
| 31. | Maijob Juma Mbogo | CO Lundo | Mjumbe |
| 32. | Edward.M.Lilanga | Kaimu DIO | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 33. | Netho.C.Sichali | Afisa Habari | Mjumbe |
| 34. | Elias.L.Katulu | Mh.Diwani Kata ya Kilosa | Mjumbe |
| 35. | CO 4781A Gift Kawiche | Kaimu DFC-TFS | Mjumbe |
| 36. | Richard.Y.Chiwalo | Mh.Diwani Kata ya Mtipwili | Mjumbe |
| 37. | Philemon.A.Ngaponda | Karani wa Vikao | Mjumbe |
| 38. | Faustine .J.Magafu | CR-LGR | Mjumbe |

**WAALIKWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 39. | Ally Hassan Liungu | Kaimu Sheikh | Mwalikwa |

## NDC/DCC/2021-2022/002: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti wa kikao aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio na kuwataka kuwa makini katika kujadili Agenda, Alifungua kikao saa 5:20 Mchana.

## NDC/DCC/2021-2022/003: UTAMBULISHO

Wajumbe wote walijitambulisha kwa majina, nafasi zao za uwakilishi na taasisi wanazoziwakilisha. Kwa ujumla washiriki wa kikao walitoka katika makundi ya watumishi wa Serikali ambao walitoka kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji (W), vyombo vya ulinzi na usalama, TFS, TARURA, RUWASA na TANESCO. Washiriki wengine walitoka taasisi za benki, viongozi wa dini na wawakilishi wa vyombo vya habari.

## NDC/DCC/2021-2022/004: AGENDA ZA KIKAO

Kikao kilipokea agenda kama zinavyojieleza hapo chini;

1. Kufungua Kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kuthibitisha Mhtasari wa kikao cha tarehe 12/11/2021
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 12/11/2021
5. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa 2022/2023
6. Mrejesho wa Bajeti 2022/2023
7. Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 cha Robo ya kwanza 2022/2023

8. Taarifa ya Utekelezaji wa mango na bajeti ya mwaka 2022/2023 cha Robo ya kwanza 2022/2023
9. Taarifa ya Utekelezaji wa Idara na Taasisi
    a) Afya
    b) Elimu
    c) Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
    d) Mifugo na Uvuvi
    e) RUWASA
    f) NIDA
    g) TANESCO
    h) TARURA
    i) TFS
    j) Taarifa ya Shamba la Mpepo
    k) Taarifa ya Hifadhi ya Liparamba
    l) Taarifa za Taasisi za Kibenk
    m) TAKUKURU
10. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti
11. Kufunga kikao

**NDC/DCC/2021-2022/005:KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE** 12/11/2021

Ulisomwa Muhtasari wa kikao cha tarehe 12/11/2021ambapo kikao kiliridhia kuwa ni kumbukumbu halali za kudumu za Halmashauri.

**NDC/DCC/2021-2022/006:YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 12/11/2021**

Yalisomwa yatokanayo na kikao cha tarehe 12/11/2021 ambapo wajumbe walipokea na kuridhia.

**NDC/DCC/2021-2022/006: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA 2022/2023.**

**Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliwasilishwa**

Katika mwaka wa fedha **2021/22**, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa iliidhinishiwa kukusanya na kutumia **Tshs 24,857,180,300.00**kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kutoka vyanzo vya mapato ya ndani na Ruzuku ya Serikali Kuu. Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni **Tshs 15,013,038,000.00** (**Tshs 13,990,432,000.00**

mishahara na **Tshs 1,022,606,000.00** matumizi mengineyo) na fedha za miradi ya maendeleo ni **Tshs 8,606,629,300.00** (**Tshs 4,710,325,999.92** fedha za ndani, **Tshs 3,868,303,300.08** fedha za nje, na **Tshs 1,237,513,000.00** fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri).

Hadi kufikia **30 Juni, 2022** Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs 23,929,052,801.55** sawa na asilimia **96.27** kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni **Tshs 1,364,144,627.61** sawa na asilimia **110.23** (**Tshs 13,121,822,250.00** sawa na asilimia **98.65** ni mishahara na **Tshs 959,132,754.59** sawa na asilimia **98.65** ni matumizi mengineyo); na miradi ya maendeleo ni **Tshs 8,490,775,432.22** sawa na asilimia **98.65** (**Tshs 5,331,738,217.91.** sawa na asilimia **113.19** ni fedha za ndani, **Tshs 3,159,037,214.31** sawa na asilimia **81.08** ni fedha za nje, na **Tshs 170,137,830.00** sawa na asilimia **77.74.** ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri).

Aidha katika kipindi hicho Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 23,324,662,042.50** sawa na asilimia **93.83** Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni **Tshs 14,146,474,362.91** sawa na asilimia **94** (**Tshs 13,121,822,250.00** sawa na asilimia **93.79** ni mishahara na **Tshs 1,024,652,112.91** sawa na asilimia **100** ni matumizi mengineyo) na fedha za miradi ya maendeleo ni **Tshs 8,140,138,207.09** sawa na asilimia **94.58** (**Tshs 4,573,059,161.98** sawa na asilimia **97** fedha za ndani, **Tshs 3,396,941,215.11** sawa na asilimia **87** ni fedha za nje, na **Tshs 188,437,830.00** sawa na asilimia **100** ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri*)*.Jedwali Na. 01 linaonesha Bajeti iliyoidhinishwa, Mapato na Matumizi ya Halmashauri kwa mwaka 2022/2023.

## 2.0 MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

Katika mwaka 2022/2023 Halmashauri ilipangiwa kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs. 1,237,513,000.00** Kati ya fedha hizo, **Tshs 515,343,000.00.**ni Mapato lindwa, na **Tshs722,170,000.00**ni Mapato yasiyolindwa. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Halmashauri imekusanya **Tshs1,364,144,627.61**sawa na asilimia **110.23 (Tshs 566,480,290.08** sawa na asilimia109.92 niMapato lindwa, na **Tshs 797,664,337.53** sawa na asilimia 110.45 ni Mapato yasiyolindwa). Jedwali Na. 02 linaonesha mchanganuo wa makusanyo ya Mapato ya Ndani kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 3.0 BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2022/2023

Katika mwaka wa fedha **2021/22,** Halmashauri iliidhinishiwa fedha za Matumizi ya Kawaida kiasi cha **Tshs 15,446,340,000.00** sawa na asilimia 62 ya bajeti.Kati ya fedha hizo Mishahara ni**Tshs 13,990,432,000** ***(Tshs 13,990,432,000*** *kutoka Serikali Kuu)*na Matumizi Mengineyo ni **Tshs 1,455,908,000.00** ***(Tshs 1,022,606,000.00*** *kutoka Serikali Kuu,* ***Tshs 433,302,000.00*** *Mapato ya Ndani).*

Hadi kufikia **30 Juni, 2022** Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs 14,623,026,850** sawa na asilimia **95** ya Bajeti*.* Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Tshs 13,121,822,250** sawa na asilimia *93.79* ***(Tshs*****13,121,822,250** *sawa na asilimia 100 kutoka Serikali Kuu)*na Matumizi Mengineyo ni **Tshs1,501,204,600.00** sawa na asilimia **103** ***(Tshs 1,022,606,000.00*** *sawa naasilimia* ***100*** *kutoka Serikali Kuu,* ***Tshs 470,598,600*** *sawa na asilimia* ***110*** *Mapato ya Ndani).*

Aidha, hadi kufikia **30 Juni, 2022** Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 14,577,730,250** sawa na asilimia **99.69** ya fedha pokelewa. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Tshs 13,121,822,250** sawa na asilimia *93.79* ***(Tshs*** **13,121,822,250** *sawa na asilimia 100 kutoka Serikali Kuu)*na Matumizi Mengineyo ni **Tshs1,455,908,000** sawa na asilimia **97** ***(Tshs1,022,606,000*** *sawa naasilimia* ***100*** *kutoka Serikali Kuu,* ***Tshs 433,302,000*** *sawa na asilimia* ***91*** *Mapato ya Ndani).* Jedwali Na. 03 linaonesha mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 4.0 BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

Katika mwaka wa fedha **2021/22,** Halmashauri iliidhinishiwa fedha za Maendeleo kiasi cha **Tshs 8,895,497,300**sawa na asilimia 36.ya bajeti.Kati ya fedha hizo **Tshs 4,710,325,999.92** kutoka Serikali Kuu, **Tshs3,896,303,300** kutoka Nje na **Tshs 288,868,000** Mapato ya Ndani. Hadi kufikia **30 Juni, 2022** Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs 8,660,913,262.22** sawa na asilimia **97** ya Bajeti*.* Kati ya fedha hizo **Tshs 5,331,738,217.91** sawa na asilimia 113.19 kutoka Serikali Kuu, **Tshs 3,159,037,214.31**

sawa na asilimia 81.08 kutoka Nje na **Tshs188,437,830.00** sawa na asilimia **58.90** Mapato ya Ndani.

Aidha, hadi kufikia **30 Juni, 2022** Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 6,309,779,045.11** sawa na asilimia **73** ya fedha pokelewa. Kati ya fedha hizo **Tshs 3,396,941,215.11** sawa na asilimia 64 kutoka Serikali Kuu, **Tshs 2,742,700,000** sawa na asilimia 87 kutoka Nje na **Tshs 188,437,830.00** sawa na asilimia **100** Mapato ya Ndani. Jedwali Na. 04 linaonesha mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023

**Jedwali Na. 04** linaonesha mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023

| KASMA | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOPOKELEWA | ASILIMIA YA MAPOKEZI | FEDHA TUMIKA HADI KUFIKIA 30 JUNI, 2022 | ASILIMIA YA MATUMIZI | BAKAA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | 4,710,325,999.92 | 5,331,738,217.91 | 113.19% | 3,396,941,215.11 | 64% | 1,934,797,002.80 |
| Fedha za Nje | 3,896,303,300.08 | 3,159,037,214.31 | 81.08% | 2,742,700,000.00 | 87% | 416,337,214.31 |
| Mapato ya Ndani | 288,868,000.00 | 188,437,830.00 | 62% | 188,437,830.00 | 100% | - |
| **Jumla Kuu** | **8,895,497,300.00** | **8,660,913,262.22** | 97.36% | **6,328,079,045.11** | 73% | **2,351,134,217.11** |

## 5.0 MIRADI YA MAENDELEO KUPITIA FEDHA ZA SERIKALI KUU (NDANI NA NJE)

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ilipanga kutekeleza jumla ya Miradi **62** ya Maendeleo yenye thamani ya **Tshs** kupitia fedha za Ruzuku ya Serikali kuu na Fedha za Nje. Hadi kufikia **30 Juni, 2022** Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs 5,874,441,215.11** sawa na asilimia **24** ya bajeti. Kati ya fedha pokelewa Halmashuri imetumia kiasi cha **Tshs 4,886,274,554.83** sawa na asilimia **83** katika utekelezaji wa miradi 62 Jedwali Na. 5 linaonesha Mchanganuo wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/22.